# MASOMO YA KUKUZA UANAFUNZI

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Shepherds Global Classroom ipo kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuwaendeleza viongozi wa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuongeza programu za mafunzo ya asili kwa kuweka chombo cha mtaala wa kozi 20 mikononi mwa viongozi wa kiroho wanaotoa mafunzo katika kila nchi duniani.

Kitabu hiki kinapatikana bure kwa njia ya kupakua kutoka katika https://www.shepherdsglobal.org/courses

Mwandishi Mkuu: Dr. Stephen K. Gibson

Hakimiliki © 2022 Shepherds Global Classroom
Ilitafsiriwa kutoka Toleo la Kwanza la Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa.

Nyenzo za wahusika wengine zilizotumika ni hakimiliki ya wamiliki husika ambazo zimeshirikishwa na kutumika humu chini ya leseni mbalimbali.

Tafsiri ya Maandiko “yaliyonukuliwa” kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, “Swahili Union Version Bible” (SUVB®).” Yametumika kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa kuhusu vibali:**

Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa na kutawanywa bure kikiwa kimechapishwa na katika mifumo ya kidigitali chini ya miongozo ifuatayo: (1) Maudhui yaliyoko kwenye kitabu hiki hayawezi kubadilishwa kwa namna yeyote ile; (2) Nakala zinazopatikana haziwezi zikauzwa kwa ajili ya kupata faida; (3) Taasisi za elimu zina uhuru wa kutumia na kukinakili kitabu hiki, hata kama wanalipisha ada za masomo ya ziada; na (4) Kitabu hiki hakiwezi kufanyiwa tafsiri pasipokuwepo na kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom.

# Yaliyomo


| Kitabu cha Mwongozo kwa ajili ya Uanafunzi | | |
|---|---|---|
| (1) Uanafunzi katika Kanisa | | 7 |
| (2) Kikundi Kidogo cha Uanafunzi | | 15 |
| (3) Kukidhi Mahitaji ya Wanafunzi Wapya | | 27 |
| (4) Utangulizi wa Mfululizo wa Masomo | | 31 |
| **Masomo ya Kukuza Uanafunzi** | **Somo la Kiongozi** | **Somo la Mwanafunzi** |
| (1) Maisha yenye kustahili Kuishi | 35 | 171 |
| (2) Kukutana na wokovu | 39 | 173 |
| (3) Uhakika wa Kukubaliwa na Mungu | 45 | 175 |
| (4) Kuwasiliana na Mungu | 49 | 177 |
| (5) Kusoma kile ambacho Mungu Alikiandika | 55 | 179 |
| (6) Kutoa Mwaliko | 59 | 183 |
| (7) Kuendeleza Utii Wangu | 67 | 187 |
| (8) Kujifunza Biblia katika ibada binafsi | 71 | 189 |
| (9) Kuomba kama Daudi | 75 | 191 |
| (10) Kusafisha Imani | 81 | 193 |
| (11) Kuanzisha Mazoezi ya Kiroho | 87 | 195 |
| (12) Kukubali Uwajibikaji wa Kiroho | 93 | 199 |
| (13) Faida za Maombi | 99 | 201 |
| (14) Kuomba kama Yesu | 103 | 203 |
| (15) Fursa ya ushindi juu ya Dhambi | 109 | 205 |
| (16) Shauku kwa ajili ya Umisheni | 113 | 207 |
| (17) Imani Idumuyo | 117 | 209 |
| (18) Tunahitaji Kanisa | 123 | 211 |
| (19) Kushinda Dhidi ya Majaribu | 127 | 213 |

| | | |
|---|---|---|
| (20) Mwongozo wa Mungu | 133 | 215 |
| (21) Vizuizi vya Maombi | 137 | 217 |
| (22) Mahusiano | 143 | 219 |
| (23) Mtindo makini wa maisha ya Kikristo | 149 | 221 |
| (24) Usemi wa Mkristo | 155 | 223 |
| (25) Maadili ya Kazi ya Kikristo | 161 | 225 |
| (26) Kufanya Maamuzi Sahihi | 165 | 227 |

# Kitabu cha Mwongozo kwa ajili ya Uanafunzi

# 1. Uanafunzi katika Kanisa

## Huduma ya Kufundisha kanisani

Wakati wa kuokoka kuna mabadiliko yanayotokea. Mtu aliyeokoka huwa na matamanio mapya na vipaumbele vipya. – kuna badiliko ambalo ni kubwa sana kiasi ambacho Biblia inamwelezea mtu huyu kama "Kiumbe kipya" (2 Wakorintho 5:17).

Lakini, mambo mengine huchukua muda. Mtu aliyeokoka haoni kwa mara moja jinsi ambavyo ataweza kutumia kanuni za Kikristo kwenye maeneo yote ya maisha yake. Anapaswa kwanza atafakari kuhusu kanuni, kisha apate jinsi ya kuzitumia.

Pia kuna mchakato binafsi wa ukuwaji wa kiroho. Mtu aliyeokoka ni "mtoto ndani ya Kristo."

► Soma 1 Wakorintho 3:1-2. Je, kwa mujibu wa aya hizi, mtu mpya aliyeokoka ni mtu wa aina gani?

► Soma Waebrania 5:13-14. Je, aya zinazohusiana na maziwa zinazungumzia kuhusu kitu gani? Je, chakula kigumu ni nini? Je, tabia ya mtu anayekulia kiroho ni ipi?

► Soma Mathayo 28:18-20. Kwenye kifungu hiki, je, ni majukumu gani ambayo Yesu aliyatoa zaidi ya uinjilisti?

Kabla ya kutoa Agizo Kuu, Yesu alieleza kwamba ana mamlaka yote mbinguni na duniani. Kisha akalipa kanisa jukumu la kuwaleta watu wawe watiifu kwa mamlaka yake.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake msihubiri injili tu, bali fundisheni mambo yote niliyowaamuru. Uinjilisti ni sehemu ya kwanza tu katika jukumu hilo. Kuwafundisha watu waliookoka kutii na kuyashika maagizo yote aliyokuwa ameamuru Yesu ni mchakato wa uanafunzi. Kushindwa katika uanafunzi ni jambo zito kama ilivyo kuanguka kwenye uinjilisti.

Huduma ya kufundisha kanisani inakusudiwa ilete watu wengi waliookoka kwenye hatua za ukuaji wa kiroho.

Kwenye Waefeso tunaambiwa kwamba Mungu huwaita watu na kuwapa majukumu ya huduma kwa ajili ya kuwajenga waumini wapya ili wasiendelee kuwa watoto wachanga (Waefeso 4:11-14). Kitendo cha wao kukua na kuwa watu wazima kiroho ni utulivu wa mafundisho ya imani.

Mchungaji ndiye hasa anayepaswa kuhusika na jukumu la kufanya uanafunzi. Paulo alimwambia Timotheo, "Ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha" (1 Timotheo 4:13). Kimsingi hakuwa anarejea kwenye jukumu binafsi la Timotheo kujifunza; alikuwa anazungumzia kuhusu huduma. Huduma ya Timotheo ilikuwa ni kuwekea fokasi kwenye kusoma na kuelezea Maandiko, akitoa mwelekeo wa kiroho, na kufundisha mafundisho ya

imani ya Kikristo. Moja ya sifa za mchungaji ni kwamba anapaswa awe mtu mwenye uwezo wa kufundisha (1 Timotheo 3:2).

Kwa kuwa kujifunza ni sehemu ya mabadiliko ya kiroho, kufundisha ni sehemu ya kazi ya uanafunzi. Waalimu ni muhimu sana katika kanisa, na kanisa ni lazima siku zote lifanye kazi ya kuwaendeleza waalimu.

"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine" (2 Timotheo 2:2). Agizo hili lilitolewa na Paulo kwa Timotheo, ikiwa ni kutoka kwa mwinjilisti na mchungaji mzoefu kwenda kwa mhudumu mpya kijana. Paulo hakuwa na uhakika kama imani ingeweza kufikishwa hadi chini kwa njia ya kuhubiri tu. Watu binafsi watahitajika wapewe mafunzo pakiwepo na juhudi maalumu na kuwaandaa katika kufundisha watu wengine. Kama mafunzo hayo hayatakamilika kwa kuwafundisha watu walioko kwenye kusanyiko, watu hawa "waaminifu" watapaswa wapewe mafunzo ya kibinafsi au wakiwa kwenye vikundi vidogo.

> "Lengo la kwanza la mpango wa Yesu ni kuwaorodhesha wanaume ambao wangeweza kuwa mashuhuda wa maisha yake na kuiendeleza kazi yake baada ya kuwa amerejea kwa Baba."
>
> - Robert Coleman, *The Master's Plan*

Kuna mafundisho mengi ya kufanyia kazi. Je, mchungaji atakuwa na nafasi gani ya kuyafanya yote, hasa wakati ambapo siyo kila mtu yuko tayari kwa mafundisho yaliyo sawa kwa wakati mmoja? Lakini Waefeso 4:11 haijasema, "alimpa mchungaji" (mtu mmoja tu na jukumu moja tu). Badala yake, kuna majukumu mbalimbali na watu kadhaa ambao wako kwa ajili ya kujaza nafasi hizo. Mungu anawaita waalimu, anawapa uwezo wa kufundisha, na anawawezesha kupitia kwa kanisa kwa ajili ya huduma ya kufundisha.

## Jumuiya ya Kikristo na Uwajibikaji wa Kiroho

Uanafunzi wa kweli ni zaidi ya kufundisha habari; Inajumuisha kuboresha maadili, vipaumbele, tabia, na mfumo wa maisha. Mchakato huu unaweza tu kutokea tu kwenye jumuiya ya Kikristo yenye uwajibikaji wa kiroho.

Tunaona katika Maandiko kwamba Mungu alikusudia watu waishi kwenye jumuiya, kuanzia na maneno ya Mungu kwamba si vyema Adamu awe peke yake (Mwanzo 2:18).

Faida za kuwepo kwa jumuiya zimeelezwa katika Mhubiri 4:9-10: "Afadhali kuwa wawili kuliko mmoja; Maana wapata ijara njema kwa kazi yao. Kwa maana wakianguka, mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo, wala hana mwingine wa kumwinua."

Mungu alimwambia Musa kwamba mpango wake kwa ajili ya Israeli ulikuwa ni ili wawe ufalme wa makuhani na taifa takatifu (Kutoka 19:6). Urithi huo ulikuwa urithishwe hadi kwenda chini kupitia kwenye familia, ulioelezwa kwenye kile kinachoitwa "Amri Kuu" (Kumbukumbu la Torati 6:4-9).

Roho Mtakatifu aliwavuvia waandishi wa Agano Jipya kutumia maandishi hayo kwenye Agano Jipya ikiwa ni kurejea kwenye kanisa (1 Petro 2:9 ).

Mungu daima alikusudia watu walio katika uhusiano naye wawe na uhusiano wao kwa wao. Uhusiano wetu na Mungu hutufanya kuwa jumuiya ya Imani, kama vile uhusiano wetu na Mungu unahitaji kujitolea, pia uhusiano wetu na watu wa Mungu unahitaji kujitolea. Ni makosa kwa mtu kufikiria kwamba anaweza kuwa na uhusuiano mzuri na Mungu lakini akachagua kutokuwa na uhusiano na watu wa Mungu.

Paulo alitumia sitiari ya mwili kuelezea kuhusu uhusiano miongoni mwa waumini wa kanisa (1 Wakorintho 12 ). Hakuna kiungo cha mwili kinachoweza kufanya kazi vizuri kama kitajaribu kujiweka peke yake nje ya mwili. Viungo ni lazima vishirikiane na kila kimoja kujali kingine, au vinginevyo mwili utakuwa haupo. Kama ikitokea kiungo kimoja kimedhuriwa, viungo vingine vyote vinaumia. Kitendo chochote cha kiungo kimoja kinaathiri mwili mzima Paulo alizungumza haya alipokuwa akishughulika na hali ya mtu aliyeko kwenye uhusiano wa ukosefu wa kimaadili, ingawaje alitumia sitiari ya mkate badala yake. Alisema, "Hamjui kwamba chachu kidogo hulichachusha donge zima?" (1 Wakorintho 5:6). Ni lazima tujione sisi wenyewe kama viungo muhimu sana kwa ajili ya jumuiya ya Kikristo.

Haiwezekani kuzitii Amrizilizo nyingi za Agano Jipya bila kuwa na hisia ya jumuiya, Ili kutimiza amri za Mungu, Wakristo lazima waishi kwa kujitoa wao kwa wao. Hii inamaanisha kwamba jumuiya ya Kikristo inaongoza kwa uwajibikaji wa kiroho.

Tunaona kwenye maeneo mengi ya Biblia ambako Wakristo wameunganishwa kwenye uwajibikaji wa kiroho.

> Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewafaa ninyi (Waebrania 13:17).

Aya hii inawaeleza waamini kujitoa kabisa kwa kuwatii na kuwanyenyekea wale walioko kwenye nafasi za mamlaka ya kiroho. Agizo hili pia linatoa uwajibikaji mkubwa kwa viongozi wa kiroho. Wajibu wao siyo tu kuongoza kwa mamlaka, lakini kuziangalia roho za watu walioko chini ya uangalizi wao. Kwa kufanya hivyo, ni lazima wawe wameshikamana na kufahamiana sana na watu wao katika kuwapa maelekezo ya kiroho, na ni lazima wawe na uhusiano na watu wao ambao unawezesha maelekezo hayo yawe yanayowezekana kutekelezeka.

Jumuiya ya Kikristo na uwajibikaji wa kiroho vinaelezwa pia katika kifungu hiki:

► Soma Waebrania 10:24-26. Je, ni kitu gani kinachoagizwa katika kifungu hiki?

Tunaagizwa hapa kwamba tuwe na ufahamivu au tuwe macho na mahitaji ya Wakristo wengine na kuwatia moyo wafanye mambo yaliyo sahihi.

► Elezea uhusiano utakaoweza kuwa muhimu miongoni mwa waumini kwa ajili ya wao kukamilisha jukumu hili.

Kutia kwetu moyo hakutakuwa kwa ufanisi endapo hatutakuwa na uhusiano ulio sahihi na watu wengine. Tunapaswa tuwaelewe vizuri na tuwaonyeshe upendo na kuhusika kwetu kwa ajili yao. Vinginevyo, watakuwa wanakwazika au wanabweteka na ushauri binafsi unaotolewa.

> Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi (Waebrania 3:12-13).

Tumeitwa kuwajibika sisi kwa sisi. Hapa kuhimizana ni lazima uwe zaidi ya kwenda katika mikutano iliyopangwa ya kanisa zima, kwa maana tumeamriwa kuhimizana "kila siku." Hii inahitaji ushirika wa mtu binafsi au kikundi kidogo. Ushirika wa aina hii hautakuwa ni kwa ajili ya kula pamoja au kutembeleana tu, bali utakuwa na kusudi la kiroho. Ili kukamilisha kusudi hili, ni lazima tupange kwa makusudi mazungumzo na mikutano ya kikundi vidogo kwa kipaumbele hicho.

Njia ambayo tunaweza kufaidiana kati ya mtu mmoja na mwingine imeelezwa katika Mithali 27:17:

> Chuma hunoa chuma; Ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki yake.

Mtu mmoja hahitajiki kuwa bora kuliko mtu mwingine kabla ya kumnufaisha kwa mwongozo wa kiroho na kumtia moyo kiroho. Kwa kweli, mwongozo wa kiroho uliotolewa kwa unyenyekevu una uwezekano mkubwa zaidi wa kukubaliwa.

> Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii (Yakobo 5:16).

Kuungama kwa makosa binafsi kwa kawaida hakutaweza kujitokeza kwenye vikundi vikubwa; kwa hiyo, agizo hili halitekelezwi kirahisi kwenye huduma au ibada za kanisa. Muktadha hapa unaonyesha sababu ya agizo hili: ili kwamba wale waliokosea waweze kurejeshwa tena.

> Mchukuliane mizigo na hivyo kuitimiza sheria ya Kristo (Wagalatia 6:2).

Mara nyingi Mkristo huhisi kwamba hakuna mtu anayejali katika kile anachokuwa anapitia. Wakristo wenzake wanaweza wakajali kama wangeelewa kiukweli matatizo anayopitia, lakini kwa kawaida wanakuwa hawamjui kiasi cha kutosha kumwelewa. Je, tutawezaje kuchukuliana mizigo ya watu wengine kama kwa uhakika hatuwajui wao ni nani hasa?

Kwenye siku za zamani baada ya kuzaliwa kwa kanisa, uhusiano wa karibu miongoni wa watu waliokuwa wameamini ulikuwa ni jambo la kawaida kabisa.

> Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe (Matendo 2:46).

John Wesley alisema kwamba hakuna kitu kama ukristo wa mtu binafsi.

► Je, unafikiri Wesley alikuwa anamaanisha nini kwa tamko lake hilo?

Uwajibikaji wa kiroho hutokea kwenye jumuiya ya Kikristo yenye afya au uwezo mkubwa.

Kuwa na uwajibikaji wa kiroho ni kuanzisha uhusiano na mtu au kikundi ambacho tunatoa taarifa zetu za kiroho, mafanikio au kushindwa kwetu katika mazoezi ya kiroho, na maamuzi yetu ya kuendeleza maeneo fulani.

Pasipo kuwepo na uwajibikaji wa kiroho hatutaweza kukamilisha maagizo yote yaliyoko kwenye maandiko, na tutapuuzia njia ambazo Mungu amezitengeneza kwa ajili ya kutupa sisi neema.

## Sifa za ukomavu wa Kiroho

Inamaanisha nini kukomaa kiroho? Unawezaje kumwelezea mkristo aliyekomaa?

Kwa sababu ukomavu huchukua muda, na hufuatana umri (Tito 2:1-5). Ni wazi kuna watu fulani wanazeeka bila kukomaa kiroho kama wanavyopaswa, na kuna vijana wanaoonesha ukomavu usio wa kawaida.

Tabia nyingi za ukomavu hazipatikani kabisa katika hatua fulani, lakini huongezeka hatua kwa hatua. Wakati mwingine wanaweza kuongezeka ghafla kwa sababu ya uzoefu wa kiroho au uzoefu katika maisha. Mtu mwenyewe akijiendeleza katika maisha yake, kuna kiwango anachoweza kufikia ambacho kinaweza kuitwa ukumavu wa kiroho.

Sifa za ukomavu wa kiroho zimeelezwa katika vifungu kadhaa vya Maandiko.

► Soma Waefeso 4:11-14, Waebrania 5:12-6:1, 1 Wakorintho 3:1-2, 1 Yohana 2:12-14.

Ifuatayo ni orodha ya sifa ambazo ni ishara za ukomavu wa kiroho. Hii siyo orodha kamili, na vidokezo vingine kwenye orodha hii haviwezi kutofautishwa kabisa na vidokezo vingine.

Mkristo aliyekomaa hawezi kuonyesha sifa hizi zote kabisa, lakini anakua. Huenda asitambue baadhi ya makosa haya, lakini ataitikia kazi inayoendelea ya Roho Mtakatifu moyoni mwake.

## Sifa Kumi za Ukomavu wa Kiroho

### (1) Kufanana na Kristo katika nia, mitazamo na matendo.

Kumfanania Kristo kunatokana na shauku ya kufahamu Kristo katika asili yake, kwa kuwa na uzoefu wa kiroho wa kifo na kufufuka kwake (Wafilipi 3:10). Hii inaweza kujumuisha pamoja na maumivu yake katika mateso. Mtu anayempenda Kristo kwa jinsi hii atabadilishwa na kufanana na yeye.

Kumfanania Kristo ni kuhamasika na upendo na siyo suala la ubinafsi au majivuno. Mkristo anataka awe anayemfanania Kristo na huwa na masikitiko anapojitambua kwamba hakumfanania Kristo katika jambo alilolisema au alilolifanya.

**(2) Uhusiano wa karibu na Mungu**

Mtu anapaswa kukua zaidi kwenye uhusiano wake na Mungu. Alama au ishara za kuwa kwenye uhusiano na Mungu ni pamoja na kufurahia uwepo wa Mungu, kulipenda neno la Mungu, na muda unaotumika kwenye maombi.

**(3) Udhihirisho wa matunda ya Roho**

Roho Mtakatifu hutengeneza tunda la kiroho katika maisha ya mwamini, ikiwa ni pamoja na u pendo, furaha, subira na kiasi. Mwamini anakuwa na uthabiti zaidi wa mara kwa mara katika ukarimu na upole anapomruhusu Roho Mtakatifu kufanya kazi katika mwenendo wake.

**(4) Ushindi juu ya dhambi ya nje na ya ndani.**

Mwamini hujifunza jinsi ya kumtegemea Mungu kwa ajili ya ushindi katika majaribu. Anakubaliana na utakaso wa Mungu ili aweze kuwa na moyo wa utakatifu. Huwa anakuza tabia na nidhamu mbalimbali ambazo zitamsaidia kuishi mfululizo katika ushindi.

Anapojikuta ameingia kwenye jaribu na kushindwa, hutubu kwa Mungu na kuomba msamaha na nguvu. Atapaswa ashirikishe mapungufu yake ya kushindwa kwa marafiki zake wa karibu waliokoka wanaomwombea (Yakobo 5:16).

**(5) Nidhamu za kiroho zinaanzishwa**

Nidhamu za kiroho ni njia za kujizoeza katika kufanya mahusiano yetu na Mungu yawe kipaumbele cha kwanza. Mtu ambaye mara kwa mara siyo mwombaji, hasomi Biblia, na kuhudhuria ibada za kanisa siyo Mkristo aliyekua.

**(6) Kukuza tabia ya Kikristo**

Mkristo hujifunza kupanga maisha yake kwa kanuni ya uaminifu, kutegemewa na wengine na kwa kazi ya uaminifu.

**(7) Kuishi maisha ya Kikristo uthabiti**

Mkristo hujifunza kutumia kanuni za Kikristo kwenye maisha yake katika misingi ya uaminifu na kutegemewa. Mkristo aliyekua anapaswa atake kufanana na Kristo wakati wote katika tabia na mitazamo yake. Anapojitambua kwamba kile anachokifanya au anachokitenda hakiendani na upendo katika moyo wake, atamtegemea Mungu katika kupata nguvu na kuwa na uwezo wa kufanya mabadiliko.

### (8) Mahusiano yenye afya au nguvu

Mkristo aliyekomaa hukuza urafiki wa kina na wakristo wengine. Anadumisha mahusiano kwa kuonyesha uaminifu, subira na msamaha. Ni mnyenyekevu na anakubali makosa, kwa sababu anaweza kutoielewa hali fulani, huenda asiwe na subira inavyopaswa au asikubali makosa haraka au asiwe na maoni sahihi kuhusu mtu mwingine.

### (9) Huduma ya mtu

Mwamini anapaswa atambulishe karama zake za kiroho. Anapaswa atafute nafasi yake kwenye kanisa ili aweze kuwa baraka kwa wengine. Mwamini anaweza akahudumu kwenye kanisa kwa kusaidia katika kufanya uinjilisti na kufanya ufuasi kwa watu wengine waweze kuwa katika maisha ya Kikristo.

### (10) Uvumilifu wa hali ngumu

Mwamini anapaswa kujifunza kumwamini mungu wakati mambo magumu yanapojitokeza. Anapaswa amtegemee Mungu anapokuwa katika hali ambazo ni ngumu. Mwamini aliyekomaa hapotezi imani yake wakati anapokuwa haelewi ni kwa nini jambo fulani linajitokeza.

## Hitimisho

Sifa za ukomavu wa kiroho hazitegemei talanta asilia.

Hazifanani na ujuzi wa huduma.

Siyo lazima ziambatane na uwezo wa uongozi. Ni vyema kiongozi akawa ni mtu aliyekomaa kiroho, lakini wakati mwingine mtu huweza akawa kiongozi kwa sababu ya uwezo wake, wakati akiwa bado hajakomaa kiroho. Wakati mwingine mtu huwa amekomaa kiroho, lakini akawa hana ule uwezo wa uongozi.

Baadhi ya aina za hulka za watu huonekana kwa hali ya asili kwamba ni zaidi ya uvumilivu na ukarimu. Sifa za asili kwa ajili ya haiba ya mtu hazifanani na kukua kiroho. Mungu hufanya kazi ndani ya haiba zetu na hutusaidaia kuleta uwiano katika mielekeo yetu. Ikiwa kama tutafanya uchambuzi wa mtu fulani maalumu, hatuwezi kutofautisha kwa uhakika kabisa kati ya utu wake wa asili na sifa za ukuaji endelevu wa kiroho.

Matatizo ya kiafya yanaweza pia yakaathiri utambuzi na mjibizo wa mtu. Hatupaswi tuwe na haraka ya kuwahukumu watu wengine.

### Mazoezi ya Kutumia

(1) Jichunguze mwenyewe katika sifa kumi za kukua kiroho. Kwa maombi, tafakari ni sifa zipi ambazo unazikosa zaidi. Panga jinsi ambavyo kwa makusudi kabisa utajiendeleza katika hizo kupitia maombi, kujifunza, ushauri kutoka kwa watu wengine, na kuwa unayetegemea msaada wa Mungu.

(2) Je, ni kwa jinsi gani kanisa kwa makusudi kabisa linaweza likatimiza jukumu lake kwa ajili ya ufundishaji na uwajibikaji wa kiroho? Andika kurasa mbili zinazoelezea utekelezaji wa mpango kazi kwa ajili ya kanisa.

# 2. Kikundi Kidogo cha Uanafunzi

## Thamani ya Vikundi Vidogo vya Uanafunzi

Huduma ya vikundi vidogo viko kwa ajili ya utendaji wa aina mbalimbali ulimwenguni kote. Kuna aina nyingi za vikundi vidogo, vilivyoundwa kwa ajili ya Madhumuni tofauti. Vikundi vidogo vinaweza vikawepo kwa ajili ya kukutana kwa mafunzo, kuwajibika kiroho, huduma, maombi, au kwa ajili ya miradi maalumu.

Makanisa mengine yamegawanyika kwenye vikundi ambavyo hukutanika majumbani kwa watu. Vikundi hivi hufanya kazi kama makanisa madogo. Makanisa ya wakati wa Agano Jipya yalifanya kazi kama hivi.

Makanisa yanayokuja na yenye ufanisi kwa kawaida yana aina fulani ya mfumo huu wa vikundi vidogo.

Katika sehemu hii, tutazungumzia kuhusu ufanisi wa vikundi vidogo kwa ajili ya uanafunzi.

## Mfano wa Wesley

John Wesley (Mwingereza, wa karne ya 18) hakuwa mtu wa kwanza katika kuunda vikundi vidogo, lakini alianzisha mfumo ambao ulikuwa na ufanisi wa kiwango cha hali ya juu sana.

Wesley aliendeleza mfumo wa ufuasi uliokuwa katika vikundi vya ukubwa wa aina mbalimbali vilivyoitwa vya kijamii, tabaka na vikosi.[1] Mbinu za Wesley hazikuwa mfumo kamili wakati wa kuanza, lakini zilikuzwa hatua kwa hatua ili kukidhi mahitaji. Watu wengi wa Wesley waliokuwa wameokoka waliomba kutiwa moyo, ushauri, na maombi. Kwa kuwa walikuwa wengi sana, aliwapanga wawe wanakutana kila siku ya Alhamisi.

Kila sehemu ambayo Wesley na wahubiri wake walipeleka injili, waliwapanga waliookoka katika vikundi vilivyokutana mara kwa mara. Kwa kuwa makutaniko yalikuwa makubwa, wengi hawakuweza kusema mahitaji yao binafsi ya kiroho na hawakuwa wakipata uangalizi waliyohitaji. Vikundi vidogo viliundwa vilivyoitwa madarasa, ambapo viongozi walihudumu kama wachungaji ili kuwatia moyo na kuwaongoza washiriki. Mwanakikundi yeyote ambaye aliendelea na dhambi ya wazi na hakubadilika aliondolewa uanachama na hakuruhusiwa kufika kwenye mkutano.

Vikundi vidogo vilivyokuwa vidogo kuliko madarasa viliundwa kusudi wanakikundi waweze kushirikishana mapito yao ya kiroho na kumpa kila mmoja wajibu wa kuwajibika kiroho. Vikundi hivi vidogo vilikuwa vinaitwa vikosi. Kwenye mikusanyiko yao kiongozi alipaswa ajieleze kuhusu hali yake yeye mwenyewe ya kiroho, kisha ndipo awaulize wengine maswali

[1] Ona “A Plain Account of the People Called Methodists,” in *The Works of John Wesley, Volume VIII* (Grand Rapids: Zondervan), 249-258.

ya kutaka kujua kuhusu hali zao za kiroho, dhambi, na majaribu. Kwenye vikundi hivi, wanakikundi walikuwa wote ni wa jinsia moja.

Mafanikio ya Wesley yalimfanya mtu aliyekuwa mashuhuri sana aliyeitwa George Whitefield kutoa taarifa hii: "Ndugu Wesley alifanya kwa hekima sana – roho zilikuwa zinaamshwa chini ya huduma yake na kuziunganisha katika darasa, na kwa ajili hiyo akatunza tunda la kazi yake. Katika hili mimi nilizembea, na watu wangu wamekuwa kama kamba ya mchanga." Mbinu za Wesley ziliendelezwa na kanisa la Methodisti la Marekani kwenye miaka ya mwanzo, lakini Umethodisti wa wakati huu umezembea kabisa katika mambo yote kwa pamoja yanayohusu kanuni za uanafunzi na mafundisho yake ya imani.

## Kulielewa Kanisa Muhimu

Jengo la kwanza kabisa la kanisa ambalo limepatikana lilijengwa takribani 250 B.K. Kwa karne mbili za kwanza, kanisa lilijiona kama watu, siyo kama jengo au shirika. Kanisa linaundwa na vikundi vya Wakristo wanaoabudu pamoja kueneza injili, na kuitii Biblia.

Vikundi vidogo vya watu ni kama matofali ya ujenzi wa kila muundo wa kanisa wenye ufanisi. Mpango wa ufuasi wa kikundi kidogo sio taasisi mpya ambayo siku moja itapitwa na wakati. Sio njia mpya ambayo inaweza kufanya kazi katika baadhi ya maeneo. Badala yake, vikundi vidogo ndio matofali ya ujenzi wa kanisa. Huduma katika vikundi vidogo inaweza kufanywa kwa njia mbalimbali ili kukabiliana na changamoto ambazo kanisa lolote la mtaa hukabiliana nazo.

Kanisa halitaweza kukamilisha kusudi lake hadi pale watu wake wanapokuwa wanatiwa moyo mara kwa mara na kupewa mafunzo kwa namna ya mtu binafsi zaidi kuliko katika kusanyiko zima au shule nyingi za Jumapili.

### Angalizo

Vikundi vidogo ni vya kiroho tu kama watu wake wanaohusika ndivyo walivyo. Ikiwa siyo wanafunzi waliojitoa kwa kipaumbele cha kumpendeza Mungu, kuishi maisha ya uaminifu, na kutimiza utume wa kanisa, kuna njia nyingi ambazo kikundi kinaweza kujikuta kinakwenda vibaya.

## Hitaji la Uwajibikaji wa Kiroho

Kuwa na uwajibikaji wa kiroho ni pamoja na kuanzisha uhusiano na mtu au kikundi ambapo unatoa taarifa za hali yako ya kiroho, mafanikio yako au kushindwa kwako katika mazoezi ya kiroho, na ahadi zako za kukua. Wanakueleza wanapofikiri kwamba unatenda vibaya. Unawaeleza mambo unayotekeleza, na wanakuuliza baadaye kama unasimama vizuri kwenye kutimiza ahadi zako.

Msingi wa kibiblia wa uwajibikaji wa kiroho kwenye jumuiya ya Kikristo umeelezwa kwa uwazi zaidi kwenye sehemu ya kwanza iliyopita. Bila ya kuwepo na uwajibikaji wa kiroho, hatutaweza kutekeleza maagizo yote yaliyoko kwenye Maandiko, na tutadharau njia ya Mungu ambayo ameiandaa kwa ajili ya kutupa sisi neema.

> Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii (Yakobo 5:16).

Mtu hataweza kukiri makosa yake binafsi maovu ya siri isipokuwa awe kwenye uhusiano ambao utamfanya ajione ana urahisi wa kufanya hivyo. Endapo atakuwa hakiri kwa mtu ambaye anamwombea kwa ajili ya makosa yake, atakuwa anapuuzia njia ya Mungu aliyoiratibu kwa ajili ya kukutana na mahitaji hayo.

> Mchukuliane mizigo na hivyo kuitimiza sheria ya Kristo (Wagalatia 6:2).

Kama tutakuwa hatuwezi kumfahamu mtu vizuri sana, tutakuwa hatujui mizigo wake mkubwa zaidi ni upi. Hatuwezi kutimiza agizo hili la kimaandiko bila ya kuwa katika uhusiano ambao utaweza kufanya mambo yawezekane.

> Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri (Waebrania 10:24).

Tunachunguzana kwa ukaribu na kwa nia ya upendo ili kuona ni maeneo gani ya kutiana moyo na kukaripia ni vya lazima. Kutiana moyo kunaweza kuwa ni kidogo, na kukaripiana kukawa hakuzai matunda isipokuwa tukiwa na uhusiano wa pekee na mtu mwingine.

Maswali yafuatayo yanaweza yakamsaidia mtu kuamua kama kuwajibika au kutowajibika kiroho kumeanzishwa katika maisha yake.

Je, nina uhusiano gani ambao unanifanya kuwe na uwezekano kwamba mtu fulani ananisaidia mimi kubeba mizigo yangu mizito zaidi, ninakiri makosa yangu kwa mtu fulani, ninamsaidia mtu mwingine katika kubeba mizigo yake, na mtu fulani anawajibikia hali yangu ya sasa ya kiroho?

Je, kuna nyakati ambazo inaweza ikatokea nikajikuta sina mtu ninayeweza kumtegemea, nyakati ambazo nina furaha ambayo hakuna mtu anayejua kuhusu hali yangu, na nyakati ambazo ningeona kama ni fedheha kwa kutoa taarifa ya wakati wangu wa maombi au wakati wa kujifunza Biblia?

Makanisa mengi hayatimizi hitaji la uwajibikaji wa kiroho isipokuwa kama yanapanga utaratibu kufanya hivyo. Kwa walio wengi, huo ni mfumo wa vikundi vidogo.

### Sifa za Kiongozi wa Kikundi Kidogo

Yesu alionyesha kipaumbele cha uanafunzi. Tangu mwanzo wa huduma yake alichagua watu wachache ambao wangechukua jukumu la kuliongoza kanisa. Hakuutumia muda wake wote kwenye kuhubiri tu kwa maelfu ya wafuasi waliokuwa wamemfuata; badala yake, mara kwa mara alikuwa anautumia muda wake katika kuwafundisha

> "Ingawa alifanya kile alichoweza katika kusaidia umati wa watu, kimsingi ilimbidi ajitolee muda wake mwenyewe kwa ajili ya watu wachache, kuliko mikusanyiko ya watu wengi, ili kwamba makundi mengi ya watu yaweze kuokolewa. Hii ilikuwa ni busara iliyokuwepo kwa ajili ya mkakati wake."
>
> - Robert Coleman, *The Master's Plan*

wanafunzi wake kumi na wawili. Yesu alipanua huduma yake kutokana na wale watu aliokuwa amewafundisha.

Mtu anayefanya huduma ya uanafunzi anapaswa awe na sifa zifuatazo hapa chini. Hataweza kuwa mzuri katika kila sifa, lakini atapaswa ajitahidi kujiongeza katika sifa zote. Kama akikosa mojawapo ya sifa hizo, atakuwa ni mtu mwenye ufanisi mdogo.

1. **Awe mtu aliyekua Kiroho.** Anapaswa awe na sifa za kukua kiroho zilizoelezwa katika sehemu iliyopita. Kama atakuwa ni mtu ambaye hajakua kiroho, hataweza kuonyesha au kuweka mfano mzuri, na hatakuwa na uzoefu atakaokuwa anauhitaji.

2. **Awe mtu anayepatikana.** Kama mpango au ratiba yake itakuwa imejaa sana na isiyokuwa umepangiliwa na kuthibitiwa kwa utaratibu mzuri, hataweza kupatikana kwa ajili ya huduma ya kikundi kidogo. Ni lazima alifanye liwe jambo la kipaumbele.

3. **Awe mtu wa kutegemewa.** Ni lazima awe mtu anayotekeleza majukumu yake. Ni lazima awe na uwezo wa kutimiza ahadi zake. Ni lazima awe na uwezo wa kukumbuka kuwafanya watu wengine watimize majukumu yao.

4. **Mtu mwenye kujiamini.** Ni lazima aamini kwamba anao uwezo wa kujifunza jinsi ya kuongoza kikundi. Kama atakuwa anao uwezo lakini hajiamini, kwanza anahitaji watu wenye uzoefu wa kumwongoza ambao wataweza kuimarisha kujiamini kwake.

5. **Awe mtu mwenye uwezo wa kutatua migogoro.** Anahitajika awe ni mtu mwenye kutunza tabia yake kwa usahihi wakati inapotokea watu kutokuikubali na kusababisha matatizo. Anapaswa aweze kuwa na uwezo wa kusaidia katika kutatua migogoro iliyopo kati ya watu wengine.

6. **Mwenye uwezo wa kufundisha.** Je, watu huwa wanamwelewa maelezo yake? Kiongozi anapaswa awe mtu asiyewafanya watu wengine wachanganyikiwe.

7. **Mwenye njaa kwa ajili ya Neno la Mungu.** Anapaswa awe mtu wa kulifurahia Neno la Mungu, ili aweze kuwakaribisha watu wengine na wao kufurahia pia. Atapaswa aifanye Biblia iwe ni muhimu sana kwake kwenye uhusiano wake na Mungu.

8. **Mtu mwenye kumtegemea Mungu peke yake.** Ni lazima aweze kutambua kwamba matokeo ya kiroho yanaweza tu kupatikana kutoka na utendaji kazi wa Roho Mtakatifu. Ni lazima awe tayari kushirikiana na Roho Mtakatifu. Ni lazima awe tegemezi kwenye upako wa kiroho kutoka kwa Mungu. Hapaswi kuwa mtu wa kujiamini sana kwamba maelezo yake yatakuwa yanafanikiwa kila mara kutokana na ustadi wake peke yake.

9. **Mtu aliye tayari kutumika.** Ni lazima awe mtu wa kujisikia kwamba anafanya jambo la thamani anapokuwa anawahudumia watu wengine. Hapaswi kuwa mtu ambaye anataka awe akitumikiwa. Hapaswi awe mtu anayetafuta huduma kwa kusudi la kuonyesha vipaji vyake alivyo navyo.

10. **Mtu aliye chini ya mamlaka ya kiroho.** Anapaswa awe anawajibika kiroho chini ya mtu mwingine. Anapaswa awe mtu anayefuata maelekezo ya viongozi wa kiroho.
11. **Mtu mwaminifu kwa kanisa.** Kiongozi wa kikundi anapaswa kuwa mshirika wa kanisa la mtaa aliyejitolea. Huduma ya ufuasi inapaswa kusababisha watu kuthamini kanisa na kujitoa zaidi kwake.
12. **Mtu mwenye Bidii ya mafanikio.** Kama atakuwa mtu mwenye nia ya kufanikiwa, hatapenda kukata tamaa haraka. Atajizoesha kwenye hali zilizopo. Atafanya kazi ya kutafuta taarifa ambazo zitamsaidia kuwa mtu atakayekuwa na ufanisi zaidi. Atatakiwa awe na uwezo wa kuvumbua njia kunapokuwa kuna matatizo au nafasi. Atakuwa na nguvu na mwenye shauku.
13. **Mtu aliye sahihi kwenye mafundisho ya imani.** Anapaswa awe mtu mwenye msingi mzuri wa mafundisho ya imani ya kibiblia na ya Kiinjili.
14. **Mtu aliyefundishika kwa ajili ya huduma.** Hakuna ulazima wa mafunzo ya huduma kufanyika kwenye taasisi za elimu. Mafunzo huanza kwa kutazama, mwamini anapoona jinsi huduma inavyofanyika. Mafunzo huongezeka kwa mshiriki kupewa majukumu akiwa katika uangalizi. Kusoma na kujifunza kutoka katika vitabu vizuri vya mafunzo ni muhimu sana.

## Kukuza Mpango kazi ya Uanafunzi

Njia iliyo bora ya uanafunzi kuweza kutokea ni kwa kanisa la mtaa kuelewa majukumu na vipaumbele vya uanafunzi na kufanya kazi kwa umoja.

Kwa hiyo, maelekezo haya yanakusudiwa kuelekezwa kwa viongozi na wanachama waliojitoa kabisa kwa ajili ya kanisa.

Kama kanisa litatambua kwamba wanahitaji kufanya vizuri zaidi kwenye huduma ya uanafunzi, wanapaswa kwanza kujifunza maandiko na kuelekeza katika kozi hii ya uanafunzi wa kristo. Viongozi wanaweza kuwasilisha masomo haya ya kujifunzia. Washiriki wote wa kanisa wanaojitoa wanapaswa kuhusika kama ikiwezekana ili kushiriki maono haya.

Sehemu ya pili ya ukuzaji ni kuchunguza kile ambacho kanisa tayari linafanya. Makanisa mengi yanayo vikundi ambavyo kwa sasa tayari vinafanya kazi, hata kama hawajakusudia kuanzisha programu za kikundi kidogo. Kwa mfano, inaweza kukawepo na kikundi cha wanamuziki katika kanisa ambacho kinakutana mara kwa mara. Panaweza kuwepo na kikundi cha uimbaji kitakochokuwa kikifanya mazoezi. Panaweza kuwepo na bodi ya mashemasi. Panaweza kuwepo na madarasa ya Biblia ya jumapili, na waalimu wa madarasa hayo ya jumapili wanaweza wakaunda kikundi chao. Vijana wa kanisa wanaweza wakawa wanakutana mara kwa mara. Kikundi kinaweza kikaundwa na watu wanaofanya kazi pamoja kwenye mradi. Kunaweza kuwepo na familia za kanisa ambazo zitakuwa zikikutana mara kwa mara kwa ajili ya ushirika. Kunaweza kuwepo na mafundisho ya Biblia ya nyumba kwa nyumba na makutaniko ya maombi.

Inawezekana vikundi hivi havikuanzishwa kwa ajili ya kusudi la uanafunzi au uwajibikaji wa kiroho, lakini vinaweza kusaidia katika kuwezesha kutimiza makusudi hayo. Kanisa lolote ambalo lina maisha ya kiroho linakuwa tayari lina vikundi vinavyofanya kazi kwa ajili ya kuendeleza maisha hayo ya kiroho. Wakati kanisa linapoamua kukuza na au kuendeleza programu yake ya uanafunzi, linapaswa liviangalie vikundi vilivyopo na kutaka kugundua ni nini kinachoendelea, kisha kufikiri jinsi makusudi yanavyoweza kufikiwa kwa njia iliyo bora zaidi.

Vikundi vipya vinaweza vikahitajika. Inawezekana vikundi vya aina mbalimbali vikahitajika. Inawezekana kukawepo na vikundi ambavyo vinatoa mafunzo ya huduma kwa vitendo. Inawezekana kukawepo na vikundi ambavyo kimsingi ni kwa ajili ya kujifunza Biblia na maombi. Inawezekana kukawepo na vikundi vidogo kwa ajili ya uwajibikaji makini wa mambo ya kiroho.

Makusudi ya kikundi hupima ni nani atakuwepo pale na ni kwa jinsi gani kikundi kinaweza kufanya kazi. Kwa mfano, kikundi kwa ajili ya uwajibikaji makini wa mambo ya kiroho kinapaswa kiwe na watu wachache wasiozidi kumi. Endapo kikundi kitakuwa kikubwa sana, usiri wa kikundi utapungua, ushirikishwaji unakuwa mdhaifu, uangalizi mkubwa unahitajika na ni muhimu, ushiriki unakuwa ni mdogo, na mahudhurio huweza yakawa mabaya sana. Kina cha ushirikishanaji binafsi utakuwa wa kiwango kidogo kama wanaume na wanawake watakuwa wako pamoja.

Kusudi la kikundi litaamua kama inapaswa kuongeza wanachama wapya au la. Kama kusudi ni kwa ajili ya uwajibikaji wa mambo ya kiroho, haitapaswa kuongezwa tena wanachama wapya baada ya kikundi kukutana mara nyingi. Watu wengi hawataweza kushirikisha hali zao za kiroho, hadi watakapojisikia kuwa wako salama pamoja na wengine katika kikundi. Kama madhumuni ya kikundi ni kufundisha mfululizo wa masomo, siyo jambo la busara kuongeza watu katika mfululizo wa vipindi vya mkutano.

Inawezekana kukawepo na kikundi cha watu wapya waliookoka. Ni muhimu sana kwamba mtu mpya aliyeokoka asisubirishwe kukaa kwa wiki kadhaa ili kujiunga na kikundi. Kwa hiyo, kikundi hiki kinahitaji kiwe na mafunzo mengi ya mfululizo yanayorudiwa rudiwa ili watu wapya wanaookoka waweze kujiunga na kikundi. Viongozi ni lazima watambue kwamba watu wapya waliookoka wakijiunga na kikundi wanaweza wakajitoa. Ukweli ni kwamba watu wengine kuondoka kwenye kikundi haimaanishi kwamba kikundi hakifanyi vizuri, Ingawaje baadhi yao watajiondoa, kikundi kipya kwa ajili ya watu waliookoka kinapaswa kiwe wazi kwa ajili watu wapya waliookoka wanaotaka kujiunga.

Kama kikundi kiko kwa ajili ya kufundishwa huduma au kupata ukuaji wa kina wa kiroho, wanachama wa kikundi ni lazima wawe watu ambao wana matamanio ya kukua kiroho na wako tayari kuwajibika kikamilifu kwa ajili ya malengo ya kikundi. Ikiwa baadhi ya wanachama watakuwa watu ambao hawajibiki kikamilifu, kikundi hakitaweza kufanya vizuri katika kufikia kwenye lengo lake.

Wanachama wengi ni lazima wapewe mafunzo kwa kupewa mialiko. Usingojee hadi watu waanze kuomba kujiunga.

Siyo kila mtu kwenye kanisa atakayeweza kushiriki kwenye shughuli za kikundi kidogo. Kama wewe ni kiongozi katika kanisa, usiwe sababu ya watu kuondoka kwa sababu ya kuwalaumu kwa kutojiunga kwenye kikundi kidogo. Ikuze huduma ya kanisa kwa kuelezea mafanikio yake.

Kwenye kikao cha kwanza, hakikisha kwamba kila mtu anaelewa umuhimu wa kikundi. Shirikisha kwa Maandiko na taarifa ambazo zinaonyesha umuhimu wa uanafunzi.

Ili kusaidia mahudhurio, kikundi kinaweza kuratibiwa kukutana kwa wiki kadhaa. Eleza kwamba kikundi kitakuwa na mfululizo maalum wa masomo na uwaambie ni lini mfululizo huu utakamilika. Kwa njia hiyo, kila mshiriki atakuwa anajua kabisa kwamba anatakiwa kufanya nini. Sisitiza hitaji la kuhudhuria kikamilifu. Mwishoni mwa kipindi hicho, kikundi kinaweza kuanza tena na wale ambao wako tayari kuendelea na mafunzo.

### Tukio la Kuzingatiwa

Petro amekuwa Mkristo kwa miaka kadhaa. Yeye ni mshiriki wa kanisa anayesaidia katika kanisa lake. Ana wasiwasi kwamba kanisa lake halina mpango wowote kwa ajili ya uanafunzi. Anadhani kanisa linapaswa kuanzisha vikundi vidogo, lakini viongozi wake hawapendezwi na jambo hilo.

► Je, Petro afanye nini?

Petro anapaswa kuzungumza na viongozi wa kanisa na kuomba kibali cha kuanzisha na kuongoza kikundi kidogo. Hapaswi kukosoa huduma ya kanisa, badala yake aeleze faida zitakazoweza kupatikana kutokana na uwepo wa kikundi hicho. Ikiwa kikundi kitafanya vizuri, kanisa litaanza kuelewa faida za aina hiyo ya huduma.

### Kuongoza Kikundi chenye Ufanisi

Mwanzoni mwa kuanza kikundi, kunakuwepo na msisimko na matarajio. Wanachama wengi hawajui hasa cha kutarajiwa, lakini wanatarajia kupata msaada kutoka kwenye kikundi.

Maelekezo yafuatayo yatasaidia kikundi kuwa na ufanisi na kutimiza kusudi lake. Kuna kanuni za muhimu kwa ajili ya utendaji wa vikundi vidogo. Kama kiongozi atakisaidia kikundi katika kufuata kanuni hizi, atapunguza hali kuvunjika moyo au kukata tamaa.

Kikao cha kwanza kinaweza kikawa tofauti na vikao vingine kwa sababu kikundi kitakuwa kinajifunza jinsi ambavyo vikao vinapaswa vifanyike.

Hata hivyo, kikao cha kwanza kitaweka mfumo utakaotumika kwa ajili ya vikao vingine vitakavyofuata baadaye. Kama mtu hataweza kuzungumza kwenye kikao cha kwanza, atategemea kutoweza kuzungumza hata kwenye vikao vya baadaye. Kama mtu atatawala majadiliano, kikundi kitategemea vikao vinavyofuata baadaye mtu huyo huyo mmoja atatawala mijadala. Kama kikao kimekuwa hakina mpangilio unaofaa, wanachama

watategemea kuwa na hali kama hiyo katika vikao vinavyofuata baadaye. Kama kikao ni kama darasa lililo na ushiriki mdogo, watategemea hali hiyo ya kufanana iendelee.

Baadhi ya wanachama wanaweza wakajiondoa baada ya vikao vichache kufanyika kwa sababu yaliyoko kwenye kikundi hicho si kama walivyotarajia. Ni muhimu kuongoza kikao kwa usahihi ili kwamba wanachama waliotegemea kupata mambo mazuri kutoka katika kikundi hicho wasikatishwe tamaa.

## Mwongozo kwa ajili ya Ufanisi

**(1) Ratibu kikundi angalao kiweze kukutana kila wiki, kama uwezekano huo utakuwepo. Baadhi ya wanachama wanaweza wakahitaji msaada wa kupanga huduma kwa ajili ya uangalizi wa watoto.**

**(2) Mfumo wa kukutana unapaswa uwe: (1) muda wa kujifunza, (2) kushirikishana mahitaji binafsi kwa ajili ya maombezi, (3) kufanya maombi.**

Ikiwa kusudi la msingi la kikundi ni kujifunza, muda wa kujifunza unaweza ukawa mrefu na sehemu nyingine zikawa fupi; lakini sehemu tatu hizi ni lazima ziwepo. Ikiwa kusudi la kikundi ni kwa ajili ya mambo ya kuwajibika kiroho, muda wa mafunzo unaweza kuwa mfupi, lakini wanapaswa kuwa na masomo fulani wanayojifunza.

Ikiwa kikundi kina mambo binafsi ya kushirikishana na kujadili lakini hawana masomo ya kujifunza, inawezekana kukatokea uvurugaji. Kikundi kinaweza kutawaliwa na baadhi ya wanachama wenye sifa kubwa.

Vifaa vya masomo huwafanya watu wote kwa pamoja wakubaliane na ukweli mbali na kile ambacho kiko ndani ya fahamu zao.

**(3) Anza kipindi na maliza kwenye muda wake kamili.**

Kama utaanza na kumaliza kwa kuchelewa, wale watu wanaothamini muda wao binafsi wataanza kuwa wachelewaji au kukwepa baadhi ya vikao.

**(4) Panga tarehe ambazo kikundi kitafikia ukomo wake.**

Wanachama wanapaswa kujua ni kitu gani watakuwa wanafanya na kwa muda gani. Kwa kawaida, wanachama wapya wasiruhusiwe kujiunga na kikundi baada ya mikutano kadhaa, isipokuwa kama kikundi kina masomo ya kurudia kwa ajili ya waogofu wapya. Kama kikundi kinajifunza masomo ya mfululizo, idadi ya masomo inaweza kutumika kupanga muda wa majuma ambayo watahitajika kukutana. Ikiwa watakuwa wanakutana kwa ajili ya uwajibikaji wa mambo ya kiroho, wanaweza wakajipangia muda wa miezi sita. Hapo mwishoni wanaweza kujipanga tena. Katika kipindi hicho baadhi ya washiriki wanaweza kuondoka na kikundi kinaweza kufikiri iwapo kitaruhusu au kutoruhusu washiriki wapya kutojiunga.

**(5) Wakati wa mafunzo, weka msisitizo kwenye kusudi la mabadiliko ya maisha kuliko kutoa tu ufahamu wa suala hilo lenyewe.**

Mwanachama ataona kwamba kikundi kinafaa ikiwa ataweza kuwa na uwezo wa kupata mambo binafsi na maalumu ya kutumia kwa vitendo kutokana na mafunzo hayo.

**(6) Ufuatiliaji wa uwajibikaji.**

Ikiwa mtu atakuwa ameshirikisha tatizo lake, kisha ikakubalika kwamba atapaswa kuchukua hatua fulani ya utekelezaji, pata mrejesho wake kwenye kikao kinachofuata cha kikundi kama atakuwa ametekeleza kile alichokuwa amesema kwamba atakifanya.

**(7) Kiongozi anapaswa awe mtu anayepatikana kwa ajili ya kukutana na mwanachama binafsi ili kutoa mwongozo wa kiroho.**

Wanachama wengine pia wanaweza wakakutana pamoja kwa nyakati zingine kwa ajili ya kutiana moyo.

**(8) Chagua mahali pazuri pa kukutanikia.**

Mahali pa kukutania patapaswa pawe mahali penye mandhari ya nyumbani. Kukaa kuwe katika hali ya mviringo kwa kadri inavyowezekana, ili kila mwanachama awe na uwezo wa kuuona uso wa mwenzake. Hii itatia moyo na shauku ya ushiriki. Kukutanika pawe ni mahali ambapo hapatakuwa na mambo ya kuvuruga au kuleta usumbufu.

**(9) Jizoeze kuwa na tabia nzuri ya usikilizaji.**

Ishara ya usikivu mzuri ni kuwasiliana kwa macho, kuwa na uso unaoonyesha umakini, kupuuzia mambo yanayoweza kuvuruga, na mwitikio kwa ucheshi wa mzungumzaji au mihemuko mingine.

**(10) Hakikisha hakuna mwanachama ambaye kila wakati ni mkimya.**

Elekeza swali la moja kwa moja kwa mwanachama ambaye siyo mzungumzaji sana ("Yohana, unafikiri nini kuhusu jambo hili?")

**(11) Usimshinikize mwanachama kushirikisha jambo lake la kibinafsi.**

Badala yake, jitahidi kutengeneza mazingira ambayo atajisikia kuwa na uhuru wa kuongea. Jenga ujasiri wa mwanachama binafsi kwa kuwasiliana naye kwa macho na kumpongeza kwa kitu anachokisema.

**(12) Jitahidi kuuliza maswali ambayo wanaweza wakayatolea majibu ili kujenga ujasiri na kujiamini kwao.**

Ikiwa mtu atatoa jibu lisilo sahihi, jaribu kusema jambo zuri kuhusu jibu lake kabla ya kulisahihisha.

**(13) Jaribu kuthibitisha au kuunga mkono kila maoni kwa namna fulani kabla ya kuanza kuyasahihisha.**

**(14) Ikiwa kutakuwepo na mtu mwenye tabia ya kuongea sana na kutaka kujibu maswali yote, tafuta namna ya kumdhibiti.**

Njia mojawapo ni kuelekeza maswali kwa wanachama wengine. Au unaweza kuuliza kwamba, "Je, ninyi wengine mnafikiria nini?" Kwenye majadiliano, unaweza ukasema, "Hebu tena tusikie kutoka kwa mtu mwingine ambaye bado hajaongelea kuhusu suala hili."

Ikiwa mwanachama bado atakuwa anazungumza sana, kiongozi anaweza kuzungumza naye nje ya darasa. Anaweza kusema jambo kama hili, "Samsoni, wewe ni mtu unayefikiria kwa haraka na una uwezo wa kujibu haraka, lakini ninajisikia kwamba baadhi ya wengine hawatapata fursa ya kushiriki kama tutakuwa tunajibu kila kitu kwa haraka. Je, unaweza kunisaidia katika kutoa nafasi kwa kila mtu ashiriki majadiliano?"

**(15) Usiruhusu kuwepo na watu wawili au watatu wawe na majadiliano ya minong'ono yao wenyewe huku wakipuuzia kikundi.**

Ikiwa mtu atataka kuendelea kubishana kwa muda mrefu kuhusu jambo fulani, mwambie kwamba majadiliano hayo yatapaswa yakamalizike baadaye nje ya kikao.

**(16) Usiruhusu mtu yeyote kuingilia kati ya watu wengine.**

Nyoosha mkono wako, na kwa ujasiri msimamishe huyo anayeingilia, na kisha ruhusu msemaji wa kwanza aendelee kuongea hadi amalize. Vinginevyo, majadiliano yatatawaliwa na wanachama wasio na adabu. Watu ambao hawana uthubutu watahisi kuvurugwa kiasi kwamba hawawezi tena kuendelea kumalizia sentensi zao.

**(17) Sikiliza Malalamiko**

Kila lalamiko linaweza kuonyesha tatizo ambalo linaweza likarekebishwa. Kama mtu atakuwa hajaridhika na kukutana kwa kikundi, anaweza akawa haelewi kusudi au anaweza akawa ana lalamiko lenye msingi.

**(18) Ikiwa mtu ataendelea tu kuwa na uhasama, uharibifu, mshindani, au aliyejikinai, hawezi akakubaliana na malengo ya kikundi.**

Kikundi kinaweza kikawa siyo kile alichokuwa anakitegemea. Zungumza naye pembeni kabisa ili kuweza kumsaidia aone kusudi la kikundi.

**(19) Kiongozi hapaswi kuwa anajua jibu la kila tatizo.**

Jukumu la kiongozi siyo kuwa na jibu kwa kila kitu bali kuongoza kikundi katika kubeba mizigo katika maombi.

**(20) Kuwa mwepesi na mvumilivu kutokana na mwingiliano wa ratiba.**

Kumbuka kwamba matukio yaliyopo kwenye maisha yetu ni sehemu ya Mungu kutuendeleza. Tatizo ni fursa.

**(21) Ikiwa mwanachama wa kikundi atakitumia kikao chote kwa ajili ushirikishaji wa mahitaji yake binafsi, jitolee kumsaidia kwa ushauri kwa wakati mwingine.**

Vinginevyo, wanachama wengine watajihisi kwamba kikao kinapokonywa kutoka kwao. Usikubali kikundi kipoteze kusudi lake, labda tu wanachama wenyewe wakubaliane kwamba kusudi lililopo linapaswa kubadilishwa.

**(22) Usiruhusu majadiliano yawe ya kichochezi.**

Usiruhusu kikundi kiwe ni jukwaa la kukosoa kanisa la mtaa na viongozi wengine.

**(23) Kumbuka kwamba ufanisi mkubwa wa kikundi unategemea sana nguvu za Mungu zitende kazi ndani yake.**

Kikundi ni muundo tu wa kimaandiko ambao Mungu hupenda kukitumia.

# 3. Kukidhi Mahitaji ya Wanafunzi Wapya

## Uwajibikaji wa Haraka kwa Mtu Mpya Aliyeokoka

Uanafunzi huanzia kwenye mazungumzo. Mtu mpya aliyeokoka anakuwa na mahitaji mengi ya dharura. Ili Kuuendeleza uhusiano wake na Mungu ambao ndiyo tu anakuwa ameuanzisha, anahitajika kujua jinsi ya kuomba na kusoma Biblia. Pia anahitaji jumuiya ya marafiki wa Kikristo kwa sababu atakuwa anapoteza marafiki wake wengi wa zamani kabla ya kuokoka. Anahitaji mwongozo kuhusiana na masuala ya mfumo wake wa maisha.

Kanisa ni lazima lianze mara moja kufanya uanafunzi kwa mtu mpya aliyeokoka. *Mara moja* haina maana ya kuanza jumapili ijayo. Inamaanisha kuanzia wakati ule alipoinua kichwa chake kutoka kwenye kuomba na akaokoka. Mtu mmoja ni lazima achukue jukumu la kuwasiliana naye kila siku kwa takribani wiki ya kwanza yote. Anapaswa akutane na Wakristo wengine kadhaa kwenye kanisa la mtaa. Anapaswa awe na nafasi za kujadili mabadiliko yanayotokea kwake na kuuliza maswali.

Mtu aliyeokoka anapaswa akaribishwe kujiunga na kikundi kidogo ili aweze kupata fursa ya kuuliza maswali na kutiwa moyo. Ikiwezekana, atapaswa atambulishwe kwa watu wengine kadhaa kwenye kikundi kabla ya siku ya kwanza ya kuhudhuria kwake kwenye kikao cha kikundi hicho. Baadhi ya wanachama wanaweza wakampa mawasiliano yao ya simu kwa ajili ya kuleta kuzoeleana na kumkaribisha kwenye kikundi. Hali hii huanza kumjengea hisia nzuri ya kuwa kwenye jumuiya ya waaminio.

Mtu mpya aliyeokoka anapaswa kujiunga na kikundi wakati watakapokuwa wanakutana kwenye kikao kinachofuata. Masomo yatabidi yawe ya kufanyika kwa kurudiarudia ili mwanachama mpya aweze kuongezwa wakati wowote. Kwa njia hii mtu mpya aliyeokoka hupata msaada wa kikundi mara moja. Wanachama watakuwa wanahitimu mafunzo yao kibinafsi kwa kadri wanapokuwa wamemaliza kujifunza masomo yote.

## Kuomba Maombi ya Paulo kwa Waamini.

Maombi ya Paulo kwa ajili ya waamini wapya yanaelezea ni mahitaji gani yanayohitajika kwa Mkristo mpya. Maombi haya yanatuongoza sisi kuomba kwa ajili ya Wakristo wachanga kwa sababu tutapaswa tuombee mambo yale yale kwa ajili yao ambayo Paulo aliomba. Maombi haya pia yanaongoza huduma zetu kwa sababu tunapaswa tushirikiane na Mungu katika yale anayoyafanya kwa ajili yake.

Tuangalie maombi ya Paulo kwa vikundi vitatu tofauti:

### Wathesalonike

► Soma 1 Wathesalonike 5:23-24.

Barua ya kwanza kwa Wathesalonike ina wito wa utakatifu. Kila mwamini anaitwa kuishi kwa ushindi na kwa usafi, na Mungu anaahidi kwamba yote yanawezekana kwa imani. Tunapaswa tuombe na kufundisha kwa lengo la kumleta kila mwamini kwenye ushindi na usafi

**Wafilipi**

► Soma Wafilipi 1:9-11.

Aya hizi zinaelezea kuhusu mchakato endelevu ndani ya maisha ya mwamini. Upendo wake unatakiwa uongezeke bila kikomo. Wakati hili likiwa linatendeka, uwezo wake wa kutambua ni mambo gani yaliyo bora zaidi unapaswa uongezeke. Anapokuwa anatambua, anarekebisha maisha yake yawe kwenye mwelekeo wa mambo bora zaidi. Haya ni lazima yawe yanafanyika kwa ajili yake kuwa moyo safi na asiyekuwa na hatia.

Watu ambao Paulo aliwaandikia aya hizi tayari walishakuwa Wakristo kwa kitambo fulani. Lakini bado, Paulo alikuwa akiomba kwamba wazidi kuongezeka katika upendo wao kwa Mungu, na kwa upendo huo, wawe na uwezo wa kuyaelewa mapenzi ya Mungu yaliyo kwa ajili yao vizuri zaidi.

Hapa kuna maswali kadhaa ambayo mwamini mchanga anapaswa kuyatilia maanani:

- Je, ni mfano gani wa mabadiliko ambayo nimefanya katika maisha yangu wakati Mungu aliponionyesha tabia, mazoea, na matendo yangu havikuwa katika ubora wake?
- Je, kuna jambo lolote katika maisha yangu ambalo nina mashaka nalo?
- Je, niko tayari kumruhusu Mungu anionyeshe kwenye maombi mabadiliko yeyote ninayopaswa kuyafanya?

**Wakolosai**

► Soma Wakolosai 1:9-12.

Paulo aliomba kwamba watu wapokee maarifa katika mapenzi ya Mungu, katika hekima yote na ufahamu wa rohoni. Mtu mpya aliyeokoka bado haelewi mambo yote yanayohusiana na mapenzi ya Mungu kwa ajili ya mfumo wa maisha yake. Hatua kwa hatua atakuwa anaona kwamba baadhi ya mambo aliyokuwa na mazoea nayo, maneno, na tabia katika maisha yake inabidi vibadilike. Kwa kuwa anampenda Mungu, atazidi kupatanisha maisha yake na mapenzi ya Mungu. Mtu anayeshughulika na uanafunzi anapaswa aombe na kumfundisha Mkristo mchanga kwa makini na uangalifu katika kuweza kutambua mapenzi ya Mungu.

Paulo alisema kwamba kama matokeo ya kuelewa vizuri zaidi mapenzi ya Mungu, "mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana." Watakuwa wawakilishi wa Mungu wanaostahili. Maisha yao yataendana na ushuhuda wao wa kubadilishwa kwa neema. Kile ambacho mtu anayeshughulika na uanafunzi ni lazima akumbuke ni kwamba hadi mchakato

huu utakapokuwa umeendelea kwa kitambo fulani, baadhi ya mambo yasiyolingana yatajionyesha kwenye maisha ya Mkristo mchanga.

Sehemu ya "mwenendo unaofaa" inajumuisha "kuzaa matunda kwa kila kazi njema." Hatupaswi kushangaa wakati tunapomwona Mkristo mchanga bado hajazaa matunda katika kila kazi iliyo njema. Anaweza kuwa bado hajawajibika na kufahamu wajibu aliyoitiwa kufanya.

Aya hizi pia zinatueleza kwamba tunaweza "kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha." Mtu ambaye anaweza kuwa na furaha ya Ukristo anapokuwa anatumika na kustahimili huwa anaongezeka kwenye ukuaji wa kiroho.

**Mambo ya Kuhitimisha kuhusu Maombi ya Paulo**

Maombi ya Paulo kwa ajili ya Wakristo wachanga yanatueleza kwa kiasi kikubwa kuhusu kazi ya uanafunzi. Tunapaswa tuwe na malengo yaliyo sahihi kwa ajili ya maendeleo ya waamini. Tunapaswa tuwe na uwezo wa kutambua mchakato endelevu. Hatupaswi tuwe watu wa kushangaa tunapoona mambo yasiyofuata utaratibu, kutoelewana na kutowajibika ndani ya Mkristo mchanga. Hatupaswi tutegemee kuona kwamba sifa zote za Ukristo zitajitokeza kwa mara moja.

Tunapaswa tutambue kwamba Paulo hakuwa anahusika kuhusu mafunzo ya huduma zao au maendeleo ya vipaji vya huduma. Alikuwa anahusika sana na maendeleo ya imani yao na tabia ya Kikristo. Hatupaswi kuridhika na watu ambao wanaweza kufanya kazi za huduma lakini wanakosa kuwa na tabia ya Kikristo.

Mwalimu ni mtu muhimu sana kwa sababu ya mfano wake wa kuigwa na kwa sababu ya thamani ya taarifa zake. Kujifunza kunasisitizwa kwenye sehemu mbili za maombi ya hapo juu. Ufahamu unahusika kwenye hatua endelevu ya kiroho. Mwalimu ana matokeo makubwa sana kupitia matumizi yake ya ukweli.

Tunapaswa tuombe maombi ya Paulo kwa ajili ya Wakristo wachanga ambayo yataleta ushawishi. Tunapaswa tuwe na ushirika na Roho Mtakatifu katika kusaidia hatua zote hizi endelevu zitokee katika maisha yao.

Maombi yafuatayo yako kwenye msingi wa maombi ya Paulo kwa ajili ya Wakristo wapya.

**Maombi kwa ajili ya Mkristo Mchanga:**

Baba wa Mbinguni,

Ninaomba kwa ajili ya ___________ kwamba umtakase kabisa. Ninaomba kwamba aweze kuwa mtakatifu katika matendo yake, tabia zake, na nia zake.

Msaidie upendo wake alio nao kwa ajili yako uweze kuendelea kukua, ili aweze kuelewa vizuri zaidi na zaidi ni nini yaliyo mapenzi yako kwake. Msaidie katika kutambua ni jambo gani lililo zuri zaidi kwake na siku zote aweze kulichagua hilo, ili kwamba maisha yake yaweza kuzaa matunda kwa ajili ya utukufu wako

Msaidie aweze kuishi kila siku kama Mkristo anavyopaswa kuishi, akikupendeza wewe katika kila jambo na kujifunza zaidi kuhusiana na njia zako. Msaidie katika kupata nguvu zitokazo kwako, ili kwamba aweze kuishi kwenye maisha ya ushindi na kustahimili majaribu kwa furaha. Siku zote awe mtu wa shukrani kwa ajili ya neema yako unayotoa.

Amina.

# 4. Utangulizi wa Mfululizo wa Masomo

## Utangulizi Kuhusu Mfululizo wa Masomo

Masomo yameandaliwa kwa ajili ya kutumika kwenye kikundi cha watu wapya waliookoka au waamini ambao wana shauku ya kukua kiroho. Masomo haya ni rahisi kuyafundisha, yakiwa na maswali yaliyowekwa kwa ajili ya kufanya majadiliano. Kutakuwepo na majadiliano mengi wakati wa somo, kisha kushirikishana kibinafsi pale mwishoni.

Kwenye maandalizi ya kila mnapokutana, kiongozi anapaswa asome somo lote, akahakikisha kwamba anayaelewa maudhui yaliyopo na umuhimu wake. Anapaswa awe na maandalizi ya kuanzisha muda wa kushirikishana kutokana na uzoefu wake mwenyewe. Anapaswa atafakari ni kwa jinsi gani atajibu maswali ya kushirikishana kwenye mwisho wa kila somo. Kwa kiwango kile ambacho anakifanya katika kushirikishana kitaweza kuweka uzito kwa kile ambacho wengine watakuwa wanashirikisha.

## Muundo wa Somo

Kitabu cha Mwongozo wa Kiongozi kinaonyesha masomo yote, ikiwa ni pamoja na nyenzo za kufundishia, dondoo za majadiliano, na aya za Maandiko. Kitabu cha Mwongozo kwa Mwanafunzi kimehusisha tu dondoo nyingi muhimu kutoka katika kila somo.

Maelezo kwa viongozi wa darasa yamejumuishwa katika kozi yote kwa maelekezo ya sehemu mahususi za masomo. *Yameandikwa kwa maandishi ya ulalo.*

Katika nyenzo za kiongozi, alama ► inaonyesha swali la kujadili au Andiko la kusoma. Kuhusu maswali ya kujadiliana, kiongozi asubiri mrejesho baada ya kuuliza maswali, badala ya kutoa majibu ya moja kwa moja. Mara nyingi mrejesho husaidia kuandaa kwa yale yanayofuata.

Kila mshiriki atapaswa kutumia Biblia yake wakati wa masomo. Aya nyingi za Maandiko kwa ajili ya masomo zimechapishwa kwenye kitabu cha nyenzo za mwalimu, lakini siyo kwenye kurasa za kitabu cha mwongozo kwa wanafunzi. Kiongozi atapaswa amwambie mwanafunzi mmoja kuitafuta aya hiyo na kuisoma kwa sauti. Mara kwa mara, anaweza kuokoa muda kwa kusoma yeye mwenyewe kutoka katika muhtasari wake, hasa wakati ambapo aya nyingi zinatumika, lakini hatapaswa kuzifanya mara nyingi yeye mwenyewe. Kuwafanya wanafunzi wazitafute aya kunawapa njia nyingine ya kushiriki, kunawapa mazoezi na kuwa na uzoefu na Biblia zao, na kuwafanya waweze kuzoea kuziona aya kwenye maudhui yake. Kunakuwepo na uimarishaji endelevu wa ufahamu kwamba Biblia ndiyo mamlaka yetu ya mwisho.

Sehemu iliyoandikwa "kwa ajili ya kushirikishana kikundi" inatoa maswali ya kuanzisha majadiliano mwishoni mwa somo. Kwa mada nyingi, majadiliano yanaweza yakaanza kirahisi, na maswali yanaweza yasihitajike. Siyo lazima maswali yote yatumike.

Maombi yaliyoko kwenye kila mwisho wa somo yatasaidia wanachama kuomba kwa ajili ya kukamilisha ukweli katika maisha yao. Mtu fulani atapaswa kuyasoma maombi pale mwishoni, na washiriki watapaswa watiwe moyo kuyarudia tena katika hilo wiki na kuyafanya maombi hayo yawe kwa ukweli yanatoka ndani ya mioyo yao.

Kila somo linamalizia na kazi za kufanya, Kikundi kinaweza mara kwa mara kikatenga muda wa kujadili matokeo ya utafiti au mafunzo yao wenyewe.

Masomo mengi yaliyopo yanatoa wito kwa wanachama au washiriki kufanya ahadi maalumu za kutumia kwa vitendo ukweli waliojifunza. Kiongozi anapaswa achukue ukumbusho wa ahadi zote uliofanywa na baadaye awatake wanachama waelezee kama wamefuatilia utekelezaji wa ahadi zao.

# MASOMO YA KUKUZA UANAFUNZI

## KITABU CHA MWONGOZO WA KIONGOZI

# Somo la 1
# Maisha yenye kustahili Kuishi

## Wazo Kuu

"Ninapata umuhimu binafsi kwenye uhusiano na Muumbaji wangu tu."

## Lengo la Somo

Kuona jinsi dhambi inavyoharibu ujumla wa maisha na kusudi lake, na jinsi ambavyo kuokoka kunaanzisha hatua ya marejesho.

## Utangulizi

► Je, ni kitu gani kinachoweza kufanya maisha ya mtu yakawa yenye thamani?

Inavyoonekana ni kwamba watu wengi kamwe hawatilii maanani kusudi la maisha ni nini. Wanaendelea na taratibu zao za kawaida za kazi na starehe, na kuishi kana kwamba maisha kamwe hayatakaa yafike mwisho.

Watu wengi wanahusika na makusudi, au umuhimu wa maisha yao. Baadhi huishi wakiwa na ufahamu wa kutokuwa na matumaini tena. Wana wasiwasi kama wanayo malengo yaliyo sahihi, na wanajihisi kutoridhika hata kama watayafikia malengo hayo. Wanajihisi kwamba kwa namna fulani kuna jambo kubwa wanalolikosa katika maisha.

Watu wengine wanakataa kwamba kuna kusudi katika maisha.

Tunafahamu kwamba tunayo kusudi kwa sababu tunajitambua kwamba sisi tumeumbwa. Kama Mungu ametuumba, ni lazima alikuwa na lengo kwa ajili yetu. Hilo lengo ndiyo njia ya ukamilifu na inayoridhisha. Kuyatumia maisha yetu kwa ajili ya mambo mengine ni kuyaletea uharibifu tu.

Mimi sitaki maisha yangu yapotee bure. Na sitegemei kama hata wewe unataka hivyo.

► Je, Mungu analo kusudi gani na sisi?

## Mpango wa Mungu kwa ajili ya Maisha Yaliyokamilishwa

Tunaweza tukapata jibu kutoka kwenye Bustani ya Edeni, mahali ambapo Mungu alipaandaa kwa ajili ya watu wa kwanza aliowaumba. Kabla ya dhambi kuleta mabadiliko yeyote, kila kitu kilikuwa katika mpangilio ambao Mungu aliweka.

> Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, "Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale … (Mwanzo 1:27-28).

> Bwana Mungu akasema, “Si vema huyo mtu awe peke yake; nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye” (Mwanzo 2:18).

Aya hizi zinatuonyesha sisi kitu ambacho Mungu alikipanga kwa ajili ya maisha ya binadamu. Mtu kwanza aliumbwa katika sura ya Mungu, na alikuwa kwenye mahusiano na Mungu. Ndoa ya kwanza ilikuwa ndiyo mwanzo wa familia na mahusiano ya zaidi miongoni mwa wanadamu. Alikuwa na jukumu la kutunza bustani, alikuwa na utawala juu uumbaji wote aliokuwa ameufanya, kwa hiyo pia alikuwa kwenye mahusiano na ulimwengu wote ambao Mungu alikuwa ameufanya.

Kwa hiyo tunayaona mahusiano makuu ya aina tatu:

- Uhusiano baina ya watu na Mungu.
- Uhusiano baina ya watu wenyewe.
- Uhusiano baina ya watu na dunia ya Mungu.

Uhusiano na Mungu ndio unaoweka haya mengine yaweze kwenda sawasawa kama inavyohitajika.

Jaribu kufikiri dunia ingekuwaje au ingefananaje leo kama kungekuwa na upatanifu (wa maono, na mtazamo) kwenye haya mahusiano matatu makubwa.

► Je, ni kwa jinsi gani mambo yangeonekana kuwa tofauti leo kati ya watu na asili ya uumbaji? (Watu wangeitumia ardhi kwa umakini zaidi. Hakuna kitu katika uumbaji ambacho kingepatwa na madhara.)

► Je, ni kwa jinsi gani mambo yangeonekana kuwa tofauti leo kati ya watu wenyewe? (Kungekuwa hakuna uhalifu, hakuna vita, au hakuna ugandamizaji.)

► Je, ni kwa jinsi gani mambo yangeonekana kuwa tofauti leo kati ya watu na Mungu? (Hakungekuwepo na dhambi, hakungekuwepo na watu kuonekana na hatia, na kungekuwepo na watu wanaoongozwa na Mungu.)

Sitaki maisha yangu yapotee bure, kwa hiyo ninahitaji kutimiza kusudi ambalo niliumbiwa nalo. Sababu ya wewe kuwepo ni kuwa katika mahusiano mazuri na Mungu pamoja na watu wake na ulimwengu wake. Nisipofuata kusudi hilo naweza pia nisingekuwepo.

Ni rahisi kuweza kuona kwamba ulimwengu wa leo siyo ule ambao Mungu alikuwa amepanga uwepo. Kwa hiyo ni nini kilichotokea?

### Kumbukumbu ya Kibiblia kuhusu Anguko la Mwanadamu

Maelezo kuhusiana na hali ya dunia ya sasa yanapatikana katika Mwanzo 3. Tilia maanani vipengele vifuatavyo vinavyohusiana na kumbukumbu hii. (Kwa kifupi toa maelezo ya anguko la mwanadamu kwenye dhambi.)

1. **Matazamio**: Mpango wa Mungu wa mwanzo uliingiliwa na dhambi ya mwanadamu.

2. **Jaribu**: Shetani alimshawishi Adamu na Hawa kwa matarajio ya kuwa huru kutokana na Mungu, na kuwa na uwezo wa kutawala maisha yao wao wenyewe, wakati aliposema, "Nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya" (Mwanzo 3:5)
3. **Kuwa na Mashaka**: Maswali ya Shetani yalikusudiwa kuwafanya watu watilie shaka hekima na unyoofu wa Mungu. Mtu anayetenda dhambi ana mashaka na Mungu – kwamba anajua na anakusudia yaliyo mazuri zaidi. Kabla ya tendo lao la dhambi, kwanza walikubaliana na ushawishi wa kutomwamini Mungu – kukosa kuwa na imani.
4. **Uasi**: Kwa kitendo cha Adamu na Hawa, walimkataa Mungu kama mamlaka na kiongozi wa maisha yao.
5. **Utengano**: Dhambi iliharibu kabisa mshikamano uliokuwepo wa mahusiano yote makubwa matatu. Walijaribu kujificha mbele za Mungu. Tabia zao wenyewe dhidi yao zilibadilika, na baadaye kukatokea kuwepo na mauaji ndani ya familia yao. Walipambana na mazingira ya asili ili kupata mahitaji yao. Hali yote ya baadaye ya ubinadamu ikawa ni kuzaliwa katika asili yenye mwelekeo wa dhambi, kufanya matendo ya uovu, na kuishi kwenye mahusiano yaliyoharibika katika maeneo yote matatu makubwa ya mahusiano.

## Kutafuta Njia ya Kurejea

Mungu hakuwaacha kabisa watu wa mwanzo kwenye hali yao mbaya waliyoisababisha wenyewe kwa sababu ya kutenda dhambi. Alirejea na kuwaita kwa kuuliza swali, "Uko wapi?" Hakuuliza swali hilo akimaanisha kwamba hakuwa na uwezo wa kuwapata. Aliuliza swali hilo kwa sababu alitaka wajitambue na wakiri kile ambacho kilikuwa kimetendeka kwenye mahusiano yao na yeye.

Mungu bado anatafuta kuwarejesha kwake watu wote waliopotea. Anatamani matengenezo – kurejesha upya uhusiano uliokuwa umekusudiwa.

Hata sasa Mungu anakuuliza swali linalofanana, "Uko wapi?"

Kama uko nje ya uhusiano na Mungu, hiyo ndiyo sababu ya wewe kujiona uliyepotea na usiyekuwa na kusudi lenye maana. Utengano vilevile husababisha kuwa na mashaka kwa ajili ya hatima ya baadaye, kifo na hukumu.

Biblia ni kitabu kikubwa kinachohusisha mitume, manabii, wafalme, sheria, na historia, lakini imebeba wazo moja tangu mwanzo hadi mwisho. Ujumbe wa Biblia nzima ni kwamba Mungu anataka kuwarejesha tena watenda dhambi kwenye uhusiano wa yeye mwenyewe na watu wake.

Jambo muhimu kuliko yote kuhusiana na wewe ni uhusiano wako na Mungu.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Jaribu kumwuliza mtu mmoja kukushirikisha ni kwa jinsi gani kuwa kwenye uhusiano na Mungu kunaleta maana katika maisha yake.*

*Kwa ajili ya majibu ya hiari:*

► Ni kwa jinsi gani utajibu hili swali, "Uko wapi?" katika uhusiano na Mungu? Je, uko kwenye uhusiano na Mungu, au bado yeye ni mgeni kwako?

► Kwa ajili ya majibu ya hiari: "Je, kuna uwezekano kwamba wakati mmoja ulimjua Mungu lakini wakati huu umevunja uhusiano wako na Yeye?"

*Uliza kuhusu mtazamo ulioko kwenye taarifa kwamba, "Jambo muhimu kuliko yote kuhusiana na wewe ni uhusiano wako na Mungu."*

► Je, kuna uwezekano wa kulisahau jambo hilo? Je, tunaishi katika njia ambayo inakubaliana au inapatana na ukweli huo?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninakushukuru wewe kwa kuniumba mimi, na kunifanya mimi kwa kusudi la kukufahamu wewe.

Asante kwa kunirejesha tena kutoka katika dhambi yangu na kunileta kwenye uhusiano uliofanywa upya na wewe. Asante kwa ajili ya msamaha wako.

Kwa kuwa nataka kuishi kwa furaha ya kukujua wewe, nitaishi kwa upendo wa utiifu kwa ajili yako. Ufanye utii wangu kwako uwezekane kwa Roho wako Mtakatifu ndani yangu

Ninaomba haya katika jina la Yesu, aliyekufa kwa ajili yangu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Mwanzo 1-3. Angalia kumbukumbu za rejea zilizopo za uhusiano. Kwenye sura ya 3, angalia vipengele vilivyoelezwa katika somo hili kwenye sehemu ya "Kumbukumbu ya Kibiblia kuhusu Anguko la Mwanadamu." Andika aya chache kuhusiana na yale ambayo utayaona katika sehemu hiyo.

# Somo la 2
# Kukutana na wokovu

## Wazo Kuu

"Kukutana na Mungu kunako sababisha wokovu huanza uhusiano wangu pamoja naye."

## Malengo ya Somo

Kuelewa ni kwanini toba na msamaha ni muhimu kwa ajili ya mwenye dhambi kuanza uhusiano pamoja na Mungu Mtakatifu.

## Utangulizi

► Je, Chanzo cha kwanza kabisa cha uhusiano wa aina yeyote ni nini?

Kabla watu hawajaweza kuwa kwenye mahusiano, ni lazima kwanza wakutane. Mwanzo wa kwanza kabisa wa uhusiano wowote ni kukutana binafsi.

Je, uhusiano wa kwanza kati ya Mungu na mwenye dhambi ukoje? Hauwezi ukawa kama wageni wawili wanaokutana, wanasalimiana, na polepole wanaanza kuzoeana. Itakuwa kama mwanzo wako wa kwanza kabisa kukutana na mtu mwingine ambaye tayari ulishawahi kumkosea sana.

Jaribu kumfikiria mtu aitwaye Yusufu ambaye amepangisha nyumba. Anapokuwa anaishi pale, anaifanyia pikipiki yake marekebisho sebuleni na kuharibu zulia la sakafu. Anachukua mishale na kuanza kulenga shabaha kwenye ukuta. Anamweka farasi ndani ya nyumba, na anasababisha mashimo kwenye kuta za nyumba anapokuwa hana furaha au kusikia njaa. Kamwe, hata wakati mmoja Yusufu hajawahi kukutana binafsi na mwenye nyumba wake.

Kisha, siku moja akiwa amekaa kwenye chumba cha tabibu wa meno sehemu ya kungojea, Yusufu anaanza mazungumzo na mgeni mmoja ambaye walikuwa hawajuani na akampenda, lakini akaja kutambua kwamba alikuwa ndiye mwenye nyumba aliyokuwa amepangisha.

► Je, ni nini kinachoenda kufanyika kabla hawajawa marafiki?

Je ni kitu gani muhimu kwa ajili ya upatanisho wakati mtu anapokuwa amemkosea mtu mwingine?

1. Mwenye kutenda makosa ni lazima akubali kwamba ametenda makosa na atubu. Kutubu maana yake ni kwamba hatakuwa anaendelea kufanya mambo mabaya dhidi ya mtu mwingine.

2. Mwenye kutendewa makosa ni lazima awe tayari kusamehe, hata kama inamaanisha kwamba mwenye kumtendea mabaya hataweza kumlipa kwa ajili ya uharibifu aliomfanyia.

Hadithi hii inaelezea mabaya yetu tunayomfanyia Mungu, ingawaje tumefanya mabaya kiasi cha kupitiliza. Kwa mara ya kwanza tulipokutana na Mungu, tayari kuliwepo na tatizo kwa sababu tumetenda yaliyo maovu kinyume chake. Tatizo hilo ni lazima litatuliwe kwanza kabla uhusiano haujaweza kuanzishwa.

Sasa tuangalie hali ya mtu ambaye ametenganishwa na Mungu na tuone ni jambo gani la muhimu kwake litakalomfanya aweze kuwa rafiki wa Mungu.

**Hali ya mtu aliyetengwa na Mungu.**

Hali ya mtu aliyetengwa na Mungu inaelezwa katika Waefeso 2:2-3:

> "Ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi; ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine."

Kulingana na mstari huu "sisi sote" hapo awali tuliishi chini ya utawala wa tamaa za mwili, iliyotufanya tuishi maisha ya dhambi. Tulikuwa miongoni mwa "wana wa uasi" amabao wanaongozwa na Shetani. "Kwa asili" tuliishi kwenye njia ambayo ilitufanya tuwe maadui wa Mungu, "watoto wa hasira" kwa muda wa kitambo fulani hadi tulipopata hasira ya Mungu tuliyokuwa tunastahili.

► Lakini siyo kila mtu ambaye hajaokoka anayeelekea kuwa mbaya kiasi hicho, sivyo? Je, umeshawahi kukutana na mtu ambaye anaonekana kama ni mtu mzuri, mwaminifu, mwenye upendo, na mwenye kuwajibika?

Je, inawezekana kuwa ni jambo gumu mtu kama huyo awe ni mwenye hatia na anayehitajika kutubu?

Kuna watu ambao hawajaokoka ambao maisha yao hayaelekei kuonyesha ni ya dhambi. Wanaweza wakajifikiria kwamba wao siyo watenda dhambi, lakini wameishi katika njia zao wenyewe, badala ya kujikabidhi kwa Mungu, Hili ni tatizo kubwa kwa mtu mzuri kuishi kwa njia yake mwenyewe.

Angalia katika Isaya 53:6.

> Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote.

Kwa mtu kudai haki ya kuchagua njia yake mwenyewe ya kuishi ni kumnyima Mwumbaji wake haki ya kumwelekeza yeye. Hii ndiyo asili ya dhambi. Huu ni uasi dhidi ya mamlaka

ya Mungu. Ilikuwa ni dhambi ya Adamu na Hawa, watu wa kwanza, wakati walipojaribu kujifanya wao wenyewe kuwa miungu, wakijaribu wenyewe kuwa huru mbali na Mungu.

Kuna aina ya mtu ambaye kwa haraka hufikiri kwamba ameokoka anapokuwa amesikia kwamba wokovu hupatikana kwa njia ya imani. Kiuhalisia hajawahi kutubu kwa ukweli, kwa sababu hakuona kwamba kulikuwa na haja ya kufanya hivyo. Hakujiona kamwe kuwa ni mtenda dhambi anayestahili hukumu ya Mungu. Kwa kuwa anakubaliana na ukweli wa Ukristo na kujiona mwenyewe kama mtu mwema, anajifikiria mwenyewe kama ni mkristo; lakini ambaye hajawahi kuwa na mabadiliko. Yeye kamwe hajawahi kuyakabidhi mapenzi yake mwenyewe; badala yake, alimkubali tu Mungu kama sehemu ya maisha na bado anaishi zaidi kulingana na matakwa yake mwenyewe. Huu siyo mwanzo wa uhusiano wa Mungu unaookoa, kwa mujibu wa maelezo ya maandiko.

Mtu anaweza akaonekana kuwa ni mzuri; lakini ikiwa hamtumikii Mungu, anavunja amri ya kwanza ya Mungu: kwamba tusiwe na miungu mingine ila yeye tu. Mtu huyu haishi kila siku kwa kujali amri za Mungu; badala yake anajiwekea malengo na kuishi kwa njia yake mwenyewe. Anajua habari zinazomhusu Mungu, lakini hajawahi kumtukuza kama ndiye Mungu. [Yaani, hajawahi kumfanya awe kweli ndiye Mungu wa maisha yake.]; kwa hiyo, anakuwa tu yupo hana sababu yoyote (Warumi 1:20-21).

Biblia inamwelezea mtu asiyeokoka kama kipofu, mtu aliye gizani, mtu aliye katika utumwa, akisukumwa na tamaa zenye uharibifu, na hata aliyekufa. Hali yake haitakuwa ya matumaini kama Mungu hatakuwa amejitoa kama msaada wa mahitaji ya mwenye dhambi.

## Neema ya Mungu ya Kuingilia kati

Mungu amefanya hatua za kwanza za kutuleta sisi katika kukutana na yeye, ili kwamba tatizo letu la dhambi liweze kutatulika au kupata ufumbuzi na uhusiano wetu na yeye uweze kuanza. Mungu alitoa Sadaka ili sisi tupata msamaha na akatupa sisi nia na uwezo wa kukubaliana na alichotoa ili kuleta mahusiano mazuri kati yake na sisi.

Mungu kwa hiari yake yuko tayari kusamehe na kulipa gharama ya msamaha huo. Alionyesha nia yake hiyo kwa kumtoa Yesu kama dhabihu juu ya msalaba.

Pamoja na dhabihu hiyo kutolewa, mwenye dhambi hatakuwa na tumaini bila neema ya Mungu kufanya kazi ndani ya moyo wake. Neema ya Mungu hufika kwenye moyo wa mwenye dhambi, na kumtia hatiani juu ya dhambi zake na kumwonyesha kwamba ana lawama kwa kujitenga kwake na Mungu. Neema ya Mungu haimwonyeshi mwenye dhambi kwamba ni mwenye hatia tu, bali inamfanya atamani msamaha na kumpa uwezo wa kuitikia Mungu.

► Je, yuko mtu anayetaka kushirikisha jinsi Mungu alivyomleta kwenye kukutana na Mungu ili kupata wokovu?

Bila ya neema, mwenye dhambi hawezi hata kumwendea Mungu. Neema huja kwa kila mtu kabla hajaanza kumtafuta Mungu, ingawaje hajawahi kufanya jambo lolote linalomfanya aweze kustahili.

Kumbuka Waefeso 2:2-3 – panatoa maelezo gani yasiyokuwa na matumaini? Lakini angalia aya mbili zinazofuata baada ya maelezo hayo:

> Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema (Waefeso 2:4-5).

Kama mtu anakuwa bado hajaokoka, siyo kwa sababu kamwe hajawahi kuwa na neema, bali ni kwa sababu hapendi kukubaliana na neema aliyo nayo.

## Kukutana Binafsi

Mkristo ni mtu ambaye amekuwa na uzoefu binafsi wa kukutana na Mungu. Inawezekana pakawepo na mchakato wakati mtu anapoanza kuielewa injili na kuwa tayari kutubu. Lakini mtu huwa Mkristo wakati ule tu anapokutana na Mungu. Wakati huo, mtu hukubaliana na neema ya Mungu kwa kutubu dhambi zake na kuamini ahadi ya Mungu ya kumpa msamaha.

Kwa kutubu, mwenye dhambi anayeamini hupokea neema ya msamaha na mabadiliko. Wokovu unalinganishwa na kupata nguvu ya kuona, kuja kwenye nuru, kukombolewa kutoka katika utumwa, kufunguliwa kutoka kwenye tamaa za uovu, na kufufuliwa tena kurejea kwenye maisha.

Matendo 26:18 inaelezea mabadiliko ambayo injili inafanya ndani ya mwenye dhambi. Paulo alitumwa "awafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi."

► Kutokana na yale ambayo tumejifunza katika somo hili, Mkristo halisi ni yupi?

Mkristo halisi ni yule ambaye amepata kukutana na Mungu wakati alipotubu dhambi zake (Luka 13:5), kwa imani akapokea msamaha (Waefeso 2:8), na akayatoa maisha yake kuwa ya utiifu kwenye Neno la Mungu (1 Yohana 3:6). Kukutanika huku kunaanzisha uhusiano wake binafsi pamoja na Mungu (1 Yohana 1:3).

Kama mtu hayuko kwenye uhusiano huu pamoja na Mungu, atakuwa amekuwa akizuia neema ya Mungu anayotoa kwake. Anapaswa atubu dhambi zake na kwa imani apokee neema ya Mungu ya msamaha na mabadiliko.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

► Baadhi wanaweza kushirikishana shuhuda zao za kukutana na Mungu kwa ajili ya wokovu, wakifanya ulinganifu wa shuhuda za "kabla na baada."

► Kila mtu anapaswa ajiulize mwenyewe, "Je, nimeshawahi kukutana na Mungu wakati nilipotubu na kuamini, nikianza uhusiano wangu pamoja na Mungu; au ninajidhania binafsi kwamba mimi ni Mkristo kwa sababu za uongo?"

► Mtu ambaye hayuko kwenye uhusiano na Mungu anaweza kutaka kushirikisha ufahamu wa hitaji lake ili kwamba kikundi kiweze kuomba kwa ajili yake.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunifikia mimi wakati nilipokuwa nimepotea na kutengwa na wewe.

Asante kwa kutoa dhabihu ya Yesu juu ya msalaba ili niweze kusamehewa.

Asante kwa kunidhihirishia hatia zangu, kwa kunipa nia ya kupokea msamaha, na kunifanya niwe na uwezo wa kukubali wewe.

Asante kwa ajili ya mabadiliko makubwa sana ambayo umeyafanya ndani ya maisha yangu. Ninataka siku zote niweze kuishi katika utii wa upendo kwa ajili yako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Waefeso 2. Jaribu kufikiria juu ya mambo ambayo Mungu ameyafanya kwa kuingilia kati katika maisha yetu. Aya ya 1-3 inaelezea hali yetu ya zamani au iliyopita; aya ya 4 inaanza kuelezea mabadiliko ambayo Mungu ameyafanya. Angalia tena marejeo yote yanayohusiana na uhusiano katika sura yote, hasa kwenye aya za 4, 6, 7, 14, na 19. Andika aya chache kuhusiana na yale unayoyaona.

# Somo la 3
# Uhakika wa Kukubaliwa na Mungu

## Wazo Kuu

"Mungu alinikubali mimi kama mtoto wake wakati nilipotubu na kuamini ahadi yake."

## Lengo la Somo

Kuona kwamba uhakika wa wokovu wa kweli unategemea katika kufuata maelekezo ya Injili

## Uhakika

► Je, ni kwa jinsi gani mtu anaweza kujua kwa uhakika kwamba ameokoka?

► Je, kuna usalama wa kuamini hisia zako? Kama sivyo, kwa nini?

*Thibibitisha majibu mbalimbali kadri iwezekanavyo. Unaweza kuelezea zaidi kwa ufasaha baadaye katika somo.*

Watu wengine hutegemea hisia zao za ndani, lakini hisia zinabadilika na zinaweza zikapotosha.

Biblia inatueleza sisi kwamba tunaweza kujua kwa uhakika kwamba tumeokoka. Tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu ametukubali sisi. Hatupaswi tuishi kwenye hofu, kwa sababu Roho wa Mungu hututhibitishia kwamba sisi ni watoto wa Mungu tuliokubalika.

> Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu (Warumi 8:16).

Uthibitisho huu ni wa uhakika na uliokamilika sana kiasi kwamba tunaweza kuwa na ujasiri kwenye ile Siku ya Hukumu, bila ya kusumbuka kwamba aidha tutapita kwenye tathmini ya Mungu au laa. Watu wengine husema kwamba wana matumaini ya kuingia mbinguni, lakini tunaweza tukawa na uthibitisho mzuri zaidi kuliko huo.

> Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa, kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu (1 Yohana 4:17).

► Maisha yaliyobadilishwa ni ushuhuda kamili wa wokovu, lakini ushuhuda huo hauwezi kuwa uhakika wa kwanza mtu kuwa nao. Kwa nini siyo hivyo?

Maisha yaliyobadilishwa ni ushahidi kamili kwamba mtu ameokoka, lakini ushahidi huo huwa haupo wakati ule wa mwanzoni. Wakati wa kuokoka, matokeo ya wokovu yanakuwa bado hayajapata muda wa kujitokeza. Kwa hiyo, wakati wa kuokoka, mabadiliko ya maisha siyo

msingi wa uthibitisho. Mwamini anaweza akawa na uhakika wa wokovu wake kwa kujua kwamba amefuata njia sahihi ya kimaandiko katika kufikia wokovu.

Njia sahihi ya kufikia kwenye wokovu inaanza na kutubu. **Kutubu** inamaanisha kwamba mwenye dhambi hujisikia yeye mwenyewe kwamba ni mwenye hatia na anastahili hukumu (1 Yohana 1:9), na kwamba yuko tayari kwa hiari yake mwenyewe kuachana na matendo yake ya dhambi.

> Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa (Isaya 55:7).

Kama mtu atakuwa hajajiona yeye mwenyewe kwamba ni mwenye hatia, bila kutoa udhuru, na anayestahili hukumu, bado atakuwa hajatubu. Kama atakiri kwamba yeye ni mwenye dhambi, lakini anahitaji dini ambayo ina fursa ya mtu kuendelea kutenda dhambi, atakuwa hajatubu kwa sababu anapenda kuendelea kutenda kile ambacho kulimfanya awe mwenye hatia. Hana ukiri wa ukweli kwamba dhambi ni uovu.

Kutubu hakumaanishi kwamba mwenye dhambi ni lazima arekebishe maisha yake na yeye mwenyewe ajifanye mwenye haki kabla Mungu hajamsamehe. Hilo jambo haliwezekani kwa sababu mwenye dhambi yuko chini ya kongwa la dhambi; lakini mwenye dhambi anapaswa awe tayari kwa hiari yake mwenyewe kwa ajili ya Mungu kumkomboa kutoka kwenye dhambi

Na baada ya toba huja imani ambayo ni muhimu kwa ajili ya wokovu. Kuwa na **imani inayookoa** inamaanisha kwamba mtu anaamini baadhi ya mambo fulani.

1. **Hujiona kwamba hawezi akafanya jambo lolote la kujihesabia haki yeye mwenyewe.**

   > Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu (Waefeso 2:8-9).

   Anajitambua kwamba hakuna lolote analoweza kulifanya ambalo linaweza kumfanya awe na uhalali wa kuokolewa hata kwa sehemu ndogo tu.

2. **Anaamini kwamba dhabihu ya Kristo inatosha kwa ajili ya msamaha wake.**

   > Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote (1 Yohana 2:2).

   *Kipatanisho* maana yake ni dhabihu ambayo inafanya msamaha wetu uwe kitu kinachowezekana. Hakuna kitu kingine ambacho ni muhimu zaidi ya dhabihu ya Kristo kwa ajili ya msamaha wetu.

3. **Anaamini kwamba Mungu anaahidi kumsamehe kwa takwa moja tu la imani.**

> Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote (1 Yohana 1:9).

Kama atafikiri kwamba kuna mahitaji mengine, ana mategemeo ya kuokolewa kwa sehemu kwa njia ya matendo badala ya kuokolewa kabisa kwa njia ya neema.

Kama atakuwa ametubu kwa ukweli na kuamini jinsi Biblia inavyoelekeza, ana haki ya kuamini kwamba Mungu amemsamehe. Haitoshi tu kuamini kwamba wokovu unatolewa; mtu anapaswa yeye mwenyewe aamini kwamba ameokolewa.

Kuna uthibitisho maalumu ambao Mungu hutoa kwa mwamini anayetubu wakati anapokuwa ametubu na kuamini:

> Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu (Warumi 8:15-16).

Kama mtu atakuwa amefuata njia ya kimaandiko ya kupokea wokovu na ni tegemezi kwenye maana halisi ya kimaandiko ya uhakika wa haraka, badala ya njia nyingine ya uhakika, haiwezekani akadanganyika. Uhakikisho huu uko kwenye msingi wa Neno la Mungu, ambao kwa namna yeyote ile ni wa kuaminika kabisa. Wakati wote Mungu hutimiza ahadi zake.

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Wakati ule mtu anapokuwa ameokoka hawezi akawa anajua tafsiri za kutubu au imani inayookoa. Kwa kuwa sasa ameokoka, anapaswa awe na uwezo wa kuangalia nyuma na kuona kwamba hayo yalitendeka.*

*Waulize wanachama wa darasa:*

► Uliza ni mambo gani washirika wana uhakika nayo ambayo kama ingekuwa wanakufa sasa hivi wangeingia mbinguni.

► Waalike washirika kwa ajili ya kushirikishana jinsi walivyopata kipengele cha toba au imani.

*Jadili uwezekano wa madhara ya mtu anayefikiria kwamba yeye ameokoka wakati huo akikataa moja wapo ya vipengele vilivyo orodheshwa hapo juu. Kwa mfano,*

► Je, ni madhara gani yatatokea endapo mtu kwa ukweli hakufikiri kwamba dhambi zake zinastahili hukumu ya Mungu?

► Itakuwaje kama mtu atafikiria kwamba mambo mema anayoyafanya yakiongezwa kwenye neema ya Mungu itamwokoa?

*Madhara ya kila kosa yanajionyesha kwenye aya hapo juu.*

*Somo hili linapaswa kumsaidia mtu aone kama amekuwa na sababu mbaya kwa ajili ya kufikiria kwamba yeye ameokoka, na litapaswa liwe msaada kwa mtu aliyeokoka kwa ukweli katika kuwa na uelewa ulio wazi wa injili ambayo tayari alishaikubali.*

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya ahadi yako ya kumsamehe mwenye dhambi ambaye anatubu na kuamini. Nimetubu dhambi zangu, na ninaamini katika ahadi yako.

Ninajua kwamba dhabihu ya Yesu juu ya msalaba inatosha kwa ajili ya msamaha wangu.

Ninajua kwamba sihitaji kuwa na hofu ya hukumu kwa sababu dhambi zangu zimesamehewa.

Asante kwa ajili ya ushuhuda wa Roho Mtakatifu wako kwamba mimi ni mtoto wako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Waebrania 10:11-25. Ni msingi gani wa uhakika wa kibinafsi unaotolewa katika kifungu hiki? Ni maelekezo gani ambayo hutolewa kwetu kwa kuwa tunao huu uhakika? Orodhesha maelekezo hayo na tafakari jinsi ya kuyakamilisha na au kuyatimiza kibinafsi.

# Somo la 4
# Kuwasiliana na Mungu

## Wazo Kuu

"Nitamjua Mungu vizuri zaidi kwa sababu ninawasiliana naye kwenye maombi."

## Lengo la Somo

Kuelewa kwamba uhusiano wetu na Mungu unadhihirishwa kwa njia ya mawasiliano yetu na yeye.

## Utangulizi

Mazoezi ya maombi ni moja ya alama za Mkristo, Hata hivyo, inawezekana kwa mtu kuwa na desturi ya maombi ambayo siyo maombi ya kweli ya Kikristo. Wakati mwingine mtu anakuwa na sababu mbaya ya kufanya maombi.

► Je, ni hali gani inaweza ikasababisha mtu kuomba wakati hajawahi kuomba tena kabla ya hapo?

Mtu anaweza kuomba kwa mara ya kwanza kwa sababu ya mgogoro ( hata wale askari wasiokuwa na dini wataomba wakiwa kwenye vita kali) au kwa sababu ya kufikiri kwamba maombi yatampatia kile anachokitaka. Ukweli ni kwamba mtu anavutiwa na maombi na siyo kwamba anavutiwa na kuokoka pamoja na kujua Mungu. Anaweza akavutiwa tu kupata vitu kutoka kwa Mungu kwa njia ya maombi.

Watu wengi wana hamu na mambo ya maroho, malaika, na nguvu za kiroho kwa ajili ya kupata faida kwenye biashara na afya. Watu hawana uhakika kama sayansi ina majibu yote yanayohitajika, na kwamba wanategemea kupata msaada wao kutoka kwenye nguvu zisizo za kawaida za asili zisizoonekana. Utafiti huu wa mafanikio kutoka kwenye nguvu hizo za asili zisizoonekana zinachukua sura ya kipagani au ya kiushirikina.

Watu wengine hufikiri kwamba maombi yana nguvu kama utaratibu wa kichawi. Wanadhani maombi yana thamani tu pale ambapo yana mlazimisha Mungu kuwapa yale wanayohitaji.

► Watu wa dini nyingine pia wanaomba. Je, ni kwa namna gani kuomba kwa Mkristo ni tofauti na kuomba kwa mpagani?

## Mkristo Hutafuta Mapenzi ya Mungu katika Maombi

Utofauti mkubwa uliopo wa maombi ya Mkristo ni kwamba tunajikabidhi kwenye mapenzi ya Mungu kuliko tu kutaka kujaribu wenyewe kupata vile tunavyovihitaji.

Mpagani huelekea kufikiri kwamba maombi ni kwa ajili tu ya kupata nguvu za kipekee zisizoonekana kwa ajili ya kufanyia jambo lolote analolitaka. Watu wengi wanachukulia

mtazamo huu wa kipagani katika maombi, wakiwa wanaomba tu wakati wanapokuwa na mahitaji au wanapokuwa kwenye majanga. Wanajaribu kumtaka Mungu atimize mapenzi yao, badala ya kujaribu kutaka kujua ni yapi yaliyo mapenzi ya Mungu.

Sisi kama wakristo tunaamini kuwa mapenzi ya Mungu ni mazuri kwetu kuliko matamanio yetu wenyewe. Tunajua kwamba kwa kuwa Mungu anazo hekima kamilifu na upendo uliokamilika, mapenzi ya Mungu ni jambo bora zaidi ambalo linaweza kutokea kwetu. Kwa hiyo, ingawa katika maombi tunaomba yale ambayo tunafikiri tunayahitaji, huwa tunamwachia Mungu achague – siyo kwa lazima, bali ni kwa sababu tunamtumaini yeye.

Tunapaswa tuombe kwa malengo kwa ajili ya kupata majibu ya maombi yetu. Kama kila siku tutakuwa tunaomba bila lengo, mara kwa mara hatutaweza kuona majibu ya Mungu katika maombi yetu. Tunaongea na Mungu kuhusiana na mahitaji yetu, tukimtaka atuonyeshe sisi ni kwa jinsi gani tunaweza kuyaona hayo mahitaji. Tunapokuwa tunaomba kwa ajili ya kupata suluhisho, hutusaidia sisi kujua ni mambo gani tunayopaswa kuombea.

Maombi siyo tu suala la kugeukia kwenye orodha ya mahitaji; bali ni kutaka kuwa na mwingiliano na Mungu. Tunapokuwa tunamweleza Mungu kuhusu mahitaji yetu, tunamwamini kwamba atatupatia mahitaji hayo kwa njia yake anayoiona yeye mwenyewe inafaa. Wakati mwingine anatuonyesha sisi mambo tunayopaswa kuyafanya.

## Mkristo Humtafuta Mungu katika Maombi

**Mkristo anathamini uhusiano wake na Mungu kuliko kile anachopata kutoka kwa Mungu.**

Tunachotafuta zaidi sana katika maombi ni kumpata Mungu mwenyewe.

Wakati mmoja kuliwepo na mtakatifu mmoja maarufu sana ambaye kwa sasa anakumbukwa kama Mtakatifu Bernadi. Bernadi wa Clairvaux alisema, "Muda wetu na Mungu, na kipaumbele tunachokiweka kwa ajili ya muda huo, ni kipimo cha kweli cha upendo wetu kwa Mungu." Upendo uko kwenye uhusiano, na uhusiano unadhirishwa katika mawasiliano." Uhusiano hauwezi ukakua pasipokuwepo na mawasiliano na uhusiano huo hushuka endapo mawasiliano yatapuuzwa.

Je, utajisikiaje kama unaye rafiki ambaye anazungumza na wewe tu wakati anapotaka kupata kitu kutoka kwako? Je, itakuwaje kama ataonekana kutokuwa na nia ya kukujua wewe vizuri zaidi au kutokuwa na nia ya kusikia kuhusu haja zako au kuhusika kwako? Huwezi kuita kwamba huo ni uhusiano mzuri, lakini watu wengi wana uhusiano na Mungu unaofanana na huo.

Upendo wetu kwa Mungu haupimwi kwa jinsi tunavyomtumikia (ingawaje upendo kwa ajili yake unapaswa utuhamasishe kutumika) au kwa kuwa makini kwa namna tunavyoishi (ingawaje upendo kwa Mungu unapaswa utusababishe kuwa waangalifu na kujilinda wenyewe dhidi ya dhambi). Mtu aliyeajiriwa na kuzingatia kazi zake tu lakini asitake kuonana na mwajiri wake au kuongea naye kuna uwezekano mkubwa kwamba kuna

mahusiano mabaya yaliyoko kati yake na yule mwajiri wake. Uhusiano wetu na Mungu unapaswa uwe mzuri zaidi ya hapo.

Mawasiliano yanaweza kuwa katika ngazi mbalimbali. Kwenye uhusiano ulio dhaifu kunakuwepo zaidi na vifungu vya maneno vya kukariri , na semi za kurudia rudia kutokana na mazoea. Uhusiano wa kina utakuwa na mawasiliano yenye maoni na hisia. Uhusiano bora una uaminifu ulio mkamilifu kabisa.

Kwa hiyo inaonekana kwamba Bernadi alikuwa sahihi. Maisha yetu ya maombi hupima kipimo chetu kwa Mungu, kama vile uhusiano wa aina yeyote unavyopimwa na mawasiliano yaliyoko ndani yake

## Maombi ni Ishara Maisha ya Kiroho

Maisha yetu ya Kiroho yamo ndani ya uhusiano wetu na Mungu, na maombi ni ishara ya uwepo wa maisha ya kiroho.

Moja ya ishara kwamba Sauli mtesaji alikuwa amebadilika ni kwamba alikuwa ameanza kuomba (Matendo ya Mitume 9:11).[2]

► Wakati mtoa huduma za msaada wa matibabu anapokuja kwenye eneo la kumwokoa mtu ambaye amejeruhiwa sana, je, huwa kwanza anafanya nini?

Kwanza huwa anakagua "ishara muhimu" (ishara za uhai), kama vile mapigo ya moyo na kupumua. Hapa anakuwa anatafuta ishara za uwepo wa maisha ya kimwili. Pia kunazo ishara muhimu za uwepo wa kiroho. Maombi ni ishara ya uwepo wa maisha ya kiroho.

Maombi ni pumzi ya roho – ishara nyeti ya kiroho.

Tunapumua kwenye maisha ya kiroho kutoka kwa Mungu na tunapumua kutoka ndani mwetu sifa na kuabudu, kunakodhihirishwa kipekee katika maombi yetu. Je, ni kwa muda gani katika maisha ya kimwili mtu anaweza kukaa bila ya kupumua? Je, ni kwa muda gani mtu anaweza kuishi maisha ya kiroho bila ya kuomba?

► Je ni wakati gani unapaswa kuomba?

## Nyakati za Kuomba

- Omba unapoanza siku.
- Omba kwa wakati maalumu ulioupanga au uliouweka kila siku.
- Omba unapokuwa kwenye majaribu.
- Omba wakati ambapo umejiona kushindwa.
- Omba wakati unapotaka kumshukuru Mungu kwa jambo fulani.

[2] Ona pia 1 Wakorintho 1:2. Maombi ni kitu ambacho Wakristo wote wanacho kama kitu cha kawaida.

## Muhtasari

1. Maombi ya Mkristo yanatofautiana na maombi ya mpagani kwa sababu tunataka mapenzi ya Mungu yatimizwe na tunathamini kumjua Mungu zaidi kuliko tunavyothamini vile tunavyopata kutoka kwake.
2. Maombi ni kipimo cha upendo wetu kwa ajili ya Mungu.
3. Maombi ni "ishara muhimu" ya uwepo wa maisha ya kiroho na inayoonyesha kwamba tuko hai kiroho.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Jadili ukweli kwamba katika maombi tunapaswa tumtafute Mungu mwenyewe zaidi sana kuliko vitu vingine vyote tunavyoweza kuvipata kutoka kwake. Jiulize:*

► Je, unaomba kwa ukweli na uhakika kwa kutumia kipaumbele hicho? Je, jambo hilo linaonyesha nini?"

*Karibisha majibu yaliyo kwenye maudhui kwamba maisha yetu ya maombi yanadhihirisha upendo wetu kwa Mungu. Uliza kama jambo hilo linasababisha tathmini binafsi isiyo na raha, kwa kuuliza swali kama:*

► Je, unahisi kwamba upendo wako kwa Mungu unaweza kwa ukweli na uhakika kupimwa kwa maisha yako ya maombi?

► Je, unahisi kwamba upendo wako kwa Mungu ni mkubwa zaidi sana kuliko maisha yako ya maombi yanavyoonyesha?"

*Jiwekee maamuzi kadhaa:*

► Ili maisha yangu ya maombi yaweze kujidhihirisha vizuri zaidi na kuongeza upendo wangu kwa Mungu, ninapaswa nifanye…"

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya upendeleo nilio nao wa kuweza kuongea na wewe. Ninayo furaha kwamba ninaweza kuongea na wewe kuhusiana na mahitaji yangu. Lakini, zaidi ya yote, Ninakushukuru kwa ajili ya upendeleo nilio nao wa kukujua wewe.

Naomba unisaidie katika kuonyesha upendo wangu kwa ajili yako kwa kuongea na wewe mara kwa mara. Ufanye upendo wangu ulio kwa ajili yako uweze kukua kwa sababu ninaanza sasa kukujua wewe vizuri zaidi.

Nisaidie katika kuufanya muda wangu na wewe uwe wa kipaumbele kikubwa zaidi sana katika maisha yangu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Angalia usemi ambao Yesu alitoa kuhusu maombi katika Mathayo 6:5-18. Andika rejea za mahitaji ya kibinafsi na rejea za uhusiano na Mungu.

# Somo la 5
# Kusoma kile ambacho Mungu Alikiandika

## Wazo Kuu

“Neno la Mungu linaongoza uhusiano wangu pamoja na Mungu.”

## Lengo la Somo

Kuona jinsi Neno la Mungu linavyotusaidia katika kumjua na kumpendeza Mungu.

## Utangulizi

► Je, sura ndefu kuliko zote katika Biblia ni ipi? (Zaburi119)

► Je, hiyo sura inahusiana na nini? (Angalizo: Je, lipo jambo ambalo limerudiwa tena na tena angalao linalokaribiana sana katika maana?)

Zaburi ya 119 ina aya 176. Neno la Mungu limetajwa sana takribani katika kila aya isipokuwa saba tu miongoni mwake. Ni wazi kwamba, hilo ndilo somo la hii Zaburi.

Maneno tofauti hutumiwa kwa ajili ya Neno la Mungu kama vile maagizo, sheria, amri, na hukumu.

Mwandishi aliyevuviwa kuandika Zaburi hii anaelezea Neno la Mungu lilimaanisha nini kwake na athari iliyokuwa nayo juu yake. Zaburi ya 119 inaonyesha umuhimu wa Biblia kwa ajili ya Mkristo.

Watu wengine hutumia Biblia kama chanzo cha mafundisho ya imani, kama chanzo cha ushahidi wa kuthibitisha jambo, kama kichocheo cha hisia zao wakati wanapokuwa wamekatishwa tamaa, au kama kitabu cha taratibu za kidini. Biblia ni nzuri kwa ajili ya madhumuni hayo, lakini kama mtu ataitumia Biblia kwa njia hizo, inaweza ikaonekana kuwa tofauti na uhusiano wake na Mungu. Biblia inapaswa iwe ya juu sana kwa ajili ya mwamini.

Tuangalie baadhi ya aya za Zaburi 119 tuone ni kitu gani ambacho mwandishi huyu alivuviwa kusema kuhusu umuhimu wa Maandiko kwa ajili yake mwenyewe.

Mwandishi anataja faida nyingi za Neno la Mungu:

- Limenihuisha (50).
- Linafariji (52).
- Ni taa (105).
- Linamfanya awe sehemu ya watu wanaomwabudu Mungu (74, 79).

## Shauku ya Maandiko ya Mtunga Zaburi

*Katika somo hili, angalia kwa uangalifu aya zilizoandikwa kwa wino mnene.*

- Alilipenda Neno la Mungu na kulifurahia ndani yake (16, 24, **47**, 48, 77, **92**, **97**, **103**).
- Alifurahia kuwa nalo kana kwamba lilikuwa ni utajiri uliokuwa mkubwa sana (**14**, **72**).
- Aliona kwamba wale watu waliokuwa nalo na kulihifadhi ndani mwao ni watu waliobarikiwa (waliokuwa na furaha) (**1**, **2**).

► Je, ni kwa nini mwandishi alipenda Maandiko sana kwa kiasi hicho?

**Mtunga Zaburi alikuwa na shauku ya Maandiko kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu.**

Je, ni kwa nini alilipenda Neno la Mungu sana kwa kiasi hicho? Je, ni kwa nini aliliona kama ni hazina kubwa sana? Siyo tu kwamba ni taarifa nzuri. Mara kwa mara anarejea Neno kama "lako" (la Mungu). Alilipenda kwa sababu alimpenda Mungu. Neno la Mungu ni udhihirisho wa asili ya Mungu.

Angalia katika aya ya 137. Anapokuwa anaangalia sheria ya Mungu na mahitaji yake, anaiona haki na hekima aliyo nayo Mungu. Kwa kuwa Mungu ni mwadilifu, sheria yake ni ya haki.

Upendo wake na kumwabudu kwake Mungu kunadhihirishwa na matumizi yake ya Maandiko – Maandiko ni kiungo kati yake na mtu anayeabudu – yakimfunua Mungu kwa mtu anayeabudu na kuongoza mwitikio wa mtu anayeabudu kwa Mungu. Maandiko yanakuwa yamevuviwa na Roho Mtakatifu, kuangazwa na Roho Mtakatifu, na kukamilishwa ndani ya maisha ya mtu anayeabudu kwa nguvu na uwezo wa Mungu.

Kwa kuwa aliona kwamba Maandiko yanaelezea asili ya Mungu, alishikwa na hasira kwa ajili ya wale watu wasiotaka kumheshimu Mungu kwa kuihalifu sheria yake. Hakuwa na hasira kwa sababu ya haki zake binafsi bali kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu (53, **104**, 126, **136**).

Hakuwa tu analiheshimu Neno la Mungu wakati alipokuwa na watu wengine waliokuwa wanafanya vivyo hivyo. Alisema hatakuwa na aibu kwa ajili ya Neno la Mungu hata kama itakuwa ni mbele ya wafalme (46).

## Maandiko Yalimwongoza Mtunga Zaburi katika kumwitikia Mungu

Mungu huwaita watu katika uhusiano wake. Kusudi la Maandiko ni kumfunua Mungu ili tuweze kuingia katika uhusiano wake. Kwa hiyo, Maandiko yanataka mwitikio kutoka kwa msomaji. Mtu hapati matokeo yaliyokusudiwa isipokuwa akiitikia kwa usahihi katika kumtafuta Mungu.

Angalia mwitikio wa mtunga Zaburi katika Maandiko:

- Aliomba kwamba Mungu aweze kumfundisha Neno lake mwenyewe (12, **18**, **27**, 33, 34).
- Aliomba kwamba awe na uwezo wa kuishi sawasawa na hilo Neno la Mungu (**35-37**, 5, 10).
- Aliomba kwamba hata moyo wake uendane na mapenzi ya Mungu (32, **80**).
- Alijua kwamba utakaso wake utatokea kupitia mwingiliano wake na Mungu katika Neno lake (**9**, **11**).
- Alidai baraka kutoka kwa Mungu kwa msingi wa kuzishika sheria za Mungu (22, **121**, **153**)
- Aliahidi kuwa mtiifu (8). "Nitazitii" au neno "Nita…" linajitokeza mara kwa mara, akiahidi kuwajibika kutokana na Maandiko.
- Aliutumia muda wake katika kutafakari juu ya Neno la Mungu kwa siku nzima (15, 97) na mapema asubuhi (147-148).

Huyu mtunga Zaburi wa zamani alikuwa na mtazamo uliokuwa na uvuvio wa umuhimu wa Neno la Mungu kwa mwamini. Uzoefu wake haukuwa wa kipekee na kwa ajili yake tu. Ni uzoefu ambao kila mmoja wetu anapaswa kuwa nao kwani Neno la Mungu linaongoza uhusiano wetu na Mungu.

### Mwitikio wetu kwenye Maandiko

Anza sasa kuwa na mwitikio ulio sahihi kwenye Maandiko:

- Tambua kazi ya Neno la Mungu kwenye uhusiano wako na Mungu.
- Ingia kwenye uhusiano na Mungu kama kutubu kwako bado hakujakamilika.
- Jihusishe kwa wakati katika Neno la Mungu. Anza na Zaburi ya 119, na omba kwa kutumia aya hizi unapokuwa unasoma. Vitabu vya Wafilipi, Tito, na Waefeso vinaweza kuja baadaye kwenye usomaji wako
- Dhamiria kuendelea kuwa na mwitikio endelevu katika kazi ya Roho Mtakatifu kupitia katika Neno lake.

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

Kama ilivyoelezwa katika somo hili, watu wengine hutumia Biblia kama chanzo chao cha mafundisho ya imani, kama chanzo chao cha aya za kuthibitisha mambo kadhaa, kama kichocheo chao wanapokuwa katika hali ya kukatishwa tamaa, au kama kitabu cha kutumika kwa ajili ya taratibu za kidini.

► Je, matumizi yako ya Biblia yamekuwa tofauti sana kutokana na uhusiano wako wa kuishi na Mungu? Je, hiyo ni kwa sababu hujayaona Maandiko kama ni kitu kinachopaswa kuwa katika maisha yako?

► Je, ni kitu gani unachoweza kukifanya ili kuyaweka Maandiko katika nafasi yake inayostahili?

► Je, ni ahadi gani maalumu ambayo uko tayari kuifanya kwa ajili ya hatima yako ya baadaye ya matumizi ya Maandiko?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya kunipa Maandiko, na kwa kujifunua kwangu wewe mwenyewe. Asante kwa kunipa ufahamu wake kupitia Roho Mtakatifu wako anayefanya kazi ndani ya moyo na akili yangu.

Naomba unisaidie kuelewa zaidi na zaidi kile unachokitaka na unavyotaka mimi niwe ili niweze kukupendeza wewe. Niwezeshe siku zote kuwa na mwitikio wa kazi yako ndani ya moyo wangu kila ninapokuwa ninasoma. Achilia Neno lako liwe endelevu kwangu katika kunibadilisha mimi kuwa kwenye mfano wa sura yako.

Bwana, ninajikabidhi katika kuutumia muda wangu kila siku katika kulitafakari Neno lako. Nipe kuwa na upendo wa kulipenda Neno lako kutokana na upendo wangu nilio nao kwa ajili yako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Katika wiki hii tafakari juu ya Zaburi ya 119. Orodhesha mambo ambayo mwandishi anasema atayafanya kwa sababu ya Neno la Mungu. Jikabidhi katika kufanya mambo ambayo yanafanana na hayo, na omba kwa ajili ya ukamilifu wake ndani ya moyo wako na maisha yako.

# Somo la 6
# Kutoa Mwaliko

## Wazo Kuu

"Ninataka niwaongoze watu wengine wamjue Mungu kama mimi ninavyofanya."

## Lengo la Somo

Kujifunza mbinu kwa ajili ya kushirikishana Injili.

## Utangulizi

►Je, kuna sababu gani ya kushirikisha injili?

Kuna sababu nyingi nzuri. Tuangalie sababu ambayo Mtume Yohana aliitoa kwenye kuwaalika watu kwa ajili ya kuokoka.

> Hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo (1 Yohana 1:3).

Tumepata uzoefu wa nini maana ya kukutana na Mungu na kuokoka, kwa ajili ya kuanzisha uhusiano pamoja naye. Kwa kuwa Mungu anawapenda watu (Yohana 3:16), tunatakiwa kuwajali na kuwafanya wamjue Mungu. Tuna mwaliko mkuu wa kuwashirikisha.

## Kuwasilisha Injili

Uwasilishaji huu wa injili ni wa hakika na unaokumbukwa. Unatumia mchoro ambao utaweza kukumbukwa na mtu yeyote anayeuona jinsi unavyowasilishwa. Unaweza ukawasilishwa kwa dakika mbili, au muda ukaongezwa kwa ajili ya majadiliano na utolewaji wa maelezo, siyo lazima uwe mchoraji mwenye uwezo mkubwa wa kuchora. Mchoro wenyewe ni mrahisi, na kutokana na urahisi wake kunamsaidia msikilizaji kuweza kukumbuka.

Sasa tutaenda kwenye hatua za uchoraji, pamoja na maelezo ya maneno yatakayoendana na kila sehemu itakayochorwa.

*Wanafunzi wanapaswa kuangalia kila hatua ya mchoro kama kiongozi wa darasa anavyochora katika ukubwa unaoonekana kwa darasa nzima. Kiongozi wa darasa asijaribu kuongeza maelezo ya ziada katika wasilisho. Yanapaswa kuwa maelezo mafupi ili wanafunzi waweze kujifunza kwa urahisi. Baada ya kielelezo cha kwanza, darasa liendelee kuangalia maelezo yaliyotolewa katika sehemu inayofuata, kisha wafanye mazoezi ya uwasilishaji.*


*Maneno ya kusema yametolewa kwa pamoja katika kila sehemu ya mchoro itakayoongezwa.*

## Kitu cha kusema kwenye kila sehemu ya Mchoro

**Sehemu ya 1**

"Mungu alimwumba kila mtu awe kwenye uhusiano pamoja naye na kuishi maisha yaliyobarikiwa. Hakupanga maisha yawe ya matatizo na mateso chungu zima."


[Chora mtu na neno "Mungu".]




**Sehemu ya 2**

"Mwanadamu ametenganishwa na Mungu kwa sababu ya dhambi. Watu wa kwanza walitenda dhambi, na tangu hapo kila mtu ametenda dhambi dhidi ya Mungu."


[Chora kujitenga kati ya watu na Mungu, na uandike "dhambi".]



**Sehemu ya 3**

"Mungu ni hakimu mwenye haki, na siku moja wenye dhambi watahukumiwa kwenda jehenamu ya milele isipokuwa wawe wametafuta rehema za Mungu na kurejea kwenye uhusiano tena pamoja na Mungu."


[Chora mshale na andika neno "motoni".]




**Sehemu ya 4**

"Hakuna lolote tunaloweza kulifanya kwa ajili ya kuturejesha tena upya kwa Mungu au kupata rehema – siyo kwa matendo mema, siyo kwenda kanisani, siyo taratibu za kimadhehebu, na wala siyo kutoa fedha...."


[Chora mshale kuonyesha kila kipengele kwenye orodha.]



**Sehemu ya 5**

“Hali yetu itakuwa mbaya sana kama Mungu hangefanya njia kwa ajili yetu ya kurejea kwake kwa njia ya Wokovu kwa kumwamini Yesu Kristo. Yesu, Mwana wa Mungu alikufa juu ya msalaba ili tuweze kusamehewa. Baada ya siku tatu, alifufuka kutoka kwa wafu.”


[Chora msalaba.]




**Sehemu ya 6**

“Lakini haitoshi tu kujua haya. Kila mtu binafsi atapaswa kufanya chaguo la kuokoka na kurejea tena kwa Mungu. Mtu ni lazima atubu, ikimaanisha kwamba ni kujutia kikamilifu kuhusu dhambi na kuwa tayari kwa hiari yake mwenyewe kuachana nazo. Mtu anayetubu na kuokoka kwa kumwamini Yesu Kristo Mungu anamsamehe makosa yake yote.”

[Chora mshale kisha andika maneno “Tubu” na “Pokea”.]



**Sehemu ya 7**

"Ni wapi unapofikiri kwamba upo katika mchoro huu? Je, umewahi kupata muda maalumu katika maisha yako ukatubu dhambi zako, ukapokea msamaha wa Mungu, na ukaanza kuishi yanayompendeza Mungu; au bado umetengwa na Mungu kutokana na dhambi yako?"

[Subiri kupata jibu. Watu wengi watakiri kwamba bado wametengwa na Mungu.]

"Uko tayari kufuata hatua hii – Kutubu, kupokea msamaha, na kuanza kuishi yenye kumpendeza Mungu? Nitapendezwa sana kuomba pamoja nanyi sasa hivi."

[Fanya maombi yanayokaribia kufanana na haya yafuatayo:]

"Bwana, ninajua mimi ni mwenye dhambi na ninayestahili adhabu ya milele. Ninajutia dhambi zangu na niko tayari kuachana nazo. Ninaomba unisamehe, siyo kwa sababu ninastahili, bali kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yangu. Asante kwa wokovu wako. Kuanzia sasa, nitaishi kwa ajili yako tu."

*Baada ya kiongozi wa darasa kuonyesha jinsi ya kuwasilisha, darasa litahusika na maelezo yafuatayo kuhusiana na sehemu hizi za kuwasilisha*

**Maelezo**

**Sehemu ya 1**

Mwanzo wa kuwasilisha unaweza kurekebishwa ili kuendana na muda wa msikilizaji. Badala ya "maisha yawe ni ya matatizo na mateso chungu zima" mwinjilisti anaweza kutumia maneno mengine ambayo msikilizaji atayaelewa Zaidi.

**Sehemu ya 2**

Ni muhimu kwa msikilizaji wako kutambua kwamba yeye binafsi ni mwenye hatia kutokana na dhambi na ametengwa na Mungu. Yuko kwenye hali ambayo imetokana na dhambi ya Adamu.

**Sehemu ya 3**

Hii inaonyesha vipengele mbalimbali vya hali ya mwenye dhambi.

**Sehemu ya 4**

Kusudi la sehemu hii ni kumwonyesha msikilizaji kwamba hapaswi kutumainia kitu kisicho sahihi kwa ajili ya wokovu. Sehemu hii inaweza kubadilishwa kulingana na mahitaji ya msikilizaji. Mwinjilisti ajaribu kutaja vitu ambavyo msikilizaji anaweza kuviamini.

**Sehemu ya 5**

Njia rahisi ya kuelezea mateso na kifo cha Yesu msalabani ni kusema kwamba "Yesu alikufa juu ya msalaba kama dhabihu ili kwamba tuweze kupata msamaha wa dhambi." Kusudi la

sehemu hii ni kumsaidia msikilizaji ajue kwamba anapaswa kutegemea wokovu ambao Mungu aliutoa.

**Sehemu ya 6**

Mwinjilisti hujaribu kumleta msikilizaji kwenye kipindi cha kuweza kufanya maamuzi. Msikilizaji anahitaji kutambua kwamba anapaswa afanye maamuzi binafsi. Anahitajika afahamu tafsiri sahihi ya toba, ili aweze kujua kwamba toba ni zaidi ya kuwa na majuto na ni zaidi ya kusema anaomba samahani. Anahitajika ajue kwamba anapaswa aombe ili amsihi Mungu kwa ajili ya msamaha.

**Sehemu ya 7**

Kwenye hatua hii, Mwinjilisti hujaribu kumleta msikilizaji kwenye kukiri hitaji lake la kuokoka. Uwasilishaji umepangwa katika kumsaidia mtu ambaye hajaokoka kutambua kuwa bado hajaokoka. Swali limeandaliwa kwa umakini mkubwa sana. Watu wengi wanafikiri wanaweza kila siku wakaomba kwa ajili ya msamaha wakati wanaendelea kuishi kwenye maisha ya dhambi. Swali linauliza kuhusu muda maalumu ambao mtu anaokoka na kuhusu maisha mapya anayoanza. Anatakiwa atambue kwamba kama bado hajawahi kuwa na uzoefu wa mabadiliko, ametengwa na Mungu kwa dhambi yake. Kisha mwinjilisti atapendekeza kufanya maombi pamoja naye kwa ajili ya wokovu.

Kama msikilizaji haelewi hitaji lake au hayuko tayari kutubu, mwinjilisti asimhimize kuingia kwenye maombi. Kama atajilazimisha kuomba bila ya kutubu kwa ukweli na kujizoesha mabadiliko, anaweza akawa na uhakika wa uongo wa wokovu au anaweza akaamini kwamba mabadiliko hayawezi yakatokea kwake. Kwa vyovyote vile, inawezekana asije kuokoka hapo baadaye.

Mchoro unaweza kuwasilishwa kwa haraka. Kama unayo nafasi ya kushirikisha injili, kwa wepesi tu unaweza ukauliza, "Je, ninaweza kuchukua angalao dakika mbili za kukuonyesha mchoro unaoelezea kile ambacho Biblia inaelezea, kwamba ni njia ya kujua kwa uhakika kama kweli umeokoka? Kwa hatua hiyo kunamfanya mtu ajue kwamba hutaenda kutumia muda wake mwingi. Kama ataonyesha kuvutiwa na anataka kuzungumzia kuhusu hiyo, hapo unaweza kuchukua muda mrefu zaidi.

Kwa kawaida, watu wengi huvutiwa na michoro. Mara nyingi mtu ataomba kuuhifadhi mchoro huo baada ya mwinjilisti kumaliza huduma.

*Onyesha uwasilishaji tena kwa mara nyingi. Epuka kuingiza ushauri wa ziada au ufafanuzi kwenye uwasilishaji kwa sababu wanafunzi watajifunza kwa urahisi zaidi kama itakuwa fupi. Baada ya maonyesho kadhaa, wanafunzi baadhi wanaweza wakafanya maonyesho kwa kubadilishana kwenye kikundi, wakati wanafunzi wenzao katika kikundi wakiwasaidia kukumbuka mambo muhimu kwa undani zaidi. Kisha, wanafunzi wanaweza wakagawanyika kwenye vikundi vya watu wawili wawili na kufanya mazoezi ya uwasilishaji kila mmoja na mwenzake.*

## Kutengeneza Nafasi za Kushirikishana Injili

Kama inaonekana kuwepo na mtu aliye tayari na wazi kusikiliza kile unavyoshirikisha katika injili, unaweza tu kwa wepesi kuuliza, "Je, ninaweza kuchukua dakika mbili kukuonyesha mchoro ambao unaelezea kile ambacho Biblia inasema kwamba ni njia ya kujua kwa uhakika kama umeokoka?"

Kwa kawaida nafasi hujitokeza mnapokuwa kwenye mazungumzo. Hapa kuna mifano ya njia za kutambua uwepo wa nafasi na kuzichangamkia.

Kama mtu analalamikia jambo fulani, baada ya mazungumzo kadhaa, uliza, "Je, ninaweza kuchukua dakika mbili kukuonyesha mchoro ambao unaelezea kile ambacho Biblia inasema kwamba ndiyo sababu za maisha kuwa magumu na kuwepo kwa matatizo mengi sana?"

Kama mtu anaonekana kuwa wa kidini zaidi, mwulize ni nini iliyo muhimu zaidi katika imani kuliko vingine. Kisha uliza, "Je, ninaweza kuchukua dakika mbili kukuonyesha mchoro ambao unaelezea kile ambacho Biblia inasema kwamba ni jambo muhimu sana la kufahamu?"

Kama mtu atakuwa anazungumzia kuhusu matatizo ya taifa, njaa au umaskini wa dunia, au madhara ya vita, mwulize, "Je, ninaweza kuchukua dakika mbili kukuonyesha mchoro ambao unaelezea kile ambacho Biblia inasema kwamba ndizo sababu za dunia kuwa katika hali hiyo?"

Onyesha kwamba hali ya dunia iko kama ilivyo kwa sababu wenye dhambi wametengwa na Mungu. Usitake kuaminisha kwamba wokovu unamaliza matatizo yote kwa mara moja, lakini onyesha kwamba wokovu ndio mwanzo wa suluhisho la Mungu. Siku moja ijayo kutakuwepo na mbingu mpya na nchi mpya na matatizo hayo hayatakuwepo tena kwa wale ambao kwa wakati huu wa sasa watakuwa wamepatanishwa na Mungu.

## Mwaliko wa kutoa ahadi

*Kutoa ahadi Kuendane na maswali yafuatayo:*

► Je, unadhani kwamba kushirikisha injili kwa njia hii inafaa?

► Je, unadhani kwamba ni kitu ambacho unaweza kukifanya?

► Je, mko watu wangapi ambao wiki hii mnaweza kujaribu kuonyesha mchoro huu kwa angalau mwamini mmoja na mtu mmoja ambaye bado hajaamini?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninayo furaha kubwa siyo kwamba unataka kuniokoa mimi tu, lakini pia ni pamoja na familia yangu, marafiki zangu, na kila mtu aliyeko katika ulimwengu huu.

Asante kwa kutupa wokovu ili kwamba kila mtu aweze kuokolewa na kuingia kwenye ushirika huu wa ajabu ambao tunao pamoja na wewe na waamini wengine.

Uliupenda ulimwengu wote kiasi cha kutosha hata kumtoa Mwanao wa pekee kwa ajili yake.

Baba, naomba unisaidie kuwa mwaminifu katika kuutangaza mwaliko wako kwa watu wote.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

1. Jiandae kutimiza ahadi yako ya kushirikisha mchoro kwa wengine wiki hii.
2. Tengeneza orodha ya watu ambao hawajaokoka unaowajua kwamba utakuwa na uwezo wa kufanya mazungumzo nao katika wiki hii. Panga kuleta somo ambalo litafungua mlango kwa ajili ya kushirikisha injili.
3. Tengeneza orodha ya baadhi ya wakristo ambao unaweza kuwaonyesha mchoro kwa lengo la kuwasaidia kujisikia kwamba wanawezeshwa zaidi kwa ajili ya kushuhudia.

# Somo la 7
# Kuendeleza Utii Wangu

## Wazo Kuu

"Natambua na kufuata mapenzi ya Mungu vizuri zaidi kwa kadri ya upendo wangu kwake unavyokua."

## Malengo ya Somo

Kujifunza jinsi ya kufuata mapenzi ya Mungu kwenye maeneo kumi ya maisha ya kila siku.

## Utangulizi

► Je, kutakuwa na matokeo gani endapo mtu atampenda Mungu zaidi?

Sababu mojawapo ya kumpenda Mungu zaidi imeelezwa katika Wafilipi 1:9-11.

> Na hii ndiyo dua yangu, kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote; mpate kuyakubali yaliyo mema; ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo; hali mmejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.

Aya hizi zinaelezea kuhusu mchakato endelevu kwenye maisha ya mwamini. Upendo wake unapaswa uwe endelevu katika kuongezeka. Wakati hilo linatokea, uweza wa kutambua ni kitu gani ambacho ni kizuri zaidi unapaswa uongezeke. Hali hii ni lazima itokee ili aweze kuwa mwaminifu na asiyekuwa na hatia.

Hatujui ukweli kuwa tunapaswa kuishi kama kwenye kipindi kile tunachokuwa tumeokoka kwa mara ya kwanza. Watu ambao Paulo aliwaandikia aya hizi hapa juu walikuwa ni watu ambao kwa muda fulani tayari walishakuwa Wakristo. Lakini bado, Paulo aliomba kwamba wanapaswa waendelee kumpenda Mungu zaidi, na kwa upendo huo, wawe na uwezo wa kuyaelewa mapenzi ya Mungu vizuri.

Tunapaswa kutarajia uboreshaji wa maisha yetu kadri Mungu anavyotupa uwezo wa kupambanua. Mungu anataka utii wetu ulio mkamilifu katika vipengele vyote vya maisha yetu, na siyo tu kushika taratibu za kidini.

Hatupaswi kudhania kwamba tayari tunajua kila kitu tunachotaka kukijua kuhusiana na jinsi ya kuishi. Tusidhanie kwamba tumefanya marekebisho yote ambayo maisha yetu yanayahitaji.

## Baadhi ya Maeneo ambayo Mwamini anapaswa Kuboresha

1. **Umakini wa ushawishi.** Je, kuna mambo unayofanya wewe ambayo hutataka watu wengine wayafanye?

2. **Kujidhibiti Binafsi.** Je, unatawala hisia zako na matamanio yako kiasi cha kutosha kufanya unachopaswa kufanya, au wakati mwingine unafanya yale mambo ambayo yanategemewa yaonekane kwa mtu ambaye hajaamini?

3. **Kuitunza Afya Yako.** Je, unautunza mwili wako kama vifaa visivyoweza kubadilishwa kufanya kazi kwa ajili Mungu? Kwa kuwa mwili wako ni mali ya Mungu, haupaswi kufanyiwa uharibifu wowote. Haupaswi uufanyie uzembe mwili wako katika kuutunza.

4. **Kuchagua Burudani.** Je, burudani yako inakusababishia vita na majaribu kwa kuleta mawazo mabaya au mtazamo mbaya? Jihadhari na chochote ambacho ni kiashiria cha dhambi kinachoonekana kwamba ni cha kuvutia au cha kumpendeza.

5. **Tabia.** Watendee watu wengine kwa heshima, kama watu walio katika sura ya Mungu na wenye matarajio ya milele. Watu ulio miongoni mwao wana mila zao za kuonyesha heshima. Unapaswa utafakari kuwa na heshima kwa njia ambayo wao wanaitambua. Kuwa na fadhila hata wakati inapotokea kwamba mtu hastahili.

6. **Maadili ya Kazi.** Je wewe ni mwaminifu kabisa katika biashara zako zote? Je, unaelezea sawasawa jinsi mambo yalivyo kabisa au unasababisha mtu kufikiri kwamba kitu fulani siyo cha kweli?

7. **Kujali Muda.** Muda ni rasilimali ya thamani ambayo tunapaswa tuitumie kwa ajili ya Mungu. Je, unaweka thamani kwenye muda wako na muda wa watu wengine kwa kuzingatia muda wa ratiba kila inapowezekana?

8. **Mavazi.** Je, mavazi yako yanaonesha kwamba yana thamani ya kuwa na heshima zinazotakiwa (ambazo hazijaribu kuwa kivutio au kuwasha tamaa kwa kile ulichovaa), na uangalifu katika kutumia fedha (siyo kununua mavazi ya gharama kubwa za kupitiliza kuliko una unavyohitaji)?

9. **Lugha.** Je, mazungumzo yako ni masafi na yenye heshima kwa Mungu na kwa watu wengine? Maneno mengi ambayo dunia huyatumia huwa matusi kwa Mungu.

10. **Kutegemewa.** Je, unatimiza ahadi? Je, watu wanaweza kuwa na mategemeo na wewe ya kufanya kile unachokisema? Je, wewe ni mtu wa kusahau ahadi zako kama zikiwa hazina manufaa?

Watu wengi hawachukulii kwa makini mahitaji yao ya kujiendeleza. Wanaona wanawajibika tu kwa maagizo yaliyo wazi katika Maandiko, bila ya kutambua kuwa maagizo hayo yanaweza kutumika kwa njia nyingi.

Tunapaswa tutatumbue kwamba kujiendeleza kwetu kumeungamanishwa na ongezeko la upendo wetu kwa Mungu. Tunahitajika tutafakari kwa kumaanisha juu ya aya tulizoanza nazo katika somo hili. Kama upendo wetu unaongezeka, kupambanua na uchaguzi wa tabia njema zinapaswa pia ziongezeke.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Uliza maswali haya kwa ajili ya majibu ya mtu binafsi:*

► Je, ni mfano gani wa mabadiliko ambayo uliyafanya kwenye maisha yako wakati Mungu alipokuonesha kwamba tabia, mwenendo, au kitendo fulani kilikuwa siyo kizuri sana?

► Je, kuna kitu chochote kwenye maisha yako ambacho unakijua kwamba unapaswa kubadilika? Je utafanya hivyo?

► Je, kuna kitu chochote kwenye maisha yako ambacho una mashaka nacho?

► Je, uko tayari kumruhusu Mungu akuoneshe katika maombi mabadiliko yeyote ambayo unapaswa uyafanye?

*Sema, " kwa mioyo wazi tuahidi kuomba pamoja wiki hii ili Mungu atuoneshe maadili yake na mabadiliko yoyote anayotaka kufanya katika maisha yetu. Je utajitoa kufanya hivyo? Wiki ijayo nitakuuliza kama ulifanya hivyo."*

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninahitaji upendo wangu kwako uwe unaongezeka bila kukoma. Ninataka niyaelewe mapenzi yako kwangu vizuri zaidi.

Naomba unisaidie mimi kupambanua ni kitu gani kinachokupendeza zaidi ili kwamba niweze kuishi maisha ambayo ni masafi na yasiyokuwa na hatia.

Naomba unisaidie kuziona tabia zangu na mwenendo wangu vinavyohitaji mabadiliko na kuongeza tabia na mwenendo ambao utakuletea wewe utukufu

Ninataka nizae matunda kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma 1 Wakorintho 13. Sura hii inaelezea maisha ya mtu ambaye ana upendo anaopaswa kuwa nao kwa ajili ya watu wengine. Acha Mungu akuonyeshe ni kwa jinsi gani anataka akubadilishe na ayafanye maisha yako yaendane zaidi na upendo. Orodhesha mabadiliko ambayo ungependelea kuyaona wewe mwenyewe.

# Somo la 8
# Kujifunza Biblia katika ibada binafsi

## Wazo Kuu

“Neno la Mungu kila siku huleta matokeo kwenye maisha na imani yangu.”

## Malengo ya Somo

Kujifunza binafsi sababu zilizo sahihi na njia sahihi kwa kujifunza Biblia.

## Utangulizi

► Je, kwa nini Wakristo wanapaswa kusoma Biblia kila siku?

► Je, kwa nini ni vigumu kwa baadhi ya watu kujifunza Biblia kila siku?

## Sababu za Kujifunza Biblia

### (1) Kwa ajili ya uhusiano wetu na Mungu

Zaburi ya 119, ambayo ndiyo sura ndefu kuliko zote katika Biblia, inataja Neno la Mungu takribani katika kila mstari. Inasema kwamba Neno la Mungu ni ufunuo wa asili ya Mungu mwenyewe na, kwa hiyo, Maandiko ndiyo njia ya kumjua Mungu

Sababu nyingine za ziada za kujifunza Biblia zimetolewa katika 2 Timotheo 3:16:

> Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.

Kutokana na mstari huu tunatambua kwamba tunapaswa tutafakari Biblia.

### (2) Kujua na kuuamini ukweli.

Hii inaweza ikawa ndiyo sababu ya watu kujifunza Biblia ambazo watu wengi wanazifikiria kwanza. Ni muhimu. “fundisho la Imani” yanarejea kwenye ukweli ambao tunaamini na kufundisha. Biblia ndio chanzo chetu cha mafundisho ya imani. Biblia inafunua asili ya Mungu, hali ya mwanadamu, na wokovu.

### (3) Kupata mwelekeo sahihi wa maisha

“Kukemea, kufanya marekebisho, na maelekezo yanayohusu haki” ni matendo ya Neno la Mungu ya kutuonesha sisi jinsi ya kuishi.

**(4) Kwa ajili ya ufanisi wa huduma**

“Kukemea, kufanya marekebisho, na maelekezo yanayohusu haki” havitokei tu kwenye kujifunza Biblia kibinafsi, bali wakati tunapolitumia Neno la Mungu katika kuwahudumia watu wengine.

> Ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema (2 Timotheo 3:17).

**(5) Kwa ajili ya ukomavu wa kiroho**

> Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga (Waebrania 5:12-13).

Kadri mtu anavyoendelea kutambua ukweli unaotoka katika Neno la Mungu, ndivyo anavyoendelea kukua na kuongeza uwezo wake wa kutumia Neno la Mungu katika kuwafundisha watu wengine.

**Malengo Yasiyofaa kwenye Kujifunza Biblia katika ibada binafsi ya**

1. **Kubuni tafsiri mpya.** Watu wengine hutafuta tafsiri za ajabu, mpya, zenye usaidizi mdogo sana unaoweza kuunga mkono kwenye Andiko. Tunapaswa kuwa wabunifu katika kutumia na kuwasilisha Andiko, lakini siyo katika kulitafsiri. Chochote Andiko linachomaanisha ndicho kinachomaanishwa, na hatupaswi kuunda maana yetu nyingine tofauti na ile iliyoko kwenye hilo Andiko.

   “Uwezo mkubwa wa Maandiko usio na ukomo hauko katika kutoa maana nyingi” (John Calvin).

2. **Kukusanya ushahidi kwa ajili ya midahalo.** Wakati mwingine Biblia inatakiwa itumike mahali penye utata, na ni muhimu kujifunza kwa kusudi hilo. Hata hivyo, hili siyo kusudi la kujifunza Biblia. Kama mtu atasoma Biblia ili kujenga tu hoja ya ushindani, hupata maono potovu na anaweza kuona tu kile anachotaka yeye kukiona.

3. **Kutiwa moyo.** Ni kweli, tunataka Biblia iwe endelevu katika kudumisha kutiwa moyo na furaha, lakini siyo kila aya iliyoandikwa inayoleta hisia za furaha. Makusudi ya Maandiko yanahusisha pamoja na mafundisho ya imani, kuonya, kufanya marekebisho, na kuadibisha katika haki. Kama mtu atakuwa anapitia vifungu kwa haraka akiwa anatafuta huko aya za kukidhi hisia zake, anakuwa haipi nafasi Biblia izungumzie ujumbe wake wote.

**Kama mtu atakuwa anapuuzia kujifunza Biblia, inawezekana kuwa hana sababu sahihi za kujifunza, zilizoorodheshwa kwanza katika somo hili. Kama hana sababu sahihi za kujifunza, anaweza kujihisi kwamba kujifunza kwake hakufanikiwi au hakukuwa na thamani yeyote.**

## Jinsi ya Kujifunza Biblia katika ibada binafsi

### (1) Anza kuomba kwa ajili ya kupata ufahamu wa kifungu.

Andaa moyo wako kupokea ujumbe kamili ulioko kwenye kifungu. Hujifunzi tu kujua mapenzi ya Mungu, bali kutendea kazi. Maombi yako ya mwanzo yanakuandaa wewe siyo tu kuelewa bali ni pamoja na kuwa mtiifu.

### (2) Tafsiri kifungu.

Aya inasema nini hasa? Toa muhtasari wa aya na orodhesha maelezo. Hakikisha tafsiri yako inalingana na aya zilizotangulia na zinazofuata baada ya aya hiyo. Hakikisha hitimisho lako halipingani na mafundisho ya kimaandiko yaliyo wazi mahali pengine. Zingatia ni jinsi gani wasomaji wa wakati huo waliielewaje aya hiyo.

### (3) Tumia kifungu hicho wewe binafsi.

- Je, kuna dhambi yeyote ya kutubu au kishawishi cha kuepuka?
- Je, kuna ahadi yeyote ya kudai?
- Je, kuna tabia yeyote inayotakiwa ibadilishwe?
- Je, kuna agizo lolote linalotakiwa kutii?
- Je, kuna mfano wowote unaotakiwa kuigwa?
- Je, kuna maombi yeyote ya kuomba?
- Je, kuna tatizo lolote la kukwepa?
- Je, kuna jaribu lolote la kuepukana nalo?
- Je, kuna jinsi yeyote ya kumtukuza Mungu kwa ajili ya haya?

Inawezekana kukawepo na mengine zaidi ya haya katika kifungu.

### (4) Omba kwa ajili ya kutimiza ukweli ndani yako.

Omba Mungu afanye mabadiliko yanayohitajika ndani ya moyo wako na katika maisha yako.

### (5) Maombi huamua utakachobadili kutokana na matumizi haya.

Mabadiliko maalumu yanapaswa yawe:

- **Binafsi** – kitu ambacho wewe mwenyewe unataka kifanyike.
- **Kwa vitendo** – siyo tu kinadharia, bali chenye matokeo katika kitu ambacho kwa uhakika kinatakiwa kifanyike.
- **Kuwajibika** – kuwajibika ndani ya muda uliowekwa kwa ajili ya utekelezaji.

Mifano: Siyo kwamba, “Ninahitaji kuomba zaidi,” bali, “Nitatenga muda wangu wa saa 12:00 kila asubuhi kwa ajili ya kuomba.” Siyo kwamba, “Nahitaji kuwatia watu moyo,” lakini, “ leo nitamtia moyo na kumsaidia binamu yangu ambaye yuko katika mazingira magumu."

Wakati mwingine hatuwezi moja kwa moja katika hali fulani za maisha yetu kufanya kwa namna iliyo mahsusi sana, lakini tunapaswa siku zote tuangalie njia za kutumia ukweli wa Mungu katika matendo na mitazamo yetu.

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

► Tulizungumza juu ya faida za masomo ya ibada binafsi. Je, kuna faida yoyote ambayo hukufikiria hapo awali?

► Kuna sababu gani ya Kujifunza Biblia ambayo itakuwa muhimu sana kwako?

Kama Mkristo ataziangalia njia hizi zinazotakiwa zitumike, kama zile zilizoorodheshwa kwenye hatua ya 3, na akajikabidhi kabisa kufanya mabadiliko kwa uhakika kama ilivyoelezwa kwenye hatua ya 5, maisha yake yataanza kuonyesha maendeleo makubwa sana.

► Kama umeanza kutumia Biblia kwenye maisha yako kwa njia hii kila siku, je, unadhani ni kwa jinsi gani italeta kwako uzito unaostahili?”

*Waombe washiriki wajitolee kufuata hatua hizi za kujifunza Biblia kila siku, angalau kwa wiki moja kisha uandae ripoti. Chukua kumbukumbu kwa ajili ya kuwauliza kuhusu matokeo yao.*

### Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya hazina uliyotupa sisi katika Maandiko.

Asante kwa kutufunulia sisi ukweli kuhusu jinsi ya kukujua wewe, jinsi ya kuishi, na jinsi ya kuwasaidia watu wengine

Nisaidie mimi katika kujifunza Neno lako kwa juhudi zaidi. Nipe ufahamu wa kuelewa kuhusu ukweli unaoufunua. Naomba unisaidie mimi niweze kuishi kwenye ukweli huo kwa uaminifu.

Amina.

### Kazi ya Kufanya

Tafakari 1 Wathesalonike 5, ukifuata hatua za Kujifunza Biblia katika ibada binafsi zilizoorodheshwa katika somo hili. Elezea matumizi yako binafsi uliyogundua ya kutumia njia hizi.

# Somo la 9
# Kuomba kama Daudi

## Wazo Kuu

"Kuzungumza na Mungu kunafanya kila sehemu ya maisha yangu iwe na maana sahihi."

## Malengo ya Somo

Kujifunza kwamba maombi ni kushirikisha matukio yetu yote na hisia zetu pamoja na Mungu na kukubaliana na mtazamo wake.

## Maombi: Kuzungumza na Mungu

Zaburi nyingi ni maombi. Nyingi ya hizo zimeandikwa na Daudi.

► Je, ulishawahi kujua kwamba kwenye mojawapo ya Zaburi mwandishi alimwomba Mungu kwa ajili ya mtu avunjwe meno? Je ulishawahi kugundua wakati wowote mambo ambayo kwenye Zaburi ni magumu kuyaelewa?

Zaburi inatueleza sisi jambo fulani muhimu kuhusiana na maombi.

Maombi ni kuzungumza na Mungu, na kuzungumza kuna umuhimu wake. Ule ukweli kwamba kuzungumza kunaendelea ni jambo muhimu sana. Ukweli kwamba watu wengine wanaweza wasitake kuzungumza na watu wengine kunaonyesha kwamba kuzungumza kwenyewe ndani yake kuna umuhimu wake.

Kwenye suluhu iliyoitishwa kwa ajili ya kuzuia kuzuka kwa vita, kiongozi mmoja alisema "Wakati watu wanapoishiwa maneno ya kuzungumza, wanakimbilia silaha zao; tuombe kwamba tunaweza kuwafanya waingie kwenye mazungumzo." Alitambua kwamba wakati wenye kufanya mazungumzo ya usuluhishi watakapoacha kuzungumza, inamaanisha kwamba watakuwa wameshindwa kufikia kwenye muafaka.

Kama ukiacha kuzungumza na Mungu au kama hutaki kuzungumzia kuhusu baadhi ya mambo, inawezekana ikawa ni kwa sababu unafikiria kwamba huwezi ukakubaliana na yeye katika mambo hayo.

Zaburi imekuwa ni maarufu sana kwenye matumizi ya maombi binafsi ya ibada, lakini kuna mambo mengine ambayo yamekuwa ni magumu kueleweka. Je, tunapaswa tufikirie nini kuhusiana na aya ambayo inamwomba Mungu kuvunja mkono wa mtu (Zaburi 10:15) au aya inayomwomba Mungu ang'oe meno yao (Zaburi 58:6)?

Zaburi inadhihirisha kwamba tunapaswa tuwe tunazungumza na Mungu kuhusu kila kitu kinachohusiana na maisha yetu na chochote tunachojisikia. Kuna mambo katika Zaburi ambayo yanaweza kuonekana yanatisha kama tutakuwa tunayafikiria kama maombi ya

kawaida yanayohusiana na kawaida za kidini. Lakini, kama tutakumbuka kwamba tunapaswa kuzungumza na Mungu kuhusiana na kila kitu, kisha ndipo tutakapoweza kutegemea kwamba mambo hayo yapo.

Je ni kwa nini tuwe tunazungumza na Mungu kuhusu kila kitu? Ni kwa sababu unachokuwa unazungumzia kitakuwa kinaonyesha nafasi yako ya uhusiano wako.

Uhusiano ni kushirikishana maisha. Kwa ujumla tunacho kikomo cha mahusiano ya kibinadamu. Kuna watu ambao unafanya kazi nao, na ukiwa pamoja nao labda unawashirikisha tu kipengele kimoja cha maisha. Kwa sababu hiyo, kuna mambo mengi sana ambayo huzungumzii habari zake.

► Kuna mtu yeyote ambaye hivi karibuni alishawahi kuwa kwa daktari au mtaalamu wa meno? Je, uliwahi kumzungumzia kuhusu hali yako ya kifedha? Je, ulizungumzia kuhusu matatizo ya familia yako? Je, uliwahi kuzungumzia kuhusu matatizo ya kifedha au yanayohusiana na familia yake?

Ukiwa pamoja na daktari wako, unashirikisha kipengele kimoja tu cha maisha na kukizungumzia. Siyo jambo la kawaida ukiwa na daktari wako kuwa na mazungumzo binafsi yasiyohusiana na hali yako kiafya. Hiyo ni kwa sababu uhusiano wako na yeye una kikomo; unahusiana na kipengele kimoja tu cha maisha yako.

Je, huwa unazungumza nini na Mungu? Je, kuna baadhi ya aina za mambo unayozungumzia? Je, unamchukulia Mungu kama mtaalamu (mfano: kama daktari, fundi wa vyuma, au fundi bomba) ambaye unampelekea aina kadhaa za matatizo yako? Je, unauweka uhusiano wako na Mungu kwenye eneo moja linaloitwa "Ukanda wa kidini?" Kwa nini hutaki kumshirikisha Mungu vipengele vingine vya maisha yako?

Kama huna mambo mengi ya kuzungumza na Mungu, uhusiano wako na Mungu ni mdogo na mdhaifu. Watu wengine huwa hawaongei na Mungu isipokuwa wakipata matatizo yanayomhitaji Mungu.

Vijana walio wengi wanadhani kuwa wakiwa kwenye mahusiano ya kimapenzi wanahitaji muda mwingi kuzungumza. Wanazungumza mambo mengi kuhusu wao, wakati wa kuzungumza juu ya kitu chochote, wanaelezea kitu kinachowahusu wao wenyewe, na kila mmoja akiwa anajifunza zaidi kutoka kwa mwenzake.

Wakati mwingine mambo hutokea kwenye uhusiano wenye mipika. Muda mwingine kwenye ndoa, mume na mke huwa hawana mazungumzo mengi. Kwa makusudi huwa hawazungumzii kuhusu mambo kadhaa. Uhusiano wao umefikia kikomo.

Je, vipi kuhusu uhusiano wako na Mungu? Ni dhaifu? kama hakuna mambo mengi ya kuzungumza na yeye. Inaweza kumaanisha kuwa unaona maeneo mengi ya maisha yako havina muunganiko na nafasi ya Mungu katika maisha yako.

Kwenye mahusiano baina ya watu, wakati mwingine baadhi ya mazungumzo fulani huwa na mipaka. Inaweza ikawa unataka mtu afanye jambo fulani, au kuacha kufanya jambo

fulani lakini yeye hayuko tayari. Baada ya kuwa limejadiliwa mara kwa mara, mada hiyo inakuwa nyeti, na hakuna mtu anayeileta isipokuwa anataka kuanzisha mabishano.

Wakati mwingine mtu hataki kuzungumza na Mungu kuhusu jambo fulani, kwa kuwa tayari anajua mapenzi ya Mungu na hayuko tayari kuyakubali. Nini itatokea kwenye uhusiano wako na Mungu kama utaendelea kukataa kufanya kile ambalo Mungu anakutaka ufanye?

► Je, ni nini hufanya uhusiano uendelee kukua?

Uhusiano hukua pale watu wanavyojifunza zaidi na kadri kila mmoja anavyofanya marekebisho. Uhusiano hukoma kukua inapoonekana hakuna kitu chochote cha maana cha kujifunza kwa mwingine au watu wanapoacha kufanya marekebisho. Tunaweza kuendelea kumjua zaidi Mungu, lakini hahitaji kubadilika. Lazima tuwe na utayari kuendelea kubadilishwa kwenye uhusiano wetu pamoja naye.

Zaburi inaonyesha kwamba kila sehemu ya maisha yetu inapaswa ijumuishwe na uhusiano wetu na Mungu, kwa kuwa waandishi wa Zaburi walieleza kupitia maombi hisia zao kuhusu kila kitu kilichowatokea.

Mbali na yale mambo yote ambayo watu kwa kawaida wanayaombea, Zaburi ina mambo mengine ambayo yanaonekana hayafai kwa maombi.

Vipi kuhusu hasira juu ya watu na nia ya kulipiza kisasi? Maombi haya ni ya kumwita Mungu ili aonyeshe kuwa yeye ni Mungu mwenye haki. Ni sahihi mtu kuwa na hisia zote tunazoziona katika Zaburi? Labda sivyo, lakini vipi ikiwa mtu anahisi hivyo? Anapaswa afanye nini? Je, kuzungumza na Mungu kuhusu jambo hilo halitakuwa ni jambo zuri la kufanya? Anapaswa ampe Mungu nafasi ya kujibu hisia zake. Hilo litakuwa ni bora zaidi kuliko kuchukua maamuzi yasiyofaa.

Vipi inapoonekana kwamba Mungu hakusaidii kama ambavyo angepaswa afanye? Baadhi ya Zaburi zinamwuliza Mungu, "Kwa nini unasimama mbali na mimi; kwa nini unajificha nisikuone wakati ninapokuhitaji?"[3] Ni kweli Mungu anafanya hivyo? Tunajua kuwa Mungu ni mwaminifu, lakini wakati mwingine huwa hatuelewi kwa nini hafanyi jambo tunalofikiri anapaswa kufanya. Ni kosa kufikiri kwamba Mungu siyo mwaminifu; lakini kama unafikiria hivyo, je, jambo zuri zaidi la kufanya ni lipi? Zungumza naye kuhusiana na jambo hilo. Mpatie nafasi ya kukuelezea. Atakusaidia katika kuona jinsi mambo yalivyo. Hilo ni jambo zuri zaidi kuliko kujaa hasira.

Je, ni sahihi kuomba kwa ajili ya kupatiwa haki yako pale watu wengine wanapokukosea? Je, ni sahihi kuomba kwa ajili ya kupatiwa thawabu wakati unapokuwa unafikiri kwamba unastahili zaidi ya kile unachopata? Je, ni sahihi kuomba kwa ajili ya kupatiwa msaada hata wakati unapojitambua kwamba unastahili kuwa kwenye hali ambayo umejiingiza

[3] Imetafsiriwa kutoka katika Zaburi ya 13:1.

mwenyewe? Maombi haya yote yako kwenye Zaburi. Zaburi inatuonyesha kwamba tunapaswa tumwendee Mungu kwa kila kitu.

Kama tutakuwa tunao uhusiano na Mungu ambao hauna ukomo, anakuwa anashirikishana nasi kila sehemu ya maisha yetu; kila kitu kimetengwa kwa ajili yake. Hii inamaanisha kwamba katika maisha yetu tunapata maana halisia kutoka kwa Mungu. Mambo tuliyo nayo ni muhimu tu kwa jinsi anavyoyaona yeye mwenyewe. Tunapaswa tuelewe mambo yanayotendeka kwetu kupitia nuru ya huo uhusiano.

Kila kitu kinapata mahali pake panapofaa na kupata thamani yake kikiletwa kwa Mungu kwa ajili ya marekebisho. Endapo huombei kila kitu, baada ya muda mambo mengi hayatakaa vizuri. Hisia zitakosa uwiano. Maamuzi yatakuwa potofu. Mitazamo itakuwa haiendani. Utaanza kukata tamaa pamoja na kuwa na uchungu.

Mtu mwenye huzuni, wasiwasi, aliyechanganyikwa na mwenye uchungu kwa watu wengine, au hata katika kufanikiwa na kujielekeza vibaya – huyu hapeleki kila kitu kwa Mungu kama anavyopaswa. Mtu mwenye wasiwasi sana haombi vya kutosha; mtu anayeomba sana, hana wasiwasi sana.

Gita ni lazima lipangwe sauti mara kwa mara, hasa ikiwa linabebwa, kugongwa, kuangushwa, kukanyagwa au kutupwa. Sisi tuko kama gita. Tunahitaji mpangilio wa kila mara ambao Mungu hutupatia tunapojielekeza kwake.

Mungu yuko karibu na wale wenye roho ya kupondeka (Zaburi 34:18). Ni lazima tuwe wapole na wanyenyekevu, tukipeleka mambo yote kwa Mungu na kumwachia ajibu kwa njia yake anayotaka mwenyewe. Tunaweza tukatafsiri mambo kwa usahihi wakati tukiwa tumeyawakilisha kwa Mungu kwa ajili ya yeye kujibu.

► Je, ni mambo gani unazungumza naye? Je, ni mambo gani ambayo wewe unahitaji kuzungumza naye?

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Tumia baadhi ya maswali yafuatayo katika kuimarisha ushirikishwaji:*

► Je, ulishawahi kujaribiwa kuwa na hasira juu ya Mungu?

► Je, ulishawahi kujisikia kwamba Mungu anapaswa afanye kitu kwa njia tofauti kabisa?

► Je, ulishawahi kuwa na badiliko la tabia inayohusu jambo fulani wakati ukiwa katika kuiombea hali hiyo?

► Je, unaweza kufikiria maeneo kadhaa ya maisha yako ambayo unakwepa kuzungumza na Mungu kwa ajili ya hayo? Kwa nini?

► Je, kuna maeneo katika maisha yako ambayo kwa uhakika hujawahi kufikiria kuomba kwa ajili yake?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninataka niweke thamani halisi ya kila kitu nilicho nacho na maana ya kila kitu ambacho kinanitokea mimi katika maisha yangu. Ninataka niweke hisia zangu zinazohusiana na kila kitu kwa ajili ya marekebisho yako.

Naomba unisaidie mimi kufunua kwako sehemu zote za maisha yangu.

Ninataka nijitoe moja kwa moja kwako. Ninataka uhusiano wangu na wewe uhusishe kila kitu kinachohusiana na mimi.

Naomba unisaidie katika kuendelea kubadilishwa kwa kukujua wewe vizuri zaidi.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari Zaburi ya 34. Andika aya moja inayohusu ujasiri wa Daudi kwamba kila kitu kinaweza kikawakilishwa kwa Mungu. Zingatia hasa aya za 15 na 18.

# Somo la 10
# Kusafisha Imani

## Wazo Kuu

"Ninakua kiroho kadri imani yangu inavostahimili majaribu."

## Malengo la Somo

Aina saba za majaribu zinazoinua imani yetu.

## Majaribu ya Imani

► Je, kuna mtu yeyote alikuwa na wakati mgumu hivi karibuni?

► umewahi kujiuliza kwanini huwa nyakati ngumu zinakuja?

Sisi sote tunakuwa na wakati wa kupitia katika nyakati ngumu, na hutokea mara chache katika maisha yako ambapo utapaswa kupitia katika mazingira magumu sana.

Maelezo kuhusu ni kwa nini nyakati ngumu katika maisha ni za thamani yametolewa katika 1 Petro 1:6-7.

> Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo.

Dhahabu huwa inapitia katika mchakato mkali wa kuisafisha kwa sababu ya thamani iliyo nayo. Mkaa hupimwa kwa tani; dhahabu hupimwa kwa kilogramu.

Imani ina thamani zaidi ya hapo, na kwa hiyo, inastahili kusafishwa.

► Je, Imani ni nini?

Wakati mwingine watu hunukuu Waebrania 11:1 kama ufafanuzi wa imani: "Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana."

Inawezekana kukawepo na imani za aina nyingi. Lakini kuna aina moja ambayo ni ya msingi katika imani zote, na ambayo ni muhimu kwa ajili ya uhusiano wetu na Mungu.

Aya katika Waebrania 11 inatupa mwendelezo zaidi wa tafsiri ya imani:

> Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao (Waebrania 11:6).

Imani ya msingi zaidi kuliko nyingine ni kuamini kwamba Mungu huwajibu wale wote wamtafutao kwa njia iliyo sahihi. Ni kuamini kwamba thawabu ya Mungu inapatikana na ni yenye thamani zaidi sana kuliko kitu kingine chochote.

Imani hupimwa wakati wa majaribu. Kwenye kipindi cha majaribu, tunakuwa na mashaka kuwa Mungu atafanya kitu chema kwa ajili yetu. Tunajaribiwa tunafikiria vitendo vingine nje ya mpango na mapenzi ya Mungu ndivyo tunavyohitajika kuvifanya.

Kutokutii ni kinyume cha kutafuta kwa bidii baraka za Mungu kwa sababu ya imani. Mtu anaamua kutokumtii Mungu kwa sababu ya ukosefu wa imani. Wakati mtu anapokuwa na mwenendo au tabia chafu dhidi ya Mungu, hiyo pia ni kukosa imani kwa sababu ni kutomwamini Mungu.

Kila jaribu ni jaribio la imani. Na jaribu la kukufanya uache Imani yako na kuwaza kufanya matendo mabaya au ukubaliane na mitazamo badala ya kumwamini Mungu. Imani ni ushindi juu ya kila jaribu, kwa imani tunamwamini Mungu na kuendelea kutafuta mapenzi yake kwa maombi na kutii.

> Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu (1 Yohana 5:4).

Mwelekeo wa dunia uko kinyume na Mungu. Dunia hujaribu kufanya mambo yaonekane kuwa kinyume na ukweli halisi, kufanya mambo mabaya yaonekane kwamba ni mambo ya kawaida. Kwa imani, Tunakumbuka kwamba Mungu ni mtoaji wa thawabu kwa wale wanaomtafuta kwa bidii. Kwahiyo, kila jaribu ni jaribu la imani; imani ni ushindi juu ya kila jaribu.

Majaribu ya imani hutuharibu wakati tunaposalimisha imani yetu, lakini yanatupatia faida kama imani yetu itaendelea kuwa endelevu. Imani yetu huongezeka na kufanyika yenye nguvu zaidi kwa kustahimili majaribu. Hiyo ndiyo sababu mojawapo ya Mungu kuruhusu majaribu yawepo kwetu. Yanaruhusu kuwepo kwa mchakato wa yale tunayohitaji.

> Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno (Yakobo 1:2-4).

Majaribu ya imani hukuza uvumilivu. Uvumilivu haumaanishi tu kwamba ni utayari wa kusubiri. Kuwa na uvumilivu inamaanisha ni kuendelea au kusonga mbele kwa imani. Yakobo aliendelea kusema zaidi kwamba, "Mmesikia habari ya subira yake Ayubu" (Yakobo 5:11). Ayubu alikuwa amechanganyikiwa na baadhi ya mambo, lakini aliendelea kushikamana na imani yake iliyokuwa katika Mungu mbali ya majanga na mazingira magumu yaliyokuwepo (Ayubu 2:9-10, 42:7).

Uvumilivu huleta sifa zote zinazohitajika kwa Mkristo. Kuendelea kuwa katika imani kunatukamilisha kabisa na kutuwezesha kiroho. Kama mtu ataendelea kujiweka kwenye

hali ya kutoamini, hataweza kukua katika imani. Siyo tu kwamba hataweza kuongezeka katika uvumilivu, lakini pia hataweza kuongezeka katika upendo, uaminifu, kujitawala, na kuwa na sifa nyingine ambazo anastahili kuwa nazo Mkristo. Ni kazi inayotokana na uvumilivu, na kuendelea katika imani, ambapo mwamini anajikuta "amekamilika kabisa, akiwa hajapungukiwa na chochote."

## Aina za Majaribu

Majaribu angalau yanaweza yakagawanywa kwenye aina saba.

1. **Mazingira magumu.** Jaribu la imani ni kipimo kilicho katika:
   - Kusababisha kuchanganyikiwa au hasira, na kukusababisha kukubaliana na tabia au mwenendo mbaya.
   - Kufanya haraka kubadilisha jambo au mazingira
   - Kutomtii Mungu kwa kurekebisha tatizo kwa njia zako mwenyewe.
2. **Kutokutenda haki na unyanyasaji.** Jaribu la imani ni jaribio la:
   - Kuwatendea watu wengine mabaya kwa sababu na wao wametenda mambo yaliyo mabaya.
   - Kutokuwa tayari kumgonja Mungu kutekeleza haki yake.
   - Kukataa kusamehe na kuonyesha upendo kama Kristo alivyofanya.
3. **Mateso ya kimwili.** Imani inaweza kuonekana kuwa haina uhai; bidii inaweza ikawa dhaifu. Jaribu la imani ni jaribio la:
   - Hisia za mfadhaiko huharibu Imani yako.
   - Kutafuta furaha au burudani nje ya mapenzi ya Mungu
4. **Msiba.** Misiba ni matukio ya kutisha ambayo huonekana kutuumiza. Jaribu la imani ni jaribio la
   - Kuwa na mashaka na upendo wa Mungu na wema wake.
   - Kuwa na shaka kuwa Mungu ndiye anayetawala.
5. **Mkanganyiko.** Jaribu la imani ni jaribu la kujitoa katika ufahamu wako dhidi ya mapenzi ya Mungu yanayojulikana.
6. **Mateso.** Mateso ni kipindi ambacho kinaonekana kwamba nguvu za giza za dunia za uovu zinatawala. Jaribu la imani ni jaribio la kukufanya uepukane na kuteseka.
7. **Jaribio la dhambi.** Jaribio la dhambi ni wakati ambapo dunia inatoa kitu fulani kinachoonekana kwamba ni bora zaidi kuliko furaha ya kiroho na zawadi ya uzima wa milele. Jaribu la imani ni jaribio la kukufanya uingie kwenye kivutio cha dhambi.

Kila kimojawapo katika haya huleta jaribu la kutia shaka katika kufuata mapenzi ya Mungu na kutafuta thawabu ya Mungu, ndiyo njia iliyo bora zaidi. Hiyo ndiyo sababu inakuwa ni jaribio la imani. Kama Mkristo ataendelea kutunza imani ya utii kwa Mungu bila ya kujali ni nini kinachotokea, imani yake itakua na nguvu sana kama itakapothibitishwa kwamba ni imani iliyo sahihi.

Mungu huwa anajua ukomo wetu. Wakati mtu anapoamua kukata tamaa, siyo kwamba katika ile hali ambayo alikuwa anapitia ilikuwa imepitiliza sana, lakini ni kwa sababu anafikiri kwamba hawezi akavumilia kile kinachokuja. Ndiyo maana mtu husema, "Siwezi nikaendelea kuvumilia zaidi," au "Siwezi nikaenda zaidi ya hapo." Anakata tamaa ya kuendelea ili aweze kuepukana na kitu anachofikiria kwamba kinakuja. Ikiwa tunaamini maarifa ya Mungu kwa ajili ya uwezo wetu na neema yake inayowezesha, tunaweza tukakabiliana na chochote kile ambacho kitajitokeza, tukitambua kwamba Mungu ataenda kutupa sisi ushindi.

> Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili (1 Wakorintho 10:13).

Jaribio la kufanana linaweza likajirudia mara nyingi. Kwa hiyo, kukubali kushindwa kwa muda hakutakusaidia wewe kuvuka. Tunakuwa na hali ya kufikiri kwamba baadhi ya majaribu ni ya kipekee, na kamwe hayawezi yakajirudia tena. Kwa ukweli hakuna jaribu la kipekee, na jaribu hilo hilo linaweza likajitokeza tena kwa njia nyingine tofauti kabisa. Kukosekana kwa imani kutakudhoofisha na kukufanya uwe na uwezekano wa kushindwa tena. Kushinda jaribu kutakuimarisha wewe kwenye jaribu lingine litakalofuata.

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Uliza watu baadhi kushirikisha kuhusu jaribu ambalo wamekuwa nalo katika siku za karibuni na matokeo yake yalikuwa ni nini. Waambie waeleze jinsi gani ilivyokuwa jaribu la imani. Watu wengine watataka kushirikisha ni majaribu gani wanayokabiliana nayo kwa sasa.*

► Je ni kitu gani unachohitaji kukumbuka ili kwamba uweze kuvumilia hili tatizo kwa imani?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kuwa nami kila siku, ukinisaidia katika kila jaribu. Naomba unisaidie imani yangu iweze kuwa na nguvu. Nisaidie mimi katika kukumbuka kwamba nyakati ngumu ni changamoto za imani, na kwamba imani yangu ni lazima iendelee kuvumilia.

Ninataka niendelee kukutii wewe haijalishi litatokea jambo gani. Nitaonyesha utiifu wangu kwa kukusikiliza wewe wakati wote.

Asante kwa ajili ya kuiendeleza imani yangu ambayo inatokea wakati unaponipitisha kwa ushindi katika majaribu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari Yakobo 5:7-11. Tambua sababu ambazo zimetolewa kwa ajili yetu kuweza kuvumilia katika imani. Manabii wanatajwa kama mifano. Je, ni watu gani unaowajua ambao waliweza kuvumilia mambo magumu kwa njia ya imani? Je, ingekuwaje kama hawangeweza kufanya hivyo?

# Somo la 11
# Kuanzisha Mazoezi ya Kiroho

## Wazo Kuu

"Ninatumia muda na juhudi katika kukuza uhusiano wangu na Mungu."

## Malengo ya Somo

Kuona ni kwa jinsi gani mambo kumi ya kufanya yanavyotusaidia kiroho.

## Utangulizi

► Je, ni kwa jinsi gani mwanariadha anaonyesha vipaumbele vyake? Vipi kuhusu mwanamuziki? Vipi kuhusu mwanafunzi?

Kwa yote haya, majibu yake yanafanana. Kwa kuwa wako makini sana na vipaumbele vyao, wanajiweka katika mazoezi yao wenyewe ili waweze kukua na kufanikiwa.

► Je, vipi kuhusu vipaumbele vya kiroho? Je, uhusiano wetu na Mungu unahitaji zoezi lolote la maana?

Mazoezi ya kiroho ni vitendo vya hiari ambavyo vimepangwa na kutunzwa kwa kusudi la kuhifadhi vipaumbele vya kiroho na kukuza uhusiano wetu na Mungu. Mifano wazi ya mazoezi hayo ni maombi ya kila siku, kusoma Biblia, na kuhudhuria katika ibada za kanisa. Ni lazima tupange, tutekeleze, na tuwekee utaratibu, kuliko kudhania kwamba vitajianzisha vyenyewe. Jambo lolote lenye thamani linahitaji kuwepo na vitendo vya mazoezi.

Matendo haya yanaweza yakaitwa "njia za neema" kwa mantiki kwamba Mungu amezifanya hizi kama mikondo ambayo itapitisha neema kama majibu ya imani yetu. Hawapati neema kwa njia ya kimawazo kana kwamba – kama dakika ishirini zitatumika kwenye maombi zitaweza kutengeneza kilo ishirini za neema. Badala yake, zina ufanisi tu wakati imani ya mwamini inadhihirishwa kupitia matendo haya. Kwa hiyo, kama mtu atakuwa anafanya kama taratibu tu za kawaida, hatapata mafanikio makubwa kutoka katika mazoezi haya.

Mazoezi ya kiroho hayatumiki kwa kusudi la kutufanya tuweze kukubalika na Mungu. Tunakubalika kwa sababu ya neema. Kama mtu hana uhakika na msamaha wa Mungu, hataweza kabisa kupata msamaha kupitia njia ya mazoezi ya kiroho.

## Baadhi ya mambo ya kutilia maanani kuhusu Mazoezi ya Kiroho.

- Ndizo njia za kuelekea kwenye lengo, na siyo kwamba zina malengo ndani yake zenyewe.
- Siyo vipimo kamili kabisa kwa ajili ya viwango vya kiroho.

- Haziwezi kuwa mbadala kwa ajili ya kumtii Mungu.
- Ni lazima ziwe za hiari kwa ajili ya kupata matokeo bora zaidi.

► Je, kwa nini mazoezi ya kiroho ni lazima yawe ya hiari kwa ajili ya kupata matokeo bora zaidi?

Kuna sababu kadhaa za ni kwa nini yanapaswa yawe ya hiari:

- Kwa sababu vipaumbele binafsi vya kweli vinawekwa kwa hiari. Kama mtu akikulazimisha kutekeleza kipaumbele, hicho ni kipaumbele chake yeye badala ya kuwa kipaumbele chako wewe.
- Kwa sababu uhusiano ulio katika misingi ya upendo huweza kukua kwa njia ya hiari tu.
- Kwa sababu neema hutolewa tu kama haya mazoezi yatadhihirisha imani ya mtu binafsi.

Ili kukuza mazoezi ya kiroho, kiongozi ni lazima aelezee faida zake kuliko kujaribu kuwalazimisha watu wazifanyie kazi.

### Orodha ya Mazoezi ya Kiroho

*Siyo muhimu sana kuangalia taarifa zote za marejeo zilizoainishwa katika sehemu hii ya somo. Kwenye kazi za kufanya mwanafunzi atatakiwa kuziangalia baadaye. Unaweza ukachagua baadhi ya taarifa za marejeo ili kuzipitia wakati somo likiwa linaendelea kwa kadri muda utakavyokuwa unaruhusu.*

1. **Maombi.** Kila Mkristo anapaswa awe na ratiba yake kwa ajili ya maombi ya kila siku.
2. **Kujifunza Biblia.** Zaburi ya 119 inaonyesha kazi inayofanywa na Neno la Mungu kwenye maisha ya mtu ya kuabudu.
3. **Kufunga kwa ajili ya maombi.** Mifano mikubwa sana katika historia nzima inaweka mfano wa Mungu kutoa majibu katika kufunga kwa ajili ya maombi. Biblia ina mifano mingi sana ya majibu ya Mungu kwenye kufunga kwa maombi. Yesu alitegemea kwamba wanafunzi wake watakuwa wanaendelea kufunga kwa ajili ya maombi baada ya huduma yake hapa duniani itakapokuwa imemalizika (Mathayo 9:15, Mathayo 6:16-18).
4. **Kuhudhuria ibada za Kanisa.** Waamini wanapaswa wakusanyike pamoja kwa ajili ya kuabudu, maombi, utakaso na kujifunza Maandiko (Waebrania 10:25).
5. **Meza ya Bwana/Ushirika Mtakatifu.** 1 Wakorintho 11:23-26 inaelezea zoezi la kanisa la Kristo katika desturi hii na kuonyesha kwamba kanisa liliendelea kuzingatia mapokeo haya.

6. **Uwajibikaji wa Kiroho.** Tunapaswa tuwe chini ya uongozi wa kiroho kutoka kwa mtu anayeongoza (Waebrania 13:17). Tunapaswa tuombe kwa pamoja kuhusu mahitaji yetu binafsi ya kiroho (Yakobo 5:16). Tunapaswa tuwe tunajua mahitaji ya marafiki zetu wa Kikristo ili kwamba tuweze kushirikishana nao mizigo yao (Wagalatia 6:2).

7. **Utoaji.** Waebrania 13:16 inatuambia tukumbuke kutenda mema na kutoa. 1 Wakorintho 16:2 Inaeleza kanisa likitoa matoleo ya kila wiki kwa ajili ya hitaji fulani. Msingi ya utowaji wa Zaka ni njia ambayo Mungu ametengeneza kwa ajili ya kuwasaidia wale walio katika huduma wakati wote.

8. **Huduma.** Mungu ametoa karama za kiroho kwa Wakristo kutumia ili kufaidiana (1 Wakorintho 12). Kila mtu ana nafasi ya huduma. Atafute wito wake na kuweka mipango mahususi ya kuutimiza.

9. **Kitabu cha kumbukumbu za kiroho.** Zoezi hili halijabainishwa katika Maandiko, lakini ni muhimu sana kukumbuka kazi ya Mungu (Zaburi 78:11). Kitabu cha kumbukumbu za kila siku kinaweza kuweka kumbukumbu za mambo magumu yaliyotokea, ushindi mbalimbali zilizopatikana, majibu ya maombi, matukio mbalimbali katika huduma, na masomo ya kiroho. Inawezekana pia ikawa kwa ajili ya kutunza orodha ya mahitaji ya maombi ili kuweza kuomba kwa lengo.

10. **Kujifunza Biblia katika ibada binafsi.** Mwamini anapaswa asome vitabu vinavyohusiana na maombi, mafundisho ya imani, na kukua kiroho.

Siyo jambo jema au la busara kwa mtu kuwa na majivuno kuhusiana na mazoezi yake. Hata hivyo, mtu hapaswi kupuuzia mazoezi ya kiroho ili kuweza kuepukana na majivuno, sawa na mwanamuziki asivyoweza kuacha kufanya mazoezi.

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

Sasa, Tumia fomu iliyotolewa mwishoni mwa somo hili kutoa ahadi kwa mazoezi haya ya kiroho.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie kudumisha mtazamo wangu juu ya vipaumbele vya kiroho kwa kutengeneza nafsi kwa nidhamu hizi za kiroho maishani mwangu.

Nisaidie kuwa mwaminifu katika kujitolea kwangu. Nilinde dhidi kiburi katika maendeleo yangu ya kiroho.

Naomba unisaidie kuwa mwaminifu na kwamba nidhamu yangu ya kiroho ni kuonyesha upendo wangu kwako na Imani yangu kwako.

Asante kwa ajili ya neema yako ambayo inafanya kazi ndani yangu juu ya mambo yote ambayo naweza kuyafanya.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Angalia taarifa zote za marejeo ambazo zilitolewa kwenye orodha ya mazoezi ya kiroho. Angalia kwa makini ni kwa jinsi gani mazoezi ya kiroho yanavyovungumziwa kuwa na uhai kwenye maisha ya Mkristo. (Hapo mwanzoni tulijifunza Zaburi ya 119, kwa hiyo siyo lazima kufanya tena marejeo yote ya sura hii katika wiki hii.)

**Ahadi Binafsi ya Mazoezi ya Kiroho.**

1. **Maombi.** Nitaomba kila siku saa __________ kwa dakika ____________.
2. **Kujifunza Biblia.** Nitajifunza Biblia kila siku saa __________. Nitafanya kipimo cha kujifunza kwangu ________________________________________ (kwa masaa au njia nyingine).
3. **Kufunga.** Nitafunga kila wiki siku ya ____________ kwa muda wa __________ (muda wa saa).
4. **Kuhudhuria ibada za Kanisa.** Nitahudhuria ibada za kanisa na mafunzo ya Biblia mara kwa mara:

   Siku ____________ Muda ____________

   Siku ____________ Muda ____________

   Siku ____________ Muda ____________
5. **Meza ya Bwana/Ushirika Mtakatifu.** Nitashiriki Meza ya Bwana au Meza ya Bwana inayotolewa kanisani kwangu, kila siku ya _____________ (kadiria muda).
6. **Uwajibikaji wa Kiroho.** Nitatoa taarifa ya hali yangu kiroho na kupokea maelekezo ya kiroho kutoka kwa _____________ (mwangalizi maalumu wa kiroho) kila siku ya_____________ (muda).
7. **Kutoa.** Nitatoa fungu langu katika _______________________________ (taja kanisa).
8. **Huduma.** Nitahudumu mara kwa mara kwa njia ifuatayo:
9. **Kumbukumbu za kiroho.** Nitatunza daftari ambalo nitasahihisha mara _______________ kwa wiki
10. **Masomo ya kujisomea katika ibada binafsi.** Nitafanya usomaji ufuatao wa ibada binafsi:

Tarehe ya kujitolea: ____________________

Itaendelea hadi: _______________________

Jina: __________________________________

# Somo la 12
# Kukubali Uwajibikaji wa Kiroho

## Wazo Kuu

“Mungu amenikuza katika jumuiya ya kiroho iliyokaribu nami.”

## Malengo la Somo

Kuona umuhimu wa mwingiliano na Wakristo wengine kwa ajili ya ukuaji wa kiroho.

## Utangulizi

Kazi muhimu hufanyiwa tathmini na mtu fulani. Tunapokuwa tunafanya kazi, tunajua kwamba tunahitajika tumridhishe yule ambaye tunafanya kazi kwa ajili yake. Tunapofanya kazi na watu, tunawataka wafikiri kuwa tunafanya kazi nzuri. Tunathamini maoni ya baadhi ya watu fulani kuhusiana na kazi yetu.

Maoni ya watu ni muhimu pia hata kwenye mahusiano. Kwenye kila uhusiano tunajifunza kurekebisha maadili na tabia zetu. Majibu ya watu wengine yanatuonyesha wakati wakiwa wamefurahishwa na wakati ambapo hawajafurahishwa.

Hata wakati tunapokuwa tunacheza mchezo tunakuwa tukifanyiwa tathmini. Kunakuwepo na masharti ya kufuata. Kucheza faulu, kutoka nje, au mikwaju inaweza ikahesabiwa. Wachezaji wengine na watazamaji hutoa maoni yao Pointi zinahesabiwa. Mafanikio yanashangiliwa, na makosa yanalaumiwa.

► Je, itatokea nini endapo mfanyakazi hatakuwa amejali kama wafanyakazi wenzake wanamwona kwamba anafanya kazi nzuri au laa?

► Je, nini kitatokea kwa mtu ambaye hajali watu wakimwona kuwa mkorofi?

► Je, unapendelea kucheza mchezo gani? Je, ni kwa jinsi gani masharti ya mchezo yanaleta athari ya jinsi unavyokuwa unaucheza mchezo huo?

Je, vipi kuhusu maisha yako ya kiroho? Je, tathmini kutoka kwa watu wengine ni muhimu? Je, kwako inakuwa ni jambo la kujali jinsi watu wengine wanavyofikiria kuhusu hali yako ya kiroho? Je, unajua marafiki wako wa karibu sana wanafikiria nini kuhusiana na hali yako ya kiroho? Je, uko tayari kufanyiwa tathmini na kujirekebisha kwa mujibu wa yale unayosikia? Je, unajua ni mahali gani unapoweza kupata tathmini iliyo sahihi?

Tunahitaji uwajibikaji wa kiroho.

Uwajibikaji wa kiroho unatupa sisi tathmini zilizo kamilifu na sahihi kutoka kwa watu ambao wanaweza kutusaidia sisi kujirekebisha na kukua kiroho.

Kuwa na uwajibikaji wa kiroho ni kuanzisha uhusiano na mtu au kikundi ambacho kinatoa mwelekeo wa kiroho.

Mtu ambaye ana uwajibikaji wa kiroho hutoa taarifa:

- Kuhusiana na hali yake ya kiroho.
- Kuhusu mafanikio na mapungufu yake kwenye nidhamu za kiroho.
- Kuhusu ahadi zake kwa siku zijazo.

## Kwa nini tunahitaji uwajibikaji wa Kiroho?

Bila ya kuwepo kwa uwajibikaji wa kiroho tutakuwa hatutekelezi amri za maandiko; tutakuwa tunapuuzia njia ambazo Mungu amezitengeneza kwa kutupa sisi neema kwa ajili ya ushindi na ukuaji wa kiroho.

> Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa… (Yakobo 5:16).

Mtu hawezi kukiri madhaifu yake ya ndani hadi awe kwenye uhusiano unaomwezesha apate urahisi wa kukiri. Kama atakuwa hatoi ukiri wa madhaifu yake kwa mtu ambaye anaweza kumwombea kwa ajili ya mambo aliyokosa, atakuwa anapuuzia njia ambayo Mungu ameiweka kwa ajili ya kukutana na mahitaji hayo. Baada ya maelekezo yaliyopo katika aya hii panatokea ahadi nyingine, "Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii."

> Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo (Wagalatia 6:2).

Hadi pale tutakapokuwa tunamfahamu mtu vizuri sana, hatutaweza kujua ni mizigo gani mizito mtu huyo amebeba. Watu wengi hawapendi kuelezea kuhusu mizigo yao mizito waliyobeba kwenye kusanyiko kubwa. Haiwezekani tukakamilisha amri hii ya kimaandiko bila ya kuwa kwenye uhusiano ambao utafanya hali hiyo iwezekane.

> Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri (Waebrania 10:24).

Tunapaswa tujipime kwa karibu sana sisi kwa sisi kwa nia ya upendo ili kuona wanahitaji vipi kutiwa moyo na ni karipio gani wanalohitaji. Kama hatuna uhusiano maalumu na mtu mwingine kutia moyo hakutakuwa vya kutosha, na karipio litapingwa.

> Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu… (Waebrania 13:17).

Wakristo wengi wanataka wawe huru na mamlaka yeyote ya kiroho. Wanajisikia kuwa huru kukataa maelekezo ya aina yeyote kutoka kwa mchungaji wao na watu wengine. Mungu anatutaka tuwe chini ya mamlaka ya kiroho. Mungu huteua watu wenye ukomavu na ufahamu kwa ajili ya kuwajibika na roho za watu wengine.

Jiulize maswali haya ya kujipima kama uwajibikaji wa kiroho umeanzishwa ndani ya maisha yako au laa.

Je, nina uhusiano gani ambao unasababisha kwamba…

- Mtu fulani ananisaidia katika kubeba mizigo yangu iliyo mikubwa sana?
- Ninakiri makosa yangu kwa mtu mwingine?
- Je ninamsaidia mtu mwingine mizigo yake?
- Kuna mtu anayewajibikia hali yangu ya sasa ya kiroho?

Je, ziko nyakati ambazo ninajihisi kwamba ninakosa aina hii ya uhusiano:

- Nyakati ambazo hakuna mtu yeyote ninayeweza kumtegemea?
- Ni wakati gani ninafurahi kwamba hakuna mtu anayejua hali yangu?
- Nyakati ambazo sitataka kutoa taarifa zangu za nidhamu za kiroho?

Je, kuna mtu ambaye ninakubali mamlaka yake ya kiroho:

- Je, ni wakati gani mimi niliwahi kuwa kwenye maelekezo yake?
- Je, ninasikiliza maonyo yake kuhusu hatari za kiroho zilizopo?

Tutafakari jinsi ya kuanzisha mahusiano ambayo yatawezesha uwajibikaji wa kiroho.

Uwajibikaji wa kiroho unafanya kazi vizuri zaidi wakati kukiwa na…

1. **Faragha.** Hutaki ushirikishwaji wa mambo yako uelezwe kwa watu wengine.

2. **Uhakika kwamba watu wengine wanakukubali na wanakujali.** Hutaki kujifunua kwa wale ambao wanaweza wakatumia madhaifu dhidi yako.

3. **Muda uliopangwa kwa ajili ya kushirikishana.** Usipopanga wakati maalumu wa kushirikishana unaweza kushindwa kushirikishana kirahisi katika kushirikishana.

Aina hii ya uwajibikaji wa kiroho unaweza kufanya kazi kati ya watu binafsi au kwenye kikundi kidogo.

Kuweza kumfanya mtu awajibike kiroho inamaanisha kwamba mara kwa mara unamwuliza…

- Je, unaendeleaje katika nidhamu za kiroho?
- Je, unao ushindi wa kiroho?
- Je, unafuatilia ahadi ulilizofanya hivi karibuni?
- Je, ni mambo gani maalumu yenye msimamo unayotaka kufanya kwa sababu ya ukweli uliojifunza hivi karibuni?

John Wesley alianzisha vikundi vidogo kwa ajili ya kuwapatia uwajibikaji wa kiroho. Walielezea kusudi lao na mtindo wao kama ifuatavyo:

"Kusudi la kukutana kwetu ni kwa ajili ya kuitii ile sheria ya Mungu, kwamba, 'Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa.'

Kwa ajili ya kusudi hili, tunakusudia…

1. Kukutana angalau mara moja kwa wiki.
2. Kufika kwa muda uliopangwa, isipokuwa hali isiyo ya kawaida izuie.
3. Kuanza wakati uleule uliokuwa umepangwa, kwa nyimbo na au maombi.
4. Kila mmoja kujieleza kwa uwazi na kwa uhuru hali halisi na ya ukweli iliyopo ya roho zetu, pamoja na madhaifu ambayo tumefanya kwa mawazo, maneno na matendo, na tamaa ambazo tumekuwa nazo tangu tulipokutana mara ya mwisho.
5. Kumaliza kila kikao kwa maombi, kulingana na mahitaji ya kila mtu aliyehudhuria.
6. Kumtaka mmoja aliyepo aeleze hali yake kwanza. Kisha kuwauliza wengine, mmoja mmoja, maswali mengi ya utafiti kadri itakavyowezekana, kuhusu hali zao za kiroho, dhambi na majaribu."

Vikundi vingi vidogo vimekuwa vikipata faida kwa kumtaka kila mwanachama kujiwekea malengo kwa ajili ya nidhamu binafsi za kiroho, kisha kutoa taarifa kila wiki ya mafanikio yake katika kuyafikia malengo hayo.

Vikundi vingine hujianzishia maagano ambayo kila mwanachama huweka msimamo wake hapo. Hapa kuna mfano wa agano la kikundi:

> Ninatoa agano langu la kukutanika na kikundi hiki kila wiki, kila itakapowezekana. Nitashirikisha kwa uaminifu matukio na hali yangu ya kiroho ya maisha yangu. Nitajitahidi kuwatia moyo, kutoa mwongozo na uwajibikaji kwa wanachama wenzangu. Nitaufungua moyo wangu kwenye ukweli unaobadilisha maisha wa Neno la Mungu. Nitahifadhi kabisa katika faragha mahitaji yote binafsi ya siri yanayoshirikishwa kwenye vikao vyetu hivi. Nitamwombea kila mwanachama wa kikundi changu kila siku. Nitajitoa kwa ajili ya kuwajibikia nidhamu za kiroho.

Mwamini anahitaji uwajibikaji wa kiroho, aidha uwe unatolewa na mtu binafsi aliyekomaa au kikundi. Hii ni njia mojawapo ambayo Mungu anaitumia kwa ajili ya kutupatia sisi neema.

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Waulize wanachama wa kikundi:*

► Je, unaona kuna hitaji binafsi kwa ajili ya uwajibikaji wa kiroho?

*Uliza baadhi ya maswali katika somo ambayo yatamsaidia mtu kutambua hitaji lake la kuwajibika.*

*Uliza kama wanafikiri kwamba wanatimiza maamrisho ya kibiblia ya uangalizi wa kiroho kwa kila mmoja.*

*Somo la 11 limeambatanishwa na fomu ya kuweka malengo ya mtu kwa ajili ya nidhamu binafsi za kiroho. Kikundi kitapaswa kujadili jinsi ya kutoa taarifa. Kwenye kikundi kidogo sana, wanachama wanaweza kutoa taarifa zao kwenye kikundi. Kikundi kikubwa kinaweza kikajigawa kwenye vikundi vidogo vya watu watatu kwa ajili ya upokeaji wa taarifa. Endapo wanachama wapya watajiunga na kikundi, usiwatake waanze kutoa taarifa mapema. Wanahitaji wapate muda wa kujihisi kwamba wako shwari na salama kwenye kikundi.*

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninataka niwe mwaminifu katika kutii amri zako zote katika Neno lako. Ninataka niwasaidie ndugu zangu wa kiume na kike katika kubeba mizigo yao; ninataka niweze kuwatia moyo; ninataka nikiri kwao madhaifu ya kushindwa kwangu ili waweze kuomba kwa ajili yangu.

Ninataka niwakubali viongozi wa kiroho ambao umewaweka kwa ajili ya kuwa waangalizi juu yangu.

Naomba unipe unyenyekevu unaohitajika kwa ajili ya kukiri makosa yangu na upendo ninaouhitaji kwa ajili ya kuwasaidia watu wengine katika madhaifu yao. Nisaidie nisiwe mtu wa hasira wakati ninapokuwa nikirekebishwa katika makosa yangu au ninapoumizwa wakati nikiwarekebisha wengine.

Asante kwa ajili ya familia ya kiroho ambayo umenipa kunisaidia mimi kwa ajili ya kukua kiroho

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Angalia katika Yakobo 5:16; Wagalatia 6:2; Waebrania 10:24, na Waebrania 13:17. Soma vifungu vinavyoshikamana na kila aya iliyoonyeshwa hapa. Jaribu kufikiria njia maalumu ambazo hivi karibuni umezitumia kutii maagizo hayo. Je, kuna hatua gani nyingine unazoweza kuzianzisha ili zikuwezeshe kuyatii maagizo hayo vizuri zaidi?

# Somo la 13
# Faida za Maombi

## Wazo Kuu

"Maombi ni mkondo wa baraka za Mungu."

## Malengo ya Somo

Kujifunza kuombea aina kumi na moja za baraka kutoka kwa Mungu.

## Utangulizi

► Je, kuna umuhimu wowote wa kuwa na orodha ya mambo ya kuombea?

► Je, kuna mtu anayeweza kuelezea jinsi unavyotumia orodha ya maombi?

Orodha ya maombi ni ya msaada sana kwa sababu inakukumbusha wewe juu ya mambo fulani unayotakiwa uyaombee. Watu wengi hupenda kuombea aina fulani za maombi lakini siyo kwa ajili ya watu wengine ambao pia ni muhimu.

Katika somo hili tunaangalia orodha ya faida za maombi. Kwa kuorodhesha faida za maombi, tutaenda kuona mambo ambayo tunapaswa tuwe tunayaombea.

## Sababu za Sisi Kuomba

Tunapaswa kuomba kwa ajili ya:

1. **Kumjua Mungu**. Fikiria unaye rafiki ambaye huwa hazungumzi na wewe ila tu anapokuwa na tatizo ya kukuomba kitu. Hayo ndiyo mahusiano ambayo watu wengi wanayo baina yao na Mungu. Hawaonyeshi shauku ya uhakika ya kumtafuta yeye. Maisha ya kufahamiana na Mungu asiye na kikomo yataendelea kuleta ufumbuzi endelevu wa mambo ya kushangaza.

2. **Kukua katika kufanana na Kristo/katika Utakatifu wa Kristo.** Jinsi tunavyomjua Mungu vizuri, tunapaswa kutaka kuwa kama yeye zaidi. Kwa kweli hatuwezi kumwabudu (ikimaanisha kumheshimu jinsi alivyo) huku tukiunganishwa kuhusu tabia za dhambi au uchafu wowote ndani yetu wenyewe. Ikiwa kweli tunamheshimu Mungu kwa kuwa upendo, mwenye huruma, mvumilivu, na aliye msafi, tunapaswa tutamani kuziona tabia hizi zikikua na au kuongezeka ndani yetu wenyewe.

3. **Wokovu na baraka kwa familia.** Baraka katika orodha hii zitakuja kwako lakini pia zitatiririka kwenda kwa wale walio karibu nawe. Afadhali kuwa na mtu mmoja mwenye utajiri wa maombi kuliko kuwa na mjomba tajiri. Manufaa mtakayoyapata kupitia maombi hayo hayana kipimo. Wewe uwe mtu huyu kwa ajili ya familia yako,

uwe mkondo ambayo kwayo baraka za Mungu hutiririka sababu ya maombi. Wataendelea hata vizazi vijavyo.

4. **Upako binafsi na upanuzi wa huduma.** Kila Mkristo anayo huduma. Siyo tu kama wachungaji na waalimu lakini kama wazazi, wanandoa, marafiki, waamini wenzako, mashuhuda, wafanyakazi, na raia wenzako. Baraka huja kwa kupitia kazi ya Roho Mtakatifu kwenye huduma zetu. Kipawa chako maalumu ulicho nacho hakitakuwa na matumizi kamili yaliyokusudiwa kama hakitapelekwa mbele za Mungu kwa ajili ya kupata mwelekeo, kuwezeshwa na Roho Mtakatifu, na kitumike kwa ajili ya utukufu wake. Tafuta umakini huo na ikuze kupitia maombi endelevu.

5. **Hekima, busana, na mwongozo.** Kwa sababu ya udhaifu, hatujui hata kuomba jinsi tunavyopaswa , lakini Roho Mtakatifu hutusaidia. Katika nyanja zote za maisha ni sawa. Ni makosa gani tungeweza kuepuka ikiwa tumetafuta utambuzi ambao Mungu hutoa? Hiyo haimaanishi kwamba tunapaswa tutafute ishara zisizokuwa za kawaida au kwa udanganyifu kufuata mawazo yasiyokuwa na maana, lakini acha Mungu atoe ufahamu wa hali kama anavyoziona yeye mwenyewe.

6. **Ufahamu wa Biblia.** Roho Mtakatifu huyo huyo ambaye aliivuvia Biblia huifunua kwetu kwa ajili ya kuifahamu wakati wa sasa. Kwenye maombi hatutafuti mafunuo mapya bali ufahamu mzuri zaidi wa kumjua Mungu na mapenzi yake yaliyofunuliwa kwenye Biblia. Hatusomi tu kwa ajili ya kujisikia tumebarikiwa, au kutiwa nguvu, bali kuruhusu kifungu kizungumze ujumbe wake uliopo kwa ajili ya maisha yetu.

7. **Mahitaji ya kifedha.** Tunaweza kuja kwa Mungu kuhusiana na mahitaji yetu, kwa sababu yeye ni Baba yetu. Kama Yesu alivyofundisha kwenye Sala ya Bwana, tunapaswa tumwulize Mungu awe mtoaji wetu wa kila siku. Tunaweza tukazungumza na Mungu kuhusu kila kitu tunachohitaji na hata vitu ambavyo tunataka, kwa kadri tutakavyokuwa tunakumbuka kwamba mwenyewe ataamua ni kitu gani kilicho chema kwa ajili yetu.

8. **Furaha na ukamilishaji.** Furaha ya Mungu ni nguvu, Ukandamizaji na kukata tamaa hutokana na ukosefu wa imani. Bila ya imani, hatutegemei kupata mambo makubwa kutoka kwa Mungu. Usijiachie kwenye kugandamizwa. Tafuta furaha kwenye uhusiano wako na Mungu zaidi sana kuliko mahali pengine popote.

9. **Kusudi na mpangilio katika maisha yetu.** Tunadhihirisha vizuri sana kipaumbele cha Mungu kwenye maisha yetu kupitia maombi. Wakati tunapomweka Mungu kuwa wa kwanza kwa kuyaweka maombi kuwa ya kwanza, maisha yote huchukua maana na mpangilio mpya. Tuna ufahamu wa kukamilisha kusudi la sisi kuwepo.

10. **Majibu maalumu na miujiza.** Majibu ya Mungu kwenye maombi yetu yote ni mwingiliano wa kimuujiza, lakini tunaona baadhi yake kuwa ni bora zaidi kuliko mengine. Hubadilisha mambo kutoka katika vile ambavyo ilitakiwa iwe. Kunapaswa kuwepo na nyakati ambazo tunatambua kwamba Mungu anatutaka sisi tumwamini

kwa ajili ya msaada maalumu. Tunapokuwa tumeyaelewa mapenzi ya Mungu kwenye hali fulani na kumtii yeye, hufanya miujiza kwa ajili yetu.

11. **Kuuendeleza ufalme wa Mungu kupitia umisheni.** Ufalme wa Mungu huendelezwa wakati mwenye dhambi anapotubu, kupokea neema, na kufanyika mmojawapo wa watu wa kumwabudu Mungu. Omba kwa ajili ya injili kuenea kwa ufanisi, siyo tu kwenye jumuiya yako, lakini pia mahali popote duniani, hasa zaidi sana mahali unapojua kwamba mmishenari yupo akiifanya kazi hiyo.

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

► Je, kuna jambo lolote katika haya ambalo hujawahi kuliombea?

► Je, unaona ni kwa nini unapaswa uyaombee mahitaji haya?

*Watake washiriki wajikabidhi kabisa katika kuombea kila siku orodha iliyoko hapa juu katika wiki ijayo.*

### Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunisaidia mimi kuona kwamba unataka kunibariki katika njia ambazo sijawahi kufikiria kabla ya hapo.

Naomba unisaidie ili maombi yangu yawe ni mkondo wa baraka zako kwa familia yangu na watu wengine wanaonizunguka.

Zaidi ya yote, ninataka nizungumze na wewe ili kwamba niweze kukujua wewe zaidi.

Asante Baba, kwa fadhila kubwa ya maombi.

Amina.

### Kazi ya Kufanya

Soma Zaburi 141-146. Zaburi zote hizi ni maombi. Angalia aina ya mambo ambayo yameombewa hapo. Angalia kauli ambazo zimetamkwa kuhusu Mungu kama sababu za kufanywa maombi.

# Somo la 14
# Kuomba kama Yesu

### Wazo Kuu

"Ninaomba vizuri ninapoona kile ambacho Mungu anataka kufanya."

### Malengo ya Somo

Kujifunza kutoka katika Sala ya Bwana umuhimu wa kuomba ili mapenzi ya Mungu yatimizwe.

### Utangulizi

► Kama ulikuwa unajiandaa kuwakilisha ombi lako kwa mtu fulani aliyeko kwenye mamlaka, ni mambo gani mazuri ambayo unatakiwa uyafahamu kabla ya muda wa kuwakilisha ombi lako kufika?

Itakusaidia kujua kama ni kitu gani anachokijali zaidi. Itakusaidia kujua malengo yake ni nini.

Yesu alitupa sisi taarifa hii kuhusiana na Baba yake. Kama tutajua ni nini ambacho Mungu anataka kufanya, tunaweza tukaomba sawasawa na mapenzi yake na tukajua kwamba atakwenda kujibu.

Sala ambayo tunaiita "Sala ya Bwana" ilikuwa ni jibu kutokana na ombi la wanafunzi, "Bwana, tufundishe kuomba."

### Shule ya chekechea ya Maombi

Sala hii ina maelekezo ya kwanza ya Yesu kwa wanafunzi wake kuhusiana na maombi, kwa hiyo kwenye shule ya maombi itakuwa kwenye kiwango cha shule ya chekechea ya maombi. Hiyo haimaanishi kwamba kamwe kuna muda wowote ambao kanuni zilizofundishwa katika sala hii zilionekana hazina umuhimu kwetu. Kwa mfano, kwenye mahesabu, ujumlishaji rahisi uliokuwa unafundishwa kwenye shule ya chekechea kamwe haujawahi kukosa umuhimu kwenye aljebra, kalkulasi, au jiometri. Mtu anayesahau kanuni za msingi za hesabu hawezi akafanya hesabu zilizo kwenye kiwango cha juu. Vivyo hivyo, kama mtu ni mjinga kwenye kanuni ambazo ni shule ya chekechea ya maombi, hawezi akaomba vizuri kama inavyostahili.

Ni jambo jema kwetu kuomba maneno haya mara kwa mara, kama Yesu alivyosema, na maombi yetu yote ni lazima yaendane na kanuni Yesu alizofundisha katika mtindo huu.

Yesu hakuanza somo lake la maombi kwa kuahidi kwamba Mungu atakwenda kuwapa kila kitu wanachoomba. Kama mtu hajui ni aina gani ya mambo anayotaka kuombea,

atakatishwa tamaa. Usije ukamwambie mtu kwamba anaweza akapata kila kitu akiomba. Katika vifungu vingine vya maandiko, Yesu alitoa ahadi kubwa kuhusu majibu ya maombi, lakini mtu anayeomba anahitaji kuelewa kile ambacho Mungu anataka kufanya.

Angalia katika Mathayo 6:9-13.

### Sala ya mfano

> Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe,
> Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.
> Utupe leo riziki yetu.
> Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.
> Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.
> Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele.
> Amina.

### Kanuni ya msingi ya Sala ya Bwana

Matumizi mengi yanaweza yakapatikana kutoka katika Sala ya Bwana, lakini kanuni moja inasimama: Kwamba tunapaswa tuombe kwa mtazamo wa Mungu, thamani, na malengo katika ufahamu.

Sala hii ina mpangilio wa mara tatu. Iko katika vifungu vitatu, na kila kifungu kimojawapo kiko katika sehemu tatu.

Utatu wa kwanza wa maombi ni: (1) Kwamba Jina la Mungu litukuzwe, (2) Kwamba ufalme wa Mungu uje, na (3) Kwamba mapenzi ya Mungu yatimizwe.

Maombi haya ni tofauti sana na yale mambo ambayo kwa kawaida yamejaza muda wetu wa maombi. Yanaonyesha inamaanisha nini kuomba kutokana na mtazamo wa kimbingu.

Sala ya Bwana inaweza ikafanyika kwa sekunde thelathini, lakini kamwe hatuna muda wa kuomba mambo yote yaliyoainishwa kwenye hiyo sala. Kuomba kwamba Jina la Mungu litukuzwe, au lipewe heshima, inaonyesha kwanza kabisa kwamba sisi wenyewe tunataka kumpa Mungu heshima. Tunaweza tukahitaji kupata kila kitu katika maisha yetu na mioyo yetu iwe inayoweza kumpa Mungu utukufu; vinginevyo, haitaleta maana kuomba kwamba jina lake litukuzwe. Tunaweza pia tukaomba kwa ajili ya wale watu wanaotuzunguka, kwamba waweze kumtukuza Mungu, ikimaanisha kwamba wenye dhambi watatubu na maisha yao yatabadilishwa yawe ya kumtukuza Mungu. Ni katika kuomba kwamba wale wanaoishi maisha ya uzembe, kana kwamba hakuna Mungu, wataanza kuishi wakiwa na heshima kwa Mungu ambayo watapaswa wawe nayo.

Kuomba kwa ajili ya ufalme wa Mungu uje ni kuomba mamlaka yake yaendelezwe ndani ya mioyo ya wanadamu. Kwa ufahamu ni kwamba, ufalme wa Mungu ni ulimwengu wote, na kwamba yeye ndiye aliye juu ya mambo yote. Lakini bado ziko mamlaka nyingine nyingi ndani ya ufalme huu ambazo ziko kwenye uasi dhidi ya mamlaka ya Mungu. Ufalme wa Mungu unaendelezwa kila wakati mtu aliyeasi anapojisalimisha kwa Mungu. Itakuwa ni

jambo la kejeli kwa mtu kuomba sala hii wakati akiwa anakusudia kutomtii Mungu. Tunapaswa kwanza tuombe kwa ajili ya ufalme wa Mungu kuja kabisa ndani ya mioyo yetu wenyewe, ndiposa uendelezwe kwa ajili ya watu wanaompinga Mungu waweze kujisalimisha kwake.

Kuomba kwamba mapenzi ya Mungu yatimizwe hapa duniani kama yanavyotimizwa mbinguni ni sawa na kuomba kwa ajili ya ufalme wa uje. Mtu hawezi akaomba kwa uaminifu wote wakati yeye mwenyewe hakusudii kumtii Mungu kabisa. Kamwe itakuwa haileti maana kuomba kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, kana kwamba ni kitu kizuri, wakati moyo wa mtu haujakubaliana na mapenzi ya Mungu. Kuomba hivi kwa uaminifu kutakuwa ni mwanzo wa kuomba kwa ajili ya moyo safi wa utakatifu.

Mwamini aliye na moyo safi wa utakatifu anapaswa awe na uwezo wa kuomba kwa ajili ya Mungu kupewa heshima, ufalme wake uje, na ukamilishwaji wa mapenzi yake kana kwamba hakuna kitu kingine kizuri zaidi kinachoweza kutendeka kuliko dunia kuwa sawasawa na vile Mungu anavyotaka iwe. Hiyo ni kuomba kutoka katika mtazamo wa kimbingu.

**Tulia kwa Kutafakari**

Je, unaamini kweli kwamba mapenzi ya Mungu ndiyo jambo bora zaidi linaloweza kufanywa ulimwenguni, mahali unapoishi na kufanya kazi, nyumbani kwako, na katika moyo wako?

**Kuombea mahitaji binafsi katika Sala ya Bwana**

Maombi yanayofuata kwa mara tatu ni kwa ajili ya mahitaji binafsi. Ni maombi kwa ajili ya mkate au riziki ya kila siku, msamaha, na ukombozi kutoka katika uovu.

Ombi la mkate au riziki ya kila siku linaweza kupanuliwa ili kujumuisha mahitaji yote ya kimsingi. Ukweli kwamba tunapaswa kuomba kwa ajili ya mahitaji ya kila siku inaonyesha kwamba Mungu anataka tuendelee kumtegemea yeye, kuliko kutegemea rasilimali tulizojilimbikizia. Ni vigumu kwa watu wengi kumtegemea Mungu ikiwa tayari wana kile wanachofikiri wanahitaji.

Maombi ya msamaha yanaonesha kwamba tunapungukiwa kuyajua mapenzi kamili ya Mungu na tunahitaji neema yake ya kila siku.

Kisha kunafuatia ombi la kwamba Mungu atulinde sisi kutokana na madhara yanayoletwa kwetu na Shetani, kimwili na kiroho kwa pamoja.

Sala inamalizia kwa mara tatu na sababu za kuomba kwa njia hiyo. Ufalme, na nguvu, na utukufu, vyote ni mali ya Mungu peke yake. Tunataka kila kitu kifanye kile kitu ambacho kiliumbiwa kwa kutimiza kusudi katika ufalme wa Mungu. Tunatambua kwamba ni nguvu ya Mungu pekee yenye uwezo wa kukamilisha kile tunachoombea. Utukufu wa ufalme na ushindi wake vyote ni mali ya Mungu.

Tunataka kila kipengele cha maisha yetu na huduma zetu ziendane sawasawa na mapenzi ya Mungu, ziwezeshwe na Mungu, na ziwe zinamletea Mungu utukufu. Tunaomba kwa ajili ya hilo na kujitoa kwa ajili ya hilo kusudi.

Hili ni somo la shule ya awali kwenye shule ya maombi. Inatoa msingi wote wa kuomba kwetu ambao kamwe hatupaswi kusahau.

Kanuni ya kuomba kama Yesu ni hii: Maombi yanatusababisha sisi kuona kila kitu kutoka katika mtazamo wa Mungu, kwa hiyo tunaweza tukaomba kwa ajili ya kitu kilicho chema kwenye macho ya Mungu.

**Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi**

*Shirikisha kuhusu mwelekeo wetu wa kuomba kutoka katika mtazamo wetu wenyewe; yaani, kuomba kwa kile kinachoonekana kwamba ni kizuri kwa ajili yetu.*

Maombi kwa ajili ya mapenzi ya Mungu na ufalme yanapaswa yaongoze kwenye utafiti wa ndani wa moyo, kama mtu anajidhania kwamba kwa uhakika anataka mapenzi ya Mungu yafanyike kwa ukamilifu kabisa katika maisha yake mwenyewe na aidha kama yuko tayari kukamilisha kabisa kufanya yaliyo mapenzi ya Mungu.

► Je, unaamini kwa ukweli kwamba mapenzi ya Mungu ni jambo lililo bora zaidi sana ambalo linaweza kufanyika katika ulimwengu, kwenye eneo unaloishi na kufanya kazi, nyumbani kwako, na ndani ya moyo wako?

Wanachama wanaweza wakatambua hitaji la kuomba kwa ajili ya mabadiliko ndani ya mioyo yao wenyewe ili waweze kuomba kwa ukweli katika mtazamo wa kimbingu.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Tunaomba kwamba jina lako liweze kupewa heshima; kwamba ufalme wako upate kuendelezwa; na wote wanaopingana na wewe waweze kujisalimisha kwako.

Tunaomba kwamba mapenzi yako yapate kutimizwa kabisa ndani ya ulimwengu huu, kwenye maeneo yetu ya kuishi, na ndani ya mioyo yetu.

Tunaomba utupatie mahitaji yetu ya kila siku.

Tunaomba utusamehe kwa ajili ya sisi kushindwa kuyatimiza kikamilifu mapenzi yako, na tusaidie katika kuwasamehe wale wote waliotukosea sisi.

Tulinde kutokana na kuanguka kwenye majaribu, na tulinde sisi kutokana na kitu chochote ambacho yule mwovu anaweza akakileta dhidi yetu

Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Iandike Sala ya Bwana, ukiacha nafasi chini ya kila mstari. Ipitie tena sala hiyo na orodhesha chini ya kila ombi maombi maalumu ambayo unaweza ukawa unayaombea kwa ajili ya kuweza kufahamu wewe binafsi jinsi ya kuitumia Sala ya Bwana.

# Somo la 15
# Fursa ya ushindi juu ya Dhambi

## Wazo Kuu

"Dhambi haiwezi ikanishinda mimi wakati nikiwa ninaruhusu nguvu za Mungu zitende kazi ndani yangu."

## Malengo ya Somo

Kutambua kwamba Mungu hutoa neema yake kwa ajili ya ushindi dhidi ya dhambi.

## Ushindi juu ya Dhambi

> Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli, Kwa kuwa amewajia watu wake, na kuwakomboa...Kama alivyosema tangu mwanzo kwa kinywa cha manabii wake watakatifu…kwamba tuokolewe na adui zetu… na ya kwamba atatujalia sisi, tuokoke mikononi mwa adui zetu, na kumwabudu pasipo hofu, kwa utakatifu na kwa haki mbele zake siku zetu zote (Imetolewa kutoka Luka 1:68-75).

► Je, adui yetu mkubwa sana ni nani?

Shetani hangeweza kuwa na nguvu juu yetu kama hatungekuwa watenda dhambi. Kamwe hatungeweza kutengwa na Mungu na kuwa chini ya hukumu yake kama hatungekuwa watenda dhambi. Dunia haingekuwa mahali pa migogoro na mateso kama siyo kwa ajili ya dhambi ya asili na utendaji wa dhambi mbalimbali unaoendelezwa.

Adui yetu mkubwa sana ni dhambi.

Mungu anatoa ahadi ya kututoa sisi kutoka katika nguvu ya maadui zetu ambazo zinatuondoa sisi katika kumtumikia yeye katika haki na utakatifu kila siku ya maisha yetu.

Waraka wa 1 Yohana unaweka msisitizo kwamba tabia kuu ya mwamini wa kweli ni ushindi dhidi ya dhambi. Tabia hii imetolewa kama msingi wa uhakikisho binafsi wa wokovu.

Mtume alitambua kwamba kuna nyakati ambapo mwamini atahitaji uhakikisho. Akaonyesha kwamba ni jambo lililo sahihi kwa mwamini kutafuta kuwa na ushuhuda ambao utakuwa ni msingi wa uhakikisho wake, kwa sababu baada ya kutoa ushuhuda ulio kwa ajili ya kusudi hilo, anasema hivi ndivyo tunavyoweza kuihakikisha mioyo yetu.

> Katika hili tutafahamu ya kwamba tu wa kweli, nasi tutaituliza mioyo yetu mbele zake (1 Yohana 3:19).

Yohana anatoa vigezo vingi kwa ajili ya kusudi hili – anaonyesha kwamba anatoa kigezo kwa kurudiarudia akisema, "Hivi ndivyo tunavyofahamu." Uhakikisho binafsi ni mojawapo

ya dhamira kuu ya waraka huu. Kwa hakika, Yohana alisema hiyo ndio iliyokuwa sababu yake ya kuandika:

> Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu (1 Yohana 5:13).

Kigezo kinachosisitizwa sana kwenye waraka huu ni ushindi dhidi ya dhambi. Hali ya kawaida ya mwamini ni ya uhuru wa kutoka katika dhambi.

> Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi… (1 Yohana 2:1a).

Hapa mtume anaonyesha kwamba mwamini anapaswa aishi pasipo kutenda dhambi, na anasema kwamba anawaandika ili kuwaonyesha umuhimu wa kuishi maisha ya ushindi

> … Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote (1 Yohana 2:1b-2).

Hapa anatambua kwamba dhambi inaweza ikatokea, ingawaje siyo lazima. Anatuthibitishia kwamba kama mwamini akitenda dhambi, dhabihu ya utakaso ("upatanisho") ya Kristo ina uwezo wa kututakasa kutokana na hiyo dhambi. Hatupaswi kudhania kwamba dhabihu hii moja kwa moja inatoa utakaso kwa mwamini wa zamani anapokuwa ametenda dhambi.

Aya inasema tu kwa wepesi kwamba dhabihu inapatikana, kama ilivyo kwa ajili ya ulimwengu wote. Tunajua kwamba ulimwengu wote hatujaokolewa moja kwa moja. Toba ni muhimu kwa ajili ya dhambi yeyote kuweza kusamehewa, aidha kama mwamini kwa wakati mmoja alikuwa ameokoka au laa.

Aya zinazofuata kutoka katika 1 Yohana zinaonyesha msisitizo wake kwamba tofauti kubwa sana iliyopo ya mwamini ni ushindi dhidi ya dhambi. Kifungu kilichoko kwenye mabano ni mawaidha yaliyoongezwa.

> Na katika hili twajua [huu ndio ushuhuda] ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake (2:3-4).
>
> Kila atendaye dhambi, [aidha alikuwa mwamini au hakuwa mwamini] afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi. Nanyi mnajua ya kuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake. Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua (3:4-6).
>
> Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyo na haki; [Haki ni jambo la ukweli, siyo la kujifanya – mtu ambaye kwa ukweli anafanya mambo yaliyo sahihi ni mwenye haki.] Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi (3:7-8).

> Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu (3:9).

> Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. [Kama atasitisha kukaa ndani ya Kristo, atatenda dhambi. Kama atatenda dhambi, atakuwa amesitisha kukaa ndani ya Kristo.] Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa (3:24).

> Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake (5:2-3). [Upendo wa kweli husababisha utiifu. Kutokuwa mtiifu kunaonyesha uwepo wa ukosefu wa upendo.]

> Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu (5:4).

Kutokana na aya hizi, inaonekana ni wazi kwamba tabia inayoleta tofauti ya mwamini ni kwamba anaishi kwa kumtii Mungu. Ushindi dhidi ya dhambi ni heshima kwa ajili ya mwamini.

> Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili (1 Wakorintho 10:13).

> Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia wampendao (Yakobo 1:12).

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Watu wengine huwa washindani dhidi ya pointi zilizoandikwa katika somo hili. Jitahidi kuyaweka majadiliano yawe katika kuzingatia Maandiko yaliyotumika.*

► Uliza, “Kama unasumbuka na jaribu, ni kwa jinsi gani ukweli huu utakuwa muhimu kwa ajili yako?”

► Watake wanachama washirikishane jinsi kuokoka kunavyoleta utakaso na nguvu za ushindi dhidi ya majaribu.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya kuniokoa kutoka kwa maadui zangu ambao wanaizuia mimi kukutumikia wewe, na kwa kunitoa kutoka kwa adui yangu mkubwa sana, ambaye ni dhambi.

Asante kwa kunisaidia mimi kuzikataa dhambi wakati nilipotubu na kuja kwako.

Nisaidie kukumbuka kukutegemea wewe kwa ajili ya neema yako ya kila siku. Ninajua kwamba kwa msaada wako ninaweza nikashinda jaribu na kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi.

Asante kwa heshima uliyonipa ya kuishi maisha ya ushindi. Ninataka niwe mwaminifu na nipokee taji la maisha ulililoliahidi kwa watu wote wanaokupenda wewe.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari Warumi 6. Angalia taarifa zote zinazoonyesha kwamba mwamini anapaswa awe na ukombozi kamili kutoka katika dhambi.

## Maelezo kuhusiana na Yohana 1:8

Maelezo yafuatayo yanaweza kuwa ni ya msaada sana kama upinzani fulani utaweza kuinuka au kujitokeza.

Watu wengine ambao wanakataa kwamba mwamini anaweza akaishi kwa ushindi dhidi ya dhambi za kukusudia wananukuu kutoka katika 1 Yohana 1:8: "Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu." Lakini inamaanisha nini "kuwa na dhambi"? Je, inamaanisha kwamba hata waamini wanaendelea kutenda dhambi za kukusudia? Hiyo haitaweza kulingana na taarifa zilizoko kwenye sura ya tatu ambazo zimenukuliwa hapo juu. Inawezekanaje Yohana awe ametengeneza taarifa hizo zote kwenye sura ya tatu kama hapo mwanzo alikuwa amesema, "Kila mtu, ikiwa ni pamoja na mwamini, huendelea kutenda dhambi?" Hiyo haitaweza kuleta maana.

Maudhui yanaonyesha maana yake. Katika aya ya saba, utakaso wa dhambi umeahidiwa. Utakaso huu ni kwa ajili ya wale "wanaotembea kwenye nuru" ikimaanisha kutembea katika ukweli, na utii kwa Mungu. Wale watu ambao kwa sasa wanaishi katika ukweli wametakaswa katika hali zao za zamani za dhambi kwa damu ya Kristo.

Lakini inawezekana kukawepo na baadhi ya watu ambao wanakataa kwamba wametenda dhambi na watahitaji utakaso. Hawa ni wale ambao wanasema kwamba "sisi hatuna dhambi" na "wanajidanganya" wenyewe. Wanadai kwamba kamwe hawatendi dhambi, au kwamba wanaweza wakatatua matatizo yao ya dhambi bila ya Kristo.

Tena katika msitari wa tisa, msamaha na utakaso vimeahidiwa. Katika mstari wa kumi, unasema kwamba wale wanaosema "hawajatenda dhambi" wanampinga Mungu.

Yohana alikuwa anaandika ili kufanya marekebisho ya makosa ya wale ambao wanasema kwamba hawadhanii kama wanahitaji utakaso na msamaha unaotolewa na Kristo – wale waliofikiria kwamba hawahitaji kuokoka. Hakuwa anasema kwamba hata waamini wanaendelea kutenda dhambi, kwa kuwa hilo litapingana na msisitizo wake na taarifa zake za moja kwa moja katika waraka huu.

# Somo la 16
# Shauku kwa ajili ya Umisheni

## Wazo Kuu

"Nina bidii kwa ajili ya wokovu wa wenye dhambi."

## Malengo ya Somo

Kuchunguza sababu zinazotuchochea kueneza injili.

## Utangulizi

► Je, ni kweli kwamba kila Mkristo anapaswa kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa wenye dhambi? Je, hiki ni kitu ambacho wahubiri peke yao wanapaswa wawajibike nacho?

► Sawa, kwa hiyo wewe binafsi unafanya nini kwa ajili ya wokovu wa wenye dhambi?

## Uinjilisti ni Kipaumbele cha Kimaandiko

*Watake wanafunzi waone kila andiko lililoko katika sehemu ya hapa chini. Baada ya kuwa kila aya imesomwa, uliza, "Je, andiko hili linaonyeshaje kwamba uinjilisti ni kipaumbele cha kimaandiko? Baada ya kuwa wametoa majibu, toa sentensi inayoendana na andiko:*

- **Mathayo 9:36-38**. Yesu aliwataka wanafunzi wake kushirikisha nia yake iliyokuwepo kwa ajili ya wenye dhambi.
- **Mathayo 28:18-20**. Yesu alitoa Agizo Kuu kwa kanisa, kuonyesha kwamba uinjilisti na uanafunzi ni wajibu wetu.
- **Matendo ya Mitume 4:29**. Wakati hapo mwanzo kanisa lilipokutana na mateso, jukumu lao la kwanza halikuwa hatari ya kimwili. Waliomba kwamba mateso hayo yasiwe na uwezo wa kuzuia kuenezwa kwa Neno la Mungu.
- **Matendo ya Mitume 11:18**. Kanisa la Wayahudi lilimtukuza Mungu kwamba wokovu ulikuwa umetolewa hata kwa watu wa Mataifa.
- **Wafilipi 1:18**. Paulo alifurahia kwamba Kristo alikuwa anahubiriwa hata wakati yeye mwenyewe akiwa gerezani.
- **Waefeso 6:19**. Paulo aliomba maombi yafanyike kwa ajili ya uinjilisti wenye ufanisi.
- **Warumi 10:13-15**. Paulo aliweka msisitizo wa hitaji la watumishi watakaopeleka injili, kwa sababu wokovu ni kwa ajili ya wale ambao huisikia injili na kuamini.

### Sababu za Mwamini kuwa anatakiwa kutamani Uongofu kwa waliopotea

- Anapaswa awe na shauku ya kufuata mfano wa Yesu, ambaye alishuka kutoka mbinguni akaja kuishi na kufa kwa ajili ya wokovu kwa watu waliopotea katika dhambi.

- Anapaswa kutamani kwamba Mungu atatukuzwa kwa kubadilishwa kwa mwasi mmoja na kuwa mtu wa kumwabudu Mungu.

- Anapaswa kuona kuenea kwa injili kama ni ushindi wa Kristo na upatanisho wake.

- Anapaswa atake kushiriki katika kazi ambayo ni kipaumbele cha Mungu.

- Anapaswa awe na huruma kwa ajili ya watu waliopotea katika dhambi ambao wanakabiliwa na hukumu ya ndani kwa ajili ya dhambi zao.

### Sababu za baadhi ya Wakristo kutofanya Uinjilisti

*Waachie wanachama wataje sababu kadhaa, kisha uwape zilizoko kwenye hii orodha kwa zile ambazo watakuwa hawajazitaja.*

- Ukosefu wa bidii ya Kiroho kwa ujumla.
- Kutojisikia binafsi kuwajibika kwa ajili ya uinjilisti.
- Kutojua jinsi ya kuanza mazungumzo ya kiroho.
- Kutojua jinsi ya kuwasilisha injili kwa njia inayokubalika.
- Hofu ya kushindwa kujibu pingamizi.
- Aibu ya kuonekana uko tofauti na ulimwengu.
- Kuwa na mashaka kwamba juhudi zake zinaweza zisiwe na ufanisi.

► Je, mojawapo ya sababu hizi ni visingizio vya kutosha?

### Kuanza kufanya Uinjilisti

► Kama mtu atakuwa hafanyi jambo lolote kwa ajili ya watu waliopotea kwenye dhambi, ni nini kinachohitajika ili kumfanya aweze kuanza kufanya?

Kama mwamini hana bidii ya kiroho, anahitaji uamsho binafsi.

Kama mtu yuko hai kiroho, ni mwenye bidii na kutambua wajibu wake binafsi wa kushiriki katika kutimiza utume mkuu, inawezekana mambo mawili yafautayo yakawa ndiyo anayohitaji kwa ajili ya kuanza kazi yake.

1. Imani – Anahitaji kutambua kile ambacho Mungu hufanya ili kuifanya Injili kuwa na nguvu.

2. Maandalizi – Anahitajika kuandaliwa ili kuwasilisha injili.

► Je, ni nini unachokihitaji ili kukuwezesha wewe kuanza?

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

► Tueleze unafanya nini katika kuieneza injili.

► Je, unaridhishwa na kile unachokifanya?

► Je, ni watu wangapi umeshirikishana nao binafsi ujumbe wa injili kwa shauku na ufanisi mkubwa kwa kipindi cha mwezi uliopita?

► Je, unadhani ni nini kitakachoweza kukusaidia wewe kuanza kushirikisha ujumbe wa injili kwa ari kubwa zaidi na kwa ufanisi mkubwa?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Uliupenda ulimwengu sana hata ukamtoa Mwanao wa pekee afe kwa ajili ya wokovu wetu. Nataka nikupende kiasi cha kutosha cha kushirikisha shauku yako ya kuokoa watu waliopotea katika dhambi. Ninajua inakupendeza wewe kwa ajili yangu mimi kubeba ujumbe wa injili kwenda kwa wenye dhambi.

Ninataka wewe utukuzwe kwa wenye dhambi kutubu na kuwa watu wa kukuabudu wewe.

Ninataka niwe na hisia ile ambayo Yesu alikuwa nayo kwa ajili ya watu waliopotea katika dhambi.

Ninakuomba uniongoze na uwezeshe juhudi zangu. Nisaidie mimi kushiriki kwenye kazi ya Roho Mtakatifu wako ya kuwaleta kwako watu waliopotea katika dhambi.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Rejea uwasilishaji wa injili ambao umefundishwa kwenye somo la 6 au mfumo mwingine wowote wa uwasilishaji wa injili unaouona kwamba unakufaa wewe. Tafakari matukio yako ya hivi karibuni katika uwasilishaji wa injili na jaribu kupima ni utafiti au mafundisho gani ya ziada yanayohitajika kwa ajili ya kuongeza ufanisi wako. Fanya msimamo maalumu wa kujitoa kwa ajili ya maandalizi hayo.

# Somo la 17
# Imani Idumuyo

## Wazo Kuu

"Tumaini langu kwa Mungu halitegemee kuteseka."

## Malengo ya Somo

Kuona ni kwanini ujasiri wetu ulio katika Mungu unapaswa kuvumilia matukio na hali zote.

## Imani kwa Maisha Halisi

► Je, kuna wakati wowote wa kulala Unawaeleza watoto wako hadithi?

Hapa kuna hadithi kabla hujaenda kitandani kulala kwa ajili yako

> Kulikuwa na msichana mdogo aliyeitwa Lucy. Lucy alikuwa msichana mzuri sana. Hakuwahi kugombana na wazazi wake au waalimu wake, na alipenda brokoli na mchicha. Alikuwa mzuri sana kiasi cha kwamba meya wa mji wake alimtunuku medali tatu za dhahabu: moja kwa ajili ya subira, ya pili kwa ajili ya ubidii, na ya tatu kwa ajili ya uaminifu. Lucy alikuwa akizivaa medali hizo kila wakati.
>
> Mtu mmoja tajiri katika mji huo alikuwa anamiliki bustani binafsi ya kupumzikia. Hakuwa anaruhusu watu wengi waingie kwenye bustani hiyo, lakini alikuwa amesikia jinsi Lucy alivyokuwa mzuri, kwa hiyo alimwambia kuwa anaweza kutembea kwenye bustani hiyo wakati wowote alinaotaka. Kulikuwa na miti mingi bustanini, lakini hakukuwa na maua, kwa kuwa tajiri alikuwa anawapenda nguruwe, na alikuwa na nguruwe wengi huko. Nguruwe walikuwa wamechimbua maua yote muda mrefu uliopita, lakini mtu huyo aliamua kuwa afadhali awe na nguruwe kuliko maua.
>
> Siku moja Lucy aling'anisha medali zake na akaenda kutembea bustanini. Aliona miti mizuri na nguruwe wazuri. Kulikuwa na nguruwe wa ukubwa tofauti tofauti. Kulikuwa na nguruwe wa rangi ya waridi, weusi, weupe, na wenye madoadoa.
>
> Lakini baadaye Lucy akaona kitu kilichomwogopesha. Alikuwa ni mbwa mwitu ambaye alikuja kumkamta nguruwe kwa chakula chake cha jioni. Alikuwa bado hajamwona Lucy, kwa hiyo Lucy alirukia nyuma ya kichaka kujificha. Mbwa mwitu alikuja karibu sana kisha akasimama, kujaribu kuamua ni nguruwe yupi wa kumla. Mbwa mwitu alitabasamu huku akiwaza jinsi atakavyofurahia chakula chake cha jioni.
>
> Lucy alikuwa akichungulia nje ya kichaka na kumwona mbawa mwitu akitabasamu. Aliona jino lake kubwa na kidogo akatetemeka kwa hofu. Kwa bahati mbaya, alipotetemeka, medali yake ya bidii iligongana na ile medali ya uaminifu, na mbwa mwitu akawa ameisikia ile sauti. Mbwa mwitu alirukia kichakani na akamkuta Lucy.

> Alipomtazama Lucy alimwona jinsi alivyo mzuri. Mbwa mwitu aliamua kuwa angekuwa bora amle Lucy kuliko nguruwe, kwa hiyo alimkamata na kumla.
>
> Siku iliyofuatia mmiliki wa bustani hiyo alipofika mahali hapo, alichokikuta ni mabaki ya Lucy ambayo ni medali ya bidii, medali ya uvumilifu, na medali ya uaminifu.

► Ulishawahi kuwaambia watoto wako hadithi kama hii kabla ya kulala? Je, kwa nini isiwe hivyo?

Hii siyo hadithi ambayo wazazi wengi wanaweza kuwasimulia watoto wao kabla ya kulala. Tunahitaji hadithi zinazoelezea kwamba ukitenda mambo maovu utahukumiwa na ukitenda mambo mema utatunukiwa/kuzawadiwa uzima wa milele. Wazazi wanataka watoto wakifikiri kwamba hivyo ndivyo kawaida hufanyika. Lakini ikiwa imani yetu inategemea kuona mwisho mwema kwa kila hadithi, imani yetu itakuwa hailingani na maisha halisi.

Kama mambo mabaya yanatokea kwa watu ambao hawaonekani kuwa wanakustahili kuyapata, je, tungechukuliaje maisha?

Imani ya Kikristo siyo:

- Matumaini yasiyo na maana ("Usijali. Kila kitu kitakuwa sawa.")
- Ustahimilivu mkali ("Maisha hayako sawa kwa hiyo unapaswa kuwa thabiti.")
- Ukwepaji matatizo usiotokana na akili ("Usinikumbushe mimi… Sitaki kufikiri juu ya hilo.")

Imani ya msingi na ya muhimu zaidi ni imani ya msingi kwa Mungu ambayo hudumu bila kujali kinachotokea. Mtu aliye na aina hii ya imani ya kustahimili huwa anaendelea kumtii Mungu.

Waebrania 11 inaelezea kuhusu mashujaa wengi wa imani. Ni watu ambao kwa kupitia imani walichagua kumtumikia Mungu hata wakati ilipomaanisha kwamba watapata mateso. Tunayo kumbukumbu ya mashujaa wa kiroho amabo waliteseka, siyo kwa sababu walikosa imani, bali kwa sababu walikuwa na hiyo imani. Imani yao iliwasaidia wawe tayari kuteseka na iliwasaidia kuona mbali zaidi kwa kutokuangalia mali na badala yake waliona mambo yasiyoonekana kwa kawaida na ya milele.

Kwa sababu ya Mungu kuwa mwenye haki, kutakuwepo na hukumu ya mwisho ya kiyama. Thawabu za urithi wa umilele zitatolewa na adhabu ya ghadhabu ya milele itatamkwa. Imani iliyo katika haki ya Mungu inatusaidia sisi kuvumilia katika hali zote ambazo siyo wakati wote zinafanya kazi katika kipindi kifupi.

► Soma Ayubu 1:1, 13-22.

Mfululizo wa mambo yaliyoko kwenye kitabu cha Ayubu unatambulishwa na taarifa zinazosema "Palikuwa na mtu," na "Ilikuwa siku moja." Kwanza kabisa tabia ya Ayubu inaelezwa katika viwango vya juu sana. Alimcha Mungu na kuepukana na uovu. Kisha

baadaye, “Ilikuwa siku moja” wakati ambapo kila kitu kwenye maisha yake kilitoweshwa isipokuwa imani yake.

Inavyoonekana kwetu ni kwamba kwa mtu kama huyo kamwe haingewezekana ikatokea siku kama hiyo. Wakati majanga yanapomjia mtu, wakati wote tutatafuta njia na sababu za kumlaumu kwa ajili ya kile kilichotokea kwake.

Tunafanya hivyo kwa sehemu ili kulinda kuamini kwetu kwamba haki inatawala dunia, na kwa sehemu kuhifadhi ufahamu wetu wa usalama. Tunataka kufikiri kwamba mambo hayo hayatakaa yatokee kwetu kama hatustahili yatutokee. Lakini imani ni lazima iendelee hata kama mambo hayo yatatokea. Biblia inatupa Ayubu kama mfano wa mtu mwenye imani inayojua kuvumilia. (Ona Yakobo 5:11 na Ayubu 42:7-8).

Ushuhuda wa imani uko wakati ambapo mwamini anavumilia na kuendelea kumtii Mungu katika hali zote. Kama mtu haelewi aina hii ya imani, atakuwa anaomba tu kwa ajili ya kupata miujiza wakati hali zinapokuwa ngumu, lakini Mungu siyo siku zote anaondoa matatizo kupitia muujiza. Baadhi ya watu huachana na imani kwa kukata tamaa kwa sababu wanadhania kwamba imani yao haifanyi kazi au kwamba Mungu ametaka washindwe. Tunapaswa tukumbuke njia nyingine pia ambazo imani hufanya kazi.

Mwandishi mzuri wa hadithi anajua jinsi ya kuwatumia watu walioko kwenye hadithi yake kwenye matatizo ambayo yanaonekana kutokuwa na suluhisho. Mwisho wa hadithi, mwandishi huwashangaza wasomaji. Maisha halisi huonekana kuwa na taarifa nyingi za kusikitisha, lakini imani ya Kikristo ni uhakika kwamba Mungu anaandika mwisho ulio wa kweli wa hadithi.

> Mchungaji na mke wake Beth walianzisha kanisa California miaka kadhaa iliyopita. Ulikuwa ni uanzishwaji wa kanisa uliokuwa na mafanikio, lakini mambo ya kutisha yalianza kutokea miaka michache baadaye wakiwa kwenye utumishi. Nyumba yao iliunguzwa kwa moto. Miezi michache baada ya tukio hilo, mchungaji alipigwa na majambazi hadi akawa taabani kabisa asiyejiweza. Baadaye alishtakiwa kwa makosa ya jinai, akafungwa jela, na baada ya hayo yote akaja kuuawa, ingawaje sababu kamili ya kifo chake kamwe haikujulikana. Haya yote yalitendeka takribani katika kipindi cha miaka minne.
>
> Je, ni kitu gani kimeendelea kumfanya Beth kuwepo katikati ya mikasa na majanga haya yote? Kwa kiwango kikubwa, ni imani iliyo katika tabia ya Mungu. Beth anajua kwamba:
>
> - Kwa kuwa Mungu ni mwenye maarifa yote, anaijua hali yake kwa undani sana. Mungu alijua kabla ya hapo mambo yote ambayo yangeenda kutokea.
> - Kwa kuwa Mungu ni mwenye mamlaka na enzi, kila kitu kiko chini ya udhibiti wake. Bado anaendelea kukamilisha kusudi lake kwenye maisha yake. Hakuna chochote kilichofanyika pasipokuwepo na kibali cha Mungu.

- Kwa kuwa Mungu ndiye mwenye hekima yote, ana uwezo wa kumwongoza katika maamuzi yote anayopaswa kufanya sasa baada ya mume wake kuondoka katika maisha ya hapa duniani.
- Kwa kuwa Mungu yuko kila mahali, amekuwa pamoja naye siku zote. Hata katika katika kipindi kigumu zaidi cha majaribu alifahamu kwamba Mungu alikuwa karibu naye na kila kitu kilikuwa chini ya mamlaka yake.
- Kwa kuwa Mungu ni muweza wa yote, ana uwezo wa kuleta majibu makubwa kwa maombi. Anaweza akaomba kwa ujasiri na kwamba Mungu atatimiza mahitaji yake, atajiletea utukufu yeye mwenyewe, na kuendeleza ufalme wa Mungu kupitia hali hii.
- Kwa kuwa Mungu ni mwenye upendo wote, amekuwa akitafuta mambo mazuri aliyokuwa anahitaji Beth na familia yake. Mungu aliuweka mkono wake wa upendo juu yao kwa kipindi chote cha mpito. Mungu alikuwa na kusudi kamili la upendo kwa ajili ya mambo ya uovu aliyokuwa ameruhusu wakabiliane nayo.
- Kwa kuwa Mungu ni Mtakatifu, anamtaka Beth awe na nia iliyo safi, kama naye Mungu alivyo na nia iliyo safi. Mungu anataka Beth aendelee kutembea akiwa karibu sana na yeye, na awe mwangalifu asiwe na tabia zozote zisizokuwa na utakatifu kwa wakati wote anapokuwa anashughulika na changamoto zake.Anamtaka awasamehe washambuliaji, wachoma moto, na waliomshtaki.
- Kwa kuwa Mungu ni nafsi, huhusiana na Beth kama mtu halisi. Anamtaka aimarishe uhusiano wake binafsi na Mungu.

Imani siyo uhakikisho kwamba tutaepukana na mateso. Imani ni kujiamini katika tabia ya Mungu ambayo hututegemeza wakati wa mateso ambayo hatuwezi kuyaelezea.

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Lengo la somo hili lilikuwa kurekebisha mwelekeo wa kufikiri kwamba Mungu anapaswa kuondoa matatizo siku zote badala ya kutusaidia sisi kuwa wavumilivu.*

► Watake washiriki kushirikishana mifano kadhaa ya hali ambazo imani iliwasaidia kuwa wavumilivu.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninataka kukuamini hata yanapotokea mambo ambayo siyaelewi. Ninajua kuwa unanitunza kila wakati.

Nisaidie kuwa na Imani yenye kuvumilia ili niendelee kukufuata wewe katika hali zote.

Asante kwa uaminifu wako kwangu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Waebrania 11. Tambua jinsi watu mbalimbali wa imani kwa uvumilivu mkubwa walivyoweza kufuata maelekezo ya Mungu kwa sababu ya kumtii yeye.

# Somo la 18
# Tunahitaji Kanisa

## Wazo Kuu

"Siwezi kutimiza makusudi yote ya Mungu kwa kufanya mimi mwenyewe."

## Malengo ya Somo

Kumsaidia mwamini kujitolea kwa ajili ya kanisa la mtaa.

## Utangulizi

► Je, ni nini kusudi la kanisa?

*Kubaliana na majibu ya aina mbalimbali. Bado siyo muhimu kwa sasa kufafanua mambo mengi.*

► Je ni nani aliye na wajibu wa kutekeleza malengo ya kanisa?

Kila Mkristo anapaswa kuwa na jukumu la kusaidia.

► Je, ni nani anayehitaji kanisa? (*Kila mtu anahitaji kuwa na kanisa.)*

Kanisa ni moja. Yesu alisema, "Nitalijenga kanisa langu, [umoja]…" (Mathayo 16:18). Kitabu cha Waefeso kinazungumzia kuhusu kanisa kama lililo moja.

> Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote (Waefeso 1:22-23).
>
> Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu (Waefeso 4:4).

Kanisa ni la ulimwengu wote. Kwa sababu ni Mungu pekee ndiye aliye na orodha ya washiriki, na hakuna shirika la kidunia, au shirika la kibinadamu linalojumuisha kanisa zima, wakati mwingine huitwa "kanisa lisilooneka."

Hata hivyo Kanisa ni la mahali au mtaa. Kanisa ni lazima lichukue mfumo mahali au mtaa husika ili kutimiza majukumu yake. Kwa mfano, mwamini hawezi kila siku akawa na ushirika na kanisa la ulimwengu katika muda wake wote wa Maisha yake; ni lazima afanye ushirika na watu fulani.

Mungu hutumia watu binafsi, lakini pia hulitumia kanisa la mtaa kwa njia nyingi maalumu. Kanisa la mtaa (siyo jengo), bali ni kikundi cha watu walioamini) ni hekalu mahali ambapo Roho Mtakatifu hukaa.

> Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? (1 Wakorintho 3:16).[4]

## Baadhi ya Madhumuni ya kanisa la mtaa katika Agano Jipya.

*Soma maoni, kisha uwe na mtu mmoja wa kusoma aya:*

1. Kuabudu na Ujenzi wa maadili kwenye kusanyiko (1 Wakorintho 14:12).
2. Kufundisha mafundisho imara ya imani (1 Timotheo 3:15).
3. Kutuma watu kwenda kufanya uinjilisti na uanafunzi (Mathayo 28:19-20).
4. Kutoa msaada wa kifedha kwa wachungaji (1 Timotheo 5:17-18).
5. Kutuma na kuwawezesha wamisionari (Matendo ya Mitume 13:2-4, Warumi 15:24).
6. Kutoa msaada wa kifedha kwa waumini wenye mahitaji (1 Timotheo 5:3).
7. Kuwatia katika nidhamu washirka wanaoanguka dhambini (1 Wakorintho 5:9-13).
8. Ubatizo na Meza ya Bwana (Mathayo 28:19, 1 Wakorintho 11:23-26).
9. Asili ya waumini katika jumuiya ya Kikristo (Matendo ya Mitume 2:42).

► Malengo haya yote yana umuhimu?

► Je, ni malengo gani katika hiyo orodha wewe umeweza kushiriki katika siku za hivi karibuni?

► Je, ni kitu gani kitakachotokea kama kanisa halitafanya hata jambo moja katika malengo yaliyoorodheshwa?

Malengo haya hayawezi kutekelezwa au kukamilishwa na watu binafsi wanaofanya kazi peke yao. Vikundi vya watu walioamini ni lazima washirikiane katika mtaa ili kukamilisha malengo haya ya kibiblia ya kanisa.

Mungu anayo mipango ya huduma za utendaji kwa ajili ya kundi la waamini la mtaa. Anatoa kile kinachohitajika na anahitaji kujitolea kutoka kwetu.

Hapa ni baadhi mifano ya jinsi kundi maalumu la mahali linavyofanya kazi:

| Kipengele Muhimu | Hatua ya Mungu | Jibu la mwanachama linalohitajika |
|---|---|---|
| Uongozi | Huwaita wachungaji | Jinyenyekeze katika kuchungwa |
| Fedha | Huamuru msaada | Kutoa msaada wa kifedha |
| Karama za kiroho | Hutoa karama za kiroho | Tumia vipawa kutumikia kwa uwiano |
| Ushirikiano | Muundo wa “mwili" | Kutambua kuwa tunategemeana. |

[4] Kuona kwamba Paulo alikuwa anazungumza nao kama kikundi cha mahali maalumu na siyo kama watu binafsi, ona 3:9. Waamini binafsi wanazungumziwa kama mahekalu ya Roho Mtakatifu katika 1 Wakorintho 6:19.

Watu wengine hupenda kujisikia huru kiroho. Wanafurahia kuwa sehemu ya Ukristo wa ulimwengu, lakini kamwe hawaungani na kanisa la mtaa, wanajisikia huru kuhudhuria popote wanapotaka jumapili, wanakataa jukumu la aina yeyote kwa ajili ya huduma yeyote ndani ya kanisa la mtaa, na wanatoa zaka zao mahali penye jambo linalowavutia. Endapo Wakristo wote wangekuwa katika hali hiyo, hakungekuwepo na kanisa la mtaa.

Watu wengine kamwe hawaoni hitaji la kanisa kuhusika kwa ajili yao. Wanategemea kuishi peke yao. Ni vigumu sana kwao kuweza kuona faida za kuhudhuria ibada za kanisa.

Baadhi ya Makanisa yamebadilisha mifumo yao ya Ibada ili kuwavutia wageni wa kanisa ambao huwa hawajitolei. Wanashindana na makanisa mengine kwa kuweka ibada ambazo ni kama maigizo. Makutano yao kuwa hadhira bila muunganiko zaidi kuliko watazamaji kwenye tamasha au mchezo wa kuigiza.

Kila Mkristo anapaswa ajitoe mwenyewe, mali zake, na kwa uwezo wake ili kusaidia kanisa la mtaa kukamilisha majukumu yake ya kibiblia. Asipofanya hivyo, hatimizi kusudi lake kama Mkristo.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Washiriki wafikirie maswali yafuatayo:*

► Je, niko chini ya mamlaka ya mchungaji? Kwa njia ipi hasa?

► Je, ninatoa msaada wa kifedha katika kusaidia huduma za kanisa la mtaa?

► Je, Ninatumia uwezo wangu kwa ajili ya kanisa langu la mtaa?

► Ninahisi kwamba ninalihitaji kanisa langu?

► Ninahisi kuwa kanisa langu linanihitaji mimi?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunipa familia ya kiroho ambayo inashirikiana nami katika mambo yote ya maisha. Asante kwa kunifanya mimi niwe sehemu ya mwili ambao unayafanya mapenzi yako hapa ulimwenguni.

Nisaidie kukumbuka kwamba ninahitaji kanisa na hilo kanisa linanihitaji pia. Nisaidie kufanya ahadi ambazo kanisa la mtaa ambalo linahitaji kutoka kwa waumini wake ili liweze kukamilisha malengo yake.

Kwa pamoja tusaidie tuwe hekalu ambamo Roho Mtakatifu anaishi na kuwapa watu wako uzima.

Amina.

**Kazi ya Kufanya**

Tafakari 1 Wakorintho 12. Tafakari juu ya maelezo yanayotolewa kuhusu kutegemeana kwa wanachama wa chombo hicho.

# Somo la 19
# Kushinda Dhidi ya Majaribu

## Wazo Kuu

"Ninaweza kuwa mshindi dhidi ya majaribu kwa uongozi na nguvu za Roho Mtakatifu."

## Malengo ya Somo

Kuelewa jinsi majaribu yanavyokuja na jinsi ya kumtegemea Mungu kwa ajili ya ushindi.

## Majaribu

► Je, ulishawahi kuwa na majaribu ambayo ulifikiria kwamba hakuna mtu mwingine yeyote atakayeweza kukielewa?

► Je, ulishawahi kushangaa kama ni kweli inawezekana kuishi katika maisha ya ushindi dhidi ya dhambi?

Mungu alishaahidi kutoa neema inayowezesha ambayo ni zaidi ya fidia kwa ajili ya madhaifu yetu katika majaribu:

> Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili (1 Wakorintho 10:13).

Aya hii inatueleza baadhi ya mambo muhimu kwetu.

1. **Kila jaribu ni jambo la kawaida kwa wanadamu wote.** Jaribu linakuja kwa sababu ya ubinadamu wetu na hushambulia baadhi ya maeneo dhaifu ya mwanadamu. Hiyo inamaanisha kwamba mahangaiko yako siyo kwamba ni ya kipekee kwako.

2. **Mstari huu unatuambia kwamba Mungu anajua mipaka yetu.** Mungu anaelewa ni kwa jinsi gani tunaweza tukachukuliana na jaribu. Kwa uhakika hatujui ni kwa kiwango gani tunaweza kuchukuliana na jaribu, lakini yeye anajua.

3. **Mungu anatukusudia sisi tuishi kwa ushindi**. Aya hii inatueleza kwamba Mungu hataacha jaribu liwe juu ya kiwango ambacho tunaweza tukastahimili kwa msaada wake. Anaweka ukomo kwenye majaribu yanayotujia, kwa sababu anataka tuishi kwa ushindi. Watu wengine hufikiri kwamba ushindi dhidi ya dhambi ni jambo lisilowezekana kwa sababu sis ni wanadamu. Kwa mujibu wa aya hii, ushindi ni wa lazima na unaotarajiwa kuwepo.

4. **Mungu hutupa vitu tunavyohitaji kwa ajili ya kutuwezesha tuishi kwa ushindi, hufanya na "mlango wa kutokea."** Neema kwa ajili ya maisha ya ushindi inatolewa kama jibu la imani.

Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu (1 Yohana 5:4).

Kama tutakuwa tunafahamu ni kwa jinsi gani inatokea kwamba wakati mwingine mwamini anashindwa na jaribu, yawezekana pia tukafahamu ni kwa jinsi gani tunaweza tukalizuia. Ni jambo la busara tukachambua mchakato ambao mtu hupitia hata kujikuta ameanguka kwenye jaribu.

Mchakato huo umeelezwa katika Yakobo 1:14-15:

> Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi...

John Wesley alichunguza kwamba hatua zinazopelekea kutenda dhambi kwa kawaida zinatokea kama ifuatavyo.[5]

1. Jaribu huinuka (kutoka katika dunia, mwili na shetani).
2. Roho Mtakatifu humtahadharisha na kumwonya mwamini kuwa mwangalifu.
3. Mtu huliangalia na kulipa nafasi lile jaribu, na linaanza kuwa kivutio kwake. (Hapa ndipo mwamini anapofanya kosa lake la kwanza kwenye mchakato huu.)
4. Roho Mtakatifu huhuzunishwa, imani ya mtu inadhoofika, na upendo wake kwa Mungu unapoa.
5. Roho Mtakatifu hukemea kwa ukali.
6. Mtu hugeuka katika kusikia ya *huzuni* ya Roho Mtakatifu na kuanza kusikiliza sauti ya *mvuto* kutoka kwa mjaribu.
7. Matamanio ya uovu huanza na kuujaza moyo wake; imani na upendo vinatoweka; na yuko tayari kufanya dhambi inayoonekana wazi kwa nje.

Mchakato huu hauchukui muda mrefu. Unaweza ukafanyika hata kwa dakika chache sana.

Kwa kuwa jaribu huongeza nguvu yake wakati linapokuwa limeshikilia nafasi katika hali yetu, mtu ambaye anachukua muda wa kuamua kufanya au kutofanya anajiweka mwenyewe kwenye hatari kubwa. Mwamini ambaye yuko makini katika kuhakikisha anadumisha ushindi dhidi ya dhambi ni lazima awe na moyo ambao umejiweka imara ili kwamba awe na uwezo wa kulikataa jaribu mara tu linapojitokeza. Mtu ambaye anakuwa

[5] Imenukuliwa kutoka *A Timeless Faith: John Wesley for the 21st Century*, na kufanyiwa uhariri na Stephen Gibson.

na mashaka anadhihirisha kwamba moyo wake haujadhamiria kwa ukamilifu kabisa kumpendeza Mungu.

Jaribu ni changamoto kwa imani yetu, kwa kuwa majaribu yanatoa nafasi kutilia shaka utii kwa Mungu kwamba ndiyo njia bora zaidi wakati huo.

Kama mwamini hawezi kuwa na mwelekeo wa kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi, inawezekana ikawa ni kwa sababu ya mojawapo ya matatizo yafuatayo:

1. Haoni kama Mungu anahitaji utiifu.
2. Haoni na haamini ahadi ya neema ya Mungu inayowezesha na inayofanya kazi.
3. Hategemei neema ya Mungu inayowezesha na inayofanya kazi badala ya kutumainia nguvu zake mwenyewe.
4. Anamtumikia Mungu akiwa na utii katika mambo fulani tu aliyochagua, badala ya utii kamili usiokuwa na masharti.
5. Hajatafuta kwa neema kuwa na kusudi moja tu la kufanya yaliyo mapenzi ya Mungu (Wafilipi 3:13-15).
6. Hadumishi nidhamu za kiroho ambazo zina uwezo wa kumtia nguvu katika kujenga uhusiano wake na Mungu

### Mambo ya Kuzingatia

Watu watatu walituma maombi ya kazi ya udereva. Mtu wa kwanza, akitaka kumshawishi anayetegemewa kuwa mwajiri wake baadaye, akasema, "Mimi ni dereva mwenye uwezo mkubwa ambaye kama ninaendesha gari katika mwendo wa kasi futi chache sana kutoka katika jabali barabarani huhitaji kuwa na mashaka nami. Mtu wa pili naye hakutaka ashindwe na mwenzake, kwa hiyo naye akasema, "Ningeweza kuendesha gari kwa mwendo wa kasi ndani ya inchi za mteremko bila kuanguka kutoka humu." Mtu wa tatu alitahamaki, kisha akamwambia yule mwajiri, "Mimi sitakuwa tayari kuhatarisha maisha yako kwa kupita karibu na hilo jabali." Je, unadhani ni nani atakayeajiriwa kutoka katika hawa watu watatu?

Hatupaswi kufikiria sana ni jinsi gani tunaweza kuwa karibu na kupata majaribu. Mungu anataka kutupa miongozo ya kibinafsi ambayo itatulinda katika maeneo yetu ya udhaifu. Tunapokuwa na maamuzi, tunapaswa kuepuka mambo yanayofanya tudhoofike kiroho, kama vile tafrija zisizofaa.

### Je, itakuwaje muumini akitenda Dhambi?

► Kama muumini akitenda dhambi, je, atapaswa asubiri kwa muda gani kabla ya kurejesha uhusiano wake na Mungu?

Kama muumini akitenda dhambi, anapaswa atubu mara moja, na anaweza akarejeshwa tena kupitia kwa wakili wetu, Yesu Kristo (1 Yohana 2:1-2). Asingoje wakati wowote ujao

ambao anafikiri ungefaa zaidi. Akiwa anataka kurejeshwa, Roho Mtakatifu tayari anampa hamu hiyo na kumrudisha kwenye uhusiano wake na Mungu. Kama toba yake ni ya kweli, ataweza kurejeshwa tena mara moja.

Mungu tayari alishaweka uwekezaji mkubwa sana kwa ajili ya wokovu wetu, katika dhabihu ya Yesu. Hatakuwa tayari kuruhusu uwekezaji huo upotee bure kwa kushindwa kutupa sisi neema tunayohitaji ili ituwezeshe kusonga mbele

> Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye? (Warumi 8:32).

*Andiko lifuatalo limeandikwa kwenye karatasi ya mwanafunzi ya kufanyia kazi.*

> Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu; Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu; utukufu una yeye, na ukuu, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele. Amina (Juda 1:24-25).

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Shirikisha kutokana na uzoefu, jinsi uelewa wa hatua za kuanzia wakati wa jaribu hadi kufikia kutenda dhambi kunavyoweza kumsaidia mtu kuacha kutoruhusu jaribu lichukue udhibiti kwenye akili yake. Ruhusu watu wengine pia washirikishe uzoefu wao.*

*Omba mtu akushirikishe jinsi moja au zaidi ya matatizo sita zilizosikilizwa hapo juu zimemsaidia kuishi kwa ushindi.*

*Waulize wale ambao wamekuwa wakihangaika na jaribu wajitoe kufanyia kazi mafundisho yaliyoko katika somo hili. Kwa mfano:*

► Unaweza kudhamiria kwamba wakati jaribu litakapojitokeza, hutachukua muda katika kulitafakari lakini mara moja utalikataa na kumtegemea Mungu kwa nguvu?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninakushukuru kwa kuwa unayajua yote yanayohusiana na mimi. Unajua mipaka na madhaifu yangu. Asante kwa kuniwekea mipaka kwa ajili ya majaribu yanayokuja kwangu na kunipa neema ili kwamba niweze kuishi kwa ushindi.

Nisaidie siku zote niweze kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu. Nisaidie siku zote niweze kukataa dhambi mara tu ninapotambua kwamba jambo hili ni dhambi.

Naomba unisaidie katika kukumbuka kwamba ni wewe peke yako unayeweza kuuridhisha moyo wangu.

Amina.

**Kazi ya Kufanya**

Soma Ufunuo 2-3. Sura hizi zina barua kwenda kwa makanisa saba. Makanisa haya yalikuwa yanakabiliwa na majaribu mbalimbali pamoja na changamoto nyingi. Jaribu kuangalia kwenye mwisho wa kila barua kwamba kuna ahadi inayotolewa kwa mtu anayeshinda.

# Somo la 20
# Mwongozo wa Mungu

## Wazo Kuu

"Ninashinda vita vya maisha kwa kufuata tu maelekezo kutoka kwa kamanda wangu."

## Malengo ya Somo

Kujifunza jinsi ya kuwa mwepesi kuhisi kwenye mwongozo wa Roho Mtakatifu.

## Maombi – Mawasiliano katika Vita

► Je, ni kitu gani ambacho kimefungwa kwenye kila gari au chombo cha usafiri cha kijeshi?

Kila kifaru, gari la deraya, ndege ya kivita, n.k. kunakuwepo na radio. Siyo radio kwa ajili ya matumizi ya muziki kutoka katika stesheni za radio wanazopenda, lakini ni radio kwa ajili ya kufanya mawasiliano.

Mawasiliano ni muhimu sana katika kushinda vita. Askari walioko vitani hawawezi wakauona uwanda wote wa mapigano. Wanaweza wasijue mahali waliko askari wenzao na adui yuko mahali gani. Hawajui ni uelekeo gani waelekeze mapigo, na ni uelekeo gani wanapaswa wawe wanaenda, bali ni kupitia njia ya mawasiliano kutoka kwa kamanda wao.

Kumekuwepo na matukio mengi ambayo askari wamekuwa wakiuawa kwa "mapigo ya moto ya askari wenzao marafiki," wakielekezewa risasi kutoka kwa askari wenzao. Kumekuwepo na nyakati ambazo maroketi na mabomu yamekuwa yakielekezwa kuua askari wenzao badala ya kuelekezwa kuua adui kwa sababu ya mawasiliano mabaya.

Kwenye vita vya kisasa, kunafanyika mkakati wa kawaida wa kujaribu kujua kituo kikuu cha mawasiliano cha adui. Upande unaofanikiwa kufanya hivyo kinakuwa na uwezekano mkubwa wa kushinda mapigano.

Sisi tuko kwenye vita vya kiroho. Shetani hutujaribu na kutudanganya. Dunia hutuvuta sisi tuingie kwenye mtindo wake wa maisha na maadili yake. Watu wanaotuzunguka wakati mwingine hutuzuia na kutukatisha tamaa kuishi kwa ajili ya Mungu. Sisi ni kama wanajeshi tulio katika nchi yenye uadui au uhasama, tukiwa na marafiki wachache sana na maadui wengi sana.

**Mungu anatutaka sisi tushinde vita vya kiroho. Maombi ndiyo njia yetu ya kuwasiliana na kamanda wetu.**

Jaribu kufikiria askari aliyeko kwenye mapigano ambaye anapuuzia amri za kamanda wake na kujiamulia kwenda kivyake au atakavyo yeye tu. Ataweza kusababisha madhara

makubwa badala ya kufanya mambo mazuri; anaweza akashindwa kuwasaidia watu wake wanaomtegemea; na huenda akauawa au akatekwa na maadui.

> Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote (Waefeso 6:18).

Aya hii inakuja pale mwishoni mwa kifungu ambacho Paulo alielezea silaha za kiroho akiwa na mtazamo wa silaha za kijeshi za wakati ule wa enzi zake. Alisema kwamba adui zetu siyo wa kimwili, bali wa kiroho.

Inawezekana kama kungekuwepo na upatikanaji wa radio kwa ajili ya wanajeshi wakati ule, Paulo angelizitumia kuelezea sehemu nyingine ya vifaa vya askari wa kiroho mwombaji. Baada ya kuwa ameelezea kuhusu silaha, alizungumzia kuhusu maombi kutumika pamoja na silaha za kiroho

Wakati tunapokuwa tuko kwenye mapigano dhidi ya nguvu za giza, tunapaswa tuwe tukiomba, tukiwa kwenye mawasiliano na kamanda wetu. Tunaitwa tuwe macho katika maombi, tuwe macho na wenye kuvumilia.

Mungu ameahidi uongozi kwa ajili ya wale wote watakaomsikiliza na kumtii yeye.

> Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako (Mithali 3:5-6).

> Hatua za mtu zaimarishwa na Bwana, Naye aipenda njia yake (Zaburi 37:23).

Tunahitaji maongozi wa Mungu wakati wote, na yeye anatuongoza katika njia ambazo hatuzijui. Hawezi kutusahau kamwe, hata kama hatuwazi kuhusu yeye. Lakini kuna nyakati nyingine ambazo tunahitaji hasa kutafuta mwongozo wake na kumwomba atusaidie kuona kwa uhalisi chaguzi zetu zilivyo. Huenda Mungu akataka kubadilisha mwenendo wetu kwa njia isiyotarajiwa.

Tunahitaji kuwa tayari kumsikiliza yeye…

1. **Wakati tunapofanya maamuzi ya kubadilisha mtazamo.** Ndoa, kazi, elimu, kujitolea kwa kanisa la mtaa.
2. **Wakati wa kufanya maamuzi ya vitendo**: Nafasi za kazi, mahali pa kuishi, manunuzi makubwa.
3. **Wakati tunapopanga na kufanya huduma**: Wito binafsi, mahali gani na nani wa kuhudumu naye, mada za kufundisha na kuhubiri.
4. **Wakati wa kushiriki kwenye mambo yanayohusu uhai wa kanisa:** Jinsi ya kuabudu, kitu cha kujifunza, kitu cha kutoa, jinsi ya kuwa sehemu ya mwili wa Kristo hapa duniani.

## Njia za kutambua Mwongozo wa Mungu vizuri zaidi:

1. **Kuwa karibu zaidi na Mungu kwa njia ya maombi.** Kama sehemu kubwa ya maisha yako yametenganishwa kwenye maongezi na Mungu, unafuata matakwa yako mwenyewe na mitazamo yenye mipaka.

2. **Usiziamini sana akili zako mwenyewe za kufikiri kuliko ukweli halisi wa kimaandiko.** Kama aya hapo juu inavyosema, "...Wala usizitegemee akili zako mwenyewe" (Mithali 3:5).

3. **Wakati wowote kuwa mtiifu kwa kile unachojua kwa uhakika kwamba kiko kwenye mapenzi ya Mungu.** Hali hiyo itaimarisha mtazamo wako. Mtu ambaye anakataa kulitii Neno la Mungu kwa ukweli hataki mapenzi ya Mungu kwa sababu Mungu hudhihirisha mapenzi yake kupitia Maandiko. Kama utakuwa mtiifu kwa sehemu tu ya kile unachojua kwamba ni mapenzi ya Mungu kwa ajili yako, itakupelekea kuchanganyikiwa zaidi – nuru itageuka kuwa giza (Luka 11:35).

4. **Usiahirishe utiifu wako kwenye mapenzi ya Mungu**. Usingojee hali zibadilike kabla ya kumtii Mungu. Huwezi ukapata mambo mazuri sana ya Mungu hadi uwe umesubiri wakati wake.

5. **Kuwa mvumilivu.** Unaweza ukahitajika kungojea wakati Mungu akifungua milango na akiandaa mazingira mbalimbali kwa ajili yako. Usichukulie mambo mikononi mwako kwa sababu ya kukosa uvumilivu. "Ukae kimya mbele za Bwana, Nawe umngojee kwa saburi" (Zaburi 37:7). Kamwe usifanye jambo ambalo unajua kwamba ni uovu kwa sababu ya nia ya haraka.

6. **Sikiliza ushauri mzuri.** "Maana kwa mashauri ya akili utafanya vita; Na kwa wingi wa washauri huja wokovu" (Mithali 24:6). Wakati Mungu anapokutaka wewe ufanye uamuzi mkubwa, mara kwa mara atakuwa analionyesha hilo kwa watu wengine walio muhimu kwenye maisha yako. Kama kuna wazee, wenye hofu ya Mungu wanaokujua na wanaokujali, hutapaswa kufanya kirahisi tu mambo ambayo wanafikiri kwamba ni makosa.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Shirikisha mfano wa uamuzi ambao unajua ulielekezwa na Mungu. Je, Mungu alikuonyeshaje kwamba ulikuwa ni uamuzi sahihi?*

*Itakuwa ni msaada kama pia utaweza kushirikisha mfano ambao ulikuwa ni uamuzi mbaya. Je, ulishindwa kufuata mojawapo ya kanuni nne za kuongozwa na Mungu vizuri zaidi? Ruhusu watu wengine pia washirikishe uzoefu wao.*

*Mtu fulani anaweza akawa wakati huu anataka kufanya uamuzi ambao yuko tayari kuujadili pamoja na kikundi.*

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nina furaha kwamba unajua matokeo yatakavyokuwa kwa uamuzi wowote nitakaoufanya. Asante kwa kupanga mambo mazuri kwa ajili yangu. Ninajua kwamba unaziongoza hatua zangu zaidi sana kuliko hata ninavyoweza kuona.

Nisaidie mimi nijifunze zaidi jinsi ya kufuata uongozi wako. Niwezeshe kukaa karibu zaidi na wewe kwa njia ya maombi. Nisaidie niwe makini na msikivu kwenye ukweli ambao unanionyesha. Nisadie mimi niweze kusubiri mwelekeo wako kwa saburi.

Ninataka nikuamini wewe kwenye kila uamuzi. Ninataka nifuate mapenzi yako kwa utiifu wa moyo wangu wote.

Asante kwa kutaka mambo yaliyo bora kwa ajili yangu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari Mithali 3:1-12. Je, ni mambo gani ya thamani, mwenendo, na tabia yanayoelezwa hapa ambayo yanaweza kuwa ni halisi na maisha ambayo Mungu huongoza na kubariki? Je, ni kwa jinsi gani wewe binafsi unaweza kuyakuza?

# Somo la 21
# Vizuizi vya Maombi

## Wazo Kuu

"Ni lazima niepukane na makosa ambayo huzuia maombi yangu."

## Malengo ya Somo

Kujifunza jinsi ya kujilinda dhidi ya matatizo tisa yanayofanya maombi yasiwe yenye matokeo yanayotarajiwa."

## Vizuizi katika Maombi

► Ni nini kinachoweza kuzuia maisha ya maombi ya mtu yasiendelee jinsi yanavyopaswa?

Mbali ya kuwepo kwa sababu nyingi za kuomba,[6] watu wengi wamejikuta wakipata matatizo ya kuanzisha kuwa na maisha ya maombi ya kumaanisha na ya uaminifu. Hapa chini kuna baadhi ya vizuizi vya kawaida ambavyo ni vizuizi vya maombi lakini vinaweza kuepukwa.

### (1) Ukosefu wa motisha

> Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko (Marko 1:35).

Watu wengine hawatafuti muda wa kuomba kwa sababu hawaoni umuhimu wake. Wanajiona kwamba wana shughuli nyingi sana za kufanya hata kushindwa kutumia muda wao mwingi kwenye maombi.

Mara nyingi kama mtu atajiona kwamba anataka kupata mambo mazuri yafanyike kabla ya kuchukua muda wa kuomba, au kwamba anataka afupishe muda wake wa maombi yake ili aendelee na shughuli zake, mtu huyu anakuwa haweki thamani sahihi kwenye maombi.

Mtu aliye katika shughuli nyingi hupuuzia maombi kwa sababu anajiona kwamba kile anachokifanya yeye ni muhimu zaidi kuliko kile anachokifanya Mungu.

Unapokuwa umeomba, unaweza ukafanya zaidi ya kuomba, lakini huwezi ukafanya kuomba zaidi hadi utakapokuwa umeomba.

### (2) Kiburi cha kiroho

> Wanafiki… wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amin, nawaambia, Wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango

---

[6] Ona somo lililoandikwa "Kuwasiliana na Mungu," na somo lililoandikwa "Faida za Maombi."

> wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi (Mathayo 6:5-6).

Je, umewahi kuwa kwenye mazungumzo ukaja kugundua kwamba mtu anayezungumza na wewe alikuwa anazungumza ili mtu mwingine asikie? Je, hali hiyo itakufanya wewe ujisikieje? Utahisi kuwa ni mazungumzo yasiyo kweli.

Wakati mwingine watu wanapokuwa wakiomba wanakuwa hawaombi kiuhalisia Mungu aweze kusikia bali wanaoongea kwa ajili ya watu wengine kusikia. Wanataka watu wengine wasikie na kuthibitisha kile wanachokiomba. Hii ni sawa na kosa wanalolifanya wanafiki wanapoomba hadharani ili tu watu waweze kuwasifia. Itakuwa pia ni kosa linalofanana kuwataka watu wajue ni kwa kiasi gani umeomba au unaomba mapema wakati gani ili wakusifie wewe. Haya ni majivuno ya kiroho na yatakuzuia katika uhusiano wako na Mungu.

Yesu alisema kwamba muda wako mwingi wa maombi unapaswa uwe mahali pa siri.

### (3) Maombi yasiyohusisha hisia

> Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi (Mathayo 6:7).

Kwenye dini za kipagani maombi yanakuwa ni vifungu vya maneno vya kurudiarudia mara kwa mara. Wapagani hutegemea kumiliki miungu yao kwa njia za miujiza na au uchawi usiyokuwa na hisia.

Mungu hasogezwi kimawazo na maombi yetu. Yeye ni hai ya mtu. Kwa hiyo, hatusemi kama ina nguvu ya uchawi ndani yao wenywewe. Usiruhusu maombi yako kukosa hisia.

### (4) Kutokusamehe

> Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu (Mathayo 6:15).
>
> "Basi, nataka wanaume wasalishe … pasipo hasira…" (1 Timotheo 2:8).

Mahusiano yako na watu wengine huathiri uhusiano wako na Mungu. Kama hauko tayari kusamehe watu wengine, basi huwezi kumtegemea Mungu awe wa msamaha kwako. Kusamehe maana yake ni kuwa tayari kwa ajili ya kuifuta adhabu ambayo walikuwa wanastahili.

Bila ya kuwepo na neema ya kusamehe, hatuwezi kuendelea kuwa kwenye uhusiano na Mungu.

### (5) Kutokiri kwa watu wengine mambo mabaya uliowafanyia

> Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako (Mathayo 5:23-24).

Yesu alisema kwamba sadaka kwa Mungu haipaswi kutolewa wakati ukiwa unajua kwamba una hatia ya kosa kwa mwingine. Unapaswa kwenda kuomba msamaha na kufanya malipizi kwanza yanayostahili, ndipo sadaka yako kwa Mungu itakapopata kibali.

Hatutoi sadaka kama ambavyo walikuwa wanatoa wakati ule wa zamani, lakini huwa tunamwabudu Mungu. Ili ibada yetu ya kumwabudu Mungu iweze kukubaliwa na yeye, ni lazima kwanza tukiri makosa ya aina yeyote ambayo tumewakosea watu wengine.

> Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe (1 Petro 3:7).

Mume anapaswa kumtendea mke wake kama kitu ambacho ni cha thamani na kidhaifu. Kama ni mtu asiyefikiria kuhusu udhaifu wake, maombi yake yatazuiliwa.

Kanuni hiyohiyo inatumika kwa mtu mwingine yeyote ambaye una mamlaka juu yake. Kama huna upendo, ni mgandamizaji, na usiyefikiria kuhusu hisia na haki za mtu mwingine, Mungu hapendezwi na wewe, na itakuwa vigumu sana kwako kuweza kufanya maombi.

**(6) Kushindwa kung'ang'ania**

> Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa (Mathayo 7:7).

Kwa mujibu wa kategoria ya kisarufi ya Kiyunani kuhusiana na vitenzi hivi, yule anayeendelea kuomba hupewa, anayeendelea kutafuta hupata, na anayeendelea kubisha hodi, mlango utafunguliwa.

Yesu alikuwa anaweka mkazo wa kuendelea kudumu kwenye maombi. Mara nyingi watu huomba mara moja au mbili tu, kisha husahau. Hawaombi katika muda mrefu wa kutosha ili hata kuweza kutambua kama maombi yao yako kulingana na mapenzi ya Mungu.

Endelea kudumu kwenye maombi kwa kutumia orodha ya mambo ambayo umekusudia kuyaombea. Orodha itakusaidia wewe kuweka umakini kwenye maombi katika nyakati ambazo wewe umechoka au unapambana na mawazo yanayokutatanisha.

Fikiria kuhusu jambo hili: "Inawezekana nisiweze kusikia kutoka kwa Mungu kila siku, lakini ninahakikisha kwamba yeye Mungu ananisikia mimi kila siku."

**(7) Kukosa Utii.**

> Na lo lote tuombalo, twalipokea kwake, kwa kuwa twazishika amri zake, na kuyatenda yapendezayo machoni pake (1 Yohana 3:22).

Aya hii inaonyesha kwamba utii ndiyo msingi wa imani. Utii huonyesha kwamba tunampenda Mungu, kwa hiyo ni jambo la muhimu kwenye uhusiano wetu na Mungu. Kutokuwa mtiifu kunaonyesha kukosekana kwa upendo kwa ajili ya Mungu ambako kutazuia maisha ya maombi.

### (8) Nia za dhambi

> Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu (Yakobo 4:3).

Mtu aliye na matamanio ya kutenda dhambi hawezi kuona mambo katika mtazamo wa Mungu na kuomba kwa uaminifu kwa ajili ya kile ambacho Mungu anakiona kama kinachofaa. Mtu huyu hutamani mambo ya dunia na hujaribu kumtumia Mungu kama njia ya kujipatia vitu hivyo.

Mkristo anapaswa awe na uwezo wa kutaka kutoka Mungu mambo yaliyo mazuri. Roho Mtakatifu atamwongoza kuomba kulingana na mapenzi ya Mungu.

N lazima tuwe tayari kutii na tuwe tayari kwa ajili ya yeye kuturidhisha mioyo yetu katika njia yake mwenyewe.

### (9) Kutokuamini

> Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao (Waebrania 11:6).

Kwa kutokuamini ahadi za Mungu ni kutilia mashaka mwenendo wake. Uhusiano na Mungu katika maombi huongeza imani yetu kwake.

## Mawazo ya Kuhitimisha

Wakati mwingine watu hushindwa kushughulikia kizuizi na hata hukaribia kuacha kuomba kabisa. Vizuizi hivi vyote vinaweza kuepukwa kwa msaada wa Mungu.

Mtu atapaswa atafute tatizo liko wapi anapokuwa ametambua kwamba hana hamu tena ya kuomba, au mara nyingi hajisikii tena kuwa katika maisha ya kiroho kwenye maombi yake.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Shirikisha ni kitu gani ambacho wakati mwingine kimekuwa ni kizuizi kwenye maisha yako ya maombi. Waulize watu wengine waangalie kwenye orodha inayowezekana kuwa ni vizuizi na ruhusu pia washirikishe uzoefu wao.*

► Tengeneza mambo maalumu ya kufanya yenye lengo la kuleta suluhisho la kuondokana na vizuizi vilivyopo kwa wakati huu.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunipa mimi kibali cha kuongea na wewe.

Ninahitaji nikufurahishe wewe kwa matendo yangu dhidi ya watu wengine. Ninataka niwe mnyenyekevu na mwenye kusamehe. Ninataka niwe mtu wa kuendelea kudumu kwenye maombi hadi pale utakaponionyesha mimi ni kitu gani unataka kufanya kuhusiana na ombi langu.

Ninataka sababu zangu za kufanya jambo lolote ziwe za uaminifu na zilizo safi. Ninataka niombe kwa imani kwa ajili ya mapenzi yako kutimizwa.

Baba, ninathamini muda wangu nikiwa na wewe. Nisaidie katika kuepuka mambo ambayo yatakuwa ni kizuizi cha uhusiano wangu na wewe. Naomba unifundishe jinsi ya kuomba.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma 1 Timotheo 2:1-8. Kutoka katika kifungu hiki, ni kwa jinsi gani unaweza kuelezea tabia au hulka ya mtu ambaye anaweza kuomba kama Mungu anavyomtaka afanye?

# Somo la 22
# Mahusiano

## Wazo Kuu

“Kanuni za Mungu zinaniongoza na kukamilisha mahusiano yangu.”

## Malengo ya Somo

Kutendea kazi kanuni za upendo, amani, na heshima.

## Utangulizi

Huwezi ukawa na sifa za Mkristo za uvumilivu na msamaha bila ya kuwa kwenye uhusiano na watu wengine.

► Je, ni sifa na shughuli gani nyingine za Mkristo ambazo watu wengine wanahitajika wahusike? *(Upendo, umoja, ushirika, uwajibikaji, upole, huruma.)*

Mambo haya huanza wakati kukiwepo na mahusiano na watu wengine. Sifa zake zinaweza zikaendelezwa na kudhihirishwa tu kwenye mahusiano. Hiyo inamaanisha kwamba mahusiano na watu yana matokeo zaidi sana kwenye maendeleo yetu ya kiroho.

Kuna takribani kanuni tatu katika Maandiko ambazo zinatumika kwenye kila aina ya uhusiano wa kibinadamu, ambazo ni: Amani, Upendo, na Heshima.

## Kanuni ya Amani

> Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao (Waebrania 12:14).

Aya hii inaelezea kwa uwazi sana umuhimu wa mahusiano. Utakatifu umeunganishwa kwa karibu sana kuitafuta amani na kila mtu.

Kuitafuta amani, angalau itakupasa umtendee kila mtu jambo ambalo unapaswa ulifanye kwake. Kwa wale ambao unapaswa uwape shukrani, heshima, au utii, ni lazima uwape. Kama hutafanya hivyo, una hatia ya kusababisha mgogoro. Kama utashindwa kutimiza wajibu wako, kutekeleza ahadi zako, kulipa kile ambacho unapaswa ulipe kwa watu wengine, utakuwa huitafuti amani. Unapokuwa umetambua kwamba umeshindwa kila ambacho ulipaswa kutoa, inakupasa utafute msamaha na utekeleze au utimize wajibu wako kwa kiasi kikubwa kadri utakavyoweza.

Lakini kuitafuta amani kunahitaji zaidi ya kutoa unachodaiwa. Hii inajumuisha pamoja na kuwa na upendo na wema usiodaiwa.

Kama utakuwa unataka amani utatafuta upatanisho wakati kunapokuwepo na mgogoro, Utakuwa tayari kusamehe na au kusamehewa. Hutakuwa na haraka ya kudhania kwamba haitawezekana kurejesha amani. Hutakubali kirahisi utengano wa kudumu.

Yesu alisema kwamba ni lazima kwenda kwa mtu aliyekukosea na umwelezee kile alichokukosea (Mathayo 18:15). Kama unaona kwamba jambo lenyewe ni dogo sana lisilohitaji kukabiliana, basi hupaswi kuwaeleza watu wengine kuhusiana na jambo hilo au kuwa na chuki dhidi ya mtu huyo aliyekukosea.

Yesu alisema ni lazima tuwe tayari kusamehe 7 mara 70 (Mathayo 18:21-22). Sababu ya kawaida ya watu huacha kanisa na kukata tamaa ya kuishi maisha ya kiroho ni kutokana na chuki ya kutendewa vibaya na Wakristo wenzake. Chuki mara nyingi huja kabla ya aina nyingine za kushindwa kiroho.

Wakati mtu anapokataa kusamehe, anaweka sehemu fulani ya maisha yake kwenye mgongano na Mamlaka ya Mungu, kwa kuwa Mungu anatutaka sisi tuweze kusamehe. Eneo hilo huwa ni himaya ambayo Shetani anaweza kusababishia athari sehemu nyingine za maisha. Kama mtu atakataa kusamehe, muda mfupi sana unaofuata hatakuwa na uwezo wa kuzuia majaribu ambayo kwa ujumla yataonekana kutokuwa na uhusiano kabisa.

Msingi wa kila kosa binafsi ni thamani ya haki zetu. Kwa kuwa tunaamini kwamba tunastahili kutendewa jambo fulani au kupewa heshima, tunajiona kuwa tumekosewa tunapokuwa hatujaipata haki hiyo. Tunaamini tunastahili kupokea mambo yaliyo bora zaidi kuliko tunayopata.

Msingi mkubwa wa kusamehe watu wengine ni kuwa na ufahamu kuhusu ukombozi. Kukomboa inamaanisha kwamba kurejesha tena kwa kununua. Kwa vile Mungu ametukomboa sisi, sisi ni mali yake, na haki zetu ni mali yake. Ni lazima kwa makusudi kabisa tuweze kutoa haki zetu kutoka kwa Mungu. Unaweza ukaomba, "Bwana, Ninatambua kwamba haki zangu zote ni mali yako. Ninakuomba wewe uchukue udhibiti juu yake na unipe kile tu unachoona kwamba ni kizuri kwangu mimi kuwa nacho." Kisha, watu watakapokuwa wanakutendea vizuri, unaweza ukamshukuru Mungu kwamba ameruhusu fadhila hiyo kwa ajili yako. Wakati mtu anapokutendea mambo mabaya, unaweza ukakumbuka kwamba Mungu anao udhibiti wa haki zako, na aliona kwamba unaweza ukakuzwa zaidi bila ya kuwa na haki hiyo kwa wakati huo.

Washauri wa kidunia mara kwa mara hutoa ushauri unaolenga katika kukusaidia wewe kumdhibiti na kumbadilisha mtu ambaye anakusababishia matatizo. Hicho siyo kipaumbele.

Kwa kusamehe watu wengine, unajiachilia kwa Mungu na unamruhusu akuendeleze wewe kadri anavyoona inafaa. Kanuni ya kusalimisha haki zako kwa Mungu inatumika kwenye kila uhusiano wa kibinadamu. (Kumbukumbu rejea nyingine kuhusu msamaha zinapatikana katika Wakolosai 3:13, Mathayo 6:15, and Warumi 12:19.)

## Kanuni ya Upendo

Mtu ambaye hatuwiwi chochote na yeye bado ni lazima tumtendee kwa upendo. Kwa kuwa tumeipokea neema, sisi tuna deni kwa Mungu. Hatuna uwezo wa kumlipa. Mungu hana mahitaji yeyote, lakini ametuagiza tutoe kwa ajili watu wengine upendo wasiostahili ambao sisi tuliupata kutoka kwake.

> Msiwiwe na mtu chochote, isipokuwa kupendana (Warumi 13:8).

Upendo ni uhakikisho au ushahidi kwamba mtu ni Mkristo kamili.

> Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona (1 Yohana 4:20).

Kuna upendo maalumu miongoni mwa Wakristo walioamini, na Yesu huyachukua yeye mwenyewe matendo yako na tabia zako dhidi ya waamini wengine. Atasema katika siku ya hukumu, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi" (Mathayo 25:40).

Lakini upendo wa Kikristo haupaswi uelekezwe tu kwa Wakristo wengine.

Katika Mathayo 5:44-45 Yesu alisema,

> Lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.

Watu wengine wanapata shida kuwa na huruma kwa wale wanaowaudhi, lakini kamwe hakuna msamaha kwa kuwa mkatili. Hatupaswi tuwatendee watu kama wanavyostahili kwa maudhi yao. Tunapaswa tuwatendee kwa upendo na huruma ikiwa wanaonekana wanastahili au hata kama hawastahili. Tunahitajika tukumbuke kwamba hapo zamani tulipokuwa waasi, hatukustahili upendo wa Mungu, lakini pamoja na kuwepo kwa hali hiyo bado alitupenda (Tito 3:2-3).

## Kanuni ya Heshima

► Je, kama nitakupa bure noti ya dola mia moja iliyochafuka na kuchanika utaipenda? Je, utaikataa kwa sababu imechafuka na imechanika?

Je, utapenda kuichukua kwa sababu thamani yake iliyo nayo haitegemei na hali ya noti hiyo ilivyo?

Kila mtu anastahili heshima kwa sababu wanadamu wameumbwa kwa mfano na sura ya Mungu (Mwanzo 1:27). Sura ya Mungu inampa kila mtu thamani ya kuwa mrithi.

Hata kama mtu atakuwa hana akili sana, au anakosa vipaji, mafunzo, na chochote kile ambacho kingeweza kumfanya afanikiwe au aweze kutumika kwenye viwango vya kawaida, ana thamani kwa sababu ni mtu aliyefanyika katika sura ya Mungu.

Thamani ya asili ya mtu aliyo nayo hubakia hata kama ameishusha chini kwa kuchagua njia za kipumbavu. Huenda aliacha shule, ameharibu afya yake, na ameanzisha mazoea mabaya, lakini ana thamani kama mtu mwenye nafsi isiyoweza kufa iliyo katika mfano wa Mungu.

Kwa sababu ya thamani ya asili ya sura ya Mungu iliyo ndani ya mwanadamu, heshima ni lazima idhihirishwe kwa kila mawasialiano na watu. Kiwango cha chini kabisa cha kuonesha heshima ni adabu.

Hila au udanganyifu ni makosa, kwa sababu kila mtu hufanya uchaguzi mbalimbali pamoja na matokeo ya milele na anahitaji kujua mambo halisi kwa ajili ya uamuzi unaofanywa. Kumfanya mtu afanye kitu sahihi kwa sababu mbaya siyo mafanikio, kwa kuwa bado hajafanya chaguo lililo sahihi.

Kwa kiasi kikubwa kadri itakavyowezekana, tunapaswa tumtendee mtu kwa heshima hata kama tabia yake ni mbaya. Hata usahihishaji wa makosa na utoaji wa adhabu kwa kufanya makosa (kwa wale wenye mamlaka kamili ya kufanya hivyo) hufanyika kwa ufahamu kwamba sisi tunashughulika na viumbe vyenye nafsi zisizoweza kufa zikiwa na kitu chenye asili ya Mungu.

## Hitimisho

Biblia hutoa maelekezo kwa ajili ya mahusiano yaliyo katika msingi wa kanuni za amani, upendo, na heshima. Kuna maelekezo ya mahusiano kati ya waume na wake, wazazi na watoto, waajiri na waajiriwa, wachungaji na makanisa, na wazee na vijana.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Kunapaswa kuwepo na mifano mingi kwa ajili ya kuzitumia kanuni hizi.*

*Shirikisha na uliza mifano ya ni lini mtu ameweza kujitahidi kutafuta amani.*

*Shirikisha kikundi na kuwaomba watoe ahadi ya kusamehe watu ambao wamekuwa na machungu dhidi yao.*

► Taka kujua hali ambayo mtu atapaswa kumwonyesha mtu fulani upendo zaidi sana kuliko itakavyoonekana kustahili.

► Jadili inamaanisha nini kumtendea mtu kwa heshima hata kama tabia yake ni mbaya.

### Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie mimi kuishi kwa mujibu wa kanuni za kimaandiko za amani, upendo na heshima kwenye mahusiano yangu yote.

Ninataka niwe mtu wa kusamehe kwa wale wote wanaonitendea mabaya. Nisaidie katika kutafuta upatanisho na wale ambao wako kwenye mgogoro na mimi.

Ninataka niwe na upendo kwa ajili ya watu wengine juu ya kiwango cha hali ya juu cha uvumilivu wa mwanadamu.

Nisaidie mimi kuheshimu kila mtu kama uliyemfanya kwa sura yako.

Amina.

### Kazi ya Kufanya

Soma Waefeso 5:22–6:9 kwa ajili ya maelekezo ya mahusiano ya aina mbalimbali. Orodhesha ni mambo gani tofauti utakayoyafanya kwenye mahusiano yako.

# Somo la 23
# Mtindo makini wa maisha ya Kikristo

## Wazo Kuu

"Maisha yangu ya kila siku yanaonyesha kwamba niko makini katika kumpendeza Mungu."

## Malengo ya Somo

Kujifunza kanuni tisa ambazo zinatuongoza sisi kwenye maamuzi maalumu ya mfumo wa maisha.

## Utangulizi

► Je, ulishawahi kuona tofauti zilizopo kati ya Wakristo, hasa kwenye masuala ya vitendo ya kile wanachokifanya na kile ambacho hawakifanyi? Je, ni kwa nini kuna tofauti hizi wakati wanatumia Biblia moja inayofanana? Kwa kuwa kuna tofauti nyingi sana miongoni mwa Wakristo, je, inajalisha ni nini tunachokifanya? Kwa nini?

Siyo Wakristo wote wanaokubaliana juu ya maelezo ya kuishi kwa mujibu wa kanuni na maadili ya kibiblia. Hata hivyo, Mkristo ni lazima awe na umakini wa kuishi kufuatana na kile anachokiamini.

Tabia, uchaguzi wa mambo ya burudani, na mavazi vyote hivi vinaonyesha kitu fulani kuhusiana na mielekeo ya moyo.

Hapa kuna baadhi ya kanuni ambazo kila mwamini anapaswa kukumbuka anapojaribu kutambua ni kitu gani kizuri zaidi kinachofaa kwenye masuala maalumu ya mfumo wa maisha.

## Kanuni kwa ajili ya Maamuzi ya Mfumo wa Maisha

### (1) Ni lazima tutii maagizo yote ya Biblia yaliyoko kwa ajili ya Wakristo.

Yesu alisema katika Mathayo 5:19,

> Basi mtu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni.

Hatuwezi tu tukarahisisha kuchagua zile pointi ambazo tunafikiria kwamba ni muhimu zaidi. Hakuna agizo lolote la kimaandiko ambalo linapaswa kupuuzwa kwa kukosa umuhimu.

### (2) Maagizo ya Mungu ni kwa ajili ya faida yetu wenyewe.

Kumbukumbu la Torati 10:12-13,

> Na sasa, Israeli, Bwana, Mungu wako, anataka nini kwako, ila umche Bwana, Mungu wako, na kwenda katika njia zake zote, na kumpenda, na kumtumikia Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote; kuzishika amri za Bwana na sheria zake, ninazokuamuru leo, upate uheri?

Mungu hawezi akaacha kutuonyesha kitu ambacho ni kizuri kwetu, au hatuamuru agizo ambalo lina madhara kwetu. Hatuwezi tukawa katika hali iliyo nzuri zaidi pasipokuwepo na vikwazo vyake. Kukataa maelekezo yake ni kutilia mashaka hekima na upendo wake. Tunathibitisha kwamba kweli tuna imani katika wema na hekima wakati tunapotii maelekezo ya Neno lake badala ya kufuata mawazo ya binadamu.

**(3) Uhuru wa Mkristo siyo Uhuru wa Kutii Mungu.**

Paulo aliandika hivi katika 1 Wakorintho 9:21:

> Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria.

Tumekombolewa kutoka katika mfumo wa sheria – mfumo wa Musa na mahitaji ya Mungu ya utashi – kama njia ya kuhesabiwa haki, kwa sababu tunaokolewa kwa neema na siyo kwa kutimiza amri za Mungu. Pia Tumekombolewa kutoka katika hukumu ya sheria, kwa kuwa dhambi tulizotenda zimesamehewa.

Hata hivyo, hatujawekwa huru kutoka katika hitaji la kumtii Mungu, Kama aya hapo juu inavyoonyesha, tuko chini ya mamlaka ya Mungu. Mapenzi ya Mungu kwetu yamefunuliwa katika Biblia.

> Na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki (Warumi 6:18).

**(4) Kama tunampenda Mungu, tunataka tuyajue mapenzi yake, na siyo kuyakwepa.**

1 Yohana 5:2-3 anasema,

> Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito.

Mtu anayempenda Mungu kwanza hatauliza, “Je, Mungu ataweza kunihukumu mimi kawa ajili ya kutenda hivi?” lakini, “Ni jambo gani ambalo Mungu atapendezwa analo zaidi kwangu?” (Wakolosai 1:10).

**(5) Maandiko yanatoa msingi wa kuweka sheria mahususi kwa ajili ya maisha yetu.**

Biblia haitoi kanuni za ujumla tu. Baadhi ya vifungu vimeorodheshwa kwenye kazi za kufanya ambazo hutoa msingi wa Kikristo wa kuishi kwa uangalifu. Baadhi ya hizo hutoa miongozo maalumu kwa ajili ya mfumo wa maisha ya Kikristo.

**(6) Sheria kuhusu mambo mengi ya maisha siyo imani zetu muhimu zaidi.**

Mafarisayo walifanya kosa la kuweka mkazo zaidi juu ya mambo madogo madogo. Katika Mathayo 23:23, Yesu aliwaambia,

> Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache.

Aya hii haisemi kwamba kuna ukweli wowote ambao haujalishi, bali inasema kwamba mambo mengine ni muhimu zaidi kuliko mengine. Tunapaswa kuzungumzia zaidi kuhusu mambo yaliyo muhimu.

**(7) Kushika sheria hakutoshi kuthibitisha utii na upendo wetu kwa Mungu.**

Katika mjadala huo huo na Mafarisayo Yesu alisema (Mathayo 23:25),

> Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na chano, na ndani yake vimejaa unyang'anyi na kutokuwa na kiasi.

Mtu anaweza kushika viwango vingi lakini asiwe na upendo kwa Mungu au hata kumtii kikamilifu. Kwa upande mwingine, mtu anaweza kumpenda Mungu kwa moyo wake wote na bado asione sababu ya viwango fulani. Kwa hiyo, mtu anayeshika viwango vingi si lazima awe wa kiroho zaidi.

**(8) Uhakika wetu katika ushuhuda na watu wengine hautegemei mambo madogo madogo yanayohusiana na mfumo wa maisha yao.**

Katika Warumi 14:10 Paulo aliwauliza Wakristo:

> Lakini wewe je! Mbona wamhukumu ndugu yako? Au wewe je! Mbona wamdharau ndugu yako? Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu.

Aya hii inatoka kwenye kifungu kinachojadili maoni tofauti waliyo nayo Wakristo katika mambo ya vitendo. Kuna kutokukubaliana kwa dhati kuhusu kile ambacho Mkristo anapaswa kufanya na kile ambacho hapaswi kufanya.

Mwamini mwingine anaweza asikubaliane na tafsiri yetu ya kifungu fulani cha Maandiko, na asiweze kuona ubaya na au madhara ya kitu ambacho tumekikataa. Huenda ikawa kwamba Mungu anafanya kazi katika nyanja tofauti za maisha yake, au kwamba Mungu amemweka

katika muktadha fulani wa kitamaduni. Hiyo haimaanishi kwamba mtu huyo anayehusika siyo Mkristo wa kweli.

**(9) Uvumilivu wa maoni tofauti hauna msamaha kwa uzembe binafsi.**

"Kila mtu na athibitike katika akili zake mwenyewe." (Warumi 14:5b).

> "Lakini aliye na shaka, kama akila, amehukumiwa kuwa ana hatia, kwa maana hakula kwa imani. Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi." (Warumi 14:23).

Kunakuwepo na matokeo mabaya wakati mtu anapokiuka dhamiri yake mwenyewe. Kama mtu ataamua kufanya jambo fulani analilofikiria yeye mwenyewe kwamba siyo sahihi, ana hatia ya dhambi. Kunazo baraka ambazo wakati mtu anapotembea katika maisha ya nuru ambayo amepewa na Mungu (1 Yohana 1:7).

### Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Hakutakuwa na ugumu katika kuanzisha majadiliano yanayohusiana na mada hii. Wanafunzi wengine wanaweza wakasisitiza haja ya makanisa kuhitaji kuwepo na kanuni zinazohusu tabia. Wanafunzi wengine wanaweza kusisitiza kuhusu kuvumiliana katika tofauti zilizopo.*

*Jaribu kupata uzingatiaji wa haki kwa kila kipengele cha kanuni tisa zilizoorodheshwa hapo juu.*

► Uliza, "Ni kanuni gani kati ya hizi ambazo unafikiri kwamba watu wengi wanasahau?"

► Uliza, "Ni kanuni gani kati ya hizi ambazo unadhani kuna uwezekano mkubwa zaidi wa wewe kuzisahau?"

### Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie niishi kwa kukubaliana na maagizo ya Neno lako. Ninajua kwamba kila kitu unachoamrisha ni muhimu.

Nisaidie niwe mwaminifu kwenye dhamiri yangu, kwa chochote ambacho watu wengine wanakifanya. Niwezesha kuwa na tabia ya Kikristo dhidi ya wale watu wote ambao hawakubaliani na mimi.

Ninataka imani yangu ijionyehe kwenye kila kitu nitakachokuwa ninafanya. Nisaidie mimi katika kila eneo la maisha yangu katika kuchagua mambo ambayo yatafanya maisha yangu yawe mfano wa neema yako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari kuhusu Maandiko yafautayo ambayo yanatoa msingi unaohusiana na tabia ya uangalifu ya Mkristo:

- 1 Wakorintho 6:19-20
- 1 Wakorintho 10:31
- 1 Wakorintho 11:14-15
- 1 Timotheo 2:9-10
- 1 Petro 3:3-4
- Kumbukumbu la Torati 22:5
- Zaburi19:14
- Zaburi101:3

Je, ni viwango gani vya binafsi utakavyotakiwa kuzingatia kwenye Maandiko hayo?

# Somo la 24
# Usemi wa Mkristo

## Wazo Kuu

"Kuna kanuni za kibiblia za mazungumzo yangu."

## Malengo ya Somo

Kujifunza kanuni tisa za kimaandiko zinazosaidia mazungumzo ya Mkristo kumpa Mungu utukufu.

## Utangulizi

Kuna msemo wa zamani unaosema, "Kalamu ina nguvu kubwa sana kuliko upanga."

► Je, hiyo inamaanisha nini?

Hiyo inamaanisha kwamba kuna nguvu kubwa sana katika wazo, katika kushawishi, na kwenye mawasiliano. Unaweza ukakamilisha zaidi sana kwa kuwapa watu motisha badala ya kuwalazimisha. Wazo – au – maudhui yanaweza kuenea na kushawishi watu wengi.

Biblia inazungumzia kuhusu nguvu ya maneno kuweza kufanya mema au mabaya. Mpango wa wokovu unakamilishwa na nguvu ya injili, iliyodhaminiwa kwa wanadamu wa kupeleka ujumbe.

## Kanuni za kibiblia za Mazungumzo.

Ni kwa jinsi gani tunaweza kuyatumia maneno katika kukamilisha mambo yaliyo mema na kuepuka yanayoleta madhara? Biblia inatoa kanuni kadhaa:

**(1) Usiwe mtu mwongeaji sana.**

> Mpumbavu huongeza maneno... (Mhubiri 10:14).
>
> Katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na maovu; Bali yeye azuiaye midomo yake hufanya akili (Mithali 10:19).
>
> Hata mpumbavu akinyamaza, huhesabiwa hekima; Akifumba midomo yake, huhesabiwa ufahamu (Mithali 17:28).

Kwa hiyo, usiwe mtu wa kuongea sana. Mtu anayezungumza sana hathamini sana maneno yake mwenyewe au maneno mengine. Husema maneno ambayo ukweli hakuwa amemaanisha, na anadhania kwamba watu wengine wanafanya vivyo hivyo. Anatoa mawazo yako bila ya kuwa na ufahamu wake. Hupaswi kutoa maoni yako kuhusu jambo lolote usilolijua; siyo kila maoni yanayotolewa yana maadili yanayofanana.

**(2) Usizungumze kabla ya kufikiria.**

Usiruhusu hisia zako zikusababishe wewe kutoa kauli ambazo baadaye utazijutia.

> Hayo mnajua, ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika (Yakobo 1:19).

> Mpumbavu hudhihirisha hasira yake yote; Bali mwenye hekima huizuia na kuituliza (Mithali 29:11).

> Asiye mwepesi wa hasira ana fahamu nyingi; Bali mwenye roho ya hamaki hutukuza upumbavu (Mithali 14:29).

**(3) Usihukumu unapoona jambo kwa mara ya kwanza.**

> Yeye ajibuye kabla hajasikia, Ni upumbavu na aibu kwake (Mithali 18:13).

> Ajiteteaye kwanza huonekana kuwa ana haki; Lakini jirani yake huja na kumchunguza (Mithali 18:17).

Migogoro mingi hutokana na kutoelewana. Muda na kuwa mwangalifu kunaweza kutatua migogoro hiyo. Kama mtu mwenye sifa njema ya uaminifu akisema kitu ambacho kinaonekana ni kibaya kwako, usiwe mwepesi kumhukumu.

> Mtu apitaye na kujisumbua kwa ugomvi usio wake; Ni kama mtu ashikaye mbwa kwa masikio yake (Mithali 26:17).

**(4) Kuwa makini na mizaha.**

Kutokana na kile ambacho maneno yanaweza yakawa nacho, ndani yake, kichekesho kisichochodhibitiwa ni kama silaha iliyoko mikononi mwa mtu aliyepagawa.

> Kama mtu mwenye wazimu atupaye mienge, Na mishale, na mauti; Ndivyo alivyo amdanganyaye mwenzake, Na kusema, "Je! Sikufanya mzaha tu?" (Mithali 26:18-19).

Usisababishe watu wakafanya makosa makubwa kwa sababu ya kuuamini utani wako. Usiwaambie kwamba wewe uko makini wakati hauko hivyo – hawatakuamini tena. Usifanye mzaha kuhusu watu wenye ulemavu. Usichekelee makosa ya mtu. Usiseme utani unaofanya dhambi kuonekana kuwa sio kitu.

**(5) Usiseme jambo lolote kwa mtu asiyekuwa mhusika.**

Kuna hali nyingi ambazo jambo linaweza likajitokeza.

Mahusiano kwa ajili ya uwajibikaji wa kiroho yanahitaji usiri. Una uwezo mkubwa sana wa kusaidia na kuponya watu wengine kama utakuwa unaweza kuyaweka mambo kuwa ni ya siri. Watu hawatakuamini wewe kwa taarifa zako za binafsi kama watafikiria kwamba utaweza kuwaambia watu wengine.

Usitawanye taarifa zinazohusiana na makosa ya watu wengine.

> Mwenye kitango akisingizia hufunua siri; Bali mwenye roho ya uaminifu husitiri mambo (Mithali 11:13).

> Moto hufa kwa kukosa kuni; Na bila mchongezi fitina hukoma (Mithali 26:20).

Kuna nyakati nyingine ambapo inahitajika jambo fulani liweze kusemwa, lakini ikawa wewe siyo mtu sahihi unayetakiwa kulisemea jambo hilo. Huwezi ukasema neno mahali ambapo mwenye mamlaka ya kulisemea yuko hapo kwa ajili hiyo.

Mtu mwoga huwaelezea watu wasiohusika kuhusu mgogoro wake uliopo badala ya kufuata utaratibu ulioko katika (Mathayo 18:15-17).

> Ujitetee na mwenzako peke yake; Bali usiifunue siri ya mtu mwingine (Mithali 25:9).

**(6) Kuwa mwangalifu katika kutoa shutuma.**

Kuna muda sahihi wa kutoa shutuma kwa njia sahihi.

> Lawama ya wazi ni heri, Kuliko upendo uliositirika. Jeraha utiwazo na rafiki ni amini... (Mithali 27:5-6a).

Hakikisha kwamba shutuma zako zina lengo la kujenga na siyo kuharibu. Unapaswa uonyesha kwamba unamjali mtu unayemshutumu na kwamba unalo lengo la kutaka kumsaidia. Kimsingi, uhusiano wenye nguvu ni muhimu kabla shutuma zako hazijaweza kusaidia.

**(7) Usiwe mdanganyifu.**

> Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake (Wakolosai 3:9).

Udanganyifu uko kwenye maisha ya dhambi na siyo kwenye maisha ya Kikristo.

> Midomo ya uongo ni chukizo kwa Bwana; Bali watendao uaminifu ndio furaha yake (Mithali 12:22).

**(8) Mazungumzo au maneno yako yawe masafi.**

> ...wala aibu wala maneno ya upuuzi wala ubishi; hayo hayapendezi; bali afadhali kumshukuru (Waefeso 5:4).

Usitake kuelezea kuhusu kashfa za zamani au za sasa isipokuwa inapokuwa ni muda rasmi muafaka wa kushughulikia hali hiyo. Usiseme kwa utani jambo ambalo lilikuwa ni jambo la lazima linalopaswa kuelezea kwa siri. Watu wa dunia kwa kawaida hutumia maneno yanayohusika na kujamiana au maneno yanayohusiana na sehemu za siri za mwili kwenye mshangao wao, lakini hali kama hiyo siyo sahihi kwa Mkristo. Ni jambo la kipuuzi na kukosa

heshima kutumia maneno yanayomtaja Mungu au Yesu kama njia ya kushangaa wakati wa msongo wa mambo, isipokuwa kama unamwita Mungu kwa dhati ili akusaidie.

**(9) Usiwagawe watu kwa maneno yako.**

> Mtu mshupavu huondokesha fitina; Na mchongezi huwafarakanisha rafiki (Mithali 16:28).
>
> Kuna vitu sita anavyovichukia Bwana; Naam, viko saba vilivyo chukizo kwake... [kitu cha saba] Shahidi wa uongo asemaye uongo; Naye apandaye mbegu za fitina kati ya ndugu (Mithali 6:16, 19).

Usijaribu kujifanya uonekane kwamba wewe ni bora zaidi kwa gharama ya mtu mwingine. Usiibue migogoro kati ya watu wengine. Usitake kusababisha maumivu kwenye ufanisi wa huduma ya mtu mwingine kwa maneno ya umbeya.

Kabla ya kusema jambo usifikirie tu kwamba "Je, ni kweli?" lakini fikiria pia kwamba "Je, ni kwa nini niseme jambo hili?"

## Hitimisho

Mkristo anapaswa kuwa tayari kuomba msamaha kama atatambua kwamba ametenda mambo mabaya kwa maneno yake. Atapaswa awe tayari kusahihisha jambo lolote alilolisema ambalo anatambua kwamba halikuwa sahihi.

Maneno ya kuumiza na yenye kuleta maudhi kutoka kwa watu wengine hayawezi kuhalalisha maneno mabaya kutoka kwako.

Kuna baadhi ya makosa katika mazungumzo ambayo hatua kwa hatua unaweza kuyaboresha. Kwa mfano, unaweza kujifunza jinsi ya kufikiri kabla ya kuzungumza. Kuna makosa mengine ambayo yanaonesha kuwepo na tatizo ndani ya moyo, kama vile kutamani kumuumiza mtu mwingine kwa maneno yako. Kama wewe una hatia ya aina hiyo ya mazungumzo, unahitajika kumwomba Mungu akusamehe na autakase moyo wako uondokane na mwelekeo huo.

Maneno yanafunua mambo mengi yaliyoko kwenye moyo wako. Usiharibu ushuhuda wako wa Kikristo kwa kuzungumza katika njia ambayo haiendani na maadili ya Ukristo.

Mazungumzo yako yanaweza kuwa ni baraka kwa watu wote wanaokuzunguka na au walio karibu na wewe. Matokeo ya maneno yako yanaweza yakaongezeka sana kama utafuata kanuni za kibiblia.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Watu wengi huona makosa yaliyo kwenye mazungumzo ya watu wengine, lakini hawaoni makosa ya kwao wenyewe. Kiongozi anaweza akashirikisha mfano ambao wakati fulani alishindwa kufuata mojawapo ya kanuni hizi au angeweza kukiri ni kanuni ipi ambayo yeye amekuwa mdhaifu ndani yake. Watake wanachama wenzako wachague kanuni ambayo wanajiona ni wadhaifu ndani yake na wajitoe kabisa kwa ajili ya kufanya maboresho kwa msaada wa Mungu.*

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie kukumbuka athari ya mazungumzo yangu ninayoweza kuwa nayo, na niwezeshe kuwajibika kwa ajili ya maneno yangu. Ninataka maneno yangu yaweze kukamilisha mambo mazuri na siyo kuleta madhara.

Ninataka ushuhuda wangu ulio kwa ajili yako uweze kuheshimika.

Nisaidie katika kuwa msafi, mwaminifu, mkarimu na mwangalifu.

Asante kwa ajili ya kibali na fursa ya kuwasilisha ukweli wako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari Yakobo 3. Tazama uwezo mkubwa wa mazungumzo ulioelezwa hapa. Kwenye aya za 13-18 ona jinsi mazungumzo yanavyotiririka kwa urahisi kabisa kutoka katika hali ya kiroho ya mtu.

# Somo la 25
# Maadili ya Kazi ya Kikristo

## Wazo Kuu

"Ninafanya vizuri sana nikiwa kazini kwa sababu Mungu ndiye mwajiri wangu."

## Malengo ya Somo

Kuona ni kwa nini Mkristo anapaswa kufanya kazi na ni sifa gani mfanyakazi wa Kikristo anatakiwa awe nazo.

## Utangulizi

► Je, Mkristo anatakiwa awe namna gani kazini tofauti na mtu asiyeamini?

Kanuni za uwajibikaji na uaminifu hutoa baadhi ya maadili kwa ajili ya Wakristo kutumia kwenye kazi zao.

► Je, Mkristo anapaswa kufanya kazi? Kwa nini?

## Mtazamo wa Kikristo juu ya Kazi.

Mkristo anapaswa kufanya kazi kwa sababu ana wajibu kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya watu wengine.

> Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwapo kwenu tuliwaagiza neno hili, kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi, asile chakula (2 Wathesalonike 3:10).

Mtu asitegemee watu wengine wachukue jukumu la kumwangalia yeye kama yeye mwenyewe hayuko tayari kufanya kile ambacho yeye binafsi anaweza kukifanya.

Je, ni kweli kwamba wako watu wengi ambao hawawezi kufanya kazi? Hapana. Kama mtu hana uwezo wa kufanya kazi ya kawaida kwa ajili ya kazi zinazoweza kumpatia mishahara, inawezekana kabisa akawa anafanya kitu kingine ambacho kinakidhi mahitaji ya watu wengine.

Mwamini ana wajibu kwa ajili ya familia yake mwenyewe.

> Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini (1 Timotheo 5:8).

Je, inakuwaje kama mahitaji ya mtu tayari unakuta yameshatolewa kutokana na utendaji kazi wake wa wakati uliopita, au kile ambacho alikuwa ameshapewa, au "anachopata kwa bahati njema"? Je, yuko huru kutoendelea kufanya kazi kwa sababu yeye mwenyewe hahitaji chochote? Hapana. Mwamini anaagizwa na Maandiko kufanya kazi ili kwamba aweze kukidhi mahitaji ya watu wengine.

> Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji (Waefeso 4:28).

Jaribu kuona tofauti iliyopo kati ya mtu mwizi, anayeiba na kuchukua kitu bure; na mtu mwingine ambaye anafanya kazi ili aweze kutoa. Mkristo siyo yule asiyeiba tu, bali ni yule ambaye anafanya kazi ili apate cha kutoa.

Kwa hiyo mwamini anapaswa kufanya kazi ili aweze kujiwezesha yeye mwenyewe na familia yake, na kutoa kwa ajili ya wengine ambao ni wahitaji.

Sasa tuangalie kwenye baadhi ya Maandiko ambayo yanatueleza jinsi Mkristo anavyopaswa kufanya kazi.

## Kanuni ya Uwajibikaji

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Waefeso 6:5-8 kwa ajili ya kikundi. Jadili maana ya kifungu hiki, kisha angalia orodha iliyoko hapa chini kwa ajili ya kuongezea kwenye uchunguzi wako.

Waefeso 6:5-8,

> Enyi watumwa, watiini wao walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo; Wala si kwa utumwa wa macho tu kama wajipendekazao kwa wanadamu bali kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo; Kwa nia njema kama kumtumikia Bwana wala si mwanadamu; Mkijua ya kuwa kila neno jema atendalo mtu atapewa lilo hilo na Bwana kwamba ni mtumwa au kwamba ni huru.

Neno *watumishi,* kama lililotumika katika Agano Jipya, linarejelea kuhusu watumwa. Hata hivyo, hilo haliwafanyi waajiri wa kisasa kuachana na dhana hio. Mfanyakazi anatofautiana na mtumwa kwa kuwa yuko huru zaidi kuhamia kwenye kazi nyingine tofauti. Uhuru huo humwezesha yeye kuweza kukubaliana au kukataa masharti ya kazi. Hata hivyo, mara tu anapokuwa amekubaliana kufanya kazi kwa ajili ya kupata manufaa fulani, anatakiwa na Maandiko kutumia maadili fulani katika kazi yake kwa kadri ile atakavyoendelea kubakia kuwa na mwajiri wake.

Kanuni zinazotokana na Waefeso 6:5-8:

1. Mfanyakazi anapaswa kumtii mwajiri wake, siyo tu kwa wakati anapokuwa anatazamwa, lakini kwa wakati wote. Hiyo pia inamaanisha kwamba hapaswi kupuuzia yale mambo ambayo ana uhakika kwamba hayakaguliwi. ("… Wala si kwa utumwa wa macho…")

2. Mfanyakazi anapaswa adumishe ubora na bidii ya kazi yake kana kwamba anafanya kazi kwa ajili ya Mungu. ("…Kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo…")

3. Mfanyakazi atabarikiwa na Mungu kwa ajili ya uaminifu katika kazi yake. ("Atapewa lilo hilo na Bwana …")

## Kanuni ya Uaminifu

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Tito 2:9-10 kwa ajili ya kikundi. Jadili maana ya kifungu hiki, kisha angalia orodha iliyoko hapa chini kwa ajili ya kuongezea kwenye uchunguzi wako

Tito 2:9-10.

> Watumwa na wawatii bwana zao, wakiwapendeza katika mambo yote; wasiwe wenye kujibu, [kubishana au kujibu kusikokuwa na heshima];
>
> Wasiwe waibaji [wezi]; bali wauonyeshe uaminifu mwema wote, ili wayapambe mafundisho ya Mwokozi wetu Mungu katika mambo yote.

Kanuni zinazotokana na Tito 2:9-10:

1. Mfanyakazi anapaswa kuwa na heshima katika kuitikia kwake kwa ajili ya maelekezo ya mwajiri wake ("...wasiwe wenye kujibu...").

   ► Je, kuna matokeo gani wakati mfanyakazi anapokuwa anazungumza na pasipo heshima kuhusu mwajiri wake kwa wafanyakazi wengine?

2. Mfanyakazi hapaswi kumwibia mwajiri wake, hata kama anafikiri anastahili malipo zaidi ("...wasiwe waibaji...").

3. Kazi ya uaminifu ni ushuhuda kwa ajili ya injili; ukosefu wa uaminifu ni aibu kwa injili ("...ili wayapambe mafundisho ya Mwokozi wetu Mungu...").

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

*Katika somo hili, mwongozo wa kushirikishana umetolewa kwenye orodha mbili za vidokezo vya kutumia.*

*Mwanachama anapaswa kujichunguza mwenyewe kwa vigezo vya kutumia, na atafakari kama dhamira yake iko safi au laa.*

*Watake wanafunzi washirikishane kuhusu mabadiliko wanayojitolea kuyafanya kwa sababu ya kutumia vifungu hivi.*

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya kunipa uwezo wa kufanya kazi na fursa ya kazi.

Nisadie mimi katika kufanya kazi iliyo nzuri kwa ajili ya mwajiri wangu, kuonyesha heshima kwake, kuelewa nini anachokihitaji kutoka kwangu, na kufanya vyema hata wakati ambapo kazi yangu haipaswi kukaguliwa.

Nataka niwe mwaminifu kwa kile ninachopata, kuwajibika kwa ajili ya mahitaji yangu na kuweza kutoa kwa ajili ya kuwapa watu wengine msaada.

Nisaidie kukumbuka kwamba ninafanya kazi kwa ajili yako na kwamba malipo mazuri kabisa yanatoka kwako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari aya hizi kuhusiana na somo la kazi na uvivu:

- Mithali 6:6-11
- Mithali 10:4-5
- Mithali 12:11
- Mithali 12:24
- Mithali 12:27
- Mithali 13:4
- Mithali 13:11
- Mithali 14:23
- Mithali 18:9
- Mithali 20:13
- Mithali 22:29
- Mithali 24:30-34
- Mithali 26:13-16

# Somo la 26
# Kufanya Maamuzi Sahihi

## Wazo Kuu

"Maadili ya milele yanaongoza maamuzi yangu."

## Malengo ya Somo

Kujifunza maswali ambayo itapaswa kuyatafakari kabla ya kufanya uamuzi.

## Utangulizi

Hadithi inasimuliwa kwamba mhubiri aitwaye Charles Stalker alikuwa akiomba asubuhi moja wakati Mungu alipozungumza naye na kumwambia, "Nataka uende katika nchi ya China." Stalker alishangaa kwa sababu hakuwa na fedha za kumpeleka. Hisia ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba alifungasha begi lake la safari na akaenda kwenye stesheni ambayo safari ndipo ilipotakiwa ianzie. Mahali hapo palitokea mtu mmoja asiyemjua na kumwuliza, "Wewe ndiye Charles Stalker?" kisha akendelea kusema, "Nimetumwa hapa ni kiwa na tiketi ya kukupeleka uende katika nchi ya China."

► Je, hii ndiyo njia ambayo kwa kawaida tunamtegemea Mungu atuonyeshe mapenzi yake?

► Je, kungekuwa na tatizo kwa mtu kutarajia kupata mapenzi ya Mungu kwa maamuzi yake kwa njia hii?

Watu wengine hutegemea miongozo isiyo ya kawaida kwa kila uamuzi wanaoufanya. Wanapuuza kufikiri kuliko kwa kawaida na hali zilizopo, kwa sababu wanadhani kwamba mapenzi ya Mungu yatakuwa kinyume na kufikiri kuliko kwa kawaida na hali zilizopo.

Ni makosa kusisitiza kwamba Mungu ni lazima atoe ufunuo usiokuwa wa kawaida kwa ajili ya maamuzi yetu kwa sababu mara nyingi haonyeshi mapenzi yake kwa njia hiyo. Mtu akipuuzia sababu na hali zilizopo, anaweza akafikiri kwamba anapata maelekezo kutoka kwa Mungu wakati kiuhalisia anafuata mihemuko au mawazo yake mwenyewe.

Wakati wowote jambo linapoamriwa na au kukatazwa waziwazi na Maandiko, tunayajua mapenzi ya Mungu. Hata hivyo, kuna maamuzi mengi katika maisha yaliyo njia mbadala ambazo kimsingi hazijaamriwa au kukatazwa na Mungu. Je, mtu anawezaje kujua mahali atakapoishi, kazi atakayokuwa nayo, na ni kwa jinsi gani anavyopaswa kutumia fedha zake?

Watu wengine, kwa sababu wanategemea kwamba mapenzi ya Mungu ni lazima yadhihirishwe mbali na sababu na hali zilizopo, wanatafuta njia isiyokuwa ya mantiki kwamba Mungu ataitumia kuwapa maelekezo. Wanaweza wakamwomba Mungu awape ishara maalumu ya kuonyesha mapenzi yake. Au wanaweza kufungua aya yeyote katika Biblia ambayo wataitumia kwenye hali yao.

## Ushauri ufaao kwa Kufanya Maamuzi Mazuri.

John Wesley alitoa maelekezo ya kivitendo ya jinsi ya kutambua mapenzi ya Mungu. Alisema kwamba maelekezo ya Mungu ya ujumla kwa ajili yetu, yaliyofunuliwa kwenye Biblia, yanatutaka tuwe watakatifu na tukamilishe mambo yaliyo mazuri. Kwa hiyo, **ili kufanya uamuzi mahususi, ni lazima tutafakari ni chaguo gani litakalotuwezesha zaidi kuwa watakatifu na kukamilisha mambo yaliyo mazuri zaidi.**

**Tunajifunza kutokana na uzoefu kwamba ni hali zipi zilizo na msaada kiroho kwa ajili yetu na ni zipi zilizo na madhara kwetu.** Hali nyingine zilizopo ni za hatari kiroho kwa mtu yeyote, lakini siyo kwa kila mtu. Kwa kadri tuwezavyo, tunapaswa tujiweke wenyewe kwenye hali ambazo zinatusaidia sisi kuwa watu wenye nguvu kiroho na tunapaswa kuepuka hali zozote ambazo zitaweza kutuletea sisi majaribu (1 Wakorintho 10:12-13).

**Kwa kuwepo na sababu na uzoefu, na kwa ushauri wa watu wengine, tunaweza pia tukatambua ni chaguo gani litakalotuwezesha kukamilisha mambo mazuri zaidi.**

Mungu kwa kawaida haonyeshi mapenzi yake kwa njia ya mafunuo maalumu. **Anatutegemea sisi tutumie kanuni za kimaandiko tunapokuwa tukitafakari kwa uangalifu na kuzipima hali zilizopo.** Roho Mtakatifu hutuongoza hata katika wakati ambao hatutambui jambo hilo. Kwa maamuzi mengi tusitazamie ufunuo bali tuombe kwa ajili ya kupewa hekima na ufahamu

Watu wanaodai miongozo maalumu kutoka kwa Mungu wakati mwingine huwa wanakataa kuwasikiliza watu wengine (Mithali 12:15). Wanaweza wakajawa na hasira wakati watu wanapohoji kuhusu maamuzi yao. Wanaonesha kiburi na ukaidi badala ya kuonesha unyenyekevu. Kwa kuwa wanajiona wao wenyewe kwamba wanaongozwa moja kwa moja na Mungu, wanapuuzia ushauri wa aina yeyote wa kibinadamu isipokuwa ule unaokubaliwa na wao.

Kwa maswali ambayo hayana majibu ya waziwazi kutoka katika Biblia, itakuwa jambo bora zaidi kwa mtu kutodai kila mara kwamba Mungu amemwelekeza jambo la kufanya. Litakuwa jambo jema kwake kusema kwamba anajaribu kupata jibu lililo bora zaidi. Kama akifanya makosa, itakuwa ni kuwachanganya watu kama atasema kwamba alikuwa na maagizo kutoka kwa Mungu. Pia, kwa kawaida, mtu hapaswi kukataa ushauri wa watu wengine kwa kudai kwamba ana ufahamu wa kipekee wa mapenzi ya Mungu.

Mbali na kanuni ambazo Wesley alizitoa, wakati unapokuwa katika kufikiri juu ya chaguzi zako, tafakari mambo yafuatayo:

1. **Je, zinaendana wazi na amri za Kiroho?** Mungu kamwe hapendezwi na wewe kutokulitii Neno lake.

2. **Je, zinaendana na vipaumbele vya Kimaandiko?** Biblia inatuonyesha sisi mambo ambayo ni muhimu kwa ajili ya Mungu. Je, uamuzi wako unazingatia mambo ya mwanzo kwanza?

3. **Je, zinaendana na mtazamo halisi wa hali zilizopo?** Unapaswa uwe na uwezo wa kuona jinsi Mungu ambavyo amekuwa akiandaa hali yako kwa ajili ya uamuzi huu.

4. **Je, ni jambo la busara?** Kwa nyakati fulani Mungu huenda akakuongoza kufanya jambo fulani ambalo halionekani kama ni la busara, lakini ikiwa kama ndivyo, ataweka wazi mapenzi yake. Kamwe usikatae sababu kama njia ya kukusaidia wewe kutambua mapenzi ya Mungu.

5. **Je, ni tabia ya Kikristo?** Usifikiri kwamba hali yeyote iliyopo ni ya kipekee sana kiasi kwamba unaweza ukafanya jambo lolote ambalo kwa kawaida litakuwa halimpendezi Mungu.

6. **Je, inaendana na kupenda watu wengine kama unavyojipenda?** Nia za ubinafsi zitapotosha utambuzi wako.

7. **Je, itakuwa na ushawishi mzuri?** Je, itakuwaje kama wengine watafanya kama wewe unavyofanya? Je, hiyo itakuwa vizuri?

8. **Je, inathibitishwa na washauri wa Mungu?** Sote tunajua jinsi ya kupata marafiki ambao watakubaliana na sisi, lakini watu ambao wanaonekana ni wa kiroho zaidi na wenye hekima watasema nini kuhusu uamuzi wako?

Wakati mapenzi ya Mungu ni jambo lisilo la kawaida sana, Mungu ana uwezo wa kuyafanya yajulikane kwako pasipokuwa na shaka yeyote. Malaika, au maono, au kichaka kinachowaka moto yameshawahi kutoa uhakika kwa baadhi ya watu hapo zamani. Mungu anaweza tu kutoa uhakikisho wa ndani usiokuwa na shaka lolote. Lakini inapotokea kwamba hakuna ujumbe ulio wazi uliopokelewa kutoka kwa Mungu, unapaswa ufuate kanuni za kuaminika kwa ajili ya kutambua chaguo sahihi. Usitegemee kupokea ufunuo maalumu kwa kila uamuzi. Kama kwa unyofu na kwa maombi unatafakari sababu kwa vipaumbele sahihi, Mungu atakuwa mwaminifu kuongoza uamuzi wako.

Katika Warumi 12:1-2 Paulo aliandika,

> Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

Aya hii inaonyesha jinsi hali ya kiroho ya mtu inavyoweza kuathiri maamuzi yake. Ili kupata mapenzi ya Mungu, ni lazima kwanza mtu ajitoe kabisa au kikamilifu kwa Mungu. Maamuzi ya Mkristo yanatofautiana sana na maamuzi ya walimwengu, kwa sababu, "yeye hafanani na ulimwengu" bali amegeuzwa na kufanya maamuzi kwa nia iliyofanywa upya.

Kusudi au nia ndio jambo muhimu zaidi katika kutambua mwelekeo wa Kimungu. Mtu anayetafuta mapenzi ya Mungu peke yake ili kwamba aweze kuwa na uamuzi wa kufanya au kutofanya yamkini atachanganyikiwa. Ikiwa mtu anatafuta mapenzi ya Mungu kulingana na njia za kimaandiko na zinazokubalika, na kwa azimio la moyo wote, hatakosa mapenzi ya Mungu.

## Kwa ajili ya Kushirikishana Kikundi

► Jadili baadhi ya kanuni za Wesley. Baadhi ya mifano inaweza ikawa na uchaguzi wa marafiki wa kutumia muda wako pamoja na wao, chaguzi za kuajiriwa, au mahusiano ya kuchumbiana (ikiwa hawajaoana). Fikiria, *"Je, ni hali gani itakayonisaidia mimi kuwa mtakatifu na kukamilisha mambo yaliyo mazuri zaidi?"*

► Watu wengine inaonekana hawawezi kudumisha utambulisho wao wa Kikristo wakiwa wameambatana na aina fulani za watu, au wakiwa kwenye maeneo fulani. Fikiria mifano mingine.

Dondoo zingine zinazoweza kujadiliwa ni:

► Jukumu la kuhamasisha katika kufanya maamuzi.

► Kosa la kusubiri ishara.

► Hatari ya kuamini hisia za ndani sana.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie nijifunze jinsi ya kukusikiliza wewe. Ninataka niwe mtakatifu na niweze kukamilisha mambo mazuri kwa kadri iwezekanavyo kwa ajili ya utukufu wa jina lako.

Uifanye nia yangu iwe safi, ili maamuzi yangu yasiweze kunipeleka mbali na mapenzi yako. Niongoze kupitia washauri wenye busara ambao umewaweka kwenye maisha yangu.

Nisaidie katika kuona mambo jinsi yalivyo na niwezeshe kufanya maamuzi yaliyo sahihi.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Chunguza Yakobo 4:13-17. Angalia ukuu wa Mungu jinsi ulivyo juu ya hali zilizopo. Je, ni ubaya gani, au majivuno gani ambayo yanarejelewa katika mstari wa 16? Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu kupanga kwa ajili ya siku zijazo?

# MASOMO YA KUKUZA UANAFUNZI

## KITABU CHA MWONGOZO WA MWANAFUNZI

# Somo la 1
# Maisha yenye kustahili Kuishi

## Wazo Kuu

"Ninapata umuhimu binafsi kwenye uhusiano na Muumbaji wangu tu."

## Mpango wa Mungu kwa ajili ya Maisha Yaliyokamilishwa

Tunafahamu kwamba tunayo kusudi kwa sababu tunajitambua kwamba sisi tumeumbwa. Kama Mungu ametuumba, ni lazima alikuwa na lengo kwa ajili yetu.

► Mwanzo 1:27-28; 2:18

Mahusiano makuu ya aina tatu:

- Uhusiano baina ya watu na Mungu.
- Uhusiano baina ya watu wenyewe.
- Uhusiano baina ya watu na dunia ya Mungu.

Uhusiano na Mungu ndio unaoweka haya mengine yaweze kwenda sawasawa kama inavyohitajika.

Jaribu kufikiri dunia ingekuwaje au ingefananaje leo kama kungekuwa na upatanifu (wa maono, na mtazamo) kwenye haya mahusiano matatu makubwa.

Sababu ya wewe kuwepo ni kuwa katika mahusiano mazuri na Mungu pamoja na watu wake na ulimwengu wake. Nisipofuata kusudi hilo naweza pia nisingekuwepo.

## Kumbukumbu ya Kibiblia kuhusu Anguko la Mwanadamu

Maelezo kuhusiana na hali ya dunia ya sasa yanapatikana katika Mwanzo 3.

1. **Matazamio**: Mpango wa Mungu wa mwanzo uliingiliwa na dhambi ya mwanadamu.

2. **Jaribu**: Shetani alimshawishi Adamu na Hawa kwa matarajio ya kuwa huru kutokana na Mungu.

3. **Kuwa na Mashaka**: Maswali ya Shetani yalikusudiwa kuwafanya watu watilie shaka hekima na unyoofu wa Mungu. Mtu anayetenda dhambi ana mashaka na Mungu – kwamba anajua na anakusudia yaliyo mazuri zaidi.

4. **Uasi**: Kwa kitendo cha Adamu na Hawa, walimkataa Mungu kama mamlaka na kiongozi wa maisha yao.

5. **Utengano**: Dhambi iliharibu kabisa mshikamano uliokuwepo wa mahusiano yote makubwa matatu.

Hali yote ya baadaye ya ubinadamu ikawa ni kuzaliwa katika asili yenye mwelekeo wa dhambi, kufanya matendo ya uovu, na kuishi kwenye mahusiano yaliyoharibika katika maeneo yote matatu makubwa ya mahusiano.

## Kutafuta Njia ya Kurejea

Mungu ana shauku ya kufanya upatanisho – kurejesha upya uhusiano unaokusudiwa.

Mungu anauliza swali lile lile alilomuuliza Adamu na Hawa: "Uko wapi?"

Ujumbe wa Biblia nzima ni kwamba Mungu anataka kuwarejesha tena watenda dhambi kwenye uhusiano wa yeye mwenyewe na watu wake.

Jambo muhimu kuliko yote kuhusiana na wewe ni uhusiano wako na Mungu.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninakushukuru wewe kwa kuniumba mimi, na kunifanya mimi kwa kusudi la kukufahamu wewe.

Asante kwa kunirejesha tena kutoka katika dhambi yangu na kunileta kwenye uhusiano uliofanywa upya na wewe. Asante kwa ajili ya msamaha wako.

Kwa kuwa nataka kuishi kwa furaha ya kukujua wewe, nitaishi kwa upendo wa utiifu kwa ajili yako. Ufanye utii wangu kwako uwezekane kwa Roho wako Mtakatifu ndani yangu

Ninaomba haya katika jina la Yesu, aliyekufa kwa ajili yangu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Mwanzo 1-3. Angalia kumbukumbu za rejea zilizopo za uhusiano. Kwenye sura ya 3, angalia vipengele vilivyoelezwa katika somo hili kwenye sehemu ya "Kumbukumbu ya Kibiblia kuhusu Anguko la Mwanadamu." Andika aya chache kuhusiana na yale ambayo utayaona katika sehemu hiyo.

# Somo la 2
# Kukutana na wokovu

## Wazo Kuu

"Kukutana na Mungu kunako sababisha wokovu huanza uhusiano wangu pamoja naye."

## Utangulizi

Mwanzo wa kwanza kabisa wa uhusiano wowote ni kukutana binafsi.

Je ni kitu gani muhimu kwa ajili ya upatanisho wakati mtu anapokuwa amemkosea mtu mwingine?

1. Mwenye kutenda makosa ni lazima akubali kwamba ametenda makosa na atubu. Kutubu maana yake ni kwamba hatakuwa anaendelea kufanya mambo mabaya dhidi ya mtu mwingine.
2. Mwenye kutendewa makosa ni lazima awe tayari kusamehe, hata kama inamaanisha kwamba mwenye kumtendea mabaya hataweza kumlipa kwa ajili ya uharibifu aliomfanyia.

Kwa mara ya kwanza tulipokutana na Mungu, tayari kuliwepo na tatizo kwa sababu tumetenda yaliyo maovu kinyume chake. Tatizo hilo ni lazima litatuliwe kwanza kabla uhusiano haujaweza kuanzishwa.

## Hali ya mtu aliyetengwa na Mungu.

► Waefeso 2:2-3

Kulingana na mstari huu, tumezaliwa tukiwa maadui wa Mungu. Sisi wote tumeishi maisha ya dhambi. Tulikuwa waasi kwa Mungu, na tulimfuata Shetani. Endapo hakuna kitu kitakachobadilika, tutakutana na ghadhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi zetu.

► Isaya 53:6.

Kwa mtu kudai haki ya kuchagua njia yake mwenyewe ya kuishi ni kumnyima Mwumbaji wake haki ya kumwelekeza yeye. Hii ndiyo asili ya dhambi. Huu ni uasi dhidi ya mamlaka ya Mungu.

Biblia inamwelezea mtu asiyeokoka kama kipofu, mtu aliye gizani, mtu aliye katika utumwa, akisukumwa na tamaa zenye uharibifu, na hata aliyekufa. Hali yake haitakuwa ya matumaini kama Mungu hatakuwa amejitoa kama msaada wa mahitaji ya mwenye dhambi.

## Neema ya Mungu ya Kuingilia kati

Mungu ametoa dhabihu kwa ajili ya msamaha wetu na kutupa shauku na uwezo wa kuitikia mwaliko.

Bila ya neema, mwenye dhambi hawezi hata kumwendea Mungu.

► Waefeso 2:4-5

Kama mtu anakuwa bado hajaokoka, siyo kwa sababu kamwe hajawahi kuwa na neema, bali ni kwa sababu hapendi kukubaliana na neema aliyo nayo.

## Kukutana Binafsi

Mtu huwa Mkristo wakati ule tu anapokutana na Mungu.

► Matendo 26:18

Injili ina uwezo wa kufungua macho yetu, ili kutugeuza kutoka gizani kwenda nuruni, na kutoka nguvu za Shetani kwenda kwenye nguvu za Mungu. Dhambi zetu zimesamehewa na tumepewa urithi kati ya wale ambao wametakaswa kwa imani katika Yesu.

Mkristo halisi ni yule ambaye amepata kukutana na Mungu wakati alipotubu dhambi zake (Luka 13:5), kwa imani akapokea msamaha (Waefeso 2:8), na akayatoa maisha yake kuwa ya utiifu kwenye Neno la Mungu (1 Yohana 3:6). Kukutanika huku kunaanzisha uhusiano wake binafsi pamoja na Mungu (1 Yohana 1:3).

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunifikia mimi wakati nilipokuwa nimepotea na kutengwa na wewe.

Asante kwa kutoa dhabihu ya Yesu juu ya msalaba ili niweze kusamehewa.

Asante kwa kunidhihirishia hatia zangu, kwa kunipa nia ya kupokea msamaha, na kunifanya niwe na uwezo wa kukubali wewe.

Asante kwa ajili ya mabadiliko makubwa sana ambayo umeyafanya ndani ya maisha yangu. Ninataka siku zote niweze kuishi katika utii wa upendo kwa ajili yako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Waefeso 2. Jaribu kufikiria juu ya mambo ambayo Mungu ameyafanya kwa kuingilia kati katika maisha yetu. Aya ya 1-3 inaelezea hali yetu ya zamani au iliyopita; aya ya 4 inaanza kuelezea mabadiliko ambayo Mungu ameyafanya. Angalia tena marejeo yote yanayohusiana na uhusiano katika sura yote, hasa kwenye aya za 4, 6, 7, 14, na 19. Andika aya chache kuhusiana na yale unayoyaona.

# Somo la 3
# Uhakika wa Kukubaliwa na Mungu

## Wazo Kuu

"Mungu alinikubali mimi kama mtoto wake wakati nilipotubu na kuamini ahadi yake."

## Uhakika

Biblia inatuhakikishia kuwa tunaweza kuwa na ujasiri kwamba Mungu ametukubali (Warumi 8:16).

Uthibitisho huu ni wa uhakika na uliokamilika sana kiasi kwamba tunaweza kuwa na ujasiri kwenye ile Siku ya Hukumu, bila ya kusumbuka kwamba aidha tutapita kwenye tathmini ya Mungu au laa (1 Yohana 4:17).

Mwamini anaweza akawa na uhakika wa wokovu wake kwa kujua kwamba amefuata njia sahihi ya kimaandiko katika kufikia wokovu.

**Kutubu** inamaanisha kwamba mwenye dhambi hujisikia yeye mwenyewe kwamba ni mwenye hatia na anastahili hukumu (1 Yohana 1:9), na kwamba yuko tayari kwa hiari yake mwenyewe kuachana na matendo yake ya dhambi (Isaya 55:7).

Kama mtu atakuwa hajajiona yeye mwenyewe kwamba ni mwenye hatia, bila kutoa udhuru, na anayestahili hukumu, bado atakuwa hajatubu.

**Imani inayookoa** ni muhimu kwa wokovu. Kuwa na imani iokoayo maana yake ni kwamba mtu anaamini mambo fulani:

1. **Hujiona kwamba hawezi akafanya jambo lolote la kujihesabia haki yeye mwenyewe** (Waefeso 2:8-9).
2. **Anaamini kwamba dhabihu ya Kristo inatosha kwa ajili ya msamaha wake** (1 Yohana 2:2).
3. **Anaamini kwamba Mungu anaahidi kumsamehe kwa takwa moja tu la imani** (1 Yohana 1:9).

Kama atakuwa ametubu kwa ukweli na kuamini jinsi Biblia inavyoelekeza, ana haki ya kuamini kwamba Mungu amemsamehe.

Kuna uthibitisho maalumu ambao Mungu hutoa kwa mwamini anayetubu wakati anapokuwa ametubu na kuamini:

> Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba. Roho mwenyewe

hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu (Warumi 8:15-16).

Kama mtu atakuwa amefuata njia ya kimaandiko ya kupokea wokovu na ni tegemezi kwenye maana halisi ya kimaandiko ya uhakika wa haraka, badala ya njia nyingine ya uhakika, haiwezekani akadanganyika. Uhakikisho huu uko kwenye msingi wa Neno la Mungu, ambao kwa namna yeyote ile ni wa kuaminika kabisa. Wakati wote Mungu hutimiza ahadi zake.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya ahadi yako ya kumsamehe mwenye dhambi ambaye anatubu na kuamini. Nimetubu dhambi zangu, na ninaamini katika ahadi yako.

Ninajua kwamba dhabihu ya Yesu juu ya msalaba inatosha kwa ajili ya msamaha wangu.

Ninajua kwamba sihitaji kuwa na hofu ya hukumu kwa sababu dhambi zangu zimesamehewa.

Asante kwa ajili ya ushuhuda wa Roho Mtakatifu wako kwamba mimi ni mtoto wako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Waebrania 10:11-25. Ni msingi gani wa uhakika wa kibinafsi unaotolewa katika kifungu hiki? Ni maelekezo gani ambayo hutolewa kwetu kwa kuwa tunao huu uhakika? Orodhesha maelekezo hayo na tafakari jinsi ya kuyakamilisha na au kuyatimiza kibinafsi.

# Somo la 4
# Kuwasiliana na Mungu

## Wazo Kuu

"Nitamjua Mungu vizuri zaidi kwa sababu ninawasiliana naye kwenye maombi."

## Mkristo Hutafuta Mapenzi ya Mungu katika Maombi

Mazoezi ya maombi ni moja ya alama za Mkristo, ingawa watu wa dini zingine pia huomba. Kitu muhimu kinachotofautisha maombi ya Kikristo ni kwamba tunanyenyekea katika mapenzi ya Mungu badala ya kujaribu tu kumfanya Mungu kutufanyia tunachotaka.

Sisi kama wakristo tunaamini kuwa mapenzi ya Mungu ni mazuri kwetu kuliko matamanio yetu wenyewe. Tunajua kwamba kwa kuwa Mungu anazo hekima kamilifu na upendo uliokamilika, mapenzi ya Mungu ni jambo bora zaidi ambalo linaweza kutokea kwetu.

Tunamwachia Mungu achague kwa sababu tunamtumaini.

Maombi siyo tu suala la kugeukia kwenye orodha ya mahitaji; bali ni kutaka kuwa na mwingiliano na Mungu.

## Mkristo Humtafuta Mungu katika Maombi

**Mkristo anathamini uhusiano wake na Mungu kuliko kile anachopata kutoka kwa Mungu.**

Tunachotafuta zaidi sana katika maombi ni kumpata Mungu mwenyewe.

> Muda wetu na Mungu, na kipaumbele tunachokiweka kwa ajili ya muda huo, ni kipimo cha kweli cha upendo wetu kwa Mungu. - Bernadi wa Clairvaux

Uhusiano bora una uaminifu ulio mkamilifu kabisa.

## Maombi ni Ishara Maisha ya Kiroho

Maombi ni pumzi ya roho – ishara nyeti ya kiroho.

Tunapumua kwenye maisha ya kiroho kutoka kwa Mungu na tunapumua kutoka ndani mwetu sifa na kuabudu, kunakodhihirishwa kipekee katika maombi yetu.

## Nyakati za Kuomba

- Omba unapoanza siku.
- Omba kwa wakati maalumu ulioupanga au uliouweka kila siku.
- Omba unapokuwa kwenye majaribu.
- Omba wakati ambapo umejiona kushindwa.

- Omba wakati unapotaka kumshukuru Mungu kwa jambo fulani.

## Muhtasari

1. Maombi ya Mkristo yanatofautiana na maombi ya mpagani kwa sababu tunataka mapenzi ya Mungu yatimizwe na tunathamini kumjua Mungu zaidi kuliko tunavyothamini vile tunavyopata kutoka kwake.
2. Maombi ni kipimo cha upendo wetu kwa ajili ya Mungu.
3. Maombi ni "ishara muhimu" ya uwepo wa maisha ya kiroho na inayoonyesha kwamba tuko hai kiroho.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya upendeleo nilio nao wa kuweza kuongea na wewe. Ninayo furaha kwamba ninaweza kuongea na wewe kuhusiana na mahitaji yangu. Lakini, zaidi ya yote, Ninakushukuru kwa ajili ya upendeleo nilio nao wa kukujua wewe.

Naomba unisaidie katika kuonyesha upendo wangu kwa ajili yako kwa kuongea na wewe mara kwa mara. Ufanye upendo wangu ulio kwa ajili yako uweze kukua kwa sababu ninaanza sasa kukujua wewe vizuri zaidi.

Nisaidie katika kuufanya muda wangu na wewe uwe wa kipaumbele kikubwa zaidi sana katika maisha yangu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Angalia usemi ambao Yesu alitoa kuhusu maombi katika Mathayo 6:5-18. Andika rejea za mahitaji ya kibinafsi na rejea za uhusiano na Mungu.

# Somo la 5
# Kusoma kile ambacho Mungu Alikiandika

## Wazo Kuu

"Neno la Mungu linaongoza uhusiano wangu pamoja na Mungu."

## Utangulizi

Zaburi ya 119 inaonyesha umuhimu wa Biblia kwa ajili ya Mkristo.

Faida nyingi za Neno la Mungu:

- Limenihuisha (50).
- Linafariji (52).
- Ni taa (105).
- Linamfanya awe sehemu ya watu wanaomwabudu Mungu (74, 79).

## Shauku ya Maandiko ya Mtunga Zaburi

- Alilipenda Neno la Mungu na kulifurahia ndani yake (16, 24, **47**, 48, 77, **92**, **97**, **103**).
- Alifurahia kuwa nalo kana kwamba lilikuwa ni utajiri uliokuwa mkubwa sana (**14**, **72**).
- Aliona kwamba wale watu waliokuwa nalo na kulihifadhi ndani mwao ni watu waliobarikiwa (waliokuwa na furaha) (**1**, **2**).

**Mtunga Zaburi alikuwa na shauku ya Maandiko kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu.** Alilipenda kwa sababu alimpenda Mungu. Neno la Mungu ni udhihirisho wa asili ya Mungu. Anapokuwa anaangalia sheria ya Mungu na mahitaji yake, anaiona haki na hekima aliyo nayo Mungu (137).

Maandiko ni kiungo kati yake na mtu anayeabudu – yakimfunua Mungu kwa mtu anayeabudu na kuongoza mwitikio wa mtu anayeabudu kwa Mungu. Maandiko yanakuwa yamevuviwa na Roho Mtakatifu, kuangazwa na Roho Mtakatifu, na kukamilishwa ndani ya maisha ya mtu anayeabudu kwa nguvu na uwezo wa Mungu.

## Maandiko Yalimwongoza Mtunga Zaburi katika kumwitikia Mungu

Kusudi la Maandiko ni kumfunua Mungu ili tuweze kuingia katika uhusiano wake. Kwa hiyo, Maandiko yanataka mwitikio kutoka kwa msomaji.

Mwitikio wa mtunga Zaburi katika Maandiko:

- Aliomba kwamba Mungu aweze kumfundisha Neno lake mwenyewe (12, **18**, **27**, 33, 34).
- Aliomba kwamba awe na uwezo wa kuishi sawasawa na hilo Neno la Mungu (**35-37**, 5, 10).
- Aliomba kwamba hata moyo wake uendane na mapenzi ya Mungu (32, **80**).
- Alijua kwamba utakaso wake utatokea kupitia mwingiliano wake na Mungu katika Neno lake (**9**, **11**).
- Alidai baraka kutoka kwa Mungu kwa msingi wa kuzishika sheria za Mungu (22, **121**, **153**)
- Aliahidi kuwa mtiifu (8).
- Aliutumia muda wake katika kutafakari juu ya Neno la Mungu kwa siku nzima (15, 97, 147-148).

**Mwitikio wetu kwenye Maandiko**

Anza sasa kuwa na mwitikio ulio sahihi kwenye Maandiko:

- Tambua kazi ya Neno la Mungu kwenye uhusiano wako na Mungu.
- Ingia kwenye uhusiano na Mungu kama kutubu kwako bado hakujakamilika.
- Jihusishe kwa wakati katika Neno la Mungu. Anza na Zaburi ya 119, na omba kwa kutumia aya hizi unapokuwa unasoma. Vitabu vya Wafilipi, Tito, na Waefeso vinaweza kuja baadaye kwenye usomaji wako
- Dhamiria kuendelea kuwa na mwitikio endelevu katika kazi ya Roho Mtakatifu kupitia katika Neno lake.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya kunipa Maandiko, na kwa kujifunua kwangu wewe mwenyewe. Asante kwa kunipa ufahamu wake kupitia Roho Mtakatifu wako anayefanya kazi ndani ya moyo na akili yangu.

Naomba unisaidie kuelewa zaidi na zaidi kile unachokitaka na unavyotaka mimi niwe ili niweze kukupendeza wewe. Niwezeshe siku zote kuwa na mwitikio wa kazi yako ndani ya moyo wangu kila ninapokuwa ninasoma. Achilia Neno lako liwe endelevu kwangu katika kunibadilisha mimi kuwa kwenye mfano wa sura yako.

Bwana, ninajikabidhi katika kuutumia muda wangu kila siku katika kulitafakari Neno lako. Nipe kuwa na upendo wa kulipenda Neno lako kutokana na upendo wangu nilio nao kwa ajili yako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Katika wiki hii tafakari juu ya Zaburi ya 119. Orodhesha mambo ambayo mwandishi anasema atayafanya kwa sababu ya Neno la Mungu. Jikabidhi katika kufanya mambo ambayo yanafanana na hayo, na omba kwa ajili ya ukamilifu wake ndani ya moyo wako na maisha yako.

# Somo la 6
# Kutoa Mwaliko

## Wazo Kuu


"Ninataka niwaongoze watu wengine wamjue Mungu kama mimi ninavyofanya."

## Mchoro wa Daraja la Kuelezea Injili

### Sehemu ya 1

"Mungu alimwumba kila mtu awe kwenye uhusiano pamoja naye na kuishi maisha yaliyobarikiwa. Hakupanga maisha yawe ya matatizo na mateso chungu zima."


[Chora mtu na neno "Mungu".]




### Sehemu ya 2

"Mwanadamu ametenganishwa na Mungu kwa sababu ya dhambi. Watu wa kwanza walitenda dhambi, na tangu hapo kila mtu ametenda dhambi dhidi ya Mungu."


[Chora kujitenga kati ya watu na Mungu, na uandike "dhambi".]



**Sehemu ya 3**

"Mungu ni hakimu mwenye haki, na siku moja wenye dhambi watahukumiwa kwenda jehenamu ya milele isipokuwa wawe wametafuta rehema za Mungu na kurejea kwenye uhusiano tena pamoja na Mungu."


[Chora mshale na andika neno "motoni".]




**Sehemu ya 4**

"Hakuna lolote tunaloweza kulifanya kwa ajili ya kuturejesha tena upya kwa Mungu au kupata rehema – siyo kwa matendo mema, siyo kwenda kanisani, siyo taratibu za kimadhehebu, na wala siyo kutoa fedha...."


[Chora mshale kuonyesha kila kipengele kwenye orodha.]



**Sehemu ya 5**

“Hali yetu itakuwa mbaya sana kama Mungu hangefanya njia kwa ajili yetu ya kurejea kwake kwa njia ya Wokovu kwa kumwamini Yesu Kristo. Yesu, Mwana wa Mungu alikufa juu ya msalaba ili tuweze kusamehewa. Baada ya siku tatu, alifufuka kutoka kwa wafu.”


[Chora msalaba.]




**Sehemu ya 6**

“Lakini haitoshi tu kujua haya. Kila mtu binafsi atapaswa kufanya chaguo la kuokoka na kurejea tena kwa Mungu. Mtu ni lazima atubu, ikimaanisha kwamba ni kujutia kikamilifu kuhusu dhambi na kuwa tayari kwa hiari yake mwenyewe kuachana nazo. Mtu anayetubu na kuokoka kwa kumwamini Yesu Kristo Mungu anamsamehe makosa yake yote.”

[Chora mshale kisha andika maneno “Tubu” na “Pokea”.]




**Sehemu ya 7**

“Ni wapi unapofikiri kwamba upo katika mchoro huu? Je, umewahi kupata muda maalumu katika maisha yako ukatubu dhambi zako, ukapokea msamaha wa Mungu, na ukaanza kuishi yanayompendeza Mungu; au bado umetengwa na Mungu kutokana na dhambi yako?”

[Subiri kupata jibu. Watu wengi watakiri kwamba bado wametengwa na Mungu.]

“Uko tayari kufuata hatua hii – Kutubu, kupokea msamaha, na kuanza kuishi yenye kumpendeza Mungu? Nitapendezwa sana kuomba pamoja nanyi sasa hivi.”

[Fanya maombi yanayokaribia kufanana na haya yafuatayo:]

“Bwana, ninajua mimi ni mwenye dhambi na ninayestahili adhabu ya milele. Ninajutia dhambi zangu na niko tayari kuachana nazo. Ninaomba unisamehe, siyo kwa sababu ninastahili, bali kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yangu. Asante kwa wokovu wako. Kuanzia sasa, nitaishi kwa ajili yako tu.”

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninayo furaha kubwa siyo kwamba unataka kuniokoa mimi tu, lakini pia ni pamoja na familia yangu, marafiki zangu, na kila mtu aliyeko katika ulimwengu huu.

Asante kwa kutupa wokovu ili kwamba kila mtu aweze kuokolewa na kuingia kwenye ushirika huu wa ajabu ambao tunao pamoja na wewe na waamini wengine.

Uliupenda ulimwengu wote kiasi cha kutosha hata kumtoa Mwanao wa pekee kwa ajili yake.

Baba, naomba unisaidie kuwa mwaminifu katika kuutangaza mwaliko wako kwa watu wote.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

1. Jiandae kutimiza ahadi yako ya kushirikisha mchoro kwa wengine wiki hii.
2. Tengeneza orodha ya watu ambao hawajaokoka unaowajua kwamba utakuwa na uwezo wa kufanya mazungumzo nao katika wiki hii. Panga kuleta somo ambalo litafungua mlango kwa ajili ya kushirikisha injili.
3. Tengeneza orodha ya baadhi ya wakristo ambao unaweza kuwaonyesha mchoro kwa lengo la kuwasaidia kujisikia kwamba wanawezeshwa zaidi kwa ajili ya kushuhudia.

# Somo la 7
# Kuendeleza Utii Wangu

## Wazo Kuu

“Natambua na kufuata mapenzi ya Mungu vizuri zaidi kwa kadri ya upendo wangu kwake unavyokua.”

## Kukua katika utii

► Wafilipi 1:9-11

Paulo aliomba kwamba Wakristo wa Filipi waendelee kumpenda Mungu zaidi, na kwa upendo huo, waweze kuelewa mapenzi ya Mungu.

Tunapaswa kutarajia uboreshaji wa maisha yetu kadri Mungu anavyotupa uwezo wa kupambanua.

## Baadhi ya Maeneo ambayo Mwamini anapaswa Kuboresha

1. **Umakini wa ushawishi.** Je, kuna mambo unayofanya wewe ambayo hutataka watu wengine wayafanye?
2. **Kujidhibiti Binafsi.** Je, unatawala hisia zako na matamanio yako kiasi cha kutosha kufanya unachopaswa kufanya?
3. **Kuitunza Afya Yako.** Je, unautunza mwili wako kama vifaa visivyoweza kubadilishwa kufanya kazi kwa ajili Mungu? Kwa kuwa mwili wako ni mali ya Mungu, haupaswi kufanyiwa uharibifu wowote. Haupaswi uufanyie uzembe mwili wako katika kuutunza.
4. **Kuchagua Burudani.** Je, burudani yako inakusababishia vita na majaribu kwa kuleta mawazo mabaya au mtazamo mbaya? Jihadhari na chochote ambacho ni kiashiria cha dhambi kinachoonekana kwamba ni cha kuvutia au cha kumpendeza.
5. **Tabia.** Watu ulio miongoni mwao wana mila zao za kuonyesha heshima. Unapaswa utafakari kuwa na heshima kwa njia ambayo wao wanaitambua. Kuwa na fadhila hata wakati inapotokea kwamba mtu hastahili.
6. **Maadili ya Kazi.** Je wewe ni mwaminifu kabisa katika biashara zako zote?
7. **Kujali Muda.** Je, unaweka thamani kwenye muda wako na muda wa watu wengine kwa kuzingatia muda wa ratiba kila inapowezekana?
8. **Mavazi.** Je, mavazi yako yanaonesha kwamba yana thamani ya kuwa na heshima zinazotakiwa, na uangalifu katika kutumia fedha?

9. **Lugha.** Je, mazungumzo yako ni masafi na yenye heshima kwa Mungu na kwa watu wengine?

10. **Kutegemewa.** Je, unatimiza ahadi?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninahitaji upendo wangu kwako uwe unaongezeka bila kukoma. Ninataka niyaelewe mapenzi yako kwangu vizuri zaidi.

Naomba unisaidie mimi kupambanua ni kitu gani kinachokupendeza zaidi ili kwamba niweze kuishi maisha ambayo ni masafi na yasiyokuwa na hatia.

Naomba unisaidie kuziona tabia zangu na mwenendo wangu vinavyohitaji mabadiliko na kuongeza tabia na mwenendo ambao utakuletea wewe utukufu

Ninataka nizae matunda kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma 1 Wakorintho 13. Sura hii inaelezea maisha ya mtu ambaye ana upendo anaopaswa kuwa nao kwa ajili ya watu wengine. Acha Mungu akuonyeshe ni kwa jinsi gani anataka akubadilishe na ayafanye maisha yako yaendane zaidi na upendo. Orodhesha mabadiliko ambayo ungependelea kuyaona wewe mwenyewe.

# Somo la 8
# Kujifunza Biblia katika ibada binafsi

## Wazo Kuu

"Neno la Mungu kila siku huleta matokeo kwenye maisha na imani yangu."

## Sababu za Kujifunza Biblia

1. **Kwa ajili ya uhusiano wetu na Mungu.** Zaburi 119 inasema kwamba Neno la Mungu ni ufunuo wa asili ya Mungu mwenyewe, kwahiyo, Maandiko ni njia ya kumjua Mungu.

2. **Kujua na kuuamini ukweli** (2 Timotheo 3:16). Biblia ndio chanzo chetu cha mafundisho ya imani.

3. **Kupata mwelekeo sahihi wa maisha** (2 Timotheo 3:16).

4. **Kwa ajili ya ufanisi wa huduma** (2 Timotheo 3:16).

5. **Kwa ajili ya ukomavu wa kiroho** (Waebrania 5:12-13).

## Malengo Yasiyofaa kwenye Kujifunza Biblia katika ibada binafsi ya

1. **Kubuni tafsiri mpya.** Tunapaswa kuwa wabunifu katika kutumia na kuwasilisha Andiko, lakini siyo katika kulitafsiri.

2. **Kukusanya ushahidi kwa ajili ya midahalo.** Kama mtu atasoma Biblia ili kujenga tu hoja ya ushindani, hupata maono potovu na anaweza kuona tu kile anachotaka yeye kukiona.

3. **Kutiwa moyo.** Kama mtu atakuwa anapitia vifungu kwa haraka akiwa anatafuta huko aya za kukidhi hisia zake, anakuwa haipi nafasi Biblia izungumzie ujumbe wake wote.

## Jinsi ya Kujifunza Biblia katika ibada binafsi

### (1) Anza kuomba kwa ajili ya kupata ufahamu wa kifungu.

Andaa moyo wako kupokea ujumbe kamili ulioko kwenye kifungu. Hujifunzi tu kujua mapenzi ya Mungu, bali kutendea kazi.

### (2) Tafsiri kifungu.

Aya inasema nini hasa? Toa muhtasari wa aya na orodhesha maelezo. Hakikisha hitimisho lako halipingani na mafundisho ya kimaandiko yaliyo wazi mahali pengine.

**(3) Tumia kifungu hicho wewe binafsi.**

- Je, kuna dhambi yeyote ya kutubu au kishawishi cha kuepuka?
- Je, kuna ahadi yeyote ya kudai?
- Je, kuna tabia yeyote inayotakiwa ibadilishwe?
- Je, kuna agizo lolote linalotakiwa kutii?
- Je, kuna mfano wowote unaotakiwa kuigwa?
- Je, kuna maombi yeyote ya kuomba?
- Je, kuna tatizo lolote la kukwepa?
- Je, kuna jaribu lolote la kuepukana nalo?
- Je, kuna jinsi yeyote ya kumtukuza Mungu kwa ajili ya haya?

Inawezekana kukawepo na mengine zaidi ya haya katika kifungu.

**(4) Omba kwa ajili ya kutimiza ukweli ndani yako.**

Omba Mungu afanye mabadiliko yanayohitajika ndani ya moyo wako na katika maisha yako.

**(5) Maombi huamua utakachobadili kutokana na matumizi haya.**

Mabadiliko maalumu yanapaswa yawe:

- **Binafsi** – kitu ambacho wewe mwenyewe unataka kifanyike.
- **Kwa vitendo** – siyo tu kinadharia, bali chenye matokeo katika kitu ambacho kwa uhakika kinatakiwa kifanyike.
- **Kuwajibika** – kuwajibika ndani ya muda uliowekwa kwa ajili ya utekelezaji.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya hazina uliyotupa sisi katika Maandiko.

Asante kwa kutufunulia sisi ukweli kuhusu jinsi ya kukujua wewe, jinsi ya kuishi, na jinsi ya kuwasaidia watu wengine

Nisaidie mimi katika kujifunza Neno lako kwa juhudi zaidi. Nipe ufahamu wa kuelewa kuhusu ukweli unaoufunua. Naomba unisaidie mimi niweze kuishi kwenye ukweli huo kwa uaminifu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari 1 Wathesalonike 5, ukifuata hatua za Kujifunza Biblia katika ibada binafsi zilizoorodheshwa katika somo hili. Elezea matumizi yako binafsi uliyogundua ya kutumia njia hizi.

# Somo la 9
# Kuomba kama Daudi

### Wazo Kuu

"Kuzungumza na Mungu kunafanya kila sehemu ya maisha yangu iwe na maana sahihi."

### Maombi: Kuzungumza na Mungu

Zaburi nyingi ni maombi, na zinatufundisha jambo muhimu kuhusu maombi.

Kama ukiacha kuzungumza na Mungu au kama hutaki kuzungumzia kuhusu baadhi ya mambo, inawezekana ikawa ni kwa sababu unafikiria kwamba huwezi ukakubaliana na yeye katika mambo hayo.

Zaburi inadhihirisha kwamba tunapaswa tuwe tunazungumza na Mungu kuhusu kila kitu kinachohusiana na maisha yetu na chochote tunachojisikia.

Unachokuwa unazungumzia kitakuwa kinaonyesha nafasi yako ya uhusiano wako.

Uhusiano ni kushirikishana maisha.

Wakati mwingine mambo hutokea kwenye uhusiano wenye mipika.

Je, vipi kuhusu uhusiano wako na Mungu? Ni wa juujuu ikiwa hakuna mambo mengi ya kuzungumza.

Lazima tuwe na utayari kuendelea kubadilishwa kwenye uhusiano wetu pamoja naye.

Hii inamaanisha kwamba katika maisha yetu tunapata maana halisia kutoka kwa Mungu.

Kila kitu kinapata mahali pake panapofaa na kupata thamani yake kikiletwa kwa Mungu kwa ajili ya marekebisho. Endapo huombei kila kitu,

- Mambo mengi hayatakaa vizuri.
- Hisia zitakosa uwiano.
- Maamuzi yatakuwa potofu.
- Mitazamo itakuwa haiendani.

Mtu mwenye wasiwasi sana haombi vya kutosha; mtu anayeomba sana, hana wasiwasi sana.

Mungu yuko karibu na wale wenye roho ya kupondeka (Zaburi 34:18). Ni lazima tuwe wapole na wanyenyekevu, tukipeleka mambo yote kwa Mungu na kumwachia ajibu kwa njia yake anayotaka mwenyewe.

► Je, ni mambo gani unazungumza naye? Je, ni mambo gani ambayo wewe unahitaji kuzungumza naye?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninataka niweke thamani halisi ya kila kitu nilicho nacho na maana ya kila kitu ambacho kinanitokea mimi katika maisha yangu. Ninataka niweke hisia zangu zinazohusiana na kila kitu kwa ajili ya marekebisho yako.

Naomba unisaidie mimi kufunua kwako sehemu zote za maisha yangu.

Ninataka nijitoe moja kwa moja kwako. Ninataka uhusiano wangu na wewe uhusishe kila kitu kinachohusiana na mimi.

Naomba unisaidie katika kuendelea kubadilishwa kwa kukujua wewe vizuri zaidi.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari Zaburi ya 34. Andika aya moja inayohusu ujasiri wa Daudi kwamba kila kitu kinaweza kikawakilishwa kwa Mungu. Zingatia hasa aya za 15 na 18.

# Somo la 10
# Kusafisha Imani

## Wazo Kuu

"Ninakua kiroho kadri imani yangu inavostahimili majaribu."

## Majaribu ya Imani

► 1 Petro 1:6-7; Waebrania 11:1, 6

Imani ya msingi zaidi kuliko nyingine ni kuamini kwamba Mungu huwajibu wale wote wamtafutao kwa njia iliyo sahihi. Ni kuamini kwamba thawabu ya Mungu inapatikana na ni yenye thamani zaidi sana kuliko kitu kingine chochote.

Kwenye kipindi cha majaribu, tunakuwa na mashaka kuwa Mungu atafanya kitu chema kwa ajili yetu. Kila jaribu ni jaribio la imani. Imani ni ushindi juu ya kila jaribu.

► 1 Yohana 5:4

Majaribu yanaruhusu mchakato tunaouhitaji.

► Yakobo 1:2-4

Majaribu ya imani hukuza uvumilivu. Kuwa na uvumilivu inamaanisha ni kuendelea au kusonga mbele kwa imani. Fadhila muhimu zaidi za Kikristo haziwezi kutokea kwa mtu ambaye hana uvumilivu kwa Imani.

## Aina za Majaribu

1. **Mazingira magumu.** Jaribu la imani ni kipimo kilicho katika:
    - Kusababisha kuchanganyikiwa au hasira, na kukusababisha kukubaliana na tabia au mwenendo mbaya.
    - Kufanya haraka kubadilisha jambo au mazingira
    - Kutomtii Mungu kwa kurekebisha tatizo kwa njia zako mwenyewe.
2. **Kutokutenda haki na unyanyasaji.** Jaribu la imani ni jaribio la:
    - Kuwatendea watu wengine mabaya kwa sababu na wao wametenda mambo yaliyo mabaya.
    - Kutokuwa tayari kumgonja Mungu kutekeleza haki yake.
    - Kukataa kusamehe na kuonyesha upendo kama Kristo alivyofanya.

3. **Mateso ya kimwili.** Jaribu la imani ni jaribio la:
   - Hisia za mfadhaiko huharibu Imani yako.
   - Kutafuta furaha au burudani nje ya mapenzi ya Mungu

4. **Msiba.** Jaribu la imani ni jaribio la
   - Kuwa na mashaka na upendo wa Mungu na wema wake.
   - Kuwa na shaka kuwa Mungu ndiye anayetawala.

5. **Mkanganyiko.** Jaribu la imani ni jaribu la kujitoa katika ufahamu wako dhidi ya mapenzi ya Mungu yanayojulikana.

6. **Mateso.** Jaribu la imani ni jaribio la kukufanya uepukane na kuteseka.

7. **Jaribio la dhambi.** Jaribu la imani ni jaribio la kukufanya uingie kwenye kivutio cha dhambi.

► 1 Wakorintho 10:13

### Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kuwa nami kila siku, ukinisaidia katika kila jaribu. Naomba unisaidie imani yangu iweze kuwa na nguvu. Nisaidie mimi katika kukumbuka kwamba nyakati ngumu ni changamoto za imani, na kwamba imani yangu ni lazima iendelee kuvumilia.

Ninataka niendelee kukutii wewe haijalishi litatokea jambo gani. Nitaonyesha utiifu wangu kwa kukusikiliza wewe wakati wote.

Asante kwa ajili ya kuiendeleza imani yangu ambayo inatokea wakati unaponipitisha kwa ushindi katika majaribu.

Amina.

### Kazi ya Kufanya

Tafakari Yakobo 5:7-11. Tambua sababu ambazo zimetolewa kwa ajili yetu kuweza kuvumilia katika imani. Manabii wanatajwa kama mifano. Je, ni watu gani unaowajua ambao waliweza kuvumilia mambo magumu kwa njia ya imani? Je, ingekuwaje kama hawangeweza kufanya hivyo?

# Somo la 11
# Kuanzisha Mazoezi ya Kiroho

## Wazo Kuu

"Ninatumia muda na juhudi katika kukuza uhusiano wangu na Mungu.”

## Utangulizi

Mazoezi ya kiroho ni vitendo vya hiari ambavyo vimepangwa na kutunzwa kwa kusudi la kuhifadhi vipaumbele vya kiroho na kukuza uhusiano wetu na Mungu.

## Baadhi ya mambo ya kutilia maanani kuhusu Mazoezi ya Kiroho.

- Ndizo njia za kuelekea kwenye lengo, na siyo kwamba zina malengo ndani yake zenyewe.
- Siyo vipimo kamili kabisa kwa ajili ya viwango vya kiroho.
- Haziwezi kuwa mbadala kwa ajili ya kumtii Mungu.
- Ni lazima ziwe za hiari kwa ajili ya kupata matokeo bora zaidi.

## Orodha ya Mazoezi ya Kiroho

1. Maombi
2. Kujifunza Biblia. Zaburi ya 119 inaonyesha kazi inayofanywa na Neno la Mungu kwenye maisha ya mtu ya kuabudu.
3. Kufunga kwa ajili ya maombi (Mathayo 9:15, Mathayo 6:16-18).
4. Kuhudhuria ibada za Kanisa (Waebrania 10:25).
5. Meza ya Bwana/Ushirika Mtakatifu (1 Wakorintho 11:23-26).
6. Uwajibikaji wa Kiroho (Waebrania 13:17, Yakobo 5:16, Wagalatia 6:2).
7. Utoaji (Waebrania 13:16, 1 Wakorintho 16:2).
8. Huduma (1 Wakorintho 12).
9. Kitabu cha kumbukumbu za kiroho (Zaburi 78:11).
10. Kujifunza Biblia katika ibada binafsi.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie kudumisha mtazamo wangu juu ya vipaumbele vya kiroho kwa kutengeneza nafsi kwa nidhamu hizi za kiroho maishani mwangu.

Nisaidie kuwa mwaminifu katika kujitolea kwangu. Nilinde dhidi kiburi katika maendeleo yangu ya kiroho.

Naomba unisaidie kuwa mwaminifu na kwamba nidhamu yangu ya kiroho ni kuonyesha upendo wangu kwako na Imani yangu kwako.

Asante kwa ajili ya neema yako ambayo inafanya kazi ndani yangu juu ya mambo yote ambayo naweza kuyafanya.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Angalia taarifa zote za marejeo ambazo zilitolewa kwenye orodha ya mazoezi ya kiroho. Angalia kwa makini ni kwa jinsi gani mazoezi ya kiroho yanavyovungumziwa kuwa na uhai kwenye maisha ya Mkristo. (Hapo mwanzoni tulijifunza Zaburi ya 119, kwa hiyo siyo lazima kufanya tena marejeo yote ya sura hii katika wiki hii.)

**Ahadi Binafsi ya Mazoezi ya Kiroho.**

1. **Maombi.** Nitaomba kila siku saa __________ kwa dakika ____________.
2. **Kujifunza Biblia.** Nitajifunza Biblia kila siku saa __________. Nitafanya kipimo cha kujifunza kwangu ________________________________________ (kwa masaa au njia nyingine).
3. **Kufunga.** Nitafunga kila wiki siku ya ____________ kwa muda wa __________ (muda wa saa).
4. **Kuhudhuria ibada za Kanisa.** Nitahudhuria ibada za kanisa na mafunzo ya Biblia mara kwa mara:

   Siku ____________ Muda ____________

   Siku ____________ Muda ____________

   Siku ____________ Muda ____________
5. **Meza ya Bwana/Ushirika Mtakatifu.** Nitashiriki Meza ya Bwana au Meza ya Bwana inayotolewa kanisani kwangu, kila siku ya _____________ (kadiria muda).
6. **Uwajibikaji wa Kiroho.** Nitatoa taarifa ya hali yangu kiroho na kupokea maelekezo ya kiroho kutoka kwa _____________ (mwangalizi maalumu wa kiroho) kila siku ya_____________ (muda).
7. **Kutoa.** Nitatoa fungu langu katika _______________________________ (taja kanisa).
8. **Huduma.** Nitahudumu mara kwa mara kwa njia ifuatayo:
9. **Kumbukumbu za kiroho.** Nitatunza daftari ambalo nitasahihisha mara _______________ kwa wiki
10. **Masomo ya kujisomea katika ibada binafsi.** Nitafanya usomaji ufuatao wa ibada binafsi:

Tarehe ya kujitolea: ____________________

Itaendelea hadi: _______________________

Jina: __________________________________

# Somo la 12
# Kukubali Uwajibikaji wa Kiroho

## Wazo Kuu

"Mungu amenikuza katika jumuiya ya kiroho iliyokaribu nami."

## Uwajibikaji wa Kiroho

Kuwa na uwajibikaji wa kiroho ni kuanzisha uhusiano na mtu au kikundi ambacho kinatoa mwelekeo wa kiroho.

Mtu ambaye ana uwajibikaji wa kiroho hutoa taarifa:

- Kuhusiana na hali yake ya kiroho.
- Kuhusu mafanikio na mapungufu yake kwenye nidhamu za kiroho.
- Kuhusu ahadi zake kwa siku zijazo.

Bila ya kuwepo kwa uwajibikaji wa kiroho tutakuwa hatutekelezi amri za maandiko; tutakuwa tunapuuzia njia ambazo Mungu amezitengeneza kwa kutupa sisi neema kwa ajili ya ushindi na ukuaji wa kiroho.

► Yakobo 5:16; Wagalatia 6:2; Waebrania 10:24, Waebrania 13:17

Jiulize maswali haya ya kujipima kama uwajibikaji wa kiroho umeanzishwa ndani ya maisha yako au laa.

Je, nina uhusiano gani ambao unasababisha kwamba…

- Mtu fulani ananisaidia katika kubeba mizigo yangu iliyo mikubwa sana?
- Ninakiri makosa yangu kwa mtu mwingine?
- Je ninamsaidia mtu mwingine mizigo yake?
- Kuna mtu anayewajibikia hali yangu ya sasa ya kiroho?

Je, ziko nyakati ambazo ninajihisi kwamba ninakosa aina hii ya uhusiano:

- Nyakati ambazo hakuna mtu yeyote ninayeweza kumtegemea?
- Ni wakati gani ninafurahi kwamba hakuna mtu anayejua hali yangu?
- Nyakati ambazo sitataka kutoa taarifa zangu za nidhamu za kiroho?

Je, kuna mtu ambaye ninakubali mamlaka yake ya kiroho:

- Je, ni wakati gani mimi niliwahi kuwa kwenye maelekezo yake?
- Je, ninasikiliza maonyo yake kuhusu hatari za kiroho zilizopo?

## Kuanzisha mahusiano yatakayoweka uwajibikaji wa kiroho

Uwajibikaji wa kiroho unafanya kazi vizuri zaidi wakati kukiwa na…

- Faragha
- Uhakika kwamba watu wengine wanakukubali na wanakujali
- Muda uliopangwa kwa ajili ya kushirikishana

Kuweza kumfanya mtu awajibike kiroho inamaanisha kwamba mara kwa mara unamwuliza…

- Je, unaendeleaje katika nidhamu za kiroho?
- Je, unao ushindi wa kiroho?
- Je, unafuatilia ahadi ulilizofanya hivi karibuni?
- Je, ni mambo gani maalumu yenye msimamo unayotaka kufanya kwa sababu ya ukweli uliojifunza hivi karibuni?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninataka niwe mwaminifu katika kutii amri zako zote katika Neno lako. Ninataka niwasaidie ndugu zangu wa kiume na kike katika kubeba mizigo yao; ninataka niweze kuwatia moyo; ninataka nikiri kwao madhaifu ya kushindwa kwangu ili waweze kuomba kwa ajili yangu.

Ninataka niwakubali viongozi wa kiroho ambao umewaweka kwa ajili ya kuwa waangalizi juu yangu.

Naomba unipe unyenyekevu unaohitajika kwa ajili ya kukiri makosa yangu na upendo ninaouhitaji kwa ajili ya kuwasaidia watu wengine katika madhaifu yao. Nisaidie nisiwe mtu wa hasira wakati ninapokuwa nikirekebishwa katika makosa yangu au ninapoumizwa wakati nikiwarekebisha wengine.

Asante kwa ajili ya familia ya kiroho ambayo umenipa kunisaidia mimi kwa ajili ya kukua kiroho

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Angalia katika Yakobo 5:16; Wagalatia 6:2; Waebrania 10:24, na Waebrania 13:17. Soma vifungu vinavyoshikamana na kila aya iliyoonyeshwa hapa. Jaribu kufikiria njia maalumu ambazo hivi karibuni umezitumia kutii maagizo hayo. Je, kuna hatua gani nyingine unazoweza kuzianzisha ili zikuwezeshe kuyatii maagizo hayo vizuri zaidi?

# Somo la 13
# Faida za Maombi

## Wazo Kuu

"Maombi ni mkondo wa baraka za Mungu."

## Sababu za Sisi Kuomba

Tunapaswa kuomba kwa ajili ya:

1. Kumjua Mungu
2. Kukua katika kufanana na Kristo/katika Utakatifu wa Kristo
3. Wokovu na baraka kwa familia
4. Upako binafsi na upanuzi wa huduma
5. Hekima, busana, na mwongozo
6. Ufahamu wa Biblia
7. Mahitaji ya kifedha
8. Furaha na ukamilishaji
9. Kusudi na mpangilio katika maisha yetu
10. Majibu maalumu na miujiza
11. Kuuendeleza ufalme wa Mungu kupitia umisheni

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunisaidia mimi kuona kwamba unataka kunibariki katika njia ambazo sijawahi kufikiria kabla ya hapo.

Naomba unisaidie ili maombi yangu yawe ni mkondo wa baraka zako kwa familia yangu na watu wengine wanaonizunguka.

Zaidi ya yote, ninataka nizungumze na wewe ili kwamba niweze kukujua wewe zaidi.

Asante Baba, kwa fadhila kubwa ya maombi.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Zaburi 141-146. Zaburi zote hizi ni maombi. Angalia aina ya mambo ambayo yameombewa hapo. Angalia kauli ambazo zimetamkwa kuhusu Mungu kama sababu za kufanywa maombi.

# Somo la 14
# Kuomba kama Yesu

## Wazo Kuu

"Ninaomba vizuri ninapoona kile ambacho Mungu anataka kufanya."

## Sala ya Bwana – Mfano wetu

Kama tutajua ni nini ambacho Mungu anataka kufanya, tunaweza tukaomba sawasawa na mapenzi yake na tukajua kwamba atakwenda kujibu.

Kama mtu ni mjinga kwenye kanuni ambazo ni shule ya chekechea ya maombi, hawezi akaomba vizuri kama inavyostahili.

Maombi yetu yote yanatakiwa kuendana na kanuni alizofundisha Yesu katika sala yake ya mfano.

► Mathayo 6:9-13.

Kwamba tunapaswa tuombe kwa mtazamo wa Mungu, thamani, na malengo katika ufahamu.

Kuomba kwamba Jina la Mungu litukuzwe, au lipewe heshima, inaonyesha kwanza kabisa kwamba sisi wenyewe tunataka kumpa Mungu heshima. Tunaweza tukahitaji kupata kila kitu katika maisha yetu na mioyo yetu iwe inayoweza kumpa Mungu utukufu.

Ufalme wa Mungu unaendelezwa kila wakati mtu aliyeasi anapojisalimisha kwa Mungu. Tunapaswa kwanza tuombe kwa ajili ya ufalme wa Mungu kuja kabisa ndani ya mioyo yetu wenyewe, ndiposa uendelezwe kwa ajili ya watu wanaompinga Mungu waweze kujisalimisha kwake.

Kamwe itakuwa haileti maana kuomba kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, kana kwamba ni kitu kizuri, wakati moyo wa mtu haujakubaliana na mapenzi ya Mungu. Kuomba hivi kwa uaminifu kutakuwa ni mwanzo wa kuomba kwa ajili ya moyo safi wa utakatifu.

## Tulia kwa Kutafakari

Je, unaamini kweli kwamba mapenzi ya Mungu ndiyo jambo bora zaidi linaloweza kufanywa ulimwenguni, mahali unapoishi na kufanya kazi, nyumbani kwako, na katika moyo wako?

## Kuombea mahitaji binafsi katika Sala ya Bwana

Ukweli kwamba tunapaswa kuomba kwa ajili ya mahitaji ya kila siku inaonyesha kwamba Mungu anataka tuendelee kumtegemea yeye, kuliko kutegemea rasilimali tulizojilimbikizia.

Maombi ya msamaha yanaonesha kwamba tunapungukiwa kuyajua mapenzi kamili ya Mungu na tunahitaji neema yake ya kila siku.

Kisha kunafuatia ombi la kwamba Mungu atulinde sisi kutokana na madhara yanayoletwa kwetu na Shetani, kimwili na kiroho kwa pamoja.

Tunataka kila kipengele cha maisha yetu na huduma zetu ziendane sawasawa na mapenzi ya Mungu, ziwezeshwe na Mungu, na ziwe zinamletea Mungu utukufu. Tunaomba kwa ajili ya hilo na kujitoa kwa ajili ya hilo kusudi.

Kanuni ya kuomba kama Yesu ni hii: Maombi yanatusababisha sisi kuona kila kitu kutoka katika mtazamo wa Mungu, kwa hiyo tunaweza tukaomba kwa ajili ya kitu kilicho chema kwenye macho ya Mungu.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Tunaomba kwamba jina lako liweze kupewa heshima; kwamba ufalme wako upate kuendelezwa; na wote wanaopingana na wewe waweze kujisalimisha kwako.

Tunaomba kwamba mapenzi yako yapate kutimizwa kabisa ndani ya ulimwengu huu, kwenye maeneo yetu ya kuishi, na ndani ya mioyo yetu.

Tunaomba utupatie mahitaji yetu ya kila siku.

Tunaomba utusamehe kwa ajili ya sisi kushindwa kuyatimiza kikamilifu mapenzi yako, na tusaidie katika kuwasamehe wale wote waliotukosea sisi.

Tulinde kutokana na kuanguka kwenye majaribu, na tulinde sisi kutokana na kitu chochote ambacho yule mwovu anaweza akakileta dhidi yetu

Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Iandike Sala ya Bwana, ukiacha nafasi chini ya kila mstari. Ipitie tena sala hiyo na orodhesha chini ya kila ombi maombi maalumu ambayo unaweza ukawa unayaombea kwa ajili ya kuweza kufahamu wewe binafsi jinsi ya kuitumia Sala ya Bwana.

# Somo la 15
# Fursa ya ushindi juu ya Dhambi

## Wazo Kuu

"Dhambi haiwezi ikanishinda mimi wakati nikiwa ninaruhusu nguvu za Mungu zitende kazi ndani yangu."

## Ushindi juu ya Dhambi

Adui yetu mkubwa sana ni dhambi.

Mungu anatoa ahadi ya kututoa sisi kutoka katika nguvu ya maadui zetu ambazo zinatuondoa sisi katika kumtumikia yeye katika haki na utakatifu kila siku ya maisha yetu. (Luka 1:68-75).

Waraka wa 1 Yohana unaweka msisitizo kwamba tabia kuu ya mwamini wa kweli ni ushindi dhidi ya dhambi.

Mtume alitambua kwamba kuna nyakati ambapo mwamini atahitaji uhakikisho. Akaonyesha kwamba ni jambo lililo sahihi kwa mwamini kutafuta kuwa na ushuhuda ambao utakuwa ni msingi wa uhakikisho wake, Kwa kurudia rudia anatumia maneno, "katika hili tutafahamu."

► 1 Yohana 3:19

Kigezo kinachosisitizwa sana kwenye waraka huu ni ushindi dhidi ya dhambi. Hali ya kawaida ya mwamini ni ya uhuru wa kutoka katika dhambi.

► 1 Yohana 2:1-2

Yohna anatambua kwamba dhambi inaweza ikafanywa, ingawa sio lazima.

Aya zinazofuata kutoka katika 1 Yohana zinaonyesha msisitizo wake kwamba tofauti kubwa sana iliyopo ya mwamini ni ushindi dhidi ya dhambi. Kifungu kilichoko kwenye mabano ni mawaidha yaliyoongezwa.

> Na katika hili twajua [huu ndio ushuhuda] ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake (2:3-4).
>
> Kila atendaye dhambi, [aidha alikuwa mwamini au hakuwa mwamini] afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi. Nanyi mnajua ya kuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake. Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua (3:4-6).

> Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyo na haki; [Haki ni jambo la ukweli, siyo la kujifanya – mtu ambaye kwa ukweli anafanya mambo yaliyo sahihi ni mwenye haki.] Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi (3:7-8).
>
> Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu (3:9).
>
> Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. [Kama atasitisha kukaa ndani ya Kristo, atatenda dhambi. Kama atatenda dhambi, atakuwa amesitisha kukaa ndani ya Kristo.] Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa (3:24).
>
> Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake (5:2-3). [Upendo wa kweli husababisha utiifu. Kutokuwa mtiifu kunaonyesha uwepo wa ukosefu wa upendo.]
>
> Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu (5:4).

Kutokana na aya hizi, inaonekana ni wazi kwamba tabia inayoleta tofauti ya mwamini ni kwamba anaishi kwa kumtii Mungu.

► 1 Wakorintho 10:13, Yakobo 1:12

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya kuniokoa kutoka kwa maadui zangu ambao wanaizuia mimi kukutumikia wewe, na kwa kunitoa kutoka kwa adui yangu mkubwa sana, ambaye ni dhambi.

Asante kwa kunisaidia mimi kuzikataa dhambi wakati nilipotubu na kuja kwako.

Nisaidie kukumbuka kukutegemea wewe kwa ajili ya neema yako ya kila siku. Ninajua kwamba kwa msaada wako ninaweza nikashinda jaribu na kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi.

Asante kwa heshima uliyonipa ya kuishi maisha ya ushindi. Ninataka niwe mwaminifu na nipokee taji la maisha ulililoliahidi kwa watu wote wanaokupenda wewe.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari Warumi 6. Angalia taarifa zote zinazoonyesha kwamba mwamini anapaswa awe na ukombozi kamili kutoka katika dhambi.

# Somo la 16
# Shauku kwa ajili ya Umisheni

## Wazo Kuu

"Nina bidii kwa ajili ya wokovu wa wenye dhambi."

## Uinjilisti ni Kipaumbele cha Kimaandiko

► Mathayo 9:36-38, Mathayo 28:18-20; Matendo ya Mitume 4:29, Matendo ya Mitume 11:18; Wafilipi 1:18; Waefeso 6:19; Warumi 10:13-15

## Sababu za Mwamini kuwa anatakiwa kutamani Uongofu kwa waliopotea

- Anapaswa awe na shauku ya kufuata mfano wa Yesu, ambaye alishuka kutoka mbinguni akaja kuishi na kufa kwa ajili ya wokovu kwa watu waliopotea katika dhambi.
- Anapaswa kutamani kwamba Mungu atatukuzwa kwa kubadilishwa kwa mwasi mmoja na kuwa mtu wa kumwabudu Mungu.
- Anapaswa kuona kuenea kwa injili kama ni ushindi wa Kristo na upatanisho wake.
- Anapaswa atake kushiriki katika kazi ambayo ni kipaumbele cha Mungu.
- Anapaswa awe na huruma kwa ajili ya watu waliopotea katika dhambi ambao wanakabiliwa na hukumu ya ndani kwa ajili ya dhambi zao.

## Sababu za baadhi ya Wakristo kutofanya Uinjilisti

- Ukosefu wa bidii ya Kiroho kwa ujumla.
- Kutojisikia binafsi kuwajibika kwa ajili ya uinjilisti.
- Kutojua jinsi ya kuanza mazungumzo ya kiroho.
- Kutojua jinsi ya kuwasilisha injili kwa njia inayokubalika.
- Hofu ya kushindwa kujibu pingamizi.
- Aibu ya kuonekana uko tofauti na ulimwengu.
- Kuwa na mashaka kwamba juhudi zake zinaweza zisiwe na ufanisi.

## Kuanza kufanya Uinjilisti

Kama mwamini hana bidii ya kiroho, anahitaji uamsho binafsi.

Kila mwamini anahtaji:

1. Imani – Anahitaji kutambua kile ambacho Mungu hufanya ili kuifanya Injili kuwa na nguvu.
2. Maandalizi – Anahitajika kuandaliwa ili kuwasilisha injili.

► Je, ni nini unachokihitaji ili kukuwezesha wewe kuanza?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Uliupenda ulimwengu sana hata ukamtoa Mwanao wa pekee afe kwa ajili ya wokovu wetu. Nataka nikupende kiasi cha kutosha cha kushirikisha shauku yako ya kuokoa watu waliopotea katika dhambi. Ninajua inakupendeza wewe kwa ajili yangu mimi kubeba ujumbe wa injili kwenda kwa wenye dhambi.

Ninataka wewe utukuzwe kwa wenye dhambi kutubu na kuwa watu wa kukuabudu wewe.

Ninataka niwe na hisia ile ambayo Yesu alikuwa nayo kwa ajili ya watu waliopotea katika dhambi.

Ninakuomba uniongoze na uwezeshe juhudi zangu. Nisaidie mimi kushiriki kwenye kazi ya Roho Mtakatifu wako ya kuwaleta kwako watu waliopotea katika dhambi.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Rejea uwasilishaji wa injili ambao umefundishwa kwenye somo la 6 au mfumo mwingine wowote wa uwasilishaji wa injili unaouona kwamba unakufaa wewe. Tafakari matukio yako ya hivi karibuni katika uwasilishaji wa injili na jaribu kupima ni utafiti au mafundisho gani ya ziada yanayohitajika kwa ajili ya kuongeza ufanisi wako. Fanya msimamo maalumu wa kujitoa kwa ajili ya maandalizi hayo.

# Somo la 17
# Imani Idumuyo

## Wazo Kuu

"Tumaini langu kwa Mungu halitegemee kuteseka."

## Imani kwa Maisha Halisi

Ikiwa imani yetu inategemea mwisho wenye furaha kila wakati, imani yetu haiendani na maisha halisi, kwa sababu mambo mabaya hutokea kwa watu ambao hawastahili kuyapata.

Imani ya Kikristo siyo:

- Matumaini yasiyo na maana ("Usijali. Kila kitu kitakuwa sawa.")
- Ustahimilivu mkali ("Maisha hayako sawa kwa hiyo unapaswa kuwa thabiti.")
- Ukwepaji matatizo usiotokana na akili ("Usinikumbushe mimi… Sitaki kufikiri juu ya hilo.")

Imani ya msingi na ya muhimu zaidi ni imani ya msingi kwa Mungu ambayo hudumu bila kujali kinachotokea. Mtu aliye na aina hii ya imani ya kustahimili huwa anaendelea kumtii Mungu.

Tunayo kumbukumbu ya mashujaa wa kiroho amabo waliteseka, siyo kwa sababu walikosa imani, bali kwa sababu walikuwa na hiyo imani. Imani yao iliwasaidia wawe tayari kuteseka.

Imani iliyo katika haki ya Mungu inatusaidia sisi kuvumilia katika hali zote ambazo siyo wakati wote zinafanya kazi katika kipindi kifupi.

Ushuhuda wa imani uko wakati ambapo mwamini anavumilia na kuendelea kumtii Mungu katika hali zote.

Mungu siyo siku zote anaondoa matatizo kupitia muujiza.

Maisha halisi huonekana kuwa na taarifa nyingi za kusikitisha, lakini imani ya Kikristo ni uhakika kwamba Mungu anaandika mwisho ulio wa kweli wa hadithi.

Imani siyo uhakikisho kwamba tutaepukana na mateso. Imani ni kujiamini katika tabia ya Mungu ambayo hututegemeza wakati wa mateso ambayo hatuwezi kuyaelezea.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninataka kukuamini hata yanapotokea mambo ambayo siyaelewi. Ninajua kuwa unanitunza kila wakati.

Nisaidie kuwa na Imani yenye kuvumilia ili niendelee kukufuata wewe katika hali zote.

Asante kwa uaminifu wako kwangu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Waebrania 11. Tambua jinsi watu mbalimbali wa imani kwa uvumilivu mkubwa walivyoweza kufuata maelekezo ya Mungu kwa sababu ya kumtii yeye.

# Somo la 18
# Tunahitaji Kanisa

## Wazo Kuu

“Siwezi kutimiza makusudi yote ya Mungu kwa kufanya mimi mwenyewe.”

## Utangulizi

Kanisa ni moja n ani la kila mahali…

► Waefeso 1:22-23, Waefeso 4:4

…hata hivyo Kanisa ni la mahali au mtaa.

## Baadhi ya Madhumuni ya kanisa la mtaa katika Agano Jipya.

1. Kuabudu na Ujenzi wa maadili kwenye kusanyiko (1 Wakorintho 14:12).
2. Kufundisha mafundisho imara ya imani (1 Timotheo 3:15).
3. Kutuma watu kwenda kufanya uinjilisti na uanafunzi (Mathayo 28:19-20).
4. Kutoa msaada wa kifedha kwa wachungaji (1 Timotheo 5:17-18).
5. Kutuma na kuwawezesha wamisionari (Matendo ya Mitume 13:2-4, Warumi 15:24).
6. Kutoa msaada wa kifedha kwa waumini wenye mahitaji (1 Timotheo 5:3).
7. Kuwatia katika nidhamu washirka wanaoanguka dhambini (1 Wakorintho 5:9-13).
8. Ubatizo na Meza ya Bwana (Mathayo 28:19, 1 Wakorintho 11:23-26).
9. Asili ya waumini katika jumuiya ya Kikristo (Matendo ya Mitume 2:42).

Malengo haya hayawezi kutekelezwa au kukamilishwa na watu binafsi wanaofanya kazi peke yao. Mungu anayo mipango ya huduma za utendaji kwa ajili ya kundi la waamini la mtaa. Anatoa kile kinachohitajika na anahitaji kujitolea kutoka kwetu.

Hapa ni baadhi mifano ya jinsi kundi maalumu la mahali linavyofanya kazi:

| Kipengele Muhimu | Hatua ya Mungu | Jibu la mwanachama linalohitajika |
|---|---|---|
| Uongozi | Huwaita wachungaji | Jinyenyekeze katika kuchungwa |
| Fedha | Huamuru msaada | Kutoa msaada wa kifedha |
| Karama za kiroho | Hutoa karama za kiroho | Tumia vipawa kutumikia kwa uwiano |
| Ushirikiano | Muundo wa “mwili" | Kutambua kuwa tunategemeana. |

Kila Mkristo anapaswa ajitoe mwenyewe, mali zake, na kwa uwezo wake ili kusaidia kanisa la mtaa kukamilisha majukumu yake ya kibiblia. Asipofanya hivyo, hatimizi kusudi lake kama Mkristo.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunipa familia ya kiroho ambayo inashirikiana nami katika mambo yote ya maisha. Asante kwa kunifanya mimi niwe sehemu ya mwili ambao unayafanya mapenzi yako hapa ulimwenguni.

Nisaidie kukumbuka kwamba ninahitaji kanisa na hilo kanisa linanihitaji pia. Nisaidie kufanya ahadi ambazo kanisa la mtaa ambalo linahitaji kutoka kwa waumini wake ili liweze kukamilisha malengo yake.

Kwa pamoja tusaidie tuwe hekalu ambamo Roho Mtakatifu anaishi na kuwapa watu wako uzima.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari 1 Wakorintho 12. Tafakari juu ya maelezo yanayotolewa kuhusu kutegemeana kwa wanachama wa chombo hicho.

# Somo la 19
# Kushinda Dhidi ya Majaribu

## Wazo Kuu

"Ninaweza kuwa mshindi dhidi ya majaribu kwa uongozi na nguvu za Roho Mtakatifu."

## Majaribu

► 1 Wakorintho 10:13

Aya hii inatueleza baadhi ya mambo muhimu kwetu.

1. Kila jaribu ni jambo la kawaida kwa wanadamu wote.
2. Mungu anajua mipaka yetu.
3. Mungu anatukusudia sisi tuishi kwa ushindi.
4. Mungu hutupa vitu tunavyohitaji kwa ajili ya kutuwezesha tuishi kwa ushindi.

Neema kwa ajili ya maisha ya ushindi inatolewa kama jibu la imani (1 Yohana 5:4).

► Yakobo 1:14-15

John Wesley alichunguza kwamba hatua zinazopelekea kutenda dhambi kwa kawaida zinatokea kama ifuatavyo.[7]

1. Jaribu huinuka.
2. Roho Mtakatifu humtahadharisha na kumwonya mwamini kuwa mwangalifu.
3. Mtu huliangalia na kulipa nafasi lile jaribu, na linaanza kuwa kivutio kwake. (Hapa ndipo mwamini anapofanya kosa lake la kwanza kwenye mchakato huu.)
4. Roho Mtakatifu huhuzunishwa, imani ya mtu inadhoofika, na upendo wake kwa Mungu unapoa.
5. Roho Mtakatifu hukemea kwa ukali.
6. Mtu hugeuka katika kusikia ya *huzuni* ya Roho Mtakatifu na kuanza kusikiliza sauti ya *mvuto* kutoka kwa mjaribu.
7. Matamanio ya uovu huanza na kuujaza moyo wake; imani na upendo vinatoweka; na yuko tayari kufanya dhambi inayoonekana wazi kwa nje.

[7] Imenukuliwa kutoka *A Timeless Faith: John Wesley for the 21st Century*, na kufanyiwa uhariri na Stephen Gibson.

Jaribu ni changamoto kwa imani yetu, kwa kuwa majaribu yanatoa nafasi kutilia shaka utii kwa Mungu kwamba ndiyo njia bora zaidi wakati huo.

Kama mwamini hawezi kuwa na mwelekeo wa kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi, inawezekana ikawa ni kwa sababu ya mojawapo ya matatizo yafuatayo:

1. Haoni kama Mungu anahitaji utiifu.
2. Haoni na haamini ahadi ya neema ya Mungu inayowezesha na inayofanya kazi.
3. Hategemei neema ya Mungu inayowezesha na inayofanya kazi badala ya kutumainia nguvu zake mwenyewe.
4. Anamtumikia Mungu akiwa na utii katika mambo fulani tu aliyochagua, badala ya utii kamili usiokuwa na masharti.
5. Hajatafuta kwa neema kuwa na kusudi moja tu la kufanya yaliyo mapenzi ya Mungu (Wafilipi 3:13-15).
6. Hadumishi nidhamu za kiroho ambazo zina uwezo wa kumtia nguvu katika kujenga uhusiano wake na Mungu

Mungu tayari alishaweka uwekezaji mkubwa sana kwa ajili ya wokovu wetu, katika dhabihu ya Yesu. Hatakuwa tayari kuruhusu uwekezaji huo upotee bure kwa kushindwa kutupa sisi neema tunayohitaji ili ituwezeshe kusonga mbele

► Warumi 8:32, Juda 1:24-25

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Ninakushukuru kwa kuwa unayajua yote yanayohusiana na mimi. Unajua mipaka na madhaifu yangu. Asante kwa kuniwekea mipaka kwa ajili ya majaribu yanayokuja kwangu na kunipa neema ili kwamba niweze kuishi kwa ushindi.

Nisaidie siku zote niweze kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu. Nisaidie siku zote niweze kukataa dhambi mara tu ninapotambua kwamba jambo hili ni dhambi.

Naomba unisaidie katika kukumbuka kwamba ni wewe peke yako unayeweza kuuridhisha moyo wangu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Ufunuo 2-3. Sura hizi zina barua kwenda kwa makanisa saba. Makanisa haya yalikuwa yanakabiliwa na majaribu mbalimbali pamoja na changamoto nyingi. Jaribu kuangalia kwenye mwisho wa kila barua kwamba kuna ahadi inayotolewa kwa mtu anayeshinda.

# Somo la 20
# Mwongozo wa Mungu

## Wazo Kuu

"Ninashinda vita vya maisha kwa kufuata tu maelekezo kutoka kwa kamanda wangu."

## Maombi – Mawasiliano katika Vita

Mawasiliano ni muhimu sana katika kushinda vita. Sisi tuko kwenye vita vya kiroho. Maombi ndiyo njia yetu ya kuwasiliana na kamanda wetu.

► Waefeso 6:18

Mungu ameahidi uongozi kwa ajili ya wale wote watakaomsikiliza na kumtii yeye.

► Mithali 3:5-6, Zaburi 37:23

Nyakati ambazo hususani tunahitaji mwongozo wa Mungu:

1. **Wakati tunapofanya maamuzi ya kubadilisha mtazamo.** Ndoa, kazi, elimu, kujitolea kwa kanisa la mtaa.
2. **Wakati wa kufanya maamuzi ya vitendo**: Nafasi za kazi, mahali pa kuishi, manunuzi makubwa.
3. **Wakati tunapopanga na kufanya huduma**: Wito binafsi, mahali gani na nani wa kuhudumu naye, mada za kufundisha na kuhubiri.
4. **Wakati wa kushiriki kwenye mambo yanayohusu uhai wa kanisa:** Jinsi ya kuabudu, kitu cha kujifunza, kitu cha kutoa, jinsi ya kuwa sehemu ya mwili wa Kristo hapa duniani.

## Njia za kutambua Mwongozo wa Mungu vizuri zaidi:

1. **Kuwa karibu zaidi na Mungu kwa njia ya maombi.** Kama sehemu kubwa ya maisha yako yametenganishwa kwenye maongezi na Mungu, unafuata matakwa yako mwenyewe na mitazamo yenye mipaka.
2. **Usiziamini sana akili zako mwenyewe za kufikiri kuliko ukweli halisi wa kimaandiko.** Kama Mithali 3:5 inavyosema, "...Wala usizitegemee akili zako mwenyewe."
3. **Wakati wowote kuwa mtiifu kwa kile unachojua kwa uhakika kwamba kiko kwenye mapenzi ya Mungu.** Hali hiyo itaimarisha mtazamo wako. Kama utakuwa mtiifu kwa sehemu tu ya kile unachojua kwamba ni mapenzi ya Mungu kwa ajili yako, itakupelekea kuchanganyikiwa zaidi – nuru itageuka kuwa giza (Luka 11:35).

4. **Usiahirishe utiifu wako kwenye mapenzi ya Mungu**. Usingojee hali zibadilike kabla ya kumtii Mungu. Huwezi ukapata mambo mazuri sana ya Mungu hadi uwe umesubiri wakati wake.

5. **Kuwa mvumilivu.** Unaweza ukahitajika kungojea wakati Mungu akifungua milango na akiandaa mazingira mbalimbali kwa ajili yako. Usichukulie mambo mikononi mwako kwa sababu ya kukosa uvumilivu. "Ukae kimya mbele za Bwana, Nawe umngojee kwa saburi" (Zaburi 37:7). Kamwe usifanye jambo ambalo unajua kwamba ni uovu kwa sababu ya nia ya haraka.

6. **Sikiliza ushauri mzuri** (Mithali 24:6). Wakati Mungu anapokutaka wewe ufanye uamuzi mkubwa, mara kwa mara atakuwa analionyesha hilo kwa watu wengine walio muhimu kwenye maisha yako. Kama kuna wazee, wenye hofu ya Mungu wanaokujua na wanaokujali, hutapaswa kufanya kirahisi tu mambo ambayo wanafikiri kwamba ni makosa.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nina furaha kwamba unajua matokeo yatakavyokuwa kwa uamuzi wowote nitakaoufanya. Asante kwa kupanga mambo mazuri kwa ajili yangu. Ninajua kwamba unaziongoza hatua zangu zaidi sana kuliko hata ninavyoweza kuona.

Nisaidie mimi nijifunze zaidi jinsi ya kufuata uongozi wako. Niwezeshe kukaa karibu zaidi na wewe kwa njia ya maombi. Nisaidie niwe makini na msikivu kwenye ukweli ambao unanionyesha. Nisadie mimi niweze kusubiri mwelekeo wako kwa saburi.

Ninataka nikuamini wewe kwenye kila uamuzi. Ninataka nifuate mapenzi yako kwa utiifu wa moyo wangu wote.

Asante kwa kutaka mambo yaliyo bora kwa ajili yangu.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari Mithali 3:1-12. Je, ni mambo gani ya thamani, mwenendo, na tabia yanayoelezwa hapa ambayo yanaweza kuwa ni halisi na maisha ambayo Mungu huongoza na kubariki? Je, ni kwa jinsi gani wewe binafsi unaweza kuyakuza?

# Somo la 21
# Vizuizi vya Maombi

## Wazo Kuu

"Ni lazima niepukane na makosa ambayo huzuia maombi yangu."

## Vizuizi katika Maombi

### (1) Ukosefu wa motisha

► Marko 1:35

Mtu aliye katika shughuli nyingi hupuuzia maombi kwa sababu anajiona kwamba kile anachokifanya yeye ni muhimu zaidi kuliko kile anachokifanya Mungu.

Unapokuwa umeomba, unaweza ukafanya zaidi ya kuomba, lakini huwezi ukafanya kuomba zaidi hadi utakapokuwa umeomba.

### (2) Kiburi cha kiroho

► Mathayo 6:5-6

### (3) Maombi yasiyohusisha hisia

► Mathayo 6:7

Mungu hasogezwi kimawazo na maombi yetu. Yeye ni hai ya mtu.

### (4) Kutokusamehe

► Mathayo 6:15, 1 Timotheo 2:8

Bila ya kuwepo na neema ya kusamehe, hatuwezi kuendelea kuwa kwenye uhusiano na Mungu.

### (5) Kutokiri kwa watu wengine mambo mabaya uliowafanyia

► Mathayo 5:23-24

Ili ibada yetu ya kumwabudu Mungu iweze kukubaliwa na yeye, ni lazima kwanza tukiri makosa ya aina yeyote ambayo tumewakosea watu wengine.

► 1 Petro 3:7

Kama huna upendo, ni mgandamizaji, na usiyefikiria kuhusu hisia na haki za mtu mwingine, Mungu hapendezwi na wewe, na itakuwa vigumu sana kwako kuweza kufanya maombi.

**(6) Kushindwa kung'ang'ania**

► Mathayo 7:7

Endelea kudumu kwenye maombi kwa kutumia orodha ya mambo ambayo umekusudia kuyaombea.

**(7) Kukosa Utii.**

► 1 Yohana 3:22

Utii ndiyo msingi wa imani.

**(8) Nia za dhambi**

► Yakobo 4:3

**(9) Kutokuamini**

► Waebrania 11:6

### Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunipa mimi kibali cha kuongea na wewe.

Ninahitaji nikufurahishe wewe kwa matendo yangu dhidi ya watu wengine. Ninataka niwe mnyenyekevu na mwenye kusamehe. Ninataka niwe mtu wa kuendelea kudumu kwenye maombi hadi pale utakaponionyesha mimi ni kitu gani unataka kufanya kuhusiana na ombi langu.

Ninataka sababu zangu za kufanya jambo lolote ziwe za uaminifu na zilizo safi. Ninataka niombe kwa imani kwa ajili ya mapenzi yako kutimizwa.

Baba, ninathamini muda wangu nikiwa na wewe. Nisaidie katika kuepuka mambo ambayo yatakuwa ni kizuizi cha uhusiano wangu na wewe. Naomba unifundishe jinsi ya kuomba.

Amina.

### Kazi ya Kufanya

Soma 1 Timotheo 2:1-8. Kutoka katika kifungu hiki, ni kwa jinsi gani unaweza kuelezea tabia au hulka ya mtu ambaye anaweza kuomba kama Mungu anavyomtaka afanye?

# Somo la 22
# Mahusiano

## Wazo Kuu

"Kanuni za Mungu zinaniongoza na kukamilisha mahusiano yangu."

## Kanuni ya Amani

► Waebrania 12:14

Kuitafuta amani, angalau itakupasa umtendee kila mtu jambo ambalo unapaswa ulifanye kwake. Lakini kuitafuta amani kunahitaji zaidi ya kutoa unachodaiwa. Hii inajumuisha pamoja na kuwa na upendo na wema usiodaiwa.

Kama utakuwa unataka amani utatafuta upatanisho wakati kunapokuwepo na mgogoro, Utakuwa tayari kusamehe na au kusamehewa.

Wakati mtu anapokataa kusamehe, anaweka sehemu fulani ya maisha yake kwenye mgongano na Mamlaka ya Mungu, kwa kuwa Mungu anatutaka sisi tuweze kusamehe.

Kwa vile Mungu ametukomboa sisi, sisi ni mali yake, na haki zetu ni mali yake. Ni lazima kwa makusudi kabisa tuweze kutoa haki zetu kutoka kwa Mungu.

## Kanuni ya Upendo

Mtu ambaye hatuwiwi chochote na yeye bado ni lazima tumtendee kwa upendo (Warumi 13:8).

Upendo ni uhakikisho au ushahidi kwamba mtu ni Mkristo kamili (1 Yohana 4:20).

Yesu huyachukua yeye mwenyewe matendo yako na tabia zako dhidi ya waamini wengine (Mathayo 25:40).

Upendo wa Kikristo lazima pia kuoneshwa kwa maadui zetu (Mathayo 5:44-45).

Kamwe hakuna msamaha kwa kuwa mkatili. Hatupaswi tuwatendee watu kama wanavyostahili kwa maudhi yao.

## Kanuni ya Heshima

Sura ya Mungu inampa kila mtu thamani ya kuwa mrithi.

Heshima ni lazima idhihirishwe kwa kila mawasialiano na watu. Kiwango cha chini kabisa cha kuonesha heshima ni adabu. Hila au udanganyifu ni makosa.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie mimi kuishi kwa mujibu wa kanuni za kimaandiko za amani, upendo na heshima kwenye mahusiano yangu yote.

Ninataka niwe mtu wa kusamehe kwa wale wote wanaonitendea mabaya. Nisaidie katika kutafuta upatanisho na wale ambao wako kwenye mgogoro na mimi.

Ninataka niwe na upendo kwa ajili ya watu wengine juu ya kiwango cha hali ya juu cha uvumilivu wa mwanadamu.

Nisaidie mimi kuheshimu kila mtu kama uliyemfanya kwa sura yako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Soma Waefeso 5:22–6:9 kwa ajili ya maelekezo ya mahusiano ya aina mbalimbali. Orodhesha ni mambo gani tofauti utakayoyafanya kwenye mahusiano yako.

# Somo la 23
# Mtindo makini wa maisha ya Kikristo

## Wazo Kuu

"Maisha yangu ya kila siku yanaonyesha kwamba niko makini katika kumpendeza Mungu."

## Kanuni kwa ajili ya Maamuzi ya Mfumo wa Maisha

Tabia, uchaguzi wa mambo ya burudani, na mavazi vyote hivi vinaonyesha kitu fulani kuhusiana na mielekeo ya moyo.

1. **Ni lazima tutii maagizo yote ya Biblia yaliyoko kwa ajili ya Wakristo** (Mathayo 5:19).
2. **Maagizo ya Mungu ni kwa ajili ya faida yetu wenyewe** (Kumbukumbu la Torati 10:12-13).Mungu hawezi akaacha kutuonyesha kitu ambacho ni kizuri kwetu, au hatuamuru agizo ambalo lina madhara kwetu.
3. **Uhuru wa Mkristo siyo Uhuru wa Kutii Mungu** (1 Wakorintho 9:21, Warumi 6:18).
4. **Kama tunampenda Mungu, tunataka tuyajue mapenzi yake, na siyo kuyakwepa** (1 Yohana 5:2-3). Mtu anayempenda Mungu kwanza hatauliza, "Je, Mungu ataweza kunihukumu mimi kawa ajili ya kutenda hivi?" lakini, "Ni jambo gani ambalo Mungu atapendezwa analo zaidi kwangu?" (Wakolosai 1:10).
5. **Maandiko yanatoa msingi wa kuweka sheria mahususi kwa ajili ya maisha yetu.** Baadhi ya vifungu vimeorodheshwa kwenye kazi za kufanya ambazo hutoa msingi wa Kikristo wa kuishi kwa uangalifu. Baadhi ya hizo hutoa miongozo maalumu kwa ajili ya mfumo wa maisha ya Kikristo.
6. **Sheria kuhusu mambo mengi ya maisha siyo imani zetu muhimu zaidi** (Mathayo 23:23).
7. **Kushika sheria hakutoshi kuthibitisha utii na upendo wetu kwa Mungu** (Mathayo 23:25).
8. **Uhakika wetu katika ushuhuda na watu wengine hautegemei mambo madogo madogo yanayohusiana na mfumo wa maisha yao** (Warumi 14:10).

9. **Uvumilivu wa maoni tofauti hauna msamaha kwa uzembe binafsi** (Warumi 14:5, 23). Kunakuwepo na matokeo mabaya wakati mtu anapokiuka dhamiri yake mwenyewe. Kama mtu ataamua kufanya jambo fulani analilofikiria yeye mwenyewe kwamba siyo sahihi, ana hatia ya dhambi. Kunazo baraka ambazo wakati mtu anapotembea katika maisha ya nuru ambayo amepewa na Mungu (1 Yohana 1:7).

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie niishi kwa kukubaliana na maagizo ya Neno lako. Ninajua kwamba kila kitu unachoamrisha ni muhimu.

Nisaidie niwe mwaminifu kwenye dhamiri yangu, kwa chochote ambacho watu wengine wanakifanya. Niwezesha kuwa na tabia ya Kikristo dhidi ya wale watu wote ambao hawakubaliani na mimi.

Ninataka imani yangu ijionyehe kwenye kila kitu nitakachokuwa ninafanya. Nisaidie mimi katika kila eneo la maisha yangu katika kuchagua mambo ambayo yatafanya maisha yangu yawe mfano wa neema yako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari kuhusu Maandiko yafautayo ambayo yanatoa msingi unaohusiana na tabia ya uangalifu ya Mkristo:

- 1 Wakorintho 6:19-20
- 1 Wakorintho 10:31
- 1 Wakorintho 11:14-15
- 1 Timotheo 2:9-10
- 1 Petro 3:3-4
- Kumbukumbu la Torati 22:5
- Zaburi19:14
- Zaburi101:3

Je, ni viwango gani vya binafsi utakavyotakiwa kuzingatia kwenye Maandiko hayo?

# Somo la 24
# Usemi wa Mkristo

## Wazo Kuu

“Kuna kanuni za kibiblia za mazungumzo yangu.”

## Kanuni za kibiblia za Mazungumzo.

Ni kwa jinsi gani tunaweza kuyatumia maneno katika kukamilisha mambo yaliyo mema na kuepuka yanayoleta madhara? Biblia inatoa kanuni kadhaa:

1. **Usiwe mtu mwongeaji sana** (Mhubiri 10:14, Mithali 10:19).
2. **Usizungumze kabla ya kufikiria** (Yakobo 1:19, Mithali 29:11).
3. **Usihukumu unapoona jambo kwa mara ya kwanza** (Mithali 18:13).
4. **Kuwa makini na mizaha** (Mithali 26:18-19).
5. **Usiseme jambo lolote kwa mtu asiyekuwa mhusika** (Mithali 11:13). Kuna nyakati nyingine ambapo inahitajika jambo fulani liweze kusemwa, lakini ikawa wewe siyo mtu sahihi unayetakiwa kulisemea jambo hilo (Mithali 25:9).
6. **Kuwa mwangalifu katika kutoa shutuma.** Kuna muda sahihi wa kutoa shutuma kwa njia sahihi (Mithali 27:5-6a). Hakikisha kwamba shutuma zako zina lengo la kujenga na siyo kuharibu.
7. **Usiwe mdanganyifu** (Wakolosai 3:9). Udanganyifu uko kwenye maisha ya dhambi na siyo kwenye maisha ya Kikristo.
8. **Mazungumzo au maneno yako yawe masafi** (Waefeso 5:4). Usitake kuelezea kuhusu kashfa za zamani au za sasa isipokuwa inapokuwa ni muda rasmi muafaka wa kushughulikia hali hiyo. Usiseme kwa utani jambo ambalo lilikuwa ni jambo la lazima linalopaswa kuelezea kwa siri. Watu wa dunia kwa kawaida hutumia maneno yanayohusika na kujamiana au maneno yanayohusiana na sehemu za siri za mwili kwenye mshangao wao, lakini hali kama hiyo siyo sahihi kwa Mkristo. Ni jambo la kipuuzi na kukosa heshima kutumia maneno yanayomtaja Mungu au Yesu kama njia ya kushangaa wakati wa msongo wa mambo, isipokuwa kama unamwita Mungu kwa dhati ili akusaidie.
9. **Usiwagawe watu kwa maneno yako** (Mithali 16:28). Kabla ya kusema jambo usifikirie tu kwamba “Je, ni kweli?” lakini fikiria pia kwamba “Je, ni kwa nini niseme jambo hili?"

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie kukumbuka athari ya mazungumzo yangu ninayoweza kuwa nayo, na niwezeshe kuwajibika kwa ajili ya maneno yangu. Ninataka maneno yangu yaweze kukamilisha mambo mazuri na siyo kuleta madhara.

Ninataka ushuhuda wangu ulio kwa ajili yako uweze kuheshimika.

Nisaidie katika kuwa msafi, mwaminifu, mkarimu na mwangalifu.

Asante kwa ajili ya kibali na fursa ya kuwasilisha ukweli wako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari Yakobo 3. Tazama uwezo mkubwa wa mazungumzo ulioelezwa hapa. Kwenye aya za 13-18 ona jinsi mazungumzo yanavyotiririka kwa urahisi kabisa kutoka katika hali ya kiroho ya mtu.

# Somo la 25
# Maadili ya Kazi ya Kikristo

## Wazo Kuu

"Ninafanya vizuri sana nikiwa kazini kwa sababu Mungu ndiye mwajiri wangu."

## Mtazamo wa Kikristo juu ya Kazi.

Mkristo anapaswa kufanya kazi kwa sababu ana wajibu kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya watu wengine (2 Wathesalonike 3:10).

Mtu asitegemee watu wengine wachukue jukumu la kumwangalia yeye kama yeye mwenyewe hayuko tayari kufanya kile ambacho yeye binafsi anaweza kukifanya.

Mwamini ana wajibu kwa ajili ya familia yake mwenyewe (1 Timotheo 5:8).

Mkristo anafanya kazi pia ili kusaidia wengine (Waefeso 4:28).

## Kanuni ya Uwajibikaji

Kanuni zinazotokana na Waefeso 6:5-8:

1. Mfanyakazi anapaswa kumtii mwajiri wake, siyo tu kwa wakati anapokuwa anatazamwa, lakini kwa wakati wote.
2. Mfanyakazi anapaswa adumishe ubora na bidii ya kazi yake kana kwamba anafanya kazi kwa ajili ya Mungu.
3. Mfanyakazi atabarikiwa na Mungu kwa ajili ya uaminifu katika kazi yake.

## Kanuni ya Uaminifu

Kanuni zinazotokana na Tito 2:9-10:

1. Mfanyakazi anapaswa kuwa na heshima katika kuitikia kwake kwa ajili ya maelekezo ya mwajiri wake
2. Mfanyakazi hapaswi kumwibia mwajiri wake, hata kama anafikiri anastahili malipo zaidi
3. Kazi ya uaminifu ni ushuhuda kwa ajili ya injili; ukosefu wa uaminifu ni aibu kwa injili

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya kunipa uwezo wa kufanya kazi na fursa ya kazi.

Nisadie mimi katika kufanya kazi iliyo nzuri kwa ajili ya mwajiri wangu, kuonyesha heshima kwake, kuelewa nini anachokihitaji kutoka kwangu, na kufanya vyema hata wakati ambapo kazi yangu haipaswi kukaguliwa.

Nataka niwe mwaminifu kwa kile ninachopata, kuwajibika kwa ajili ya mahitaji yangu na kuweza kutoa kwa ajili ya kuwapa watu wengine msaada.

Nisaidie kukumbuka kwamba ninafanya kazi kwa ajili yako na kwamba malipo mazuri kabisa yanatoka kwako.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Tafakari aya hizi kuhusiana na somo la kazi na uvivu:

- Mithali 6:6-11
- Mithali 10:4-5
- Mithali 12:11
- Mithali 12:24
- Mithali 12:27
- Mithali 13:4
- Mithali 13:11
- Mithali 14:23
- Mithali 18:9
- Mithali 20:13
- Mithali 22:29
- Mithali 24:30-34
- Mithali 26:13-16

# Somo la 26
# Kufanya Maamuzi Sahihi

## Wazo Kuu

"Maadili ya milele yanaongoza maamuzi yangu."

## Ushauri ufaao kwa Kufanya Maamuzi Mazuri

John Wesley alisema kwamba mapenzi ya Mungu kwa ujumla kwetu ni kuwa watakatifu na kufanya mema. Hivyo, **ili kufanya uamuzi maalum, tunapaswa kuzingatia ni chaguo gani litatusaidia zaidi kuwa watakatifu na kutimiza mema mengi zaidi.**

**Mungu anatutarajia sisi kutumia kanuni za Maandiko huku tukifikiri kwa makini na kupima mazingira yetu.**

Watoto wa Mungu wanaodai kuongozwa maalum na Mungu mara nyingine hukasirika wanapohojiwa maamuzi yao. Wanakuwa na kiburi na jeuri badala ya unyenyekevu. Mtu hastahili kukataa ushauri wa wengine kwa kudai ana maarifa maalum ya mapenzi ya Mungu.

Mbali na kanuni ambazo Wesley alizitoa, wakati unapokuwa katika kufikiri juu ya chaguzi zako, tafakari mambo yafuatayo:

1. Je, zinaendana wazi na amri za Kiroho?
2. Je, zinaendana na vipaumbele vya Kimaandiko?
3. Je, zinaendana na mtazamo halisi wa hali zilizopo?
4. Je, ni jambo la busara?
5. Je, ni tabia ya Kikristo?
6. Je, inaendana na kupenda watu wengine kama unavyojipenda?
7. Je, itakuwa na ushawishi mzuri?
8. Je, inathibitishwa na washauri wa Mungu?

Wakati mapenzi ya Mungu ni jambo lisilo la kawaida sana, Mungu ana uwezo wa kuyafanya yajulikane kwako pasipokuwa na shaka yeyote. Lakini inapotokea kwamba hakuna ujumbe ulio wazi uliopokelewa kutoka kwa Mungu, unapaswa ufuate kanuni za kuaminika kwa ajili ya kutambua chaguo sahihi. Usitegemee kupokea ufunuo maalumu kwa kila uamuzi. Kama kwa unyofu na kwa maombi unatafakari sababu kwa vipaumbele sahihi, Mungu atakuwa mwaminifu kuongoza uamuzi wako.

► Warumi 12:1-2

Ili kupata mapenzi ya Mungu, ni lazima kwanza mtu ajitoe kabisa au kikamilifu kwa Mungu. Kusudi au nia ndio jambo muhimu zaidi katika kutambua mwelekeo wa Kimungu.

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Nisaidie nijifunze jinsi ya kukusikiliza wewe. Ninataka niwe mtakatifu na niweze kukamilisha mambo mazuri kwa kadri iwezekanavyo kwa ajili ya utukufu wa jina lako.

Uifanye nia yangu iwe safi, ili maamuzi yangu yasiweze kunipeleka mbali na mapenzi yako. Niongoze kupitia washauri wenye busara ambao umewaweka kwenye maisha yangu.

Nisaidie katika kuona mambo jinsi yalivyo na niwezeshe kufanya maamuzi yaliyo sahihi.

Amina.

## Kazi ya Kufanya

Chunguza Yakobo 4:13-17. Angalia ukuu wa Mungu jinsi ulivyo juu ya hali zilizopo. Je, ni ubaya gani, au majivuno gani ambayo yanarejelewa katika mstari wa 16? Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu kupanga kwa ajili ya siku zijazo?